# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 7 Mei, 2020

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa naomba tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ABDALLAH -KATIBU MEZANI**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara na Randama ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAYA - (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI MALIASILI NA UTALII):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu !

**NDG. RAMADHANI ABDALLAH -KATIBU MEZANI**

## MASWALI NA MAJIBU

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 222

### Halmashauri Kutenga 10% kwa ajili ya Wanawake na Vijana

**MHE. GODFREY W. MGIMWA** aliuliza:-

Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaeleza wazi juu ya kuwawezesha wananchi kiuchumi hasa kwenye suala la ujasiriamali:-

Je, Serikali ipo tayari kutoa agizo la msisitizo kwa Halmashauri zote nchini kutenga fedha za asilimia 10 kwa wanawake na vijana bila kukosa kila mwaka kama inavyotakiwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 kwa kuongeza Kifungu cha 37A(1) – (4) kinachoelekeza Halmashauri zote kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Aidha, ili kuimarisha usimamizi wa Sheria, Waziri mwenye dhamana ametunga Kanuni za usimamizi wa utoaji na urejeshaji wa mikopo hiyo zilizotangazwa kwenye Tangazo

la Serikali Na. 286 la tarehe 5 Aprili, 2019. Hivyo, suala la mikopo hiyo kwa sasa linasimamiwa kwa mujibu wa sheria tofauti na awali.

Na. 223

**Kituo cha Afya Kata ya Ulowa – Ushetu**

**MHE. LUCY T. MAYENGA** aliuliza:-

Serikali ilitenga fedha kujenga Kituo cha Afya eneo la Nyalwelwe katika Kata ya Ulowa, Wilayani Ushetu:-

Je, nini sababu ya kutopelekwa fedha hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imetumia jumla ya Shilingi bilioni 1.9 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu na Kituo cha Afya Ukene katika Halmashauri hiyo. Mpango wa Serikali ni kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya katika maeneo yaliyobaki kikiwemo Kituo cha Afya cha Ulowa kadri upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kawaida huwa inapokea vipaumbele vya vituo vya kupeleka fedha kutoka kwenye Halmashauri na Mikoa na sio sahihi kuwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI huwa inachagua maeneo ya kupeleka fedha. Kwa mwaka 2020/2021, tumetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha jumla ya maboma 555 ya Zahanati na Vituo vya Afya kwenye Halmashauri 184 na Halmashauri zote tayari zimewasilisha Vituo vyao vya kipaumbele. Kwa Halmashauri ya Ushetu wao wamewasilisha maboma ya Zahanati za Bugomba A, Makongoro na Nshimba. Sina

taarifa kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliwahi kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya kwenye Eneo la Nyalwelwe.

Na. 224

**Vijana Wanaohifadhi Kasa**

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA** aliuliza:-

Suala la ukusanyaji mapato ni la Muungano:-

(a) Je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudi za vijana wa Nungwi Mnarani Kaskazini Unguja ambao wanahifadhi Kasa?

(b) Kwa kuwa wageni mbalimbali hutembelea eneo hilo na kulipa pesa kidogo: Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa ruzuku ili kuboresha shughuli hiyo na Serikali kujipatia mapato kwa kazi hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua juhudi na michango ya makundi mbalimbali yanayoshiriki katika kuchangia pato la Taifa ikiwemo kundi la vijana wa Nungwi Mnarani, Kaskazini Unguja ambao wanahifadhi Kasa.

(b) Ofisi imepokea ushauri wa Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka na kuahidi kulifanyia kazi kwa kuliwasilisha suala hili, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili iweze kuangalia uwezekano wa kutoa ruzuku na kushauri kuongezwa kiingilio kwa ajili ya kuboresha shughuli ya uhifadhi na hatimaye kuimarisha mapato.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Malembeka kuwa, moja ya vipaumbele vya Serikali zetu mbili ni kuhakikisha inashajihisha makundi yote ambayo yanajitoa katika kuchangia pato la Taifa kwa namna moja au nyingine ikiwemo kundi la vijana.

Na. 225

**Wajawazito Wanaoenda Kliniki bila Wenza**

**MHE. ZAINAB M. BAKAR** aliuliza:-

Kumekuwa na tabia ya baadhi ya zahanati kutotoa huduma kwa akinamama wajawazito wanapoenda kuanza kliniki bila ya wenza wao:-

Je, Serikali haioni kwamba tabia hii inaendeleza vifo kwa wajawazito kwa kukosa huduma hiyo?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaendelea kuimarisha Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto ikiwemo huduma kwa akinamama kabla ya ujauzito, wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua. Aidha, Serikali imeendelea kutoa huduma kwa akinamama wakati wa ujauzito katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya, zikiwa ni pamoja na kupimwa wingi wa damu, shinikizo la damu, magonjwa mbalimbali kama Malaria, UKIMWI na Kaswende.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kutambua dalili za hatari au magonjwa wakati wa ujauzito na kuweza kuchukua hatua stahiki mapema ili kuzuia matatizo yatokanayo na

uzazi. Vilevile, Serikali inasisitiza wajawazito wote kuhudhuria kliniki mapema wakiwa na wenza wao ili kuweza kupata huduma hizi ndani ya muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sera ya Afya ya mwaka 2007, huduma za afya ya uzazi hutolewa bure bila malipo na huduma hizi hutolewa muda wote katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, huduma hizi hutolewa kwa kila mjamzito bila kujali kama amekwenda na mwenza wake au hakwenda. Hata hivyo, Serikali inasisitiza kwamba ni vyema mjamzito akaambatana na mwenza wake ili wapate elimu ya afya kwa pamoja na ikibidi wapate baadhi ya vipimo kwa pamoja ili kuweza kuhakikisha afya bora ya mtoto aliyeko tumboni. Katika eneo hili la utoaji huduma kwa wanawake wakati wa ujauzito (*Antenatal Care*).

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imefanikiwa kuongeza kiwango cha akinamama wajawazito 1,744,668 waliohudhuria kliniki wakati wa ujauzito, ambapo wajawazito 1,343,228 walitimiza mahudhurio manne au zaidi *(ANC4+)* sawa na asilimia 77 ikilinganishwa na asilimia 41 kwa mwaka 2015/2016 wakati Serikali ya Awamu ya Tano ikiingia madarakani. Hii ni kutokana na huduma nzuri zinazopatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo watoa huduma za afya wanawahudumia akinamama wajawazito bila kujali kama wameenda na wenza wao ama hawakwenda nao. Aidha, Serikali inaendelea kuwasisitiza wanaume juu ya umuhimu wa kuwasindikiza wenza wao pindi wanapohudhuria kliniki ya ujauzito.

Na. 226

**Mradi wa Maji wa Mabokweni Hadi Chongoleani**

**MHE. MUSSA B. MBAROUK** aliuliza:-

Miongoni mwa Miradi ya Maji Vijijini ya Vijiji Kumi (10) kwa kila Halmashauri ni pamoja na Mradi wa Maji wa

Mabokweni, Kiruku, Mpirani, Bwagamoyo hadi Chongoleani; Mradi huu hautoi maji na wananchi wanaendelea kutaabika:-

Je, tatizo ni nini?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Mabokweni uliopo katika Halmashauri ya Jiji la Tanga ulisanifiwa kuhudumia vijiji/mitaa mitano (5) ya Mleni, Kibafuta, Mpirani, Ndaoya na Chongoleani. Mradi huu ambao unagharimu kiasi cha Sh.2,412,977,490.00 utakapokamilika utawapatia huduma ya majisafi na salama wananchi wapatao 15,750. Mpaka sasa matenki mawili (*water sump & storage tank*) yamejengwa, ujenzi wa nyumba ya pampu na ufungaji wa pampu na umeme pamoja na ujenzi wa vituo 24 vya kuchotea maji umekamilika.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa, Serikali kupitia Wizara ya Maji imeukabidhi mradi huo kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiijini Tanga kwa kuzingatia Sheria ya Maji Na.5 ya mwaka 2019 kwa ajili ya kuukamilisha na hatimaye kusimamia uendeshaji ili wananchi wanufaike na mradi huo. Hadi sasa, wananchi wapatao 2,500 wa Vijiji vya Kibafuta na Kiruku wanapata huduma ya maji kufuatia kuunganisha maji katika vituo vitano vilivyopitiwa na mtandao.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia Wataalam wa ndani (*Force Account*) ili kukamilisha mradi huo kwa wakati na kwa gharama nafuu. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2020.

Na. 227

## Mradi wa Maji wa Igongwi

**MHE. EDWARD F. MWALONGO** aliuliza:-

Mradi wa Maji wa Igongwi unaotarajiwa kuhudumia Vijiji vya Kitulila, Luponde, Njomlole Uwemba, Ikisa na Madobole umechukua muda mrefu kukamilika:-

Je, nini kauli ya Serikali kuhusu mradi huu muhimu kwa wananchi?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Igongwi ni miongoni mwa miradi ya maji iliyoanza kutekelezwa katika Programu ya Sekta ya Maji kabla ya kukabidhiwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira (*RUWASA*) Wilaya ya Njombe. Mradi huu unajumuisha Vijiji vya Kitulila, Luponde, Njomlole, Uwemba, Ikisa, Madobole, Luvuyo na Madope. Mradi wa Maji wa Igongwi ulipangwa kutekelezwa katika vipande vitano (*Lot one* hadi *Lot five*) na hadi sasa umefikia asilimia 63.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya mradi huu kuchukua muda mrefu ilisababishwa na upungufu wa usanifu katika kuchagua vyanzo vya maji ambavyo havitoshelezi mahitaji. Kwa sasa Wizara ipo kwenye hatua ya kupitia usanifu baada ya kupata vyanzo vingine vya maji vinavyokidhi mahitaji ya sasa. Baada ya kukamilisha usanifu, ujenzi wa mradi huu utaendelea kwa kutumia Wataalam wa ndani na unatarajia kukamilika katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Na. 228

**Hitaji la Meli ya Abiria Ziwa Nyasa**

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA** aliuliza:-

Je, ni lini meli ya abiria itaanza kufanya kazi katika Ziwa Nyasa?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA*) imekamilisha ujenzi wa meli moja mpya iitwayo *MV*-Mbeya II yenye uwezo wa kubeba abiria 300 na mizigo tani 200 kwa wakati mmoja katika Ziwa Nyasa tangu mwezi Septemba, 2019.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa meli hiyo ipo katika majaribio na ukaguzi kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Nchini *(TASAC)*. Ukaguzi huo utakapokamilika na kubainika kuwa unakidhi viwango vya kiufundi na usalama itapewa cheti cha ubora na kuruhusiwa kuanza kufanya kazi mwishoni mwa mwezi Mei 2020.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa, wananchi wanaoishi kandokando ya Ziwa hilo watatumia fursa hii adhimu kusafiri na kusafirisha mazao na bidhaa zao ndani na nje ya nchi kwa lengo la huduma za kijamii na kufanya biashara na hivyo kuimarisha hali zao kiuchumi na kuinua uchumi wa nchi.

Na. 229

**Barabara ya Monduli – Engaruka**

**MHE. JULIUS K. LAIZER** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2015 ya

ujenzi wa barabara ya lami kutoka Monduli kwenda Monduli Juu kwa Sokoine?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara anayoizungumzia Mheshimiwa Mbunge inaitwa Ngaresh - Enguik (kilomita 11) ambayo ni barabara ya mkoa inayosimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Nchini *(TANROADS)* katika Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Nchini, imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Kazi hiyo imefanywa na Mhandisi Mshauri *M/s Advance Engineering Solution* ya Tanzania kwa gharama ya Shilingi milioni 190 na imekamilika mwezi Juni, 2019.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa kazi ya upembuzi, usanifu na uandaaji wa nyaraka za zabuni kumeiwezesha Serikali kufahamu gharama za ujenzi wa barabara hiyo na hivyo kuanza hatua za awali za kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hiyo.

Na. 230

**Bwawa Lililopo Kijiji cha Nyamgogwa – Wilaya ya Nyang'hwale**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza:-

Katika Kijiji cha Nyamgogwa kilichopo Kata ya Shabaka kuna bwawa kubwa lililojengwa tangu enzi za ukoloni. Bwawa hili lilikuwa linategemewa na Kata tano za

Shabaka, Nyag'hwale, Kaboha, Busolwa na Kata jirani ya Bulela kwa kunyweshea mifugo, kilimo cha bustani cha matunda na mbogamboga lakini kwa sasa bwawa hilo limechakaa.

Je, Serikali ina mpango wa kulifufua bwawa hili ili liendelee kutoa huduma husika?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassoro Amar, Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wataalam wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji walitembelea bwawa hilo mwezi Januari, 2019 na kuona uchakavu wa sehemu ya utoro wa maji (*spillway*) ambapo kwa sasa bwawa hilo haliwezi kutunza maji kufikia kiwango cha juu kinachotakiwa. Aidha, chini ya bwawa hilo kuna shamba lenye takribani ukubwa wa zaidi ya hekta 100 linalomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya Nyang'hwale ambapo zinatumika kwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imefanya Mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji (*RNIMP* 2018) Serikali imepanga kujenga, kukarabati na kuboresha jumla ya mabwawa 111 katika awamu mbili (2), ambapo awamu ya kwanza mabwawa 51 yataendelezwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hadi 2025 likiwemo bwawa la Nyamgogwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na bwawa hili kujengwa kipindi cha ukoloni, Serikali katika bajeti ya mwaka 2020/2021 imeona haja na imepanga kufanya upembuzi yakinifu utakaohusisha pia usanifu mpya wa bwawa na miundombinu ya shambani, tathmini ya mazingira na jamii ili kupata gharama halisi na kuendeleza mradi utakaokuwa na tija na kuwanufaisha wananchi wengi zaidi. Aidha, Mpango wa

Serikali ni kujenga upya bwawa hilo baada ya tathmini ya upembuzi yakinifu kukamilika na kutegemea upatikanaji wa fedha.

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 – Wizara ya Maliasili na Utalii**

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa moja kwa moja nitumie nafasi hii kumkaribisha mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dkt. Hamisi Kigwangalla unaweza kuendelea tafadhali, una nusu saa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kufuatia Taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na mwenye kurehemu kwa kuendelea kutujalia afya njema na kutuwezesha kuwatumikia Watanzania. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu hotuba hii ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwa namna ya kipekee kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo ameongoza nchi yetu kwa busara na ujasiri wa hali ya juu na kwa namna ambavyo uongozi wake umeiwezesha Wizara ya Maliasili na Utalii kutekeleza

majukumu yake kwa ufanisi na kwa mafanikio makubwa. Natoa pia shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge), Waziri Mkuu kwa kuniongoza katika kutekeleza shughuli mbalimbali za Wizara kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi na miongozo mingine iliyopo. Kupitia uongozi wao wa Mheshimiwa Rais, Dkt.John POmbe Joseph Magufuli na viongozi wengine wakuu, Wizara imeendelea kutimiza wajibu wake kwa kuimarisha uhifadhi na kuendeleza utalii kwa ufanisi zaidi na hivyo kuchangia katika juhudi za kukuza uchumi na kuleta ustawi wa wananchi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe binafsi pamoja na uongozi wote wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi wa hali ya juu. Aidha, naishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya Uenyekiti wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Kemirembe Julius Lwota (Mbunge) ambayo pamoja na mambo mengine imejadili, kushauri, kutoa maoni na kupitisha Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Wizara itaendelea kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote walionitangulia kumpongeza Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mbunge) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mbunge) kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira; na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mbunge) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu (Mbunge) kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwako binafsi, Bunge lako Tukufu, wananchi na familia za marehemu kwa kuondokewa na Mheshimiwa

Rashid Ajali Akbar, Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini; Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve; na Mheshimiwa Dkt. Augustino Philip Mahiga, Mbunge na aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mheshimiwa Constantine John Kanyasu (Mbunge), Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii; Profesa Adolf Mkenda, Katibu Mkuu na Dkt. Aloyce Nzuki, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo; Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara; watumishi na wadau wote kwa ushirikiano wanaondelea kutupatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara na hatimaye kuweza kuwatumikia wananchi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa dhati na kwa namna ya kipekee kabisa wananchi wa Jimbo la Nzega Vijijini kwa kuendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya kibunge lakini pia na Serikali niliyopewa na Mheshimiwa Rais. Aidha, nimshukuru kwa dhati mke wangu mpenzi Dkt. Bayoum Kigwangalla na familia yangu; watoto wangu Sheila, Hawa na HK *junior* kwa upendo wao, uvumilivu na dua katika utekelezaji wa majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maliasili na utalii ni miongoni mwa sekta za uchumi nchini ambazo zinatoa mchango mkubwa katika ukusanyaji wa mapato na kuendeleza maisha ya Watanzania wengi ikiwemo fursa za kutoa ajira. Mathalani, sekta ndogo ya utalii, kupitia vivutio mbalimbali inachangia zaidi ya asilimia 17.6 ya pato la Taifa, asilimia 25 ya fedha zote za kigeni na kuajiri zaidi ya watu milioni 5.5 kwa mwaka. Kutokana na umuhimu huo, Wizara katika kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinaendelea kuhifadhiwa na kutumiwa kwa njia endelevu, inatoa rai kwa wadau wote kwa ujumla kuendelea kushirikiana nasi.

Mheshimiwa Spika, utalii duniani na hapa nchini umeathirika sana kutokana na mlipuko wa Homa Kali ya Mapafu ijulikanayo kama *COVID-19*. Katika kukabiliana na janga hili, mataifa ambayo ni masoko muhimu ya utalii nchini katika Mabara ya Ulaya, Amerika, Asia na kwingineko duniani yamechukua hatua mbalimbali za kudhibiti kusambaa kwa ugonjwa huu. Hatua hizo zinajumuisha kuzuia raia wake kusafiri. Kwa sababu hiyo, Mashirika ya Ndege takribani yote yamesitisha kufanya safari za kimataifa za abiria. Hali hii imeleta anguko kubwa katika sekta ya utalii hapa nchini na duniani kote. Hali hii itachukua muda kurejea katika hali ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, hata janga la *COVID-19* likiisha bado utalii utaendelea kuathirika hapa nchini kwa muda mrefu kutokana na mdororo wa uchumi duniani ambao unatarajiwa kutokea kutokana na mtikisiko unaoletwa na janga hili. Hata kama tukijipa matumaini makubwa kabisa ambayo kwa kweli ni matumaini tu kwamba janga hili litaisha mwezi Oktoba na kwamba hakutakuwa na athari za mdororo wa uchumi baada ya hapo bado madhara kwenye sekta ya utalii yatakuwa ni makubwa sana kama ifuatavyo: Idadi ya ajira za moja kwa moja katika sekta ya utalii zitashuka kutoka 623,000 zilizotarajiwa hadi kufikia 146,000 na idadi ya watalii itashuka kutoka 1,867,000 waliotarajiwa hadi kufikia watalii 437,000.

Mheshimiwa Spika, katika hali hiyo, mapato ya Serikali kutoka katika sekta ya utalii yatashuka kutoka shilingi trilioni 2.6 zilizotarajiwa hadi kufikia shilingi bilioni 598. Hapa naomba iingie kwenye *Hansard* hii niliyoitamka kuliko iliyokuwa imeandikwa awali. Kwa vyovyote vile, hali inaweza kuwa ngumu zaidi kuliko maoteo haya ya matumaini yanavyoonyesha.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii imefanya uchambuzi na tathmini ya athari za *COVID-19* kwenye sekta nzima ya utalii. Taarifa ya uchambuzi na tathmini hii pamoja na mapendekezo kadhaa ambayo ilihusisha wadau na wataalam kadhaa ilishawasilishwa

Hazina ili iunganishwe na uchambuzi mpana na tathmini ya kina zaidi ya athari za janga hili kwa uchumi wa nchi yetu. Mapendekezo ya taarifa hii ambayo yako chini ya mamlaka ya Wizara tayari tumekwishayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, madhara haya ya *COVID-19* yameathiri sana taasisi zetu ambazo kwa kawaida zinachangia sana kwenye uchumi wa nchi yetu. Kwa mfano, katika mwaka 2020/2021, *TANAPA* ililenga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 363.9 lakini kutokana na hali inavyoendelea, makisio sasa yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 64 tu. *NCAA* ilikadiria shilingi bilioni 162.7 sasa tunaweza tukakusanya shilingi bilioni 58. *TFS* ilikadiria shilingi bilioni 153.6 sasa ni shilingi bilioni 121 na *TAWA* ilikadiria shilingi bilioni 58.1 sasa ni shilingi bilioni 22.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi, mapato yanatarajiwa kushuka kwa takribani asilimia 75. Upungufu huo wa mapato ni mkubwa kwa sekta na unaweza kusababisha baadhi ya taasisi za uhifadhi zilizo chini ya Wizara kushindwa kujiendesha. Katika kukabiliana na hali hiyo, Wizara imeendelea kuwashirikisha wadau wa sekta ili kuweka mikakati ya namna ya kuisaidia sekta isiathirike zaidi ya tunavyo tathmini.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara iliidhinishiwa maduhuli ya shilingi bilioni 71.54 kutoka vyanzo vya Idara, Mifuko na Taasisi. Hadi Machi, 2020 shilingi bilioni 47.01 zimekusanywa sawa na asilimia 66 ya makadirio. Aidha, Mashirika ya *TANAPA*, *NCAA*, *TAWA* na *TFS* yaliidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 701.81. Hadi kufikia Machi, 2020 Mashirika hayo yalikuwa yamekusanya shilingi bilioni 503.87 sawa na asilimia 72 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ukusanyaji wa mapato unaendelea kukabiliwa na changamoto ya mlipuko wa ugonjwa wa *COVID-19* ambao utaathiri kwa kiasi kikubwa mapato ya *TANAPA, NCAA, TAWA* na *TFS*. Mathalani, kwa kipindi cha robo ya nne, taasisi hizo zilikadiria kukusanya shilingi bilioni 132.18 lakini kutokana na athari za mlipuko wa

ugonjwa huu, taasisi hizo zinatarajia kukusanya shilingi bilioni 33.46 sawa na anguko la asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara iliidhinishiwa kutumia shilingi bilioni 120.20 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kiasi hicho kinajumuisha shilingi bilioni 71.31 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 48.89 ni miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2020, Wizara ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya shilingi bilioni 61.45 sawa na asilimia 51 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 47.66 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 13.79 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yetu, Wizara kwa mwaka 2019/2020 tumepata mafanikio mbalimbali ikiwemo mafanikio katika eneo la udhibiti wa ujangili na uvamizi wa maeneo ya hifadhi; kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii; mapitio ya Kanuni na Miongozo mbalimbali; uendelezaji wa mashamba na upandaji miti lakini pia kukamilisha taratibu za kuanzishwa kwa mfumo wa Jeshi USU na uendelezaji wa maeneo ya Malikale. Pia tumepata mafanikio katika eneo la ulinzi wa wananchi dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu na kuimarika na kuongezeka kwa umaarufu wa Tanzania katika uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwenye tasnia ya uwindaji wa kitalii, Wizara imeendelea na utaratibu wa kugawa vitalu kwa njia ya mnada kwa mbinu za kielektroniki ambao umeongeza uwazi, uwajibikaji na kuruhusu nguvu ya soko kuamua bei ya vitalu. Awamu ya kwanza ya mnada ilifanyika Juni, 2019 ambapo jumla ya vitalu 7 kati ya 26 vilivyotangazwa viliuzwa na kuingiza jumla ya Dola za Marekani 831,000 sawa na asilimia 98 ya ada ya vitalu vyote 26 endapo utaratibu wa zamani ungeendelea kutumika.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa mkakati wenye matokeo ya haraka wa uendelezaji wa mazao ya utalii wa fukwe, utalii wa meli na utalii wa mikutano. Vilevile, Wizara

kwa kushirikiana na Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Katavi, Songwe na Morogoro mwezi Septemba, 2019 ilifanya jukwa la uwekezaji katika sekta ya utalii. Pia onyesho la utalii la Karibu Kusini lilifanyika sanjari na jukwa hilo kwa lengo la kufungua fursa za utalii na uwekezaji katika Ukanda wa Kusini. Aidha, mwezi Machi, 2020 Wizara kwa kushirikiana na Mikoa ya Kanda ya Ziwa, KIgoma na Tabora ilizindua maandalizi ya onyesho la Kimataifa la jukwa la uwekezaji lijulikanalo kama *Great Lakes International Tourism Expo* ama kwa kifupi *GLITE* ambalo kama isingekuwa kuzuka kwa Janga la Virusi vya *Corona* lingefanyika mwezi Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, pia tumefanya jitihada mbalimbali katika kutangaza utalii wa ndani kwa kutumia mbinu mbalimbali za mitandao lakini pia watu mashuhuri kupitia kampeni mbalimbali kama za kupanda Mlima Kilimanjaro; kutembelea hifadhi za Taifa mpya lakini pia hifadhi za mazingira asilia na kuanzishwa kwa *channel* ya utalii ijulikanayo kama *Tanzania Safari Channel* na Tamasha la Urithi ambalo limeendelea kufanyika kwa mwaka wa tatu mfululizo. Sambamba na hilo, kushiriki na kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye utalii wa ndani hususani utalii wa shughuli mbalimbali kama vile shunghuli za mbio za Marathon ikiwemo ile maarufu zaidi ya *Kili Marathon*.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maendeleo. Wizara imeendelea kutekeleza miradi 11 ya maendeleo ambayo inalenga kuendeleza utalii Kanda ya Kusini, kujenga uwezo wa maeneo ya hifadhi, mapori ya akiba na kikosi dhidi ya ujangili; usimamizi endelevu wa maliasili; kuendeleza misitu ya hifadhi ya mazingira asilia; na kujenga uwezo wa taasisi za mafunzo ya misitu na ufugaji nyuki. Pia kujenga uwezo wa jamii katika kusimamia misitu kwa tija na misingi endelevu na kuongeza thamani kwa mazao ya misitu. Maelezo ya kina juu ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa 2019/2020 yamefafanuliwa zaidi kuanzia aya ya 24 hadi ya 113 ya kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nigusie changamoto. Baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika

utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 ni pamoja na kuwepo na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa na maeneo ya shoroba; kuongezeka kwa migongano kati ya binadamu na wanyamapori; uhaba wa watumishi pamoja na wafanyakazi wenye ujuzi na utaalam katika fani mbalimbali hususani fani ya ukarimu. Pia kuharibika kwa miundombinu ya barabara kutokana na mvua nyingi zilizonyesha mwaka huu pamoja na hili janga la mlipuko wa gonjwa la *Corona* duniani.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Wizara imeendelea kufanya mapitio ya sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali; na kushirikisha wadau katika kuhifadhi maliasili na malikale na kuboresha miundombinu katika maeneo yaliyohifadhiwa na vivutio vya utalii. Aidha, Wizara imeimarisha ulinzi kwa wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu, kuhamasisha na kutekeleza mikakati ya upandaji miti, kuanzisha na kuendeleza viwanda vya mazao ya misitu na nyuki, kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili na malikale. Vilevile, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau katika kuendeleza na kuimarisha vyuo vya mafunzo ya utalii na kutumia njia ya kielekitroniki kuwahamasisha kuhusu vivutio mbalimbali vya utalii na kuhamasisha kuvitembelea baada ya kugonjwa wa corona kudhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 wizara itajikita katika kusimamia na kuendeleza sekta zake ili ziweze kuendelea kuchangia ipasavyo katika uchumi wa Taifa letu. Maeneo ya Mpango huo ni pamoja na ukusanyaji wa maduhuli hapa kwa 2020/2120 wizara inakadiria kukusanya shilingi bilioni 65.26 kutoka katika vyanzo ya idara, mifuko na taasisi zilizoko chini yake. Kati ya fedha hizo idara zitakusanya shilingi bilioni 22.66, taasisi zinazopata ruzuku zitakusanya shilingi bilioni 18.85 na mifuko ya uwifadhi ya *TWPF* na TAFF itakusanya shilingi 23.75. Aidha, Mashirika ya *TANAPA, NCAA, TAWA* na *TFS* yanakadiria kukusanya shilingi bilioni 738.23 kati

ya fedha hizo, *TANAPA* itakusanya shilingi bilioni 363.91, NCAA shilingi bilioni 162.66, TAWA shilingi bilioni 58.06 na *TFS* Shilingi bilioni 153.06.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2020/2021 wizara inakadiria kutumia shilingi bilioni 114.59 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 69.57 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 45.02 miradi ya maendeleo. Makadirio ya matumizi ya kawaida yanajumuisha mishahara shilingi 50.85 na matumizi mengineyo shilingi 18.72 Aidha, shilingi 45.02 zitatumika kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 44.32 zitatoka kwa washirika wa maendeleo na shilingi 700,000,000 zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, wizara kupitia sekta ndogo ya wanyamapori itaendelea kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya wanyamapori, kukamilisha mapitio ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009, Sheria ya TANAPA, NCAA na TAWIRI; na kuandaa Sheria ya kuanzisha TAWA. Aidha, wizara itaratibu upandishwaji hadhi mapori tengefu ya Inyonga, mbuga ya Wembere na misitu ya Litumbandyosi - Gesimazowa kuwa mapori ya akiba na kuanzisha Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori *(WMA)* Kilosa Moani. Aidha, vilevile wizara kupitia TANAPA itaimarisha ulinzi na usimamizi wa hifadhi za Taifa na kujenga na kukarabati miundombinu mbalimbali katika hifadhi ili kuwezesha shughuli za utalii kufanyika kwa tija.

Mheshimiwa Spika, wzara kupitia *NCAA* itaendelea kuboresha miundombinu kwa kukarabati barabara viwanja vya ndege ndani ya ndani ya eneo la hifadhi na kukamilisha mapitio ya matumizi mseto ya ardhi, sheria iliyoanzisha mamlaka na mpango wa jumla ya matumizi ya eneo. Aidha kupitia TAWA wizara itafanya siku doria 337.517 katika mapori ya Akiba, mapori tengefu na maeneo ya aridhi owevu na *WMAS* na kuimarisha ulinzi wa wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile TAWIRI itaidadi wanyamapori nchini katika mifumo ya ikolojia ya Serengeti Tarangire, Manyara, moyowosi kigosi Saadani, Burigi – Chato na Hifadhi ya Taifa Saadani.

Mheshimiwa Spika, Wizara itafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya Mwaka 1998, kuendelea na mapitio ya Sheria ya Misitu Sura 323 na Sheria iliyoanzisha TAFORI Sura 270. Aidha, Wizara kupitia TFS itaanzisha shamba jipya la miti lenye ukubwa wa hekta 3,000 katika Wilaya ya Nzega na kuongeza hifadhi nne (4) za misitu ya asili zenye hekta 37,000 katika wilaya za Babati na Simanjiro. Wizara itapandisha hadhi misitu 10 ya hifadhi yenye ukubwa wa hekta 25,862 kuwa misitu ya hifadhi ya mazingira asilia pia kukarabati njia za kutembea watalii zenye urefu wa kilomita 355 na kuanzisha kampuni tanzu itakayosimamia miradi ya kuongeza thamani na kuzalisha bidhaa mseto za mazao ya misitu na nyuki.

Mheshimiwa Spika, wizara itafanya mapitio ya sheria ya utalii ya mwaka 2008 na kuandaa programme ya taifa ya uendelezaji utalii na kuendelea kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora wa nyota. Pamoja na hatua hizi wizara kupitia *TTB* itaendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kwa kushiriki maonyesho ya utalii katika masoko ya kimkakati. Aidha *TTB* itaendelea kutangaza mazao mapya ya utalii ikiwa ni pamoja na utalii wa fukwe, utalii wa mikutano, utalii wa utamaduni, utalii wa meli na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, juhudi mbalimbali za kutangaza utalii zitafanyika kupitia maonesho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa yakiwemo *site*, ambayo ni swahili *Intenational tourism expo,* Karibu Kili fair, Karibu Utalii Kusini, Glite na *East Africa Trade Fair*. Katika kuimarisha utowaji wa mafunzo ya utalii nchini wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii utaanzisha kampasi mpya ya Mwanza na programu ya mafunzo ya utalii katika ngazi ya cheti kampasi ya Arusha.

Mheshimiwa Spika, wizara pamoja na kazi nyingine itafanya tathimini ya hali ya uhifadhi ya maeneo matano ya mali kale, upimaji mipaka ya vituo vitano ya mambo ya kale na kuratibu mahadhimisho ya Tamasha la mwezi wa urithi wa utamaduni wa mtanzania ama urithi *festival* pia kumbikizi ya vita vya maji maji na siku ya Kimondo Duniani. Aidha

wizara kupitia Shirika la Makumbusho ya Taifa litajenga onesho la Historia ya Tanzania kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni, wakati wa harakati za kudai uhuru na Tanzania ikiwa huru. Vile vile shirika litakusanya taarifa za kihistoria za Marais ili kuanzisha makumbusho ya Marais itakayojengwa jijini dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 wizara itatekeza miradi sita ya maendeleo ambayo ni mradi wa kuendeleza utalii ukanda wa kusini yani *REGROW*, Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi Ujangili; Mradi wa Kuzuia na Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara; Mradi wa Panda Miti Kibiashara; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki; na Mradiwa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu *FORVAC*.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina maeneo mengine kuhusu mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ni kama ilivyoonyeshwa kuanzia aya 116 hadi 156 ya kitambu changu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, nimalizie mafanikio katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yametokana na ushirikiano wake na nchi mbalimbali, mashirika, taasisi na marafiki wa uhifadhi. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau na washirika wa maendeleo kwa kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Canada, China, Korea Kusini, Marekani, Norway, Ubelgiji, Ufini, Ujerumani, Uswisi na Jumuiya ya Nchi za Ulaya. Pia Mashirika na taasisi ni pamoja na *AfDB*, *AWF, AWHF, EU, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, ICOMOS, ILO, IUCN, KfW, NORAD, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNWTO, USAID, WCS, WHC, World Bank, Wild Aid, WMF na WWF. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/ 2021, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe shilingi 114,593,952,000 kwa matumizi ya Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii. Kati ya fedha hizo, shilingi 69,573,850,000 ni kwa ajili

ya matumizi ya kawaida na shilingi 45,020,102,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi 50,852,545,000 za mishahara ya *personnel emolument* na shilingi 18,721,305,000 za matumizi mengineyo. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha Shilingi 700,000,000 fedha za ndani na Sh.44,320,102,000 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe mwenyewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii itapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii: *www.maliasili.go.tz.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII, MHESHIMIWA DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA (MB) WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWAMWAKA WA FEDHA 2020/2021 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

***1. Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

***2. Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuendelea kutujalia afya njema na kutuwezesha kuwatumikia Watanzania. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Hotuba ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa

fedha 2020/2021 ikiwa ni hotuba yangu ya tatu (3) tangu Mheshimiwa Rais aliponiteua kuongoza Wizara hii. Nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu; kwa kuniongoza katika kutekeleza shughuli mbalimbali za Wizara na Taifa kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na miongozo mingine. Kupitia uongozi wao, Wizara imeendelea kutimiza wajibu wake kwa kuimarisha uhifadhi na kuendeleza utalii kwa ufanisi zaidi na hivyo kuchangia katika juhudi za kukuza uchumi na ustawi wa wananchi.

***3. Mheshimiwa Spika,*** ninakupongeza wewe binafsi pamoja na uongozi wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi. Aidha, ninaishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Kemilembe Julius Lwota (Mb) kwa kujadili, kushauri na kupitisha Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa uwazi kabisa niseme kwamba Kamati hii imekuwa na mchango mkubwa kwangu kutokana na maoni na ushauri wake inayotoa katika kufanikisha malengo ya Wizara. Wizara itaendelea kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati.

***4. Mheshimiwa Spika,*** ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia kumpongeza Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira; na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu (Mb) kwa

kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa ninaungana na Waheshimiwa Wabunge kutoa salamu za pole kwako binafsi, Bunge lako Tukufu, wananchi na familia za marehemu kwa kuondokewa na Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar, Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini; Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve; na Mheshimiwa Dkt. Augustino Philip Mahiga, Mbunge na aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Vifo vya Wabunge hao vimeleta majonzi makubwa kwa Waheshimiwa Wabunge na Taifa kwa ujumla kutokana na kukosa michango yao ambayo imekuwa chachu ya utendaji wa Bunge letu Tukufu. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi, Amina.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Mheshimiwa Constantine J. Kanyasu (Mb), Naibu Waziri; Profesa Adolf F. Mkenda, Katibu Mkuu; na Dkt. Aloyce K. Nzuki, Naibu Katibu Mkuu; kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, ninawashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara, watumishi na wadau wote kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara na hatimaye kuweza kuwatumikia wananchi kwa ufanisi zaidi.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Nzega Vijijini kwa kuendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu. Ninapenda kuwahimiza kuendelea kushiriki katika shughuli za uhifadhi wa maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Aidha, ninamshukuru kwa dhati mke wangu mpenzi Dkt. Bayoum Kigwangalla na familia yangu kwa upendo wao, uvumilivu na dua katika utekelezaji wa majukumu yangu.

***8. Mheshimiwa Spika,*** kwa upekee ninatoa pole kwa ndugu, marafiki na watumishi wote wa Wizara kutokana na watumishi waliopoteza maisha wakati wakitekeleza majukumu yao. Watumishi watano (5) walipoteza maisha ambapo mmoja

(1) aliuawa na majangili, mmoja (1) kuumwa na nyoka, wawili

(2) kwa ajali ya gari na mmoja (1) akiwa katika mazoezi ya utayari. Kwa hakika, hawa ni mashujaa ambao wamekufa wakitetea rasilimali za nchi yetu, Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahala pema peponi - Amina. Aidha, ninatoa pole kwa watumishi waliojeruhiwa wakati wanatekeleza majukumu yao. Vilevile, ninatoa pole za dhati kwa wananchi ambao kutokana na uvamizi wa wanyamapori wakali na waharibifu, wamepoteza ndugu, kujeruhiwa na kuharibiwa mali zao.

***9. Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii imegawanyika katika sehemu kuu sita (6): **Kwanza,** Utangulizi; **Pili,** Dira, Dhima na Majukumu ya Wizara; **Tatu,** Mchango wa Maliasili, Malikale na Utalii katika Uendelezaji wa Uchumi wa Viwanda; **Nne,** Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii; **Tano,** Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020; na **Sita**, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

## 2.0 DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA

***10. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa dhamana ya kusimamia uhifadhi wa maliasili, malikale na maendeleo ya utalii. Dhamana hiyo inaongozwa na Dira ya Wizara ambayo ni *"Maliasili na malikale zilizohifadhiwa kwa manufaa ya Watanzania wakati ikiongoza kuchangia ukuaji wa uchumi"*. Kutokana na Dira hiyo, Dhima ya Wizara ni *"Uhifadhi endelevu wa maliasili na malikale na kuendeleza utalii kwa manufaa ya Taifa"*.

***11. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatekeleza majukumu yake ya uhifadhi wa maliasili na malikale na kuendeleza utalii kupitia Idara za Wanyamapori; Misitu na Nyuki; Utalii; Malikale; Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu; na Sera na Mipango. Aidha, inatekeleza majukumu yake kupitia Vitengo vya Fedha na Uhasibu; Habari na Mawasiliano ya Serikali; Ununuzi na Ugavi; Ukaguzi wa Ndani; Sheria; Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; na Utafiti na Mafunzo.

***12. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia: Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Shirika la Makumbusho ya Taifa (NMT), Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT), Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka (CAWM), Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi (PWTI), Chuo cha Misitu Olmotonyi (FTI), Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI), Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BTI), Kituo cha Elimu ya Uhifadhi Wanyamapori kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga (CBCTC), Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB). Aidha, Wizara ina Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori (TWPF), Mfuko wa Misitu (TaFF), Mfuko wa Mambo ya Kale (NFA), na Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL).

## 3.0 MCHANGO WA MALIASILI NA UTALII KATIKA UENDELEZAJI WA UCHUMI WA VIWANDA

***13. Mheshimiwa Spika,*** Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025 imedhamiria kuifikisha nchi katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Dira hiyo imebainisha mikakati mbalimbali ikiwemo uendelezaji na matumizi ya maliasili na utalii ili nchi iwe na uchumi wenye uwezo wa kushindana na kuhimili mitikisiko ya kiuchumi. Maliasili na utalii ni miongoni mwa sekta za uchumi nchini

ambazo zinatoa mchango mkubwa katika ukusanyaji wa mapato na kuendeleza maisha ya Watanzania wengi ikiwepo fursa za kutoa ajira. Shughuli za ufugaji wa wanyamapori katika mashamba na ranchi zinatoa fursa za kuanzisha viwanda vya kuchakata ngozi, kutengeneza mapambo na kusindika nyamapori. Aidha, takribani asilimia 90 ya watalii wanaotembelea nchini wanakuja kujionea wanyamapori waliohifadhiwa katika mazingira yao asilia. Watalii wanaokuja nchini ni soko kubwa la bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini.

***14.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ina rasilimali kubwa ya misitu ambayo hutoa malighafi ya viwanda vya kutengeneza samani, karatasi, nishati, vifaa vya ujenzi na mapambo. Aidha, hifadhi za Taifa, misitu ya lindimaji, mapori ya akiba, tengefu na ardhioevu hutoa huduma za kiikolojia kama vile uhifadhi wa vyanzo vya maji ambayo hutumika kwa matumizi ya viwanda na kuzalisha nishati ya umeme. Vilevile, mazao ya nyuki yanatumika kwa chakula na malighafi za viwanda vya kutengeneza vipodozi, madawa na vyakula. Pia, nyuki ni rafiki wa mazingira na mchavushaji mkuu wa mimea, hivyo husaidia kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo.

***15.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta Ndogo ya Utalii kupitia vivutio mbalimbali vinavyotokana na wanyamapori, misitu, urithi wa malikale inaendelea kuchangia katika uchumi na fedha za kigeni. Mchango wa utalii katika Pato la Taifa kwa sasa ni zaidi ya asilimia 17 na asilimia 25 ya fedha zote za kigeni. Aidha, shughuli za kiuchumi katika sekta ya maliasili na utalii zinaajiri zaidi ya watu milioni 5.5 kwa mwaka. Kutokana na umuhimu wa maliasili, malikale na utalii katika uchumi wa viwanda, Wizara inatoa rai kwa wadau wote kwa ujumla kushirikiana na Wizara katika kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinaendelea kuhifadhiwa na kutumiwa kwa njia endelevu.

**Athari za Ugonjwa wa Corona (COVID-19) katika Sekta ya Utalii**

***16.*** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mchango huo, Sekta Ndogo ya Utalii imeathirika kutokana na mlipuko wa homa kali ya mapafu ijulikanayo kama *COVID-19* iliyotangazwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) Machi, 2020 kuwa ni janga la kimataifa. Katika kukabiliana na janga hilo, mataifa ambayo ni masoko muhimu ya utalii nchini katika mabara ya Ulaya, Amerika na Asia yamechukua hatua mbalimbali za kudhibiti kusambaa kwa ugonjwa huo. Hatua hizo zinajumuisha kuzuia raia wake kusafiri na baadhi ya mashirika ya ndege kutofanya safari nje ya nchi, hali iliyosababisha kuathirika kwa sekta hiyo. Ugonjwa huo umeleta madhara makubwa katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

***17.*** ***Mheshimiwa Spika,*** moja ya sekta muhimu zilizoathiriwa ni utalii. Sekta hiyo kabla ya madhara hayo ilikuwa inachangia asilimia 25 katika mapato yote ya kigeni inayopata nchi yetu. Sekta hii imeathiriwa zaidi kutokana na ukweli kwamba inategemea zaidi mapato ya watalii wanaotoka nje ya nchi ambao kwa sasa kutokana na ugonjwa huu, wameshindwa kusafiri na wengi wao wamesitisha safari za kuja nchini kutalii.

***18.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuona madhara ya awali ya ugonjwa huu, Wizara ilifanya tathmini ya awali (rapid assessment) iliyojikita katika kipindi cha tangu ugonjwa huo uanze hadi tarehe 06 Aprili, 2020. Tathmini hiyo ilibaini kuwa madhara makubwa ya Corona katika sekta ya utalii yalianza kuonekana mwanzoni mwa Machi, 2020 tofauti na miezi ya Februari na Januari, 2020 ambapo hali ilikuwa shwari. Aidha, tathmini imebaini kuwa mashirika 13 ya ndege yalisitisha kuja nchini tangu tarehe 25 Machi, 2020 na hivyo kuondoa uwezekano wa kuendelea kupata watalii kutoka nje ya nchi. Mashirika yaliyositisha safari zake ni pamoja ni: Emirates, Swiss, Oman air, Turkish, Egyptian air, South African Airways, Rwandair, Qatar, Kenya Airways, Uganda Airlines, Fly

Dubai na KLM. Vilevile, kampuni yetu ya ndege ya Air Tanzania imesitisha safari za nje ya nchi.

***19. Mheshimiwa Spika,*** madhara haya yanaonekana kuwa makubwa zaidi ambapo tayari kuna dalili za kushuka kwa mapato yaliyotarajiwa kukusanywa na Taasisi kubwa zilizo chini ya Wizara ambazo ni TANAPA, NCAA, TFS na TAWA. Kwa mfano, katika mwaka 2020/2021 TANAPA ililenga kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 363.9, lakini kutokana na hali inavyoendelea makisio sasa yanakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 64 au chini ya hapo; NCAA ilikadiria Shilingi bilioni 162.7, sasa ni Shilingi bilioni 58; TFS ilikadiria Shilingi bilioni 153.6, sasa ni Shilingi bilioni 121; na TAWA ilikadiria Shilingi bilioni 58.1, sasa ni Shilingi bilioni 22.

***20. Mheshimiwa Spika,*** kama hali itatulia mwezi Oktoba, 2020, idadi ya ajira za moja kwa moja katika Sekta ya Utalii zitashuka kutoka 623,000 zilizotarajiwa hadi kufikia 146,000; watalii watashuka kutoka 1,867,000 waliotarajiwa hadi kufikia watalii 437,000; na mapato yanayotokana na utalii yatashuka kutoka Shilingi trilioni 2.6 zilizotarajiwa hadi kufikia Shilingi milioni 598. Upungufu huo wa mapato ni mkubwa kwa sekta na unaweza kusababisha baadhi ya Taasisi za uhifadhi zilizo chini ya Wizara kushindwa kujiendesha ikiwa ni pamoja na kulipa mishahara. Katika kukabiliana na hali hiyo, Wizara imeendelea kuwashirikisha wadau wa sekta ili kuweka mikakati ya namna ya kuisaidia sekta isiathirike zaidi.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII

***21. Mheshimiwa Spika,*** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii imepitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, Kamati imechambua na kutoa maoni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo yafuatayo: usimamizi wa ukusanyaji

maduhuli, utekelezaji wa miradi ya maendeleo, migogoro ya mipaka kati ya maeneo yaliyohifadhiwa na wananchi, uhaba wa watumishi, ugawaji wa vitalu kwa njia ya mnada wa kielekitroniki, uharibifu wa vyanzo vya maji, mgongano wa kisheria, matumizi mseto katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na wanyamapori walio katika hatari ya kutoweka (hususan faru na mbwa mwitu).

***22. Mheshimiwa Spika,*** maeneo mengine ni vifo vya wanyamapori kutokana na kugongwa na magari, gharama za kuendesha hifadhi mpya, usimamizi wa shoroba za wanyamapori na uanzishwaji wa Jumuiya za Uhifadhi wa Wanyamapori kwa Jamii (WMAs), ulinzi wa wananchi dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu, mifumo ya kielekitroniki ya kutambua wageni wanaotembelea vivutio vya utalii, kuendeleza na kutangaza vivutio vya utalii, uhaba wa huduma za malazi ya bei nafuu, uhifadhi wa misitu ya asili na uanzishaji wa mashamba ya miti.

***23. Mheshimiwa Spika,*** ushauri wa Kamati umezingatiwa katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na utaendelea kuzingatiwa katika mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

## 5.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

***24. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2019/2020 kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 - 2020/2021) na Mpango Mkakati wa Wizara (2016/17 - 2020/21). Masuala mengine yaliyozingatiwa ni Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2015- 2020; sera na sheria za sekta ndogo za usimamizi wa maliasili,

malikale na maendeleo ya utalii; na Maagizo ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

### 5.1. Ukusanyaji Maduhuli

***25.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020, iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 71,538,430,944** kutoka vyanzo vya idara (**Shilingi 22,657,242,000**), mifuko (**Shilingi 21,878,865,008**) na taasisi (**Shilingi 26,987,619,944**). Hadi Machi 2020, **Shilingi 47,010,442,123** zimekusanywa sawa na asilimia 66 ya makadirio ya idara, mifuko na taasisi. Aidha, mashirika ya TANAPA, NCAA, TAWA na TFS yaliidhinishiwa kukusanya **Shilingi 701,805,841,651**. Hadi Machi 2020, mashirika hayo yalikuwa yamekusanya **Shilingi 503,865,454,314** sawa na asilimia 72 ya makadirio. Mashirika hayo yametumia fedha hizo kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya kuhifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii pamoja na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, ukusanyaji wa mapato unaendelea kukabiliwa na changamoto ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 ambao utaathiri kwa kiasi kikubwa mapato ya TANAPA, NCAA, TAWA na TFS. Mathalan kwa kipindi cha robo ya nne, Taasisi hizo zilikadiria kukusanya **Shilingi 132,175,324,282** lakini kutokana na athari za mlipuko huo, Taasisi hizo zinatarajia kukusanya **Shilingi 33,460,938,400** sawa na anguko la asilimia 75.

### 5.2. Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

***26.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara iliidhinishiwa kutumia **Shilingi 120,202,637,734** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kiasi hicho kinajumuisha **Shilingi 71,312,649,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 48,889,988,734** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi Machi 2020, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 61,445,191,014** sawa na asilimia 51 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 47,655,044,638**

ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 13,790,146,376** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### 5.3. Mafanikio

***27.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo:-

#### 5.3.1. Udhibiti wa Ujangili na Uvamizi wa Maeneo ya Hifadhi

***28.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuongeza juhudi katika kukabiliana na ujangili, biashara haramu ya nyara, mazao ya misitu na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa. Taarifa za ufuatiliaji wa matukio hayo zinaonesha kuwa ujangili umepungua kwa takriban asilimia 80. Kutokana na taarifa ya sensa ya mwaka 2019, idadi ya ndovu imeongezeka kutoka 59 mwaka 2014 hadi 1,200 mwaka 2019 katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi. Aidha, idadi ya ndovu haijabadilika katika mfumo ikolojia wa Tarangire - Manyara. Vilevile, idadi ya mizoga ya ndovu katika mapori ya akiba, tengefu, ardhioevu na WMAs imepungua kutoka 14 mwaka 2018 hadi mizoga mitatu (3) mwaka 2019. Pia, uvunaji haramu wa miti iliyo hatarini kutoweka na uvamizi katika misitu ya hifadhi umepungua kwa takribani asilimia 85. Mafanikio hayo yametokana na kuimarika kwa ulinzi ambapo jumla ya siku - doria 402,208 zimefanyika na kuwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 9,085 waliochukuliwa hatua mbalimbali za kisheria.

#### 5.3.2. Kuongezeka kwa Mapato yatokanayo na Utalii

***29.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mapato yatokanayo na utalii wa kimataifa yameongezeka kutoka Dola za Marekani Bilioni 2.4 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani Bilioni 2.6 mwaka 2019. Aidha, wastani wa siku za kukaa watalii nchini zimeongezeka kutoka siku 10 mwaka 2018 hadi siku 13 mwaka 2019. Vilevile, matumizi ya watalii kwa

siku yameongezeka kutoka Dola za Marekani 193 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani 266 mwaka 2019. Mafanikio hayo, pamoja na mambo mengine yametokana na jitihada za kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi.

### 5.3.3. Kupandishwa Hadhi Maeneo ya Hifadhi

***30.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeongeza idadi ya Hifadhi za Taifa kutoka 16 hadi 22 na misitu ya hifadhi ya mazingira asilia kutoka 17 hadi 19. Ongezeko la Hifadhi za Taifa limetokana na kupandisha hadhi mapori ya akiba ya Burigi, Biharamulo, Kimisi; Ibanda; na Rumanyika - Orugundu kuwa Hifadhi za Taifa za Burigi - Chato, Ibanda - Kyerwa na Rumanyika - Karagwe; sehemu ya Pori la Akiba Selous kuwa Hifadhi ya Taifa Nyerere; sehemu ya Pori la Akiba Ugalla kuwa Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla na Pori la Akiba Kigosi kuwa Hifadhi ya Taifa Kigosi. Aidha, ongezeko la misitu ya hifadhi ya mazingira asilia limetokana na kupandisha hadhi misitu ya hifadhi ya Uzigua na kuunganishwa kwa misitu mitatu (3) ya Pugu, Kazimzumbwi na Vikindu kuwa Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Pugu - Kazimzumbwi. Vilevile, Wizara imepandisha hadhi maeneo ya misitu ya Aghondi (ha. 2,161) na Kilinga (ha. 10,916.44) iliyopo mkoani Singida na Mlima Simu (ha. 1,657) uliopo Mkoa wa Manyara kuwa misitu ya hifadhi. Jitihada hizo zinalenga kuimarisha uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori na misitu.

### 5.3.4. Mapitio ya Kanuni na Miongozo Mbalimbali

***31.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa Kanuni za Uuzaji wa Nyamapori, Tangazo la Serikali Na. 84 la mwaka 2020; Kanuni za Uwekezaji wa Miundombinu ya Utalii katika Misitu ya Hifadhi, Tangazo la Serikali Na. 85 la mwaka 2020; na Kanuni za Uwekezaji katika Maeneo Maalumu ya Wanyamapori, Tangazo la Serikali Na. 28 la mwaka 2020. Aidha, Wizara imepitia Kanuni za Huduma za Malazi za mwaka 2015, Tangazo la Serikali

Na. 25 la mwaka 2020; na Kanuni za Ufugaji wa Wanyamapori ya mwaka 2013, Tangazo la Serikali Na. 83 la mwaka 2020.

***32.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kanuni hizi zitasaidia katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa sekta ya maliasili na utalii ikiwemo kuwapatia wananchi fursa ya kufanya biashara ya nyamapori, kupunguza ujangili, kuongeza mapato ya Serikali, kupata takwimu na taarifa za wageni kwa ajili ya mipango na usimamizi endelevu wa sekta ndogo ya utalii, kupata kitoweo na kuvutia uwekezaji kwenye maeneo yaliyohifadhiwa.

### 5.3.5. Kuendeleza Mashamba na Upandaji Miti

***33.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TFS imepanda jumla ya hekta 8,726 za miti kwenye mashamba 23 ya Serikali Kuu. Aidha, jumla ya miche ya miti milioni 7.6 imegawiwa na kupandwa na wananchi ikijumuisha miche 800,000 iliyopandwa katika Jiji la Dodoma kupitia Kampeni ya Dodoma ya Kijani. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za viwanda vya mazao ya misitu, kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, kuendeleza uoto wa asili, na kuhifadhi mazingira na bioanuwai.

### 5.3.6. Kukamilisha Taratibu za Mfumo wa Jeshi Usu

***34.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetoa mafunzo ya utayari kwa watumishi 4,556 kutoka taasisi za TANAPA, NCAA, TAWA na TFS ikiwa ni maandalizi ya utekelezaji wa mfumo wa Jeshi Usu. Aidha, Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali unaojumuisha Sheria za Wanyamapori Sura 283, Sheria ya Misitu Sura 323, Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282 na Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro Sura 284 kuhusu kuanzishwa rasmi kwa Jeshi hilo umeandaliwa na kusomwa kwa mara ya kwanza katika Bunge la 11, mkutano wa 18 tarehe 28 Januari, 2020. Vilevile, Wizara

inaendelea kukamilisha maandalizi ya muundo jumuishi wa maendeleo ya utumishi katika Jeshi Usu kwa taasisi zote zinazohusika ili kuleta ufanisi zaidi katika utendaji kazi.

### 5.3.7. Uendelezaji wa Maeneo ya Malikale

***35.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha ukarabati wa Nyumba ya Makumbusho ya Dkt. David Livingstone, Kigoma - Ujiji na miundombinu ya barabara yenye urefu wa kilometa tano (5) katika Kituo cha Michoro ya Miambani Kolo, Kondoa. Aidha, ukarabati wa Makumbusho ya Nyumba ya Utamaduni na majengo ya Kijiji cha Makumbusho katika Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na Makumbusho ya Azimio la Arusha umekamilika.

### 5.3.8. Kuboresha Mfumo wa Ukusanyaji Maduhuli

***36.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeimarisha matumizi ya mfumo jumuishi (MNRT Portal) wa kutoa leseni, vibali, kukusanya takwimu na mapato ya vyanzo mbalimbali vya Wizara na Taasisi zake. Mfumo umefungamanishwa na mifumo mingine ya TEHAMA ya Serikali kwa ajili ya kubadilishana taarifa na kurahisisha huduma kwa wateja.

Katika kutekeleza hilo, Wizara imefanya upanuzi wa miundombinu ya TEHAMA katika vituo vya Endamaghay, Nasera Rock, Kakesio, Masamburai, Seneto, Lemala na Endoro katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Aidha, watumishi wa Wizara na Taasisi zake pamoja na wadau 2,000 wamepatiwa mafunzo ya namna ya kutumia mfumo huo. Vilevile, Wizara imeendesha minada miwili (2) ya vitalu vya uwindaji kwa njia ya kielekitroniki, kusajili na kutoa leseni ya kuendesha biashara ya utalii kwa kampuni 1,991.

### 5.4. Masuala Mtambuka

#### 5.4.1. Utatuzi wa Migogoro katika Maeneo ya Hifadhi

***37. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufanya jitihada mbalimbali zikiwemo kushirikiana na wizara nyingine, viongozi na wananchi kutatua migogoro iliyopo baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa. Katika kushughulikia migogoro ya mwingiliano wa matumizi ya ardhi, Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ametoa kibali kwa vijiji 920 kati ya 975 vilivyokuwemo ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa kurasimishwa kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii. Aidha, Serikali imeridhia kufuta Mapori Tengefu 12 yenye ukubwa wa ekari 707,660 na misitu ya hifadhi saba (7) yenye ukubwa wa hekta 46,715 yaliyopungukiwa sifa, hivyo kutolewa kwa wananchi kwa ajili ya shughuli za maendeleo kama vile kilimo na mifugo.

***38. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na TAMISEMI inaendelea na maandalizi ya mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 343 vinavyopakana na maeneo yaliyohifadhiwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni imetatua mgogoro wa matumizi ya ardhi katika Kituo cha Magofu ya Kunduchi, Dar es Salaam ambapo shughuli za mazishi katika eneo hilo zimesitishwa na ulinzi umeimarishwa.

#### 5.4.2. Ushirikishaji Wadau na Elimu kwa Umma

***39. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana na wananchi, sekta binafsi na wadau wengine katika kuhifadhi na kusimamia maliasili, malikale na uendelezaji utalii. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara kupitia TFS imetoa mafunzo ya usimamizi shirikishi wa misitu kwa kamati za maliasili za vijiji 154, kufundisha vikundi 19 vya ufugaji nyuki, kugawa mizinga 2,040, kuwezesha ujenzi wa hosteli mbili (2), na kuchangia vifaa vya ujenzi kama vile mbao na saruji vyenye

thamani ya shilingi 68,705,200 katika miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, TaFF imekuza na kusambaza jumla ya miche 3,968,028 ya miti aina mbalimbali. Vilevile, Wizara kupitia TAWA imetoa gawio la jumla ya Shilingi 6,495,488,526 kwa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori 12, vijiji 42 na halmashauri za wilaya 39 kwa ajili ya uhifadhi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

***40. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TANAPA imetoa elimu ya uhifadhi kwa viongozi 340 wa vikundi vya ulinzi shirikishi kutoka kwenye wilaya, kata, vijiji na kamati za maliasili za vijiji vinavyozunguka hifadhi, pamoja na kufadhili miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara kupitia taasisi zake (TANAPA, TAWA na NCAA) imetoa mizinga ya nyuki 1,155 kwa vikundi vya ufugaji nyuki katika vijiji vinavyozunguka hifadhi za Taifa za Kitulo na Mahale. Vilevile, TANAPA kwa kushirikiana na wadau wa Mto Ruaha Mkuu, Mto Katuma na Mto Tarangire imetoa elimu ya utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji katika vijiji 169 vinavyozunguka hifadhi za Taifa za Ruaha, Kitulo na Udzungwa katika wilaya za Kilolo, Mufindi, Makete, Wanging'ombe, Mbarali, Babati na Kondoa. Pia, TANAPA imepanda miti ya asili 150,000 katika eneo la hekta 40 la msitu katika ukanda wa chini wa Mlima Kilimanjaro ili kulinda vyanzo vya maji. Aidha, Wizara kupitia NCAA imetoa elimu ya upandaji miti kwa kata 16 ndani na nje ya Hifadhi ya Eeneo la Ngorongoro. Vilevile, jumla ya miche ya miti 355,650 ilisambazwa katika maeneo ya taasisi, serikali za vijiji na watu binafsi ndani na nje ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ili kuhifadhi mazingira.

***41. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa elimu na uhamasishaji kwa umma kuhusu uhifadhi na uendelezaji utalii kupitia Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), Nanenane, Kili/ Karibu Fair, Siku ya Utalii Duniani, Karibu Utalii Kusini na Swahili *International Tourism Expo* (S!TE). Aidha, elimu imeendelea kutolewa katika matamasha ya: Mwezi wa Urithi wa Utamaduni, Siku ya Vimondo Duniani, Mvinyo

Dodoma, Utalii na Kumbukizi ya Vita vya Majimaji na Jumuiya ya Afrika Mashariki Utamaduni *Festival* (JAMAFEST). Vilevile, Wizara imetoa elimu kupitia Siku ya Utumishi wa Umma, Siku ya Wanyamapori Duniani, Tamasha la maadhimisho ya miaka 60 ya Hifadhi ya Taifa Serengeti na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na miaka 60 tangu kuvumbuliwa kwa fuvu la Zamadamu (*Zinjanthropus boisei*) katika eneo la Olduvai Gorge.

### 5.4.3. Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

***42.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeshiriki katika Mkutano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Baraza la Mawaziri wa Sekta za Mazingira na Maliasili uliofanyika Februari, 2020. Mkutano huo ulipitisha Itifaki ya Mazingira na Maliasili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; na Sera ya Misitu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mkakati wa utekelezaji wake. Miongozo hiyo inatoa fursa kwa nchi wanachama kushirikiana katika usimamizi, matumizi endelevu ya rasilimali za misitu, kuhifadhi mazingira na kudhibiti biashara haramu za rasilimali za misitu na wanyamapori. Aidha, Wizara ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa pamoja wa Mawaziri wanaosimamia Sekta za Mazingira, Maliasili na Utalii wa SADC uliofanyika Oktoba, 2019 jijini Arusha. Kupitia mkutano huo, nchi wanachama zilipata fursa ya kupata taarifa za maendeleo ya uhifadhi wa maliasili na kubadilishana uzoefu katika kukabiliana na ujangili na biashara haramu ya nyara, mabadiliko ya tabianchi na maendeleo ya utalii.

***43.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeshiriki katika Mkutano wa 18 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa CITES uliofanyika Agosti, 2019; Mkutano wa 43 wa Kamati ya Urithi wa Dunia Julai, 2019; Mkutano wa 22 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa UNESCO Novemba, 2019; Mkutano Mkuu wa Shirika la Utalii Duniani Septemba, 2019; Mkutano wa 13 wa Uhifadhi wa Wanyamapori Wahamao (CMS) na Mkutano wa tisa (9) wa Kisera wa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria Februari, 2020. Katika

mikutano hiyo, nchi wanachama zilipata fursa za kubadilishana uzoefu na kuweka mikakati ya pamoja ya kuhifadhi na kuendeleza sekta ya maliasili na utalii.

### 5.4.4. Utawala na Uendelezaji Rasilimaliwatu

***44.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara na Taasisi zilizo chini yake imeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa kujenga nyumba na ofisi 76, kununua mitambo mitatu (3), magari 75, pikipiki 33 pamoja na ununuzi wa samani na vitendea kazi vya ofisi. Aidha, jumla ya watumishi 144 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na 523 ya muda mfupi ndani na nje ya nchi ili kuwajengea uwezo wa kufanya kazi. Vilevile, Wizara na taasisi zake imeajiri watumishi 389 wa kada mbalimbali na inategemea kukamilisha ajira za watumishi wengine 676 ifikapo Juni, 2020.

***45.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia maslahi, maadili, ustawi na afya za watumishi ikiwa ni pamoja na kuwawezesha watumishi waliojitokeza wanaoishi na VVU na Ukimwi ili kupata lishe bora. Aidha, katika kuboresha afya za watumishi, kupambana na magonjwa yasiyoambukiza na kujenga umoja, Wizara imeanzisha utaratibu maalum wa mazoezi Novemba, 2019 unaosimamiwa na mkufunzi wa michezo kutoka Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo. Katika utaratibu huo, watumishi hufanya mazoezi ya viungo kuanzia saa 11:00 hadi 12:30 jioni katika Uwanja wa Jamhuri, Jijini Dodoma.

***46.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetoa mafunzo ya ujasiriamali wa ufugaji nyuki kwa watumishi kwa lengo la kuwajengea uwezo na hamasa ya kuanzisha miradi ya kufuga nyuki, kuuza asali na biashara ya bidhaa zinazotengenezwa kwa asali na nta. Kupitia mafunzo hayo, watumishi 33 wameanzisha miradi ya ufugaji nyuki yenye jumla ya mizinga 503 katika Msitu wa Hifadhi Aghondi, Manyoni.

## 5.5. Majukumu ya Wizara

### 5.5.1. Sekta Ndogo ya Wanyamapori

***47. Mheshimiwa Spika,*** Sekta Ndogo ya Wanyamapori inajumuisha shughuli za uhifadhi, usimamizi, mafunzo na utafiti wa wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Utekelezaji wa shughuli hizo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Wanyamapori ya mwaka 2007 na kusimamiwa na Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Sura 283, Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282, Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro Sura 284 na Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania Sura 260. Aidha, shughuli hizo hutekelezwa kupitia Idara ya Wanyamapori, TAWA, TANAPA, NCAA, TAWIRI, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori – Mweka, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori – Pasiansi, na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga.

### 5.5.2. Masuala Mahsusi ya Sekta Ndogo ya Wanyamapori

#### (i) Uhifadhi wa Wanyamapori Waliopo Hatarini Kutoweka

***48. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa na inatekeleza mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha kuwa wanyamapori walio hatarini kutoweka wanaendelezwa kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo. Mikakati hiyo inajumuisha Mpango Mkakati wa Kuhifadhi Sokwe Mtu (2018 - 2023), Mpango Mkakati wa Taifa wa Uhifadhi wa Faru (2019 - 2023) na Mpango Mkakati wa Kuhifadhi Twiga (2020-2025). Katika kutekeleza Mkakati wa Kuhifadhi Faru, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi, imeleta faru weusi tisa (9) kutoka Afrika ya Kusini.

### (ii) Ulinzi wa Wananchi Dhidi ya Wanyamapori Wakali na Waharibifu

***49.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara imetengeneza mfumo unaoruhusu wananchi kutoa taarifa za matukio kupitia simu za mkononi kwenye namba maalum iliyotolewa na Wizara. Mfumo huo ulianza kufanyiwa majaribio Novemba, 2019. Aidha, Wizara imeendelea kutumia teknolojia ya kuwafunga baadhi ya ndovu vifaa maalum vya kielekitroniki kwa lengo la kufuatilia nyendo zao ili kuepusha migongano na wananchi wanaoishi kando ya maeneo yaliyohifadhiwa. Katika mfumo huo, ndovu 26 wamevishwa *radio collar* kwa ajili ya ufuatiliaji wa mienendo yao katika eneo la Maswa - Makao. Vilevile, katika kuhakikisha maisha ya wananchi na mali zao zinalindwa ipasavyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Wanyamapori Wakali na Waharibifu.

***50.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kulipa kifuta machozi na kifuta jasho kwa wahanga wa matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu. Hadi Machi, 2020 Wizara imelipa jumla ya Shilingi 984,768,000 kwa waathirika 9,060 kama kifuta machozi na kifuta jasho. Aidha, Wizara kupitia TAWA imefanya jumla ya siku doria 6,612 za kupambana na wanyamapori wakali na waharibifu ambapo wanyamapori wakali 61 waliuawa baada ya kuhatarisha maisha ya wananchi na mali zao. Vilevile, Wizara imehamisha jumla ya simba 36 waliokuwa wanahatarisha maisha ya watu na mifugo kutoka Wilaya ya Serengeti na makundi sita (6) yenye mbwa - mwitu 83 katika Wilaya ya Loliondo na kuwapeleka katika maeneo ambayo hawataleta madhara. Pia, TAWA imeendelea kutoa elimu kuhusu namna ya kujikinga na wanyamapori wakali na matumizi ya mbinu zisizo angamizi za kupambana na wanyamapori hao katika maeneo yenye changamoto zaidi.

### (iii) Kuimarika na Kuongezeka kwa Umaarufu wa Tanzania katika Uhifadhi

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na juhudi za kuimarisha uhifadhi, usimamizi na utangazaji wa vivutio vya utalii. Kupitia jitihada hizo, Hifadhi ya Taifa Serengeti kupitia uratibu wa Kampuni ya *World Travel Awards* imetangazwa kuwa hifadhi bora katika Bara la Afrika na kupata tuzo. Umaarufu huo umetokana na kuwepo kwa uhifadhi endelevu wa wanyamapori watano (5) muhimu (simba, ndovu, nyati, chui na faru) pamoja na wingi wa nyumbu na matukio yake ya kuhama kati ya Hifadhi ya Taifa Serengeti na Hifadhi ya Maasai Mara ya nchini Kenya. Kutokana na umaarufu huo, kampuni ya filamu ya *XIX Entertainment* ya Marekani imetengeneza makala inayojulikana kama *Serengeti Series* ambapo sehemu ya kwanza ya makala hiyo imeanza kuoneshwa.

### (iv) Uwindaji wa Kitalii

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na utaratibu wa kugawa vitalu kwa njia ya mnada wa kielekitroniki ambao umeongeza uwazi, uwajibikaji na kuruhusu nguvu ya soko kuamua bei ya vitalu. Awamu ya kwanza ya mnada ilifanyika Juni, 2019 ambapo jumla ya vitalu saba (7) kati ya 26 vilivyotangazwa viliuzwa na kuingiza jumla ya Dola za Marekani 831,000 sawa na asilimia 98 ya ada ya vitalu vyote 26 endapo utaratibu wa zamani ungeendelea kutumika. Aidha, katika kuhakikisha kuwa minada inaendeshwa bila kuathiri ustawi wa tasnia, Wizara ilifanya tathmini ya utendaji kazi kwa kampuni za uwindaji wa kitalii kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2017 hadi Disemba, 2019 na kuziweka katika makundi mawili (2). Kundi la kwanza la kampuni ni lenye vitalu vinavyofanya vizuri na kundi la pili ni lenye vitalu vyenye utendaji usioridhisha. Kufuatia matokeo hayo, Wizara imeongeza muda wa umiliki wa vitalu hadi Disemba, 2021 kwa kampuni zenye vitalu vinavyofanya vizuri, ambapo mnada wa vitalu hivyo utafanyika

Septemba, 2021. Kwa vitalu vyenye utendaji usioridhisha, muda wake wa umiliki utafikia ukomo tarehe 31 Disemba, 2020 na utaratibu wa kuviuza kwa mnada utaanza Septemba, 2020.

### 5.5.1.1 Idara ya Wanyamapori

***53. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa Kanuni za Usimamizi wa Uuzaji wa Nyamapori **"***Wildlife Conservation (Game Meat Selling) Regulations 2020*" ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kanuni hizo zinatoa fursa kwa wananchi kupata kitoweo cha nyamapori kwa bei nafuu. Wizara ipo katika hatua za mwisho za kuandaa mwongozo wa uanzishaji wa bucha za nyamapori ili kurahisisha utekelezaji wa Kanuni hizo.

***54. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya marekebisho ya Kanuni za Ufugaji wa Wanyamapori za mwaka 2013 kupitia Tangazo la Serikali Na. 84 la mwaka 2020. Kanuni hizo zimeweka mazingira wezeshi ya kuanzisha maeneo ya ufugaji, upatikanaji wa wanyamapori mbegu kwa bei nafuu na kutumia wanyamapori katika mashamba, bustani na ranchi. Aidha, Wizara imeandaa Kanuni za Uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Wanyamapori *"The wildlife Conservation (Special Wildlife Investment Concession Areas) Regulations,* Tangazo la Serikali Na. 28 la mwaka 2020. Kanuni hizo zimetoa muda mrefu wa uwekezaji wa kimkakati wa hadi miaka 30 na zinaruhusu kampuni kupendekeza miradi bunifu ya kukuza utalii.

***55. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018, Wizara ilifungua shughuli za uwindaji wa wenyeji katika maeneo ya majaribio ya Kilwa Kaskazini, Kitwai, Kisarawe, Simbanguru na Ugalla kwa Tangazo la Serikali Na. 664 la Novemba, 2018. Aidha, kutokana na kuongezeka kwa mahitaji na kuimarika kwa ulinzi wa wanyamapori, Wizara imeongeza maeneo ya wazi ya Ipemba Mpezi,

Talamai na Msitu wa Matundu kwa ajili ya uwindaji wa wenyeji kupitia Tangazo la Serikali Na. 961 la Disemba, 2019.

### 5.5.1.2 Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)

***56.*** ***Mheshimiwa Spika,*** TANAPA imepewa jukumu la kusimamia shughuli za uhifadhi na uendelezaji wa utalii katika hifadhi za Taifa. Katika kutekeleza azma hiyo, Shirika limeendelea kuimarisha shughuli za intelijensia, kuongeza matumizi ya teknolojia kwenye ulinzi wa hifadhi hivyo kubaini wahusika wa mitandao yote ya ujangili na kuivunja kwa wakati kabla haijafanya uhalifu.

***57.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa mipaka ya hifadhi inatambulika, Shirika limeweka jumla ya alama za mipaka 62 kwenye Hifadhi za Tarangire (35) na Burigi - Chato (27). Aidha, Shirika limeweka alama za mipaka ya maji (maboya) 29 katika eneo la Funguni, Hifadhi ya Taifa Saadani. Vilevile, mipaka ya hifadhi yenye jumla ya kilomita 258 imesafishwa katika Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara (kilometa 140) na Saadani (kilometa 118). Shirika linaendelea na zoezi la uwekaji wa alama za mipaka kwenye maeneo yaliyobakia ili kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na kupunguza migorogoro kati ya hifadhi na wananchi.

***58.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na mimea vamizi inayotishia ustawi wa wanyamapori na mazingira yao, Shirika limeondoa mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 1,365 katika hifadhi za Taifa za Tarangire, Saadani, Ziwa Manyara, Arusha, Kitulo, Rubondo na Mahale. Aidha, Shirika limeondoa hekta 127 za uoto vamizi wa vichaka katika hifadhi za Ziwa Manyara, Saadani na Saanane.

***59.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kuimarisha mifumo ya teknolojia na mawasiliano katika hifadhi mpya za Burigi - Chato, Nyerere, Kigosi, Ibanda - Kyerwa, Rumanyika - Karagwe na Ugalla. Aidha, Shirika

limeendelea kuboresha mifumo ya malipo ikiwemo ya kulipa kabla mgeni hajafika kwenye malango ya kuingia, maeneo ya makambi, *online bookings*, viwanja vya ndege na kutumia simu za mkononi. Vilevile, Shirika limeboresha mifumo ya teknolojia katika malango 46 ya hifadhi za Kilimanjaro, Tarangire, Mikumi, Udzungwa, Rubondo, Gombe, Arusha, Ziwa Manyara, Kitulo, Ruaha, Serengeti, Mkomazi, Katavi na Mahale ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma. Pia, katika kuendeleza utalii wa faru katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi, ujenzi wa uzio wa umeme wenye urefu wa kilometa 13 upo katika hatua za ukamilishaji ambapo utalii wa faru unatarajiwa kuanza rasmi Juni, 2020. Aidha, Shirika limekarabati barabara zenye jumla ya kilometa 2,700 na kuboresha miundombinu ya mawasiliano.

### 5.5.1.3 Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA)

***60. Mheshimiwa Spika,*** NCAA inasimamia shughuli za uhifadhi, uendelezaji wa utalii na ustawi wa jamii zinazoishi ndani ya eneo la hifadhi. Katika kutekeleza shughuli hizo, Mamlaka imefanya jumla ya siku doria 15,434 ambazo zimewezesha kukamatwa wahalifu 66 wa makosa ya aina mbalimbali. Aidha, Mamlaka imeimarisha kikosi maalum cha kudhibiti ujangili kwa kuwapatia mafunzo ya utayari na ukakamavu pamoja na vifaa vya doria. Vilevile, Mamlaka imedhibiti kwa kung'oa, kufyeka na kuchoma moto mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 1,900.

***61. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imekarabati kilometa 340 za barabara, kati ya hizo, kilometa 90 zipo ndani ya eneo la kreta ambazo zinapitika vizuri sasa baada ya kuharibika kutokana na mvua. Aidha, Mamlaka imejenga kilometa 10 za njia za kutembea watalii katika Msitu wa Hifadhi Nyanda za Juu katika eneo la Endoro kuelekea kwenye mapango ya Tembo na maporomoko ya maji. Vilevile, njia za kutembea watalii kwenye kreta za Empakai na Endoro zinaendelea

kufanyiwa matengenezo. Pia, Mamlaka inafanya maboresho ya miundombinu ya utalii katika eneo la Ndutu kwa kujenga mtandao wa barabara wenye kilometa 23 kutoka eneo la Golini hadi Ndutu. Aidha, Mamlaka inaendelea na upembuzi yakinifu na tathmini ya athari za kimazingira katika eneo la Olduvai panapotarajiwa kujengwa kiwanja cha ndege kwa kiwango cha lami.

***62.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ya jamii zinazoishi ndani na nje ya eneo la hifadhi. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa madarasa matatu (3) katika shule za msingi za Masamburai (1) na Loresho (2), ufadhili kwa wanafunzi 1,714 kuanzia ngazi za shule ya msingi hadi chuo kikuu, utoaji wa chanjo ya kimeta kwa mifugo 17,097 na ujenzi wa mabwawa mawili (2) katika vijiji vya Alailelai na Misigyo. Aidha, Mamlaka imenunua na kusambaza tani 1,800 za mahindi kwa wananchi wanaoishi katika eneo la hifadhi na kutoa fedha jumla ya Shilingi milioni 36 kwa vyama 12 vya ushirika ikiwa ni mtaji wa kuendeleza shughuli za kuongeza kipato kwa wanachama.

### 5.5.1.4 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA)

***63.*** ***Mheshimiwa Spika,*** TAWA inasimamia shughuli za uhifadhi wa wanyamapori na uendelezaji wa utalii katika mapori ya akiba 24, mapori tengefu 27 na maeneo matatu (3) ya ardhioevu. Aidha, Mamlaka ni msimamizi wa shughuli za uhifadhi katika maeneo 38 ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori. Katika kutekeleza majukumu yake, Mamlaka imeboresha huduma za utalii katika mapori ya akiba kwa kujenga hosteli ya kisasa katika Pori la Akiba Swagaswaga na kambi ya kulala wageni katika Pori la Akiba Kijereshi. Aidha, Mamlaka imenunua boti moja (1) kwa ajili ya shughuli za utalii katika eneo la kihistoria la Magofu ya Kilwa Kisiwani. Vilevile, Mamlaka imeshiriki katika maonesho ya 48 ya

uwindaji wa kitalii yaliyofanyika nchini Marekani (*Safari Club International Convention*) Februari, 2020.

***64. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imefungua barabara za utalii zenye urefu wa kilometa 179 katika mapori ya akiba ya Mpanga Kipengere (kilometa 13), Kijereshi (kilometa 88), na Maswa (kilometa 66). Aidha, njia za kupita wageni *(walkways)* zenye urefu wa mita 340 zimejengwa kuelekea kwenye maporomoko ya maji ya Kimani katika Pori la Akiba Mpanga Kipengere. Vilevile, awali Mamlaka ilifanya ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Mtemere katika eneo ambalo sasa ni Hifadhi ya Taifa Nyerere.

***65. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya kazi**,** Mamlaka inaendelea na ujenzi wa nyumba 16 za watumishi na vituo 11 vya askari katika mapori ya akiba ya Maswa, Mkungunero, Uwanda, Lukwati Piti, Lukwika-Lumesule/Msanjesi, Swagaswaga na Moyowosi; Pori Tengefu Ziwa Natron; na Kikosi Dhidi Ujangili (KDU) Kanda ya Bunda. Aidha, ujenzi wa ofisi nne (4) katika mapori ya akiba ya Rungwa – Kizigo - Muhesi, Lukwika - Lumesule na Swagaswaga; na KDU Manyoni unaendelea.

### 5.5.1.5 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI)

***66. Mheshimiwa Spika,*** TAWIRI imepewa jukumu la kufanya na kuratibu utafiti wa wanyamapori. Katika kutekeleza majukumu yake, Taasisi imeendelea na utafiti kuhusu mchango wa wanyamapori katika kueneza magonjwa ya homa ya mbuzi na kondoo, kutupa mimba au homa ya vipindi (brucellosis), kimeta na kaswende ya nyani.

***67. Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya awali ya utafiti yanaonesha kuwa nyati, swala granti na swala tomi wameambukizwa zaidi ugonjwa wa homa ya mbuzi na kondoo. Aidha, utafiti umebaini kuwa maambukizi

ya ugonjwa wa kutupa mimba yapo juu kwa wanyamapori. Vilevile, Taasisi imebaini kuwa matukio mengi ya milipuko ya kimeta yanatokea wakati wa kiangazi kuanzia Julai hadi Septemba hivyo ugonjwa huu unaweza kudhibitiwa kwa kuchanja mifugo mwanzoni mwa majira ya kiangazi. Pia, utafiti umebaini kuwa asilimia 80 ya vyanzo vya maji vilivyopo katika eneo la Ngorongoro vina vimelea vya magonjwa ya homa za matumbo kutokana na uhaba wa vyoo au baadhi ya wananchi kutokutumia vyoo kabisa.

***68.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi kupitia Mradi wa Tathmini ya Ufanyaji Kazi wa Mfumo Ikolojia Serengeti imefanya utafiti kuhusu madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la idadi ya watu katika mfumo ikolojia. Utafiti umebaini kuwa ongezeko la mifugo katika maeneo yanayozunguka mfumo ikolojia na shughuli nyingine za binadamu zimeathiri shoroba na maeneo ya mtawanyiko wa wanyamapori. Hali hii imesababisha kuongezeka kwa migongano baina ya binadamu na wanyamapori hususan simba, mbwa mwitu na fisi.

***69.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imefanya utafiti kuhusu tatizo la mamba wanaotishia usalama wa wananchi katika Ziwa Rukwa. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mamba wanaoleta madhara ni wale walioko nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Utafiti umeainisha hatua za kuchukua ikiwa ni pamoja na kuvuna mamba hao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori. Hatua nyingine ni kuchimba visima vya maji ili kuepusha mwingiliano wa wananchi na mamba ziwani, kuweka alama za tahadhari kwenye maeneo hatarishi na kuepuka kutumia mitumbwi midogo. Pamoja na utafiti uliofanyika, TAWIRI imefanya ukarabati wa vituo vya Serengeti na Njiro na ukarabati wa vituo vya Kihansi, Kingupira na Mahale unaendelea.

### 5.5.1.6 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka

***70.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka kimepewa jukumu la kutoa mafunzo, ushauri wa kitaalam na kufanya utafiti kuhusu uhifadhi wa wanyamapori na uendelezaji utalii. Katika kutekeleza majukumu yake, Chuo kimedahili wanafunzi 846 katika ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa waongoza watalii 413. Vilevile, Chuo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha *Manchester Metropolitan* cha Uingereza kimekamilisha mtaala kwa ajili ya kozi ya Uzamili ya Ikolojia na Uhifadhi wa Wanyamapori wa Afrika (*Master of Science in African Wildlife Ecology and Conservation)*.

***71.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo kimekamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa uzio wa matofali wenye urefu wa mita 670 kuzunguka eneo la Chuo. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni ukarabati wa jengo la maabara ya zahanati ya Chuo, hosteli ya wanafunzi na barabara za ndani ya Chuo.

### 5.5.1.7 Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi

***72.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi imepewa jukumu la kutoa mafunzo ya uhifadhi wa wanyamapori na himasheria katika ngazi ya Astashahada nne na tano za Baraza la Taifa la Ushauri wa Elimu ya Vyuo vya Ufundi (NACTE). Katika kutekeleza majukumu yake, Taasisi imedahili jumla ya wanafunzi 300 katika ngazi ya Astashahada ya Awali na Astashahada ya Uhifadhi Wanyamapori na Himasheria. Aidha, Taasisi imetoa mafunzo ya muda mfupi ya Himasheria na Uhifadhi wa Wanyamapori kwa washiriki 69 kutoka wilaya za Kigoma, Tanganyika, Babati, Ngorongoro, Kondoa na Karatu. Vilevile, Taasisi imeendesha mafunzo ya Jeshi Usu ya utayari kwa watumishi 468 kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Pia, mtaala wa kozi ya waongoza watalii na

ulinzi umepitishwa na NACTE na mafunzo yataanza kutolewa kuanzia mwaka wa masomo 2020/2021.

***73. Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeanza ujenzi wa maktaba na kununua samani za ofisi (meza na viti) 100, vitanda 150, magodoro 200, vifaa vya jiko la porini na jenereta moja (1). Aidha, Taasisi imeboresha kambi ya mafunzo Fort Ikoma kwa kuweka umeme, kujenga ofisi, vyoo na kukarabati mahanga.

### 5.5.1.8 Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu – Sekamaganga

***74. Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu - Sekamaganga kimepewa jukumu la kuzijengea uwezo jamii zinazoishi jirani na maeneo yenye wanyamapori ili kushiriki katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili. Kituo kimekamilisha taratibu za usajili na kutambuliwa na NACTE na kwa sasa kinaendelea na taratibu za udahili wa wanafunzi katika ngazi hiyo**.** Katika kutekeleza majukumu yake, kituo kimetoa mafunzo ya namna ya kufanya doria kwa jumla ya washiriki 298 ambao ni vikundi vya doria na wajumbe wa kamati za maliasili za vijiji. Aidha, kituo kimekamilisha ujenzi wa jengo la maktaba na chumba cha kompyuta.

### 5.5.1.9 Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania (TWPF)

***75. Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania umepewa jukumu la kuwezesha uhifadhi wa wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Mfuko umewezesha shughuli za kupambana na ujangili na kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathirika kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, Mfuko umewezesha kufanya mapitio

ya Kanuni za WMAs, uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi na ufugaji wanyamapori na uandaaji wa Kanuni za Uuzaji wa Nyamapori.

### 5.5.3. Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki

***76.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki inajumuisha shughuli za uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki. Utekelezaji wa shughuli hizo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Misitu (1998) na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (1998). Aidha, usimamizi wa shughuli hizo unatekelezwa kupitia Sheria ya Misitu Sura 323, Sheria ya Ufugaji Nyuki Sura 224, Tangazo la Kuanzisha Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania Na. 269/2010 na Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania Sura 270. Vilevile, shughuli hizo hutekelezwa kupitia Idara ya Misitu na Nyuki, TFS, TAFORI, FTI, FITI, BTI na TaFF.

### 5.5.2.1 Masuala Mahsusi ya Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki

#### (i) Ufugaji Nyuki na Masoko ya Mazao ya Nyuki

***77.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwanufaisha wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi kupitia miradi ya ufugaji nyuki. Katika kutekeleza hilo, Wizara kupitia mfuko wa Misitu wa Tanzania imetoa mafunzo ya ufugaji nyuki kwa wananchi 1,225 na vikundi 144; mizinga 5,288 na seti 160 za mavazi ya ufugaji nyuki. Aidha, Mfuko umeendelea kuwezesha ujenzi wa viwanda vipya viwili (2) katika mikoa ya Tabora (Sikonge) na Geita (Bukombe). Vilevile, Mfuko umewezesha kuanza kwa ukarabati wa viwanda vitatu (3) katika mikoa ya Katavi (Mlele), Kigoma (Kibondo) na Singida (Manyoni). Aidha, katika jitihada za kuboresha na kuongeza makundi ya nyuki, Wizara kupitia Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora imeanzisha mradi na mafunzo maalum ya kuzalisha malkia. Katika kutekeleza sehemu ya mkakati huo, Chuo kimetoa mafunzo kwa wafugaji nyuki 68.

### (ii) Udhibiti wa Moto

***78. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TFS imeendelea na jitihada mbalimbali ya kudhibiti matukio ya moto katika misitu ya hifadhi, hifadhi za wanyamapori na maeneo mbalimbali ya wananchi kwa kutoa elimu kupitia mikutano, kuandaa mipango ya udhibiti wa moto na kufuatilia matukio ya moto kwa kutumia *satellite*. Maeneo yaliyoathirika na matukio ya moto ni mikoa ya Iringa, Lindi, Katavi, Mbeya na Ruvuma. Katika kukabiliana na changanoto za matukio ya moto, Wizara imeendesha jumla ya mikutano 229 kwenye vijiji 239 katika wilaya 35, kujenga minara minne (4) ya kufuatilia matukio ya moto na kukarabati minara 19. Aidha, Wizara imenunua mtambo maalum wa kuzima moto wa msituni wenye uwezo wa kuzima moto hadi umbali wa mita 100. Vilevile, mipaka yenye urefu wa kilometa 81,223 imesafishwa katika misitu 89. Kutokana na jitihada hizo, matukio ya moto yamepungua kutoka asilimia 11 mwaka 2018 hadi asilimia nane (8) mwaka 2019.

### 5.5.2.2 Idara ya Misitu na Nyuki

***79. Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Misitu na Nyuki imepewa jukumu la kuandaa na kusimamia sera, sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa misitu na ufugaji nyuki. Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuratibu mikutano mitatu (3) ya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Misitu (NAFAC) na mkutano wa Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ufugaji Nyuki (NABAC). Ushauri mbalimbali uliotolewa kuhusu namna bora ya kusimamia na kuendeleza sekta ndogo ya misitu na nyuki unaendelea kutekelezwa. Aidha, Wizara imefanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (1998) na tathmini ya Sheria ya Misitu Sura 323.

### 5.5.2.3 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS)

***80. Mheshimiwa Spika,*** TFS imepewa jukumu la kusimamia misitu ya hifadhi ya asili, misitu iliyo katika

maeneo yasiyohifadhiwa, mashamba ya miti na hifadhi za nyuki za Serikali kuu pamoja na kuendeleza na kuzalisha mbegu bora za miti na vipando.

***81.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala umeendelea na jitihada mbalimbali za kuongeza uzalishaji wa mazao ya nyuki. Hadi Machi, 2020 jumla ya tani 163 za asali na tani 388 za nta zilivunwa. Aidha, Wakala umejenga vituo viwili (Dodoma na Dar es Salaam) vya kuuzia asali pamoja na kutoa taarifa mbalimbali za ufugaji nyuki. Vilevile, mafunzo ya ufugaji nyuki, uchakataji, ufungashaji na masoko yalitolewa kwa vikundi 19 vya wafugaji nyuki. Pia, sampuli 70 za asali zilikusanywa katika wilaya 30 na kufanyiwa uchambuzi ili kuhakiki ubora kwa lengo la kutimiza vigezo vya kuuzwa katika soko la ndani na nje ya nchi. Matokeo ya uhakiki huo yalionesha kuwa asali ya Tanzania inakidhi vigezo vya kuuzwa katika nchi za Jumuiya ya Ulaya.

#### 5.5.2.4 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI)

***82.*** ***Mheshimiwa Spika,*** TAFORI imepewa jukumu la kufanya na kuratibu utafiti wa misitu na ufugaji nyuki na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi ya teknolojia bora katika nyanja za misitu na ufugaji nyuki. Katika kutekeleza majukumu yake, Taasisi imefanya utafiti wa kubaini na kushauri namna ya kukabiliana na vyanzo vya kufa au kukauka kwa miti kwenye mashamba ya Serikali na watu binafsi. Matokeo ya utafiti huo yameonesha kuwa miti ya misindano na mikaratusi iliyopandwa kwenye mashamba ya Mbizi na Kawetire inakauka kutokana na ukosefu wa madini aina ya *Boroni* na *Phosphorus*.

***83.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeainisha hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto hiyo. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza mbolea yenye madini aina ya *Boroni* na *Phosphorus* kwenye udongo au kunyunyizia madini hayo kwenye miche au miti ikiwa bustanini na shambani. Aidha, Taasisi imeanza kufanya utafiti juu ya

uvunaji wa utomvu kwenye miti ya misindano ili kubaini spishi za miti na umri unaofaa kutoa utomvu mwingi na madhara ya uvunaji kwenye ukuaji na ubora wa mbao. Aidha, Taasisi imeanza kufanya utafiti na kuandaa mfumo wa kutoa taarifa za uhalifu kwenye misitu iliyopo kwenye Milima ya Tao la Mashariki ili kuboresha uhifadhi wa bioanuai.

### 5.5.2.5 Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki

***84.*** ***Mheshimiwa Spika,*** vyuo vya taaluma ya misitu na ufugaji nyuki vinajumuisha Chuo cha Misitu Olmotonyi, Chuo cha Viwanda vya Misitu na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki. Vyuo hivyo vimepewa jukumu la kutoa mafunzo ya uhifadhi, usimamizi na matumizi endelevu ya misitu na ufugaji nyuki katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Chuo cha Misitu Olmotonyi kimedahili wanafunzi 825 na kutoa mafunzo kuhusu usimamizi shirikishi wa misitu kwa vijiji 12 katika wilaya za Loliondo na Lindi, uanzishaji na usimamizi wa vitalu vya miti. Chuo cha Viwanda vya Misitu kimedahili wanafunzi 195 na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki wanafunzi 353.

### 5.5.2.6 Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF)

***85.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Misitu Tanzania umepewa jukumu la kuwezesha wadau wa sekta ndogo ya misitu na ufugaji nyuki kwenye uhifadhi, usimamizi na uendelezaji misitu na ufugaji nyuki. Katika kutekeleza majukumu yake, Mfuko umewezesha ujenzi wa jengo la utawala la FTI, ukarabati wa jengo la utawala na ununuzi wa vifaa vya kuchakata mazao ya nyuki vya BTI, ununuzi wa samani za maktaba ya FITI na vifaa vya kupimia ubora wa mbao vya FITI na TAFORI. Aidha, vikundi 126 vimepewa mafunzo ya ufugaji nyuki, mizinga 5,700 na vifaa bora vya ufugaji wa nyuki. Vilevile, mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki na

utengenezaji wa mizinga yametolewa kwa vikundi 37. Pia, Mfuko umewezesha uanzishwaji na uboreshaji wa vituo nane (8) vya ukusanyaji na uchakataji wa mazao ya nyuki. Vituo hivyo ni Geita Mbogwe (1), Shinyanga - Kahama (1), Dodoma - Kondoa (1), Mbeya - Rungwe (1), Tabora - Igunga (2), Mara – Bunda (1) na Chuo cha Ufugaji Nyuki (1).

***86. Mheshimiwa Spika,*** Mfuko umewezesha upandaji miti kwenye maeneo yaliyoharibika yenye hekta 3,801 katika misitu ya asili. Maeneo hayo ni katika mashamba ya miti, Ziwani (Mtwara) hekta 106, Biharamulo hekta 350, Nishati (Nzega) hekta 459, Tanganyika (Katavi) hekta 86, Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero hekta 2500, na Chuo Kikuu cha Kilimo - SUA lililopo Ifinga Songea hekta 300.

***87. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na Mfuko ni pamoja na kuwezesha utekelezaji wa miradi mitatu (3) ya utafiti ambapo miradi miwili (2) inatekelezwa na SUA na mradi mmoja (1) unatekelezwa na TAFORI. Aidha, Mfuko umewezesha ukusanyaji wa taarifa kwa ajili ya vipindi 24 vya radio, vipindi 6 vya televisheni na majarida ya Misitu ni Mali na Utafiti wa Misitu. Vilevile, Mfuko umewezesha utekelezaji wa miradi 187 (miradi 60 mipya na miradi 127 inayoendelea) ya uhifadhi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu. Aidha, Mfuko unaendelea kufadhili wanafunzi 21 katika vyuo vya FTI, BTI na FITI.

### 5.5.4. Sekta Ndogo ya Utalii

***88. Mheshimiwa Spika,*** Sekta Ndogo ya Utalii imepewa jukumu la kuendeleza utalii nchini ikiongozwa na Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999 na kusimamiwa na Sheria ya Utalii Sura 29 na Sheria ya Bodi ya Utalii Sura 364. Aidha, jukumu hilo linatekelezwa kupitia Idara ya Utalii, TTB na NCT.

### 5.5.3.1 Masuala Mahsusi ya Sekta Ndogo ya Utalii

#### (i) Kuendeleza Mazao ya Utalii

***89.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na jitihada za kuendeleza utalii nchini ikiwemo utalii wa meli, mikutano, fukwe, utamaduni, malikale, matukio na jiolojia. Jitihada hizo zinakwenda sanjari na uongezaji wa shughuli za utalii katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo *balloon safaris, night game drive, walking safaris, canopy walk, cultural tours*. Aidha, Wizara imeandaa mkakati wenye matokeo ya haraka wa uendelezaji wa mazao ya utalii wa fukwe, mikutano na meli. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Katavi, Songwe na Morogoro Septemba, 2019 ilifanya Jukwaa la Uwekezaji katika Sekta ya Utalii. Pia, Onesho la Utalii Karibu Kusini lilifanyika sanjari na Jukwaa hilo kwa lengo la kufungua fursa za utalii na uwekezaji katika Ukanda wa Kusini. Aidha, Machi 2020, Wizara kwa kushirikiana na mikoa ya Kanda ya Ziwa, Kigoma na Tabora ilizindua maandalizi ya Onesho la Kimataifa na Jukwaa la Uwekezaji lijulikanalo kama *Great Lakes International Tourism Expo (GLITE)* litakalofanyika Jijini Mwanza Juni, 2020.

#### (ii) Kuboresha Mafunzo Kuendana na Mahitaji ya Soko

***90.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia NCT imefanya mapitio ya mitaala yote na inaendelea kukamilisha mitaala ya kitaifa katika ngazi ya Shahada katika fani ya Utalii na Ukarimu. Aidha, programu mpya ya mafunzo ya uratibu wa matukio (*Technical Certificate in Event Management*) imeanzishwa ili kukidhi mahitaji ya soko hususan uratibu wa matukio. Vilevile, Chuo kwa kushirikiana na Taasisi ya *Confucious* ya China ambayo inashirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeanza kutoa mafunzo ya lugha ya Kichina ili kutoa fursa kwa wahitimu kuweza kuongea lugha zaidi ya moja. Pia,

mafunzo ya lugha za Kifaransa na Kiingereza yameendelea kuimarishwa.

### (iii) Kutangaza Utalii wa Ndani

***91.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha utalii wa ndani nchini, Serikali imeanzisha chaneli maalum iitwayo Safari Channel kwenye Shirika la Utangazaji la Taifa. Chaneli hii imesaidia sana kuonesha vivutio mbalimbali tulivyonavyo hapa nchini ili kuhamasisha Watanzania kuvitembelea. Wadau mbalimbali pia wameunga mkono juhudi za kukuza utalii wa ndani kwa kuandaa na kushiriki katika matukio mbalimbali kama vile Twendezetu Burigi, HK Kilimanjaro Challenge, Mkwawa Trails Run, Rock City Marathon, Ngorongoro Marathon, Kigamboni Marathon, Selous Marathon, Morogoro Marathon na Serengeti Marathon. Aidha, pamoja na matukio hayo, Serikali imeendelea na juhudi mbalimbali zikiwemo za kuadhimisha miaka 60 ya Hifadhi ya Taifa Serengeti na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na kuendelea kuhamasisha matumizi ya utambulisho wa Taifa letu (Tanzania Unforgettable) katika kukuza zaidi utalii nchini. Kupitia jitihada hizo, takwimu zinaonesha kuwa katika mwaka 2019, jumla ya wafuatiliaji (followers) 1,064,215 walisambaza ujumbe kupitia mitandao ya kijamii (facebook, twitter, instagram, youtube na destination portal user) na kushawishi Watanzania kutembelea vivutio vya utalii. Takwimu hizo zikilinganishwa na mwaka 2018, kuna ongezeko la wafuatiliaji 286,900 sawa na asilimia 37.

***92.*** ***Mheshimiwa Spika,*** utalii wa ndani ni muhimu kwa sababu tatu kuu: Kwanza, unatoa fursa ya wananchi kupumzika kwa namna nzuri zaidi. Pili, unasaidia kufanya wananchi wathamini zaidi vivutio tulivyonavyo na hivyo kuongeza mwamko wa kuhifadhi na kuvitunza. Tatu, ni chanzo cha mapato kwa taasisi zetu za uhifadhi, jambo ambalo ni muhimu sana ingawa kwa sasa watalii kutoka nje wameshindwa kuja kwa sababu ya janga kama la Coronavirus. Hivyo, lengo la

Serikali ni kuendelea na juhudi za kuvitangaza vivutio vya utalii ili Watanzania wengi watembelee vivutio vya utalii na kushiriki katika biashara za utalii na hivyo kuchangia zaidi katika pato la Taifa.

### 5.5.3.2 Idara ya Utalii

***93. Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Utalii imepewa jukumu la kuandaa na kusimamia sera, sheria, kanuni na miongozo ya kuendeleza utalii. Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imekamilisha kazi ya kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora wa nyota katika Mkoa wa Dodoma ambapo jumla ya hoteli 24 zilikaguliwa. Kati ya hizo, jumla ya hoteli 11 zilipata alama zinaonesha viwango vya ubora kama ifuatavyo: hoteli tatu (3) zilipata nyota tatu, hoteli tano (5) zilipata nyota mbili na hoteli tatu (3) zilipata nyota moja. Hoteli 13 hazikukidhi viwango vya ubora wa nyota. Aidha, ukaguzi wa wakala wa biashara za utalii umefanyika katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo malango ya kuingilia wageni ya hifadhi za Taifa za Manyara, Kilimanjaro, Tarangire na Mikumi; na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ili kuhakikisha wanazingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo.

### 5.5.3.3 Bodi ya Utalii Tanzania (TTB)

***94. Mheshimiwa Spika,*** TTB imepewa jukumu la kutangaza utalii ndani na nje ya nchi. Utangazaji wa vivutio vya utalii umefanyika kupitia maonesho ya kimataifa katika nchi za Kanada, Ufaransa, Kenya, Israel, India, Uholanzi, Ubelgiji, Marekani, Jamhuri ya Czech, Urusi, China na Uganda. Njia nyingine ni pamoja na misafara ya utangazaji utalii katika nchi za Ujerumani na Austria, kutumia watu mashuhuri, mawakala wa utalii, ziara za waandishi wa habari wa nje, matumizi ya TEHAMA, vyombo vya habari na fainali za michezo ya mpira wa miguu (AFCON) kwa vijana chini ya miaka 17 uliofanyika Tanzania. Pia, vivutio vya utalii vimetangazwa kwa kutumia Mabalozi wa Hiari wa Utalii

akiwemo Mtanzania Bw. Mbwana Samatta, anayecheza katika moja ya ligi bora duniani (Uingereza). Aidha, Bodi imeendelea kuandaa na kushiriki katika Onesho la Kimataifa la Utalii (S!TE) ambapo mwaka 2019 waoneshaji zaidi ya 170 walishiriki kutoka nchi za Afrika ya Mashariki na Kusini. Waoneshaji hao walikutana na wakala wa biashara za utalii wa kimataifa takriban 300 kutoka masoko mbalimbali ya utalii duniani.

***95. Mheshimiwa Spika,*** Bodi imeendelea kushirikiana na Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) kutangaza utalii katika nchi ya India ambapo ndege zetu zimeanza kufanya safari zake na nchi ya China ambapo mipango ya kuanza safari imekamilika. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, imeendelea kuboresha chaneli maalumu ya kutangaza vivutio vya utalii “*Tanzania Safari Channel”.* Vilevile, Bodi imeendelea kutumia utambulisho mpya wa kutangaza utalii Tanzania (*Tanzania Destination Brand*) ujulikanao kama “Tanzania *Unforgettable”.*

### 5.5.3.4 Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT)

***96. Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Taifa cha Utalii kimepewa jukumu la kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri katika fani ya utalii na ukarimu. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 550 katika ngazi ya Astashahada (523) na Stashahada (27). Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 900 waliopo katika mnyororo wa thamani katika kuendeleza utalii. Kazi nyingine zilizofanyika ni kukarabati miundombinu ya kutolea mafunzo katika kampasi za Temeke, Bustani na Arusha; kununua vitendea kazi; na vifaa mbalimbali vya kutolea mafunzo.

### 5.5.3.5 Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL)

***97. Mheshimiwa Spika,*** Tozo ya Maendeleo ya Utalii ilianzishwa mwaka 2013 kwa Sheria ya Utalii Na. 29 ya

mwaka 2008. Tozo hiyo imewezesha kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi, ukaguzi wa wakala wa biashara za utalii nchini, uendelezaji utalii ikiwemo utalii wa kihistoria, utoaji wa mafunzo katika fani ya utalii na ukarimu na utafiti wa watalii wanaoondoka nchini.

### 5.5.5. Sekta Ndogo ya Mambo ya Kale

***98. Mheshimiwa Spika,*** Sekta ndogo ya Mambo ya Kale inajumuisha shughuli za utafiti, utambuzi, uhifadhi, ulinzi, uendelezaji na utangazaji wa malikale. Shughuli hizo zinaongozwa na Sera ya Malikale ya mwaka 2008 na kusimamiwa na Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 na Sheria ya Makumbusho Sura 281. Aidha, shughuli hizo zinatekelezwa kupitia Idara ya Mambo ya Kale na Shirika la Makumbusho la Taifa.

#### 5.5.5.1. Masuala Mahsusi ya Sekta Ndogo ya Mambo ya Kale

**Tamasha la Urithi wa Utamaduni**

***99. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, sekta binafsi na wadau imeendelea kuimarisha mazao ya utalii ikiwa ni pamoja na kuendelea kuadhimisha Tamasha la Urithi wa Utamaduni *(Urithi Festival).* Tamasha hilo limefanyika katika mikoa 10 ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Manyara, Pwani, Kigoma, Geita, Mtwara, Mwanza, na Mjini Magharibi, Zanzibar. Kupitia tamasha hilo, wananchi walipata fursa ya kupata elimu kuhusu historia, utamaduni, malikale, lugha, chakula, mavazi, imani, mila na desturi za maeneo hayo na kutembelea vivutio vya utalii.

#### 5.5.5.2. Idara ya Mambo ya Kale

***100. Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Mambo ya Kale imepewa jukumu la kuandaa na kusimamia sera, sheria, kanuni na miongozo ya utafiti, uhifadhi na kuendeleza malikale. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara

imekarabati vituo vya taarifa na kumbukumbu vya Kumbukizi za Dkt. Livingstone Kigoma - Ujiji; Nyumba ya Kumbukizi ya Mwalimu Nyerere, Magomeni - Dar es Salaam; na makaburi ya kihistoria yaliyopo katika Kituo cha Kunduchi Dar es Salaam na Kaole, Bagamoyo. Aidha, Wizara imenunua boti ya kusafirisha watalii, watumishi na wananchi kwenda kwenye magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Vilevile, Wizara kupitia TAWA, TANAPA, TFS na NCAA imejenga nyumba moja (1) ya watumishi na watafiti katika Kituo cha Nyayo za Zamadamu – Laetoli.

### 5.5.5.3. Shirika la Makumbusho ya Taifa

***101.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Makumbusho ya Taifa limepewa jukumu la kufanya utafiti, kuhifadhi, kukusanya, kuonesha na kuelimisha umma kuhusu urithi wa utamaduni na wa asili wa Taifa. Katika kutekeleza majukumu yake Shirika limefanya utafiti katika nyanja za Jiolojia, Palaentolojia, Akiolojia na Biolojia ambapo mikusanyo 2,130 ilivumbuliwa na imeongezwa kwenye makumbusho. Aidha, utafiti wa biolojia umeendelea kufanyika ili kuainisha na kupata mikusanyo ya vipepeo na nondo wachavushao na kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu na uhifadhi wa vipepeo na nondo hao. Vilevile, Shirika kwa kushirikiana na wadau imefanya mkutano wa kitaalam wa kimataifa kuhusu mitazamo na kanuni mpya za makumbusho katika karne hii na hasa suala la mikusanyo iliyopo nje ya nchi.

***102.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limekamilisha ujenzi wa nyumba tano (5) za jamii za Wamwera (2) kutoka Mkoa wa Lindi, Wamakua (2) Mkoa wa Mtwara na Waha (1) Mkoa wa Kigoma, katika Kijiji cha Makumbusho. Aidha, onesho la kihistoria la mchango wa Tanzania katika ukombozi wa Bara la Afrika limejengwa katika Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni, Dar es Salaam. Vilevile, Shirika limekarabati majengo ya Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni

kwa ajili ya kuweka onesho jipya la kudumu la Historia ya Tanzania kabla na baada ya uhuru.

**5.5.5.4. Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale**

***103. Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale umewezesha kugharamia ukusanyaji wa taarifa za maeneo mapya ya malikale ya Lemaguru, Arusha; Kiwasihi Kigera, Mara; Mogitu, Manyara; Ndala, Tabora; na Nang'oma, Lindi ambayo yatatumika kuhuisha rejesta ya Taifa ya maeneo ya mali kale. Aidha, Mfuko umewezesha utafiti kwenye nyanja za Akiolojia tano (5) Paleontolojia tatu (3) Paleonthropoliojia mbili (2) katika mikoa ya Arusha, Manyara, Mbeya, Tanga, Mara, Lindi na Tabora na utafiti wa tunu 35.

**5.5.6. Miradi ya Maendeleo**

***104. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/2020, jumla ya **Shilingi 48,889,988,734** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi nane (8) ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,000,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 47,889,988,734** ni fedha za nje. Hadi Machi 2020, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 13,790,146,376** sawa na asilimia
28 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 671,817,955** ni fedha za ndani na **Shilingi 13,118,328,421** ni fedha za nje. Utekelezaji wa Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

**5.5.6.1. Mradi wa Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini – REGROW**

***105. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia. Mwaka 2019/2020, **Shilingi 20,300,000,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara, viwanja vya ndege na mabanda ya kupokelea wageni katika hifadhi zilizo kusini mwa Tanzania na kufanya uperembaji na tathmini ya mradi. Hadi Machi, 2020 **Shilingi 3,942,918,771** zimetolewa na

kutumika. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 230,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 3,712,918,771** ni fedha za nje.

### 5.5.6.2. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi Ujangili

***106. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa na Serikali kwa kutumia fedha za ndani. Mwaka 2019/2020, **Shilingi 500,000,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya kukarabati nyumba 58 katika mapori ya akiba; kuboresha miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na ofisi katika mapori ya akiba; na kuwajengea uwezo askari wanyamapori katika kulinda na kusimamia rasilimali za wanyamapori. Hadi Machi, 2020 **Shilingi 300,000,000** zimetolewa na kutumika.

### 5.5.6.3. Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili

***107. Mheshimiwa Spika,*** mradi unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali za Ujerumani na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi unatekelezwa katika halmashauri za wilaya za Ngorongoro na Serengeti na TAWA. Mradi unalenga kuwezesha jamii kushiriki katika usimamizi endelevu wa maliasili. Mwaka 2019/2020, jumla ya **Shilingi 13,864,220,734** fedha za nje ziliidhinishwa. Hadi Machi 2020, **Shilingi 2,179,400,000** zimetolewa na kutumika.

### 5.5.6.4. Mradi wa Kuendeleza Misitu ya Hifadhi ya Mazingira Asilia

***108. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP). Aidha, mradi huu unatekelezwa kwenye misitu sita(6) ya hifadhi ya mazingira asilia ya Chome, Magamba, Mkingu, Minziro, Udzungwa na Rungwe. Lengo la mradi ni kuwezesha Wizara, halmashauri za wilaya na asasi zisizokuwa za Serikali kuboresha usimamizi wa sheria za mazingira ili

kulinda mifumo ikolojia, na bioanuwai kwa ajili ya ustawi na usimamizi wa rasilimali za misitu. Mwaka 2019/2020 **Shilingi 4,294,680,000** ziliidhinishwa. Hadi Machi, 2019 **Shilingi 1,332,494,650** fedha za nje zimetolewa na kutumika.

**5.5.6.5. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi za Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki**

***109. Mheshimiwa Spika,*** mradi unatekelezwa kwa fedha za ndani kwa lengo la kuwezesha taasisi za mafunzo na utafiti zilizo chini ya Idara ya Misitu na Nyuki kutekeleza majukumu yake. Mwaka 2019/2020, **Shilingi 420,058,000** ziliidhinishwa. Hadi Machi, 2020 **Shilingi 141,817,955** zimetolewa na kutumika.

**5.5.6.6. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii katika Kusimamia Misitu kwa Tija na Misingi Endelevu**

***110. Mheshimiwa Spika,*** mradi unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali za Ubeligiji na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi huu unatekelezwa katika wilaya za Uvinza, Kigoma, Kasulu, Kibondo, Kakonko na Buhigwe. Mwaka 2019/2020 **Shilingi 4,073,260,000** fedha za nje ziliidhinishwa. Hadi Machi, 2020 **Shilingi 1,150,665,000** fedha za nje zimetolewa na kutumika.

**5.5.6.7. Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu – FORVAC**

***111. Mheshimiwa Spika,*** mradi unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali za Ufini na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi huo unalenga kuimarisha uwezo wa wananchi kusimamia rasilimali za misitu na kuongeza thamani ya mazao ya misitu. Mradi unatekelezwa katika mikoa ya Tanga, Lindi, Mtwara na Ruvuma. Katika mwaka 2019/2020, **Shilingi 4,742,850,000** fedha za nje ziliidhinishwa. Hadi Machi, 2020 **Shilingi 4,742,850,000** fedha za nje zimetolewa na kutumika.

### 5.6 Utekelezaji wa Majukumu ya Kimkakati

***112.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutekeleza Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere ulioko kwenye Hifadhi ya Taifa Nyerere. Katika kutekeleza mradi huo, Wizara ilipewa jukumu la kusafisha eneo ambalo bwawa la kuzalisha umeme linajengwa na kufanya ulinzi kwa watumishi na wafanyakazi katika eneo husika. Katika kutekeleza kazi hizo, Wizara kupitia TANAPA na TAWA imeendelea kuimarisha ulinzi kwa kupeleka askari 108 na magari matano (5) ya doria. Aidha, Wizara kupitia TAFORI imefanya tathmini na kutoa ushauri kuhusu athari za kiikolojia ambazo zinaweza kutokea kwenye uoto wa mimea katika njia ya kusafirishia umeme (400 kV transmission line) kutoka kwenye eneo la uzalishaji hadi kituo kidogo cha kupoozea umeme kilichopo eneo la Chalinze, Bagamoyo. Tathmini imebaini uwepo wa aina nne (4) za spishi zilizo hatarini kutoweka ambazo ni *Lannea shweinfurthii, Millettia micansa, Rytiginia bugoyensis na Xylotheca tettensi.* Vipando vya miti hiyo vimekusanywa na kuoteshwa katika Kituo cha Utafiti wa Misitu Kibaha kwa utafiti zaidi wa kuendeleza uhifadhi wake.

***113.*** ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kuwa mwaka 2016, Serikali ilitoa Tamko la kusitisha biashara ya kukamata na kusafirisha wanyamapori hai nje ya nchi kwa muda wa miaka mitatu (3). Katika kipindi hicho Wizara ilifanya ukaguzi wa mazizi yote ya wafanyabiashara ya nyara ili kubaini aina na idadi ya wanyamapori waliopo kwenye mazizi hayo. Kwa sasa Wizara imekamilisha utaratibu wa kuwarudishia wafanyabishara hao fedha walizolipia ada mbalimbali za Serikali ambapo jumla ya Shilingi 173,289,430.60 zitalipwa.

### 5.7 Changamoto na Utatuzi Wake

#### 5.7.1 Changamoto

***114.*** ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara

katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 ni pamoja na: kuwepo uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa na shoroba; kuongezeka kwa migongano kati ya binadamu na wanyamapori; uhaba wa watumishi pamoja na wafanyakazi wenye ujuzi na utaalamu katika fani mbalimbali, hususan ukarimu; kuharibika kwa miundombinu ya barabara kutokana na mvua nyingi zilizonyesha, hali iliyosababisha ugumu wa kufikika kwenye baadhi ya maeneo mbalimbali yenye vivutio vya utalii. Aidha, kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Corona (COVID-19) duniani fursa za kutangaza utalii hazitakuwa na matokeo chanya kwa sababu ya zuio la wageni kusafiri kutoka nchi moja hadi nyingine. Hali hiyo itasababisha kupungua kwa idadi ya watalii, mapato na kuathiri soko la ajira na mnyororo wa thamani katika sekta ya utalii.

### 5.7.2 Utatuzi wa Changamoto

***115. Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Wizara imeendelea kufanya mapitio ya sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali; na kushirikisha wadau katika kuhifadhi maliasili na malikale na kuboresha miundombinu katika maeneo yaliyohifadhiwa na vivutio vya utalii. Aidha, Wizara imeimarisha ulinzi kwa wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu, kuhamasisha na kutekeleza mikakati ya upandaji miti, kuanzisha na kuendeleza viwanda vya mazao ya misitu na nyuki, kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili na malikale. Vilevile, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau katika kuendeleza na kuimarisha vyuo vya mafunzo ya utalii na kuendelea kuwasiliana na mamlaka husika ili kupata vibali vya ajira za watumishi kuhusu utangazaji utalii, Wizara itatumia njia za kielekitroniki ikiwemo mitandao ya kijamii kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii kwa lengo la kuhamasisha kutembelea nchini baada ya COVID-19 kudhibitiwa.

## 6.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

***116.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na miongozo mingine, umezingatia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021 – 2022/2023, majukumu ya Wizara, Sera, Mpango Mkakati wa Wizara (2016/17 - 2020/21), Mipango Mikakati ya Taasisi zilizopo chini ya Wizara, maelekezo ya viongozi wa Serikali na mikataba ya kikanda na kimataifa.

### 6.1 Ukusanyaji Maduhuli

***117.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inakadiria kukusanya **Shilingi 65,256,218,761** kutoka katika vyanzo vya idara, mifuko na taasisi zilizo chini yake. Kati ya fedha hizo, idara zitakusanya **Shilingi 22,657,242,000**; taasisi zinazopata ruzuku zitakusanya **Shilingi 18,846,563,910;** na Mifuko ya uhifadhi ya TWPF na TaFF itakusanya **Shilingi 23,752,412,851**. Aidha, Mashirika ya TANAPA, NCAA, TAWAna TFS yanakadiria kukusanya **Shilingi 738,230,093,590.** Kati ya fedha hizo, TANAPA itakusanya **Shilingi 363,899,596,000,** NCAA **Shilingi 162,663,179,000,** TAWA **Shilingi 58,063,935,590** na TFS **Shilingi 153,603,383,000.** Mashirika hayo hukusanya maduhuli kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali, mifuko ya uhifadhi na maendeleo ya utalii.

### 6.2 Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

***118.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 114,593,952,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 69,573,850,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 45,020,102,000** miradi ya maendeleo. Makadirio ya matumizi ya kawaida yanajumuisha mishahara **Shilingi 50,852,545,000** na matumizi mengineyo **Shilingi 18,721,305,000.** Aidha, **Shilingi 45,020,102,000** zitatumika kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo,

**Shilingi 44,320,102,000** zitatoka kwa washirika wa maendeleo na **Shilingi 700,000,000** zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali**.**

### 6.3 Kazi Zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake

#### 6.3.1 Sekta Ndogo ya Wanyamapori

##### 6.3.1.1 Idara ya Wanyamapori

***119. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Wanyamapori, kukamilisha mapitio ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009, Sheria ya TANAPA, NCAA na TAWIRI; na kuandaa Sheria ya kuanzisha TAWA. Aidha, Wizara itafanya mapitio ya kanuni za Utalii wa Picha na Matumizi ya Uvunaji wa Wanyamapori na kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Jeshi Usu na kuwezesha watumishi wa Idara ya Wanyamapori na Misitu kushiriki katika mafunzo hayo. Vilevile, Wizara itaendelea kuhakiki matukio ya athari zinazosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu na kulipa kifuta machozi na kifuta jasho kwa wananchi watakaoathiriwa na wanyamapori hao. Pia, Wizara itaendelea kuwalinda wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na kukamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Wanyamapori Wakali na Waharibifu.

***120. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuratibu upandishaji hadhi mapori tengefu ya Inyonga, mbuga ya Wembere na misitu ya Litumbandyosi - Gesimazowa kuwa mapori ya akiba na kuanzisha Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) Kilosa Moani. Aidha, Wizara itafanya mapitio ya mpango wa kanda ya usimamizi wa maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori na Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara.

### 6.3.1.2 Shirika la Hifadhi za Taifa

***121.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ulinzi na usimamizi wa hifadhi, Shirika litaendesha siku doria 358,000 na kuwezesha operesheni 56 za kuzuia ujangili na kununua silaha 200, mahema 75, sare za uwandani na ofisi kwa watumishi. Aidha, Shirika litajenga: uzio wa faru wenye urefu wa kilometa 14 katika Hifadhi ya Taifa Burigi - Chato; ghala la kuhifadhia silaha katika Hifadhi ya Saadani; na minara mine (4) ya usalama katika hifadhi za Taifa Mkomazi na Serengeti. Vilevile, Shirika litaendelea kutumia vifaa vya teknolojia ya kisasa vikiwemo ndege ndogo zisizo na rubani (*drones)*, kamera zinazotambua joto la binadamu (*thermal image cameras* 93*)*, miwani ya kuona masafa marefu wakati wa usiku (*long range night goggles)* katika hifadhi za Taifa za Ruaha, Tarangire, Mikumi, Serengeti na Kisiwa cha Rubondo. Pia, Shirika litadhibiti mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 972 na kuotesha miti ya asili 100,400 katika hifadhi za Taifa za Arusha, Kisiwa cha Rubondo, Ziwa Manyara na Tarangire.

***122.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa maji kwa wanyamapori wakati wa kiangazi, Shirika litajenga mabwawa 15 yenye jumla ya mita za ujazo 51,447 katika hifadhi za Taifa za Saadani, Ruaha, Mkomazi, Katavi na Mikumi. Aidha, Shirika litawezesha chanjo za mifugo kwenye vijiji vinavyopakana na hifadhi ili kuzuia maambukizi ya magonjwa na kuanzisha vikundi 116 vya uhifadhi kupitia mpango wa ujirani mwema. Vilevile, elimu ya uhifadhi itatolewa katika vijiji 573 vinavyozunguka hifadhi zote za Taifa na kuwezesha miradi ya ujirani mwema ya maji, elimu na afya katika vijiji 17.

***123.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaanzisha maeneo maalum ya utalii katika hifadhi za Taifa za Ruaha, Katavi, Nyerere, Burigi - Chato na Kitulo na kuanzisha kanda za kitalii katika hifadhi zinazotembelewa na wageni wengi. Shirika litaendelea kukamilisha taratibu za kuanzisha

utalii wa kutumia gari ya kwenye kamba (cable cars) katika Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro. Aidha, Shirika litaanzisha bidhaa mpya za utalii ikiwa ni pamoja na utalii wa kiberenge, kupanda farasi, kupanda puto na boti katika hifadhi za Taifa zenye kutembelewa na watalii wachache za Mkomazi na Mahale na hifadhi za Taifa mpya za Burigi - Chato na Nyerere, Mto Ugalla na Kigosi. Vilevile, Shirika litatenga maeneo 53 ya kujenga loji na mahema ya kudumu ya wageni katika hifadhi za Taifa za: Mikumi (5), Mkomazi (10), Tarangire (5), Kitulo (5), Ibanda - Kyerwa (6), Rumanyika – Karagwe (3) na Burigi - Chato (19). Pia, Shirika litajenga hoteli ya watalii yenye vitanda 50 katika Hifadhi ya Taifa Katavi na kujenga malazi ya gharama nafuu yenye jumla ya vitanda 321 kwa ajili ya watalii wa ndani katika hifadhi za Taifa Kisiwa cha Rubondo (92), Mikumi (8), Burigi – Chato (150) na Saadani (71).

***124.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaendelea na ujenzi wa uwanja wa mchezo wa gofu eneo la Fort Ikoma katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Uwanja wa Ndege Mugumu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti. Aidha, Shirika litajenga nyumba 11 za watumishi katika hifadhi za Taifa za: Kilimanjaro (3), Kitulo (2), Mkomazi (1), Serengeti (2), Rubondo (2) na Mahale (1). Vilevile, Shirika litajenga maeneo maalum ya utalii wa gari - nyumba (caravan) katika hifadhi za Taifa za Katavi, Nyerere na Ruaha. Pia, Shirika litajenga kivuko na kununua boti ya kitalii katika Ziwa Victoria itakayotoa huduma za utalii wa maji katika hifadhi za Taifa za Rubondo, Saanane, Burigi - Chato na Serengeti (Ghuba ya Speke).

***125.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika litajenga barabara zenye urefu wa kilometa 444 katika Hifadhi 21 na kukarabati barabara zenye urefu wa kilometa 6,580 katika hifadhi zote za Taifa. Aidha, Shirika litajenga madaraja mapya mawili (2) katika hifadhi za Taifa Tarangire na Kitulo na kukarabati njia za kutembea watalii zenye urefu wa kilometa 316 katika hifadhi za

Taifa Arusha, Kilimanjaro, Udzungwa, Rumanyika na Karagwe. Vilevile, Shirika litachimba visima virefu 18 vya maji na kujenga kilometa 10 kati ya kilometa 13 za mfumo wa maji katika Hifadhi ya Taifa Ruaha. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na kununua magari 23, vifaa na mitambo ya barabara nane (8), ununuzi wa helikopta moja (1) kwa ajili ya kuimarisha shughuli za doria katika Hifadhi ya Taifa Nyerere, injini za boti sita (6), pikipiki 11 na mashine ya kuchimba visima vya maji.

### 6.3.1.3 Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

***126.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka itaendelea kuboresha miundombinu kwa kukarabati barabara, viwanja vya ndege ndani ya eneo la hifadhi, vyoo na kujenga vyoo vipya. Aidha, Mamlaka itaboresha huduma za kijamii kwa kuendeleza miradi ya miundombinu ya maji, elimu, ufugaji nyuki na chakula kwa wakazi waishio ndani ya eneo la hifadhi. Pia, Mamlaka itakamilisha mapitio ya matumizi mseto ya ardhi, sheria iliyoanzisha Mamlaka na Mpango wa Jumla wa Matumizi ya Eneo. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na kuimarisha mfumo wa Jeshi Usu, kuibua na kutangaza vivutio vya utalii, kuhamisha makao makuu ya Mamlaka kwenda Mji wa Karatu na kununua mitambo na mashine za kuwezesha ujenzi.

### 6.3.1.4 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania

***127.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka itafanya siku doria 337,517 katika mapori ya akiba, mapori tengefu, maeneo ya ardhioevu yenye umuhimu wa kimataifa chini ya Mkataba wa Ramsar na WMAs; kuimarisha shughuli za intelijensia, vikosi maalum vya ulinzi, matumizi ya teknolojia; na kutoa mafunzo ya Jeshi Usu kwa watumishi takriban 300. Aidha, Mamlaka itaendelea kuimarisha ulinzi wa wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na kununua

magari nane (8) ya doria. Vilevile, Mamlaka itaanza ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu katika Jiji la Dodoma na kujenga nyumba ya watumishi katika Pori la Akiba Lukwati - Piti. Pia, Mamlaka itaandaa mipango ya usimamizi ya jumla ya mapori ya akiba ya Lukwati - Piti, Pande na Maswa na kufanya mapitio ya mpango shirikishi wa usimamizi wa Magofu ya Kilwa Kisiwani.

***128.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka itafungua mtandao wa barabara za utalii zenye urefu wa kilometa 205 katika mapori ya akiba ya Mpanga Kipengere, Swagaswaga, Mkungunero na Pande pamoja na kujenga madaraja madogo 11, daraja moja (1) kubwa na *drifts* sita (6) katika mapori ya akiba ya Mpanga Kipengere, Mkungunero, Lukwika -Lumesule na Msanjesi. Aidha, Mamlaka itajenga njia ya kutembea watalii yenye urefu wa mita 150 kuelekea kwenye maporomoko ya maji ya Lyamakunohila katika Pori la Akiba Mpanga Kipengere na njia za kutembea watalii katika eneo la kihistoria la Magofu ya Kilwa Kisiwani. Vilevile, Mamlaka itajenga mabanda ya kulala wageni na eneo la mapokezi katika eneo la kihistoria la Kilwa Kisiwani, mageti manne (4) ya kitalii katika mapori ya akiba ya Mpanga Kipengere, Swagaswaga na Selous pamoja na kambi mbili (2) za watalii katika mapori ya akiba ya Mpanga Kipengere na Swagaswaga.

***129.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka itashiriki katika maonesho ya kimataifa ya uwindaji wa kitalii yatakayofanyika nchini Marekani (*Safari Club International na Dallas Safari Club Conventions*). Aidha, Mamlaka itaendelea kutoa gawio la mapato yanayotokana na utalii kwa WMAs, vijiji na halmashauri za wilaya kwa ajili ya uhifadhi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

#### 6.3.1.5 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania

***130.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi itaidadi wanyamapori nchini katika mifumo ya ikolojia ya Serengeti, Tarangire

- Manyara, Moyowosi - Kigosi, Burigi - Chato na Hifadhi ya Taifa Saadani. Kazi nyingine ni kutathmini shoroba za wanyamapori nchini na kuzipanga kulingana na umuhimu katika uhifadhi na ustawi wa jamii. Aidha, Taasisi itaanza ujenzi wa jengo la Makao Makuu na kuanzisha Kituo cha Utafiti wa Wanyamapori Kanda ya Kusini.

#### 6.3.1.6 Vyuo vya Taaluma ya Wanyamapori

##### (i) Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka

***131.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo kitaendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada, Stashahanda na Shahada katika fani ya uhifadhi wanyamapori na utalii pamoja na kozi fupi za waongoza utalii. Aidha, Chuo kitajenga madarasa, uzio na kukarabati barabara za ndani ya chuo na hosteli za wanafunzi. Vilevile, Chuo kitanunua magari mawili (2) kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

##### (ii) Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi

***132.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi itaendelea kutoa mafunzo ya Astashahada ya Uhifadhi wa Wanyamapori na Himasheria kwa kudahili wanafunzi 300. Aidha, Taasisi itaimarisha utoaji wa mafunzo kwa vitendo, kukamilisha ujenzi wa maktaba, kununua samani na kuandaa kanuni za uendeshaji wa Taasisi.

##### (iii) Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu – Sekamaganga

***133.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo kitaendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 130 wakihusisha askari wanyamapori wa vijiji 80 ambao wanatumika kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu na kufanya doria katika maeneo ya WMAs, viongozi na wajumbe wa kamati za maliasili za vijiji 20 na waongoza watalii 30. Aidha, Kituo kitakamilisha taratibu za kuanzisha kozi ya

Astashahada ya Awali ya Waongoza Watalii, kujenga maabara ya sayansi na kutengeneza tovuti ya Kituo. Vilevile, Kituo kitanunua basi dogo, kukarabati majengo na kununua samani kwa ajili ya maktaba. Pia, kituo kitaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa WMA's za Mbarang'andu, Kimbanda na Kisungule (Namtumbo), Chingoli na Nalika (Tunduru), Mchimalu (Nanyumbu), Ndonda (Nachingwea) na Mungata (Rufiji).

### 6.3.1.7 Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania

***134.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko utawezesha uhakiki na ulipaji wa kifuta machozi na kifuta jasho kwa wananchi wanaopata madhara kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, Mfuko utawezesha utafiti, kuidadi wanyamapori, shughuli za mafunzo na operesheni maalum za kuzuia ujangili. Vilevile, Mfuko utawezesha kazi za kupandisha hadhi maeneo yaliyohifadhiwa, mapitio ya sera, sheria na kanuni, kutoa elimu kwa wananchi na usimamizi wa nyara za Serikali.

### 6.3.2 Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki

### 6.3.2.1 Idara ya Misitu na Nyuki

***135.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya Mwaka 1998, kuendelea na mapitio ya Sheria ya Misitu Sura 323 na Sheria iliyoanzisha TAFORI Sura 270. Aidha, Wizara itafanya utafiti wa kubaini mchango halisi wa sekta ya misitu na nyuki kwenye Pato la Taifa na kuandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Manzuki na Elimu Ugani. Vilevile, Wizara itawezesha mikutano minne (4) ya Kamati ya Ushauri wa Misitu (NAFAC) na mikutano minne (4) ya Kamati ya Ushauri wa Ufugaji Nyuki (NABAC). Kazi nyingine zitakazofanyika ni kutayarisha mwongozo wa uandaaji wa Mpango wa Usimamizi wa Mashamba ya Miti, kuandaa Mkakati wa Kutoa Huduma za Ugani kuhusu Misitu, kuandaa Mwongozo wa Kuongeza Thamani ya

Mazao ya Nyuki na kutoa mafunzo kwa ajili ya vyama vya ushirika wa wafugaji nyuki.

#### 6.3.2.2 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

***136. Mheshimiwa Spika,*** Wakala utaendelea kuhudumia mashamba 23 ya miti yenye ukubwa wa hekta 518,089. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuzalisha tani 17 za mbegu bora za miti, kuotesha miche 32,510,900, kupanda miti kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 8,188, kupalilia hekta 42,612, kupogoa miti hekta 13,805 na kupunguza miti hekta 6,238. Aidha, Wakala utaanzisha shamba jipya la miti lenye ukubwa wa hekta 3,000 katika Wilaya ya Nzega na kuongeza hifadhi nne (4) za misitu ya asili zenye hekta 37,000 katika wilaya mbili (2) za Babati (Salame) na Simanjiro (Lalatema, Landrokesi na Lendanai). Vilevile, Wakala utakamilisha taratibu za kuhifadhi kisheria eneo la hifadhi ya nyuki lenye ukubwa wa hekta 21,790 katika Wilaya ya Chunya na hekta 263,449 za misitu katika wilaya za Hanang, Ikungi, Mufindi, Ileje na Momba. Pia, Wakala utaimarisha uhifadhi wa misitu sita (6) yenye hekta 23,046 iliyokabidhiwa na halmashauri za wilaya za Nyasa na Mbinga zilizokuwa na changamoto ya uvamizi.

***137. Mheshimiwa Spika,*** Wakala utaandaa mipango ya usimamizi ya misitu 40 yenye ukubwa wa hekta milioni 1.36, kukamilisha mipango 45 ya usimamizi ya misitu na kuendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuendeleza Jeshi Usu. Aidha, Wakala utasafisha njia za kudhibiti moto kwenye misitu ya asili na mashamba ya miti yenye urefu wa kilometa 5,819; kujenga uwezo wa vikosi 15 vya wazima moto vyenye jumla ya watu 282; kujenga minara miwili (2) na kukarabati minara 17 ya kufuatilia matukio ya moto. Vilevile, kampeni za udhibiti moto zitafanyika kwenye vijiji 316 vinavyozunguka misitu 55 na kuandaa mipango nane (8) ya usimamizi wa moto. Pia, Wakala utafanya mikutano ya vijiji 52 ya kuelimisha kamati za maliasili za vijiji 208, shule 10 na washiriki 1,290 wanaojihusisha na biashara ya mazao ya misitu na nyuki.

***138. Mheshimiwa Spika,*** Wakala utapandisha hadhi misitu 10 ya hifadhi yenye ukubwa wa hekta 25,862 kuwa misitu ya hifadhi ya mazingira asilia. Aidha, Wakala utaandaa na kutekeleza mpango wa uendelezaji wa miundombinu ya utalii katika misitu ya hifadhi na kuimarisha kambi 35 za kupumzikia watalii, na kuzitangaza. Vilevile, njia za kutembea watalii zenye urefu wa kilometa 355 zitakarabatiwa, maeneo ya burudani manne (4) yataanzishwa na kujenga maeneo matatu(3) ya kuona mandhari.

***139. Mheshimiwa Spika,*** Wakala utahakiki mipaka ya misitu ya hifadhi 58, hifadhi za nyuki tatu (3) na kuimarisha mipaka ya misitu ya hifadhi 169 kwa kupima upya kilometa 363, kusafisha kilometa 484, kuweka mabango 2,341 na vigingi 2,016 katika mipaka mipya. Aidha, Wakala utaandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji 20 vinavyozunguka misitu ya hifadhi ili kuondoa migogoro kati ya Wakala na vijiji.

***140. Mheshimiwa Spika,*** Wakala utachangia shughuli za maendeleo ya jamii zinazozunguka hifadhi za misitu na nyuki kwa kutoa miche ya miti 14,851,120 na vifaa vya ufugaji nyuki ikiwemo mizinga 1,000. Aidha, Wakala utajenga hosteli moja (1) na kukarabati madarasa katika shule za msingi na sekondari 12; kuchangia madawati 300, vifaa vya ujenzi na kukarabati ofisi za vijiji vitatu (3); na kukarabati na kujenga miundo mbinu ya maji. Vilevile, Wakala utaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa jamii juu ya ufugaji nyuki, uanzishaji bustani za miti na upandaji miti na kuwezesha uanzishaji wa hifadhi za nyuki za kijiji zenye ukubwa wa hekta 5,000.

***141. Mheshimiwa Spika,*** Wakala utaanzisha kampuni tanzu itakayosimamia miradi ya kuongeza thamani na kuzalisha bidhaa mseto za mazao ya misitu na nyuki. Kampuni hiyo itasimamia miradi minne (4) ya majaribio ya uzalishaji mizinga (Kondoa), uchakataji wa mazao ya misitu (Shamba la Miti Meru), uchakataji na ufungishaji

wa asali (Manyoni), na uzalishaji wa vimbaka - *tooth picks* (Shamba la Miti Ruvu Kaskazini).

***142.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala utaendelea kuhudumia manzuki 146 na kuanzisha manzuki mpya 21 ambazo zinatarajiwa kuzalisha tani 91 za asali na tani 10 za nta. Aidha, Wakala utaanzisha vikundi 86 vya ufugaji nyuki na kutoa elimu ya ufugaji bora wa nyuki kwa wafugaji 1,190.

***143.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala utajenga ofisi 12, vituo 15 vya ulinzi ndani ya misitu na kukarabati majengo 63 na mifumo 45 ya maji. Aidha, Wakala utakarabati vituo sita (6) vya mambo ya kale vya Mji Mkongwe na Magofu ya Kaole (Bagamoyo), Tembe la Kwihara na Jengo la Afya (Tabora), Michoro ya Miambani ya Kolo (Kondoa) na Magofu ya Tongoni (Tanga). Pia, Wakala utanunua magari madogo 31, malori mawili (2), pikipiki 61 na mtambo mmoja (1).

***144.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala utawezesha watumishi 1,632 kupata mafunzo ya muda mfupi (565), muda mrefu (270) na mafunzo ya Jeshi Usu (797). Aidha, Wakala utashiriki maonesho na matukio 12 ya kitaifa na kimataifa; na utandaa na kurusha vipindi 45 vya televisheni, 79 vya redio na makala 14 kuhusu uhifadhi.

**6.3.2.3 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania**

***145.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi itafanya utafiti kuhusu ubora wa mbao kutoka kwenye misitu mbalimbali nchini, nishati ya mkaa kutoka kwenye miti inayokua haraka na njia mbadala za kuzalisha nishati ya mkaa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Tafiti nyingine zitakazofanyika ni kubaini matumizi ya maji kwa miti ya kigeni na madhara ya shughuli za binadamu katika vyanzo vya maji ili kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya maeneo sahihi ya kupanda miti hiyo. Vilevile, Taasisi itaendelea kufanya utafiti juu ya mtawanyiko na madhara ya viumbe vamizi kwenye uzalishaji na

bioanuai katika misitu. Pia, Taasisi itaendelea kufanya utafiti unaohusu uvunaji wa utomvu kwenye miti ya misindano ili kubaini umri sahihi wa kuvuna utomvu, madhara kwenye ukuaji wa miti na ubora wa mbao. Aidha, Taasisi itaendelea kuandaa mwongozo wa kufanya utafiti wa misitu na nyuki nchini, kununua vitendea kazi na kuboresha miundombinu. Katika kupanua wigo wa upatikanaji wa mazao ya misitu, Taasisi itaanzisha mashamba ya majaribio mapya manne (4) ya miti ya asili (2) na miti ya kigeni (2).

### 6.3.2.4 Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki

***146.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Viwanda vya Misitu kitadahili wanafunzi 250, Chuo cha Misitu Olmotonyi 1,000 na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki wanafunzi 400. Aidha, Chuo cha Viwanda vya Misitu kitakarabati ofisi mbili (2), madarasa mawili (2) na bwalo la chakula. Vilevile, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kitajenga kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki. Pia, Chuo kitaendelea na uzalishaji wa malkia kwenye vituo vya Manyoni (Singida), Handeni (Tanga) na Ukimbu (Kigoma). Lengo la Serikali ni kuhakikisha upatikanaji wa wataalam wenye weledi stahiki kwa ajili ya kusimamia sekta ndogo ya misitu na nyuki ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika pato la Taifa.

### 6.3.2.5 Mfuko wa Misitu Tanzania

***147.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko utaendelea kuwezesha ujenzi wa viwanda vya kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki, ununuzi na usimikaji wa mitambo na vifaa vingine muhimu kwa ajili ya viwanda vinne (4) vya kuchakata na kufungasha asali. Kazi nyingine zitakazofanywa na Mfuko ni kuwezesha miradi mipya mitano (5) na miradi 79 inayoendelea ya ufugaji nyuki na ujenzi wa vituo vitano (5) vya ukusanyaji wa mazao ya nyuki.

***148. Mheshimiwa Spika,*** Mfuko utawezesha uanzishwaji wa vitalu na upandaji miti katika shule 60 katika wilaya 30 za mikoa saba (7) ya nyanda kame, kuzalisha miche ya mbao na matunda milioni 1.2, kupanda miti hekta 730 katika mashamba ya Biharamulo, Pagale na Longuza. Aidha, Mfuko utagharamia mafunzo ya Stashahada kwa wanafunzi 15 na Astashahada wanafunzi 12 katika vyuo vya misitu na ufugaji nyuki; na kuwezesha TAFORI kuanzisha mfumo wa kielekitroniki wa usimamizi na uratibu wa utafiti wa misitu na nyuki. Vilevile, Mfuko utawezesha kurusha vipindi 24 vya redio na 12 vya televisheni kuhusu uhamasishaji, uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali ya misitu.

### 6.3.3 Sekta Ndogo ya Utalii

#### 6.3.3.1 Idara ya Utalii

**149. Mheshimwa Spika,** Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Utalii ya mwaka 2008 na kuandaa Programu ya Taifa ya Uendelezaji Utalii. Aidha, itabainisha vivutio vipya vya utalii na maeneo ya uwekezaji katika mikoa ya Mbeya, Geita, Simiyu, Mwanza, Njombe na Morogoro. Vilevile, Wizara itaandaa majukwaa ya uwekezaji ili kuhamasisha wawekezaji katika biashara za utalii ikiwemo huduma za malazi. Pia, Wizara itafanya mikutano ya kamati ya uwezeshaji wa masuala ya utalii kwa kushirikisha wadau mbalimbali na mikutano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na kuendelea kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora wa nyota, kufanya uhakiki na ukaguzi wa wakala wa biashara za utalii pamoja na kufanya utafiti wa watalii wanaoondoka nchini. Aidha, Wizara itafuatilia upokeaji wa wageni nchini na katika maeneo ya malazi na utalii kwa kutumia mfumo wa kielekitroniki wa usajili wa wageni.

### 6.3.3.2 Bodi ya Utalii Tanzania

***150. Mheshimiwa Spika,*** Bodi itaendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kwa kushiriki maonesho ya utalii katika masoko ya kimkakati katika nchi mbalimbali zikiwemo China, India, Urusi, Israeli, ukanda wa Afrika na Falme za Kiarabu. Katika hatua nyingine, ziara za utangazaji utalii zitafanyika katika masoko ya Bara la Asia, Ulaya na Australia. Aidha, Bodi itazindua video mpya ya utangazaji utalii na kuisambaza kwenye vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii ndani na nje ya nchi. Vilevile, Bodi itaendelea kutangaza mazao mapya ya utalii ikiwa ni pamoja na utalii wa michezo, utalii wa mvinyo, utalii wa madini na utalii wa kwenye maji. Pia, Bodi itaimarisha utangazaji wa mazao ya utalii ikiwemo utalii wa mikutano, utalii wa utamaduni na utalii wa meli.

***151. Mheshimiwa Spika,*** Bodi itaweka matangazo ya utalii wa Tanzania kwenye masoko ya kimkakati nchi za nje na kuendelea kuteua mabalozi wa hiari wa utalii katika masoko hayo. Aidha, Bodi itaendelea kutumia makundi ya watu maarufu kama wasanii wa muziki na waigizaji sinema wa ndani na wa kimataifa katika utangazaji utalii. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kuweka mabango ya kutangaza utalii katika majiji ya Dar es Salaam, Arusha na Mwanza pamoja na viwanja vya ndege vya JNIA, Dodoma na Mwanza; na kuendelea kuandaa Onesho la Swahili *International Tourism Expo* (S!TE) 2020. Vilevile, Bodi itaendelea kuhamasisha wadau kuhusu matumizi ya utambulisho mpya wa Tanzania kiutalii (*Tanzania Unforgettable*) na kuandaa tuzo za utalii zinazolenga kuwatambua na kuwapa hati za shukrani watanzania na raia wa kigeni wanaojitolea kutangaza utalii ndani na nje ya nchi.

***152. Mheshimiwa Spika,*** Bodi itaendelea kutangaza utalii kupitia Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), Nanenane, Kili/Karibu *Fair*, Siku ya Utalii Duniani na Karibu Utalii Kusini. Maonesho

mengine yatakayofanyika ni Tamasha la Mvinyo Dodoma, GLITE, *East Africa Trade Fair* na Lamadi Utalii *Festival*. Aidha, Wizara itatoa elimu kwa umma kuhusu utalii wa ndani kupitia vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na Chaneli maalum ya kutangaza utalii "Tanzania *Safari Channel*" na mitandao ya kijamii.

#### 6.3.3.3 Chuo cha Taifa cha Utalii

**153. Mhesimiwa Spika,** Chuo kitadahili wanafunzi 670 katika ngazi ya astashahada na wanafunzi 78 ngazi ya stashahada na kutoa mafunzo kwa washiriki 300 katika mnyororo wa utalii. Aidha, Chuo kitaanzisha kampasi mpya ya Mwanza na programu ya mafunzo ya utalii katika ngazi ya cheti kampasi ya Arusha. Vilevile, Chuo kitajenga miundombinu ya kutolea mafunzo katika kampasi ya Arusha na kufanya ukarabati katika kampasi ya Bustani, Temeke na Arusha. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kuendelea kufanya utafiti na kutoa ushauri katika fani ya utalii na ukarimu, kufanya mapitio na kuhuisha muundo wa Chuo.

### 6.3.4 Sekta Ndogo ya Mambo ya Kale

#### 6.3.4.1 Idara ya Mambo ya Kale

***154. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itafanya tathmini ya hali ya uhifadhi wa maeneo matano (5) ya malikale, kuandaa mpango kabambe na miongozo ya uhifadhi na usimamizi wa maeneo ya malikale na kuhuisha rejesta ya maeneo ya malikale. Kazi nyingine zitakazofayika ni upimaji wa mipaka ya vituo vitano (5) vya mambo ya kale, kuratibu maadhimisho ya Tamasha la Mwezi wa Urithi wa Utamaduni, Kumbukizi ya Vita vya Majimaji na Siku ya Kimondo Duniani.

#### 6.3.4.2 Shirika la Makumbusho ya Taifa

***155. Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaendeleza maeneo 20 ya malikale; kuboresha vituo saba (7) vya makumbusho ya Taifa; na kujenga Onesho la Historia ya

Tanzania kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni, wakati wa harakati za kudai uhuru na Tanzania ikiwa huru. Aidha, Shirika litafungua masoko ya bidhaa za sanaa katika Makumbusho ya Azimio la Arusha, Kijiji cha Makumbusho - Dar es Salaam na kuboresha Jukwaa la Sanaa, Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni. Vilevile, Shirika litakusanya taarifa za kihistoria za Marais ili kuanzisha Makumbusho ya Marais itakayojengwa Dodoma.

## 6.4 Miradi ya Maendeleo

***156.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 45,020,102,000** kutekeleza miradi sita (6) ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 44,320,102,000** ni fedha za nje na **Shilingi 700,000,000** ni fedha za ndani.

**Miradi ya maendeleo itakayotekelezwa ni: -**

(i) Mradi wa Kuendeleza Utalii Ukanda wa Kusini (REGROW);
(ii) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi Ujangili;
(iii) Mradi wa Kuzuia na Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara;
(iv) Mradi wa Panda Miti Kibiashara;
(v) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki; na
(vi) Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu (FORVAC).

## 7.0 SHUKRANI

***157.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yametokana na ushirikiano wake na nchi mbalimbali, mashirika, taasisi na marafiki wa uhifadhi. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau na washirika wa maendeleo kwa kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Canada, China, Korea

Kusini, Marekani, Norway, Ubelgiji, Ufini, Ujerumani, Uswisi na Jumuiya ya Nchi za Ulaya. Mashirika na taasisi ni pamoja na AfDB, AWF, AWHF, EU, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, ICOMOS, ILO, IUCN, KfW, NORAD, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNWTO, USAID, WCS, WHC, World Bank, Wild Aid, WMF na WWF.

## 8.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

***158.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/2021, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe **Shilingi 114,593,952,000** kwa matumizi ya **Fungu 69** - Wizara ya Maliasili na Utalii. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 69,573,850,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 45,020,102,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

***159.*** ***Mheshimiwa Spika,*** fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha **Shilingi 50,852,545,000** za mishahara na **Shilingi 18,721,305,000** za matumizi mengineyo. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha **Shilingi 700,000,000** fedha za ndani na **Shilingi 44,320,102,000** fedha za nje.

## 9.0 HITIMISHO

***160.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii itapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii: **www.maliasili.go.tz**.

***161.*** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana

Mheshimiwa Dkt. Hamis Kingwangalla kwa kuwasilisha hoja yako vizuri kabisa kwa umakini na ufasaha mkumbwa.

Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kemirembe tafadhali endelea una dakika 20.

**KEMIREMBE J. LWOTA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba taarifa hii iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani. Naomba nichukue fursa hii, kukushukuru wewe binafsi, kwa kuliongoza vema Bunge la 11 ukisaidiwa na Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge. Hakika, mchango wako katika mila, desturi na uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge utakumbukwa katika vizazi vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nitumie fursa hii pia, kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii ambao majina yao yameorodheshwa katika Ukurasa wa 20 wa Taarifa yangu, kwa kuniamini na kunichagua niwe kiongozi wao kwa kipindi chote. Busara na ushauri wao kwangu na kwa Serikali vimekuwa ndio nguzo ya utendaji bora wa Kamati hii. Nawatakia Wabunge wote kila la heri katika Uchaguzi Mkuu ujao na Mungu akipenda tukutane tena katika Bunge la 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi Wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Kwa Mwaka Fedha 2019/2020 hali ya Upatikanaji wa fedha, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Maliasili na Utalii iliidhinishiwa bajeti ya shilingi bilioni 120.2. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 71.5 ilitengwa kwa

ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 44.8 ilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha za miradi ya maendeleo, shilingi bilioni 1 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi 47.8 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2020 Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 39.4 ikiwa ni sawa na asilimia 32.8 ya bajeti yote iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni 31.6 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia 44.3 ya bajeti iliyotengwa kwa matumizi ya kawaida, na shilingi bilioni 7.8 zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 15.9 ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kati ya fedha za maendeleo zilizopokelewa, hakuna fedha ya ndani iliyokuwa imepokelewa mpaka taarifa hii imefika.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa upatikanaji wa fedha hususan utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kwa namna yoyote, Kamati ilitarajia kwamba kufikia Robo ya Tatu ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 walau nusu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge iwe imepokelewa na Wizara kutekeleza miradi hiyo. Aidha, kutotolewa kwa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kunaweza kukwamisha shughuli za uhifadhi kwasababu mwenendo wa upatikanaji wa fedha za nje kutekeleza miradi umekuwa ni wa kusuasua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukusanyaji wa maduhuli katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Idara mbalimbali za Wizara ya Maliasili na Utalii, pamoja na taasisi na mifuko iliyo chini ya Wizara hiyo ziliidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 71.5. hadi kufikia Februari, 2020 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 40.2 sawa na asilimia 56 ya malengo waliyojiwekea. Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kwamba kiwango hicho ni pungufu kwa takribani shilingi milioni 868.9 ukilinganisha na makusanyo ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambayo yalikuwa shilingi bilioni 41.10.

Mheshimiwa Spika, kwa mwenendo huu, aidha malengo ambayo Wizara inajiwekea katika makusanyo ni makubwa kuliko uhalisia wa uwezo wa makusanyo, au kuna mapungufu katika utekelezaji wa jukumu la ukusanyaji wa mapato hayo. Kwa upande mwingine, mashirika ya uhifadhi chini ya Wizara yaliidhinishiwa kukusanya shilingi milioni 701.8 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya hifadhi zetu. Hadi kufikia Februari, 2020 makusanyo yalikuwa shilingi milioni 472.5 sawa na asilimia 67 ya malengo waliyojiwekea. Kamati inapongeza wizara kwa jitihada za mashirika ya uhifadhi katika makusanyo, kwasababu mchango wao katika kuingizia Taifa mapato ni mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipanga kutembelea ili kukagua miradi ya maendeleo mitatu (3) kati ya miradi nane (8) iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Lengo la ukaguzi huo ilikuwa ni kujionea hali halisi ya utekelezaji kulingana na bajeti iliyotengwa katika kila mradi uliokaguliwa. Maelezo ya kina kuhusu uchambuzi wa Kamati katika miradi iliyokagawiwa fedha, yanapatikana kuanzia Ukurasa wa 8 wa Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2019/2020, Upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo, katika miradi yote ambayo Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi, changamoto kubwa imekuwa ni kutotolewa kwa wakati na kwa ukamilifu kwa Fedha za Bajeti ya Maendeleo iliyopangwa kwa Mwaka wa Fedha husika. Manufaa ya Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii yataonekana pale tu Serikali itakapotoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati na kwa ukamilifu ili kukamilisha Miradi iliyosimama na inayoendelea kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Fedha za Nje kutolewa kwa uchache kama ambavyo nimeeleza hapo awali, Kamati imebaini kwamba, sehemu kubwa ya fedha za bajeti na mpango wa maendeleo katika Wizara hii inategemea

ufadhili kutoka nje. Lakini pia, Kamati imebaini kwamba Wizara inatenga fedha za ndani kidogo na hata kiasi hicho kidogo kilichotengwa hutolewa kwa uchache au kutotolewa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati umefika ambapo Wizara inapaswa kuja na mikakati endelevu ya kuhakikisha inaanza kutenga fedha zaidi kutokana na vyanzo vya ndani ili kutekeleza miradi ya uhifadhi ambayo ndio kitovu cha uendelevu wa maliasili zetu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Makusanyo ya Maduhuli katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara ya Maliasili na Utalii imepanga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 65.2 kutoka katika idara mbalimbali, taasisi na mifuko chini ya Wizara. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kwamba makadirio haya ni pungufu kwa shilingi bilioni 6.2 ukilinganisha na makadirio ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambayo yalikuwa shilingi bilioni 71.5.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mashirika na taasisi za uhifadhi ambayo ni TANAPA, *TAWA, NCAA* na *TFS*, Wizara inakusudia kukusanya jumla ya shilingi milioni 738.2. Makadirio haya ni ongezeko la asilimia 5.1 ya makadirio ya makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambayo yalikuwa ni shilingi milioni 701.8.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona *(Covid-19)* kuathiri sekta ya utalii duniani kote, ni dhahiri kwamba malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 yanaweza yasifikiwe. Hivyo basi, Wizara inashauriwa kuweka mipango endelevu ya kuhakikisha kuwa, makadirio ya makusanyo ya taasisi na mashirika ya uhifadhi yanaakisi hali halisi ya vyanzo vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/ 2021, Wizara inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 69.5 kwa

ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya Fedha inayoombwa, shilingi bilioni 50.8 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 18.7 inaombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kufanya uchambuzi wake, imebaini kwamba Bajeti ya Matumizi ya Kawaida imepungua kwa asilimia 8.7 ukilinganisha na Bajeti ya shilingi 71.5 kwa Matumizi kama hayo kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kamati haijaridhishwa na makadirio haya kwa sababu, kupungua kwa bajeti ya matumizi ya kawaida kunaweza kuathiri utendaji wa Wizara katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 45.02 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha inayoombwa, shilingi milioni 700 ni fedha za ndani, na shilingi bilioni 44.3 ni fedha za nje. Bajeti ya Mpango wa Maendeleo imepungua kwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na bajeti ya shilingi milioni 48.8 ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, katika bajeti hiyo, kiasi cha kwa fedha za ndani ni pungufu kwa shilingi milioni 300 ikilinganishwa na bajeti ya maendeleo ya shilingi bilioni moja kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kueleza maoni na ushauri wa Kamati. Katika muundo wa bajeti na hali halisi ya upatikanaji wa fedha; Kamati inaona kwa kuwa Kamati imebaini kuwepo kwa mtiririko usioridhisha wa mapato katika bajeti inayotengwa kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, hivyo basi, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa katika bajeti zijazo, makadirio yawe yanaakisi hali halisi ya mapokeo ya fedha. Kwa kufanya hivi, Wizara itakuwa na uwezo wa kupanga kulingana na vipaumbele vya utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kwamba kwa sasa dunia inapitia changamoto kubwa itakonayo na mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya *Corona (Covid-19).* Ugonjwa

huu siyo tu unasababisha vifo vya watu ambao ni nguvu kazi, lakini umeaanza kuathiri uchumi wa nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania na hasa sekta ya utalii. Sekta hii imekuwa ikichangia wastani wa asilimia 17 ya pato la Taifa na asilimia 25 ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, makusanyo yatokanayo na sekta hii yanatarajiwa kushuka kwa kuwa kwa sasa nchi haipokei idadi kubwa ya watalii kutoka nje ya nchi kama ilivyokuwa hapo awali. Hivyo basi, Kamati inashauri kwamba Wizara iandae mkakati madhubuti wa makusanyo ambao utaakisi hali iliyopo hivi sasa. Mkakati huo uende sambamba na kutoa ahueni kwa wafanyabiashara mbalimbali waliowekeza katika Sekta ya Utalii ambao wamekuwa msaada katika kulisaidia Taifa kukusanya mapato yake katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri Serikali kuchukua hatua za ziada ili kuvutia watalii kutoka nje kwa kupunguza tozo mbalimbali zinazoathiri Sekta ya Utalii ikiwemo *landing fees* kwa mashirika ya ndege zinazotua nchini, kupunguza tozo katika hifadhi *(park fees)*, kutoa masharti nafuu ya maombi ya *visa* au kufuta kabisa *visa (visa exemption)* kwa nchi ambao zinaleta watalii wengi nchini na kuondoa kwa muda kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* katika sekta hii. Vilevile Wizara inaweza ikarejesha kwa muda utaratibu wa *single entry* katika hifadhi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mpango wa dharura. Kamati inashauri Wizara kwa kushirikiana na mashirika ya uhifadhi yakiwemo Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA)* pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania *(TAWA)* wawe na Mkakati au Mpango wa Dharura *(Contingency Plan)* endapo litatokea jambo lolote duniani ambalo litaathiri Sekta ya Utalii, mashirika hayo ya uhifadhi yaweze kuendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi bila kutegemea fedha za mapato yatokanayo na watalii. Mpango huo unaweza kuanzisha mfuko maalum wa kuwezesha uhifadhi

kwa lengo la kuwa na akiba ya fedha katika nyakati za uhaba wa mapato.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza jitihada za Wizara katika kufanya tathmini ambayo inalenga kuongeza wigo wa walengwa, aina ya wanyama na kubainisha umbali. Suala hili ni la kibajeti na hivyo Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kufanya marekebisho ya viwango vya malipo katika Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi ili ziendane na hali halisi ya madhara yatokanayo na mwingiliano baina ya wanyamapori na binadamu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na changamoto kubwa ya uharibifu wa misitu hasa inayomilikiwa na vijiji na Halmashauri za Wilaya. Hali hii imepelekea Kamati hii kuishauri Serikali kuipandisha Wakala wa Huduma za Misitu *(TFS)* kuwa Mamlaka. Lengo la uamuzi huu ni kuanzisha mamlaka moja itakayokuwa na nguvu za kisheria za kudhibiti matumizi ya rasilimali zote za misitu nchini bila kujali umiliki. Taarifa iliyowasilishwa na Wizara ilionyesha kwamba mchakato huo umeanza kwa kukusanya taarifa na kuandaa andiko litakalopelekwa ngazi za juu kwa ajili ya maamuzi. Kamati inashauri Serikali kuharakisha zoezi hili na kulitaarifu Bunge juu ya hatua zilizochukuliwa katika Mkutano ujao wa Bunge la Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangalla, Naibu Waziri Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Katibu Mkuu Prof. Adolf Mkenda, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Aloyce Nzuki pamoja na Watendaji wote wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru watumishi wote wa Bunge kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, napenda kuwashukuru wanawake jasiri wa Chama cha Mapinduzi wa Mkoa wa Mwanza walionileta hapa Bungeni. Nawashukuru kwa namna tulivyoshirikiana katika shughuli mbalimbali za utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa hii Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais wetu mpendwa, Jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Nawaahidi ushirikiano zaidi katika miaka mitano ijayo. Kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee pia, napenda kuwashukuru wanangu Baraka na Abraham na baba yao mume wangu mpendwa, Said Othman kwa ushirikiano walionipa katika utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lipokee Taarifa hii ili lijadili na kukubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2019/ 2020 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa

Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utaliikwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii ina sehemu kuu tano (5) ambapo Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi, Sehemu ya Pili niUchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka Wa Fedha 2019/2020. Sehemu ya Tatuni Uchambuzi wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Sehemu ya Nne ya ni maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati na Sehemu ya Tano ni Hitimisho.

## 1.2 Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (6) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya **Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii**. Aidha, kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bungekinatoa mamlaka mahsusi kwa Kamati hii kushughulikia Bajeti za Wizara hiyo ambayo imepewa mamlaka ya kusimamia uhifadhi wa maliasili, malikale na maendeleo ya utalii.

**Mheshimiwa Spika**,jukumu la uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hiyolilitanguliwa na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Ukaguzi huo ulifanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI YAKWA MWAKA FEDHA 2019/2020

## 2.1 Hali ya Upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, **Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii**liliidhinishiwa

bajeti ya **shilingi 120,202,637,734**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 71,538,430,944**ilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 48,889,963,734** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo**shilingi 1,000,000,000** ni fedha za ndani na **shilingi 47,889,963,734** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2020 Wizara ilipokea jumla ya**shilingi 39,436,673,780** ikiwa ni sawa na **asilimia 32.8** ya bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kati ya fedha zilizopokelewa, **shilingi31,624,744,175** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na **asilimia 44.3**ya bajeti iliyotengwa kwa matumizi ya kawaida, na **shilingi 7,811,929,605** zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ikiwa ni sawa na **asilimia 15.9**ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kati ya fedha za maendeleo zilizopokelewa, hakuna fedha ya ndani iliyokuwa imepokelewa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa upatikanaji wa fedha hususan za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kwa namna yoyote, Kamati ilitarajia kwamba kufikia Robo ya Tatu ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 walau nusu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge iwe imepokelewa na Wizara kutekeleza miradi hiyo. Aidha, kutotolewa kwa fedha za ndani kwa ajili yautekelezaji wa miradi ya maendeleo, kunaweza kukwamisha shughuli za uhifadhi kwa sababu mwenendo wa upatikanaji wa fedha za nje kutekeleza miradi umekuwa ni wa kusuasua.

## 2.2 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Idara mbalimbali za Wizara ya Maliasili na Utalii, pamoja na taasisi na mifuko iliyo chini ya Wizara hiyoziliidhinishiwa kukusanya **shilingi Shilingi 71,538,430,944**. Hadi kufikia Februari, 2020 Wizara ilikuwa

imekusanya **shilingi 40,238,104,363** sawa na **asilimia 56** ya malengo waliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kwamba kiwango hicho ni pungufu kwa takribani **shilingi 868,901,709**ukilinganisha na makusanyo ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambayo yalikuwa **shilingi 41,107,006,072**.Kwa mwenendo huu, aidha malengo ambayo Wizara inajiwekea katika makusanyo ni makubwa kuliko uhalisia wa uwezo wa kukusanya, au kuna mapungufu katika utekelezaji wa jukumu la ukusanyaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, mashirika ya uhifadhi chini ya Wizara yaliidhinishiwa kukusanya**shilingi 701,805,841,651** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya hifadhi zetu. Hadi kufikia Februari, 2020 makusanyo yalikuwa **shilingi 472,530,749,828** sawa na **asilimia 67** ya malengo waliyojiwekea. Kamati inapongeza jitihada za mashirika ya uhifadhi katika makusanyo, kwa sababu mchango wao katika kuingizia taifa mapato ni mkubwa.

### 2.3 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Kamati ilishauri masuala mbalimbali yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu Bajeti husika.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako kwamba, katika masuala yaliyotolewa ushauri, yapo ambayo yamezingatiwa kikamilifu, baadhi yanaendelea kuzingatiwa na mengine hayajazingatiwa kikamilifu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti. Kwa muhtasari, naomba niweke msisitizo katika machache kama ifuatavyo:-

a) Kamati ilishauri Serikali iharakishe mchakato wa kugawa vitalu kwa njia ya mnada. Katika maelezo yake kwa Kamati, Wizara ilisema kwamba Serikali imeanza kutekeleza ugawaji wa vitalu kwa njia ya mnada kupitia mfumo wa kielektroniki wa Wizara (MNRT Portal). Ugawaji wa vitalu kwa njia ya mnada ulianza rasmi mwezi Juni 2019 ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano 2016/2017-2020/2021. Kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na Wizara kwa sababu mfumo huu utasaidia kuongeza uwazi, kuziba mianya ya rushwa na kuongeza ukusanyaji wa maduhuli.

b) Kamati ilishauri kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara iajiri watumishi wa kutosha ili kukabili changamoto ya upungufu wa watumishi katika sekta ya uhifadhi, hususan askari wa wanyamapori. Katika kutekeleza maoni haya, napenda kulitaarifu Bunge kwamba, Wizara imeajiri jumla ya watumishi 389 wa kada ya wanyamapori na misitu. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba bado mahitaji ya watumishi katika Wizara hii ni makubwa. Kwa sasa mahitaji ya watumishi kwa taasisi na mashirika ya uhifadhi ni takriban watumishi 3,800. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha zaidi ili kuajiri Watumishi wa kutosha katika sekta ya uhifadhi wa maliasili zetu.

c) Kamati ilishauri Wizara kutoa mafunzo yanayohusu kuanzisha na kuendeleza misitu ya jamii/wananchi wanaozunguka misitu ya hifadhi kwa lengo la kuimarisha ushiriki wa wananchi katika uhifadhi wa misitu na hifadhi za nyuki. Lengo ni kuhakikisha kuwa zoezi la uhifadhi wa rasimilimali misitu linakuwa shirikishi na wananchi wanakuwa sehemu ya zoezi hilo.

Kamati ilipewa taarifa kwamba, Wizara kupitia programu mbalimbali, imetoa mafunzo yanayohusiana na uanzishaji wa mashamba madogo ya miti (woodlots), kilimo misitu, uhifadhi wa misitu na ufugaji

nyuki. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, jumla ya kamati za maliasili za vijiji 306 katika wilaya mbalimbali nchini zilipewa mafunzo ya usimamizi wa misitu kwa pamoja.

Aidha, kupitia miradi ya matumizi bora ya ardhi jumla ya vijiji 100 vimepatiwa elimu ya uhifadhi wa misitu na nyuki ambapo imewezesha vijiji hivyo kutenga takriban hekta 12,000 za misitu ya hifadhi ya vijiji na kuongeza ushiriki wao katika kuhifadhi misitu ya Serikali Kuu inayopakana na vijiji hivyo. Kamati inapongeza jitihada hizi ambazo zinafanywa na Serikali.

d) Kamati ilipendekeza kwamba, Wizara iharakishe mchakato wa kupandisha hadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS)ili kuwa mamlaka itakayokuwa na nguvu za kisheria katika kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu nchini. Katika maelezo yake kwa Kamati, Wizara ilisema kwamba inaendelea na utaratibu wa kuipandisha hadhi TFS ili iwe mamlaka. Katika kutekeleza azma hiyo, rasimu ya andiko la Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya kupandisha hadhi TFS imeandaliwa na kuwasilishwa kwa wadau kwa ajili ya maoni ambapo maoni hayo yamepokelewa na yanafanyiwa kazi.

Kamati inapongeza hatua zilizochukuliwa na inaishauri Wizara kukamilisha mchakato huo mapema iwezekanavyo.

e) Kamati ilishauri kwamba Kanuni za Kifuta Jasho na Machozi zipitiwe kwa kuwa viwango vya malipo vilivyopo haviridhishi. Kamati ilifuatilia utekelezaji wa ushauri huu, na kufanya vikao na Wizara ili kujua hatua iliyofikiwa. Pamoja na jitihada ambazo zimefanywa, Kamati ina maoni kwamba ushauri huu haujafanyiwa kazi ipasavyo na hivyo basi, Wizara inapaswa kuwasilisha kwa kamati taarifa yenye mapendekezo ya namna ambavyo Kanuni hizo zinapaswa kuwa.

### 2.4 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipanga kutembelea ili kukagua miradi ya maendeleo mitatu (3) kati ya miradi nane (8)iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Lengo la ukaguzi huo likuwa ni kujionea hali halisi ya utekelezaji wake kulingana na bajeti iliyotengwa katika kila mradi uliokaguliwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo katika mikoa ya Mara, Mwanza, Taborana Shinyanga kati ya tarehe 12 hadi tarehe 18 Machi, 2020. Miradi iliyofanyiwa ukaguzi wa utekelezaji wake ni ifuatayo:-

#### 2.4.1 Mradi Na. 4648 – Ujenzi wa Jengo la Utawala la Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora (BTI)

**Mheshimiwa Spika**, Jengo hilo lilianza kujengwa mnamo mwaka 1959, na lilipokamilika matumizi yake yalikuwa yakibadilika mara kwa mara. Mnamo mwaka 2013, jengo hilo lilifanyiwa tathmini ya ukarabati na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kuonekana kuhitaji **shilingi milioni 180**ili kukamilisha kazi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo Kamati imebaini kwamba pamoja na chuo kuwa kinaomba fedha hizo kila mwaka, lakini fedha zilikuwa hazitolewi. Hata hivyo, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Bunge lilitenga jumla ya**shilingi milioni 200** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huo.Mnamo Februari, 2020 chuo kilipokea jumla ya **shilingi milioni 150** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Hadi wakati Kamati inakagua mradi, mchakato wa kutafuta mzabuni ndio ulikuwa umeanza.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishauri wizara kubadili mpango wa nradi kwa kutofanya ukarabati wa jengo

na badala yake kutumia *force account* kujenga jengo jipya la utawala kwa fedha iliyopatikana.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kwamba chuo pia kina changamoto ya kutokuwa na maabara, na upungufu wa vifaa vya kufundisha. Kamati ilishauri kwamba Wizara inapofanya makadirio ya mipango ya bajeti zijazo ihakikishe inatenga fedha kwa ajili ya kuwezesha chuo hicho kuwa na maabra na vifaa vya kufundishia vya kutosha.

### 2.4.2 MradiNa. 4811 – *Sustainable Natural Resources Management in Tanzania*

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulikuwa unatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti na Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro kwa lengo la kuziwezesha jamii zinazopakana na hifadhi katika halmashauri hizo kushiriki katika uhifadhi.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ilikuwa na lengo la kufanya shughuli zifuatazo:-

a) Kuimarisha utendaji wa TAWA

b) Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji maduhuli na kufanya utafiti wa vyanzo vipya vya mapato

c) Kusaidia halmashauri za Serengeti na Ngorongoro katikamasuala ya sera, sheria na taratibu zinazohusu mgawanyo wa faida zitokanazo na uhifadhi wa maliasili; na

d) Kuzijengea halmashauri hizo uwezo wa kujua mbinu za kutatua migogoro inayotokana na muingiliano kati ya wanyamapori na binadamu

**Mheshimiwa Spika**, kwa sababu ambazo zilizokuwa nje ya uwezo, Kamati haikufanikiwa kufika katika halmashauri hizo kwa sababu ya mlipuko wa ugonjwa

wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19). Hata hivyo, Kamati ilipokea taarifa kuhusu mradi huo hapa Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, Katika maelezo yake kwa Kamati, Wizara ilisema kwamba, mradi huu ulianza kutekelezwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa miaka minne hadi Mwaka wa Feha 2019/2020 kwa jumla ya bajeti ya **shilingi bilioni 13.8**. Fedha za mradi zilikuwa ni za ufadhili kutoka nje. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 mradi uliidhinishiwa kutumia**shilingi bilioni 2.14** ambapo hadi wakati taarifa inawasilishwa, kiasi cha **shilingi bilioni 1.09** kilikuwa kimetolewa na kutumika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, baada ya mradi huu kukamilika, Wizara haijaweka mpango wa kibajeti wa kutekeleza shughuli za mradi katika halmashauri hizo na halmashauri nyingine nchini. Ukitathmini malengo ya mradi, shughuli zilizokuwa zinazofanywa zinapaswa kuwa endelevu na hivyo kuhitajika kwa jitihada za makusudi za kubuni namna bora ya kuendeleza mradi huo katika halmashauri nyingine nchini.

## 2.5 Maoni ya Jumla Kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

### 2.5.1 Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika miradi yote ambayo Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi, changamoto kubwa imekuwa ni kutotolewa kwa wakati na kwa ukamilifu kwa Fedha za Bajeti ya Maendeleo iliyopangwa kwa Mwaka wa Fedha husika. Manufaa ya Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii yataonekana pale tu Serikali itakapotoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati na kwa ukamilifuili kukamilisha Miradi iliyosimama na inayoendelea kutekelezwa.

### 2.5.2 Fedha za Nje Kutolewa kwa Uchache

**Mheshimiwa Spika**, kama ambavyo nimeeleza hapo awali, Kamati imebaini kwamba, sehemu kubwa ya fedha za bajeti na mpango wa maendeleo katika Wizara hii inategemea ufadhili kutoka nje. Lakini pia, Kamati imebaini kwamba Wizara inatenga fedha za ndani kidogo na hata kiasi hicho kidogo kilichotengwa hutolewa kwa uchache au kutototolewa kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, wakati umefika ambapo Wizara inapaswa kuja na mikakati endelevu ya kuhakikisha inaanza kutenga fedha zaidi kutokana na vyanzo vya ndani ili kutekeleza miradi ya uhifadhi ambayo ndio kitovu cha uendelevu wa maliasili zetu.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

### 3.1 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 **Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii** imepanga kukusanya maduhuli ya jumla ya **shilingi 65,256,218,761** kutoka katika idara mbalimbali, taasisi na mifuko chini ya Wizara.Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kwamba makadirio haya ni pungufu kwa **shilingi 6,282,212,183** ukilinganisha na makadirio ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambayo yalikuwa **shilingi 71,538,430,944**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mashirika na taasisi za uhifadhi ambayo ni TANAPA, TAWA, NCAA na TFS, Wizara inakusudia kukusanya jumla ya **shilingi 738,230,093,590**. Makadirio haya ni ongezeko la **asilimia 5.19** ya makadirio ya makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambayo yalikuwa ni **shilingi 701,805,841,651**.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona *(Covid-19)* kuathiri sekta ya utalii duniani kote, ni dhahiri kwamba malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 yanaweza yasifikiwe. Hivyo basi, Wizara inashauriwa kuweka mipango endelevu ya kuhakikisha kuwa,makadirio ya makusanyo yataasisi na mashirika ya uhifadhi yanaakisi hali halisi ya vyanzo vilivyopo.

### 3.2 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 **Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii** inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 69,573,850,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya Fedha inayoombwa, **shilingi 50,852,545,000** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi bilioni 18,721,305,000** inaombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kamati kufanya uchambuzi wake, imebaini kwamba Bajeti ya Matumizi ya Kawaida imepungua kwa **asilimia8.78** ukilinganisha na Bajeti ya **shilingi 71,538,430,944**kwa Matumizi kama hayo katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.Kamati haijaridhishwa na makadirio haya kwa sababu, kupungua kwa bajeti ya matumizi ya kawaida, kunaweza kuathiri utendaji wa Wizara katika baadhi ya maeneo.

### 3.3 Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, **Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii** inaomba kuidhinishiwa **shilingi 45,020,102,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha inayoombwa, **shilingi 700,000,000** ni fedha za ndani, na **shilingi 44,320,102,000** ni fedha za nje. Bajeti ya Mpango wa Maendeleo imepungua kwa **asilimia 7.89** ukilinganisha na bajeti ya **shilingi 48,889,963,734** kwa

utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Aidha, katika bajeti hiyo, kiasi cha kwa fedha za ndanini pungufu kwa **shilingi 300,000,000**ukilinganisha na bajeti ya maendeleo ya **shilingi 1,000,000,000** kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WAKAMATI

### 4.1 Masuala ya Jumla

#### 4.1.1 Muundo wa Bajeti na Hali ya Upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Kamati imebaini kuwepo kwa mtiririko usioridhisha wa mapato katika bajeti inayotengwa kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, hivyo basi, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa katika Bajeti zijazo, makadirio yanaakisi hali halisi ya mapokeo ya fedha. Kwa kufanya hivi, Wizara itakuwa na uwezo wa kupanga kulingana na vipaumbele vya utekelezaji wa majukumu yake.

#### 4.1.2 Makusanyo Katika Sekta ya Utalii

**Mheshimiwa Spika**, sote tunafahamu kwamba, kwa sasa dunia inapitia changamoto kubwa itakonayo na mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (Covid-19). Ugonjwa huu sio tu unasabisha vifo vya watu ambao ni nguvu kazi, lakini umeaanza kuthiriuchumi wa nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania na hasa sekta ya utalii.Sekta hii imekuwa ikichangia wastani wa **asilimia 17** ya pato la taifa na **asilimia 25** ya fedha za kigeni.Kwa hali hiyo, makusanyo yatokanayo na sekta hii yanatarajiwa kushuka kwa kuwa kwa sasa nchi haipokei idadi kubwa ya watalii kutoka nje ya nchi kama ilivyokuwa hapo awali.

Hivyo basi, Kamati inashauri kwamba Wizara iandae mkakati madhubuti wa makusanyo ambao utaakisi hali iliyopo hivi sasa. Mkakati huo uende sambamba na kutoa ahueni kwa wafanyabiashara mbalimbali waliowekeza katika sekta ya utalii ambao wamekuwa

msaada katika kulisaidia taifa kukusanya mapato yake katika sekta hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inashauri Serikali kuchukua hatua za ziada ili kuvutia watalii kutoka nje kwa kupunguza tozo mbalimbali zinazoathiri sekta ya utalii ikiwemo *landing fees*kwa mashirika ya ndege yanayotua nchini, kupunguza tozo katika hifadhi *(park fees)*, kutoa masharti nafuu ya maombi ya viza*(visa exemption)*, na kuondoa kwa mudakodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* katika sekta hii. Vilevile, Wizara inaweza ikarejesha kwa muda utaratibu wa *single entry* katika hifadhi zetu.

### 4.1.3 Mpango wa Dharura

**Mheshimiwa Spika**, Kamatiinashauri Wizara kwa kushirikiana na mashirika ya uhifadhi yakiwemo Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) wawe na Mkakati/Mpangowa Dharura *(Contingency Plan)*endapo litatokea jambo lolote duniani ambalo litaathiri sekta ya utalii, mashirika hayo ya uhifadhi yaweze kuendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi bila kutegemea fedha za mapato yatokanayo na watalii. Mpango huo hiyo unaweza kuanzisha mfukomaalum wa kuwezesha uhifadhi kwa lengo la kuwa na akiba ya fedha katika nyakati za uhaba wa mapato.

## 4.2 Masuala Mahsusi

### 4.2.1 Marekebisho ya Viwango vya Malipo Katika Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Wizara katika kufanya tathmini ambayo inalenga kuongeza wigo wa walengwa, aina ya Wanyama na kubainisha umbali. Suala hili ni la kibajeti, na hivyo Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kufanya

marekebisho ya viwango vya malipo latika Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi ili ziendane na hali halisi yamadhara yatokanayo na muingiliano baina ya wanyamapori na binadamu.

### 4.2.2 Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa kuongeza idadi ya Hifadhi za Taifa kutoka hifadhi 16 hadi 22. Kabla ya kuanzishwa kwa hifadhi mpya 6, ni hifadhi 5 kati ya 16 zilizokuwa zina uwezo wa kujiendesha zenyewe na kuzalisha ziada iliyosaidia kuendesha Hifadhi za Taifa nyingine 11.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia hali ya uchumi wa dunia ya sasa, Kamati inashauri Wizara iandae mpango mkakati wa haraka kuweza kujua ni kwa namna gani Shirika la Hifadhi la Taifa (TANAPA) litawezeshwa na Serikali kujiendesha ili kuweza kushiriki katika uhifadhi endelevu. Serikali inaweza kuangalia namna bora ya kulipunguzia shirika majukumu yake kwa Serikali kuu ikiwemo gawio, pamoja na baadhi ya kodi na tozokwa shirika hilo kupunguzwa kama sio kusamehewa kabisa.

### 4.2.3 Wakala wa Misitu Tanzania (TFS)

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na changamoto kubwa ya uharibifu wa misitu hasa inayomilikiwa na vijiji na Halmashauri za Wilaya, hali iliyopelekea Kamati hii kuishauri Serikali kuipandisha Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kuwa Mamlaka. Lengo la uamuzi huu ni kuanzisha mamlaka moja itakayokuwa na nguvu za kisheria za kudhibiti matumizi ya rasilimali zote za misitu nchini, bila kujali umiliki. Taarifa iliyowasilishwa na Wizara, ilionyesha kwamba mchakato huo umeanza kwa kukusanya taarifa na kuandaa andiko litakalopelekwa ngazi za juu kwa maamuzi. Kamati inashauri Serikali kuharakisha zoezi hili na kulitaarifu Bunge juu ya hatua zilizochukuliwa katika Mkutano ujao wa Bunge la Bajeti.

### 4.2.4 Mamlaka ya Usimamizi wa WanyamaporiTanzania (TAWA)

**Mheshimiwa Spika**, tangu ianze kutekeleza majukumu yake Mwaka 2016, TAWA imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo kuimarika uhifadhi kunakotokana na kupungua kwa ujangili, kudhibitiwa kwa vitendo vya uingizaji na ulishaji wa mifugo katika Mapori ya Akiba na kuanzisha na kufanya mabadiliko ya kimfumo wa usimamizi wa uhifadhi kutoka wa kiraia kwenda Jeshi Usu. Aidha, TAWA imesaidia kuimarisha utalii kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaotembelea vivutio vinavyosimamiwa na Mamlaka hiyo. Hata hivyo, taasisi hiyo haina Sheria mahsusi inayosimamia utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwamba, Wizara ifanye tathmini na kuona iwapo kuna uwezekano na ulazima wa kuanzishwa kwa Sheria mahsusi kuiwezesha TAWA kutekeleza kwa majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, tathmini hiyo ibainishe masuala ya kisera, kisheria na kibajeti ambayo yanaweza kuathiriwa kutokana na mapendekezo ya tathmini hiyo.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*:-

1. Mhe. Kemirembe Rose Julius Lwota, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Nape Moses Nnauye, Mb
3. Mhe. Boniface Mwita Getere, Mb
4. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb
5. Mhe. Magdalena Hamis Sakaya, Mb
6. Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb

7. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb
8. Mhe. Lucy Fidelis Owenya, Mb
9. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb
10. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb
11. Mhe. Neema William Mgaya, Mb
12. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb
13. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
14. Mhe. Risala Saidi Kabongo, Mb
15. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb
16. Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa, Mb
17. Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb
18. Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb
19. Mhe. Zainab Nuhu Mwamwindi, Mb
20. Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb
21. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb
22. Mhe. Timotheo Paul Mnzava
23. Mhe. Pauline Philip Gekul, Mb
24. Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo, Mb
25. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Maliasili na UtaliiMhe. Dkt. Hamisi A. Kigwangalla (Mb), Naibu Waziri Mhe. Constantine J. Kanyasu(Mb), Katibu MkuuProf. Adolf F. Mkenda, Naibu Katibu Mkuu Dkt.Aloyce K. Nzukipamoja na watendaji wote wa Wizara na taasisi zake kwaushirikiano wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema Shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Yona Kirumbi na Ndg. Monica Mwamunyange wakisaidiwa na Ndg. Mwimbe John, kwa kuratibu vema Shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lipokee Taarifa hii ili lijadili na kukubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Kemirembe Rose Julius Lwota,Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

7 Mei, 2020

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kemilembe Lwota kwa hotuba hiyo nzuri sana kwa niaba ya Kamati yako na hongera sana kwako kwa kazi nzuri ambayo umeifanya kama Mwenyekiti na hongera kwa Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi nzuri sana ambayo mmeifanya *so far.*

Pia nimefurahi kusikia utambulisho maalum, sikujua bwana, kumbe shemeji! Ahsante sana, yote mema. *(Kicheko/ Makofi)*

Sasa katika uchangiaji ataanza Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, atafuatiwa na Mheshimiwa Raphael Michael.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ya kwanza ya kuchangia katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Awali ya yote napenda nikupongeze wewe binafsi kwa sababu sasa hivi dunia yote iko kwenye mtikisiko mkubwa sana wa gonjwa hili la *Corona (Covid 19).* Kwa kweli kama Bunge, umeendelea kutuongoza vizuri kiasi cha kwamba tahadhari zote zinaendelea kuchukuliwa. Huu ni mfano mzuri sana kwa Bunge letu na naomba nikupe pongezi nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umekuwa ni mfano mzuri kwa kipindi chote hiki ulichotuongoza, umesimama imara panapotakiwa kusimama imara, nami niseme kwamba wewe pamoja na Naibu wako nawatakia kila la heri ili wananchi wa Kongwa na wa Mbeya Mjini waweze kuwapatia kura bila tatizo lolote lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Hamisi Kigwangalla na Naibu wake kwa hotuba nzuri ambayo wameiandaa. Nimefurahishwa na mambo makuu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Waziri amekuwa ni muwazi, amezungumza kuhusu jinsi Sekta yake ya Utalii ambavyo sasa inapambana na janga hili kubwa la *Corona*. Amesema kabisa kwamba tutarajie mapato sasa kupitia sekta hii yatapungua kwa asilimia 75. Ukiangalia kwenye *World Economic Outlook* wanasema uchumi sasa kwa mwaka 2020 utapungua kwa -3% *(negative 3%).* Sasa yote haya lazima tuangalie, sisi kama nchi tunatokaje hapa tulipo?

Mheshimiwa Spika, tumemsikia sana Mheshimiwa Rais ambaye amekuwa mstari wa mbele kutuonyesha na kutuondoa hofu Watanzania kwamba hii *Corona* ni janga la kidunia. Sisi kama Watanzania hatuna *exceptions,* tuchukue tahadhari lakini tuendelee kupambana na kuchapa kazi. Kwa sababu leo hii *Corona* hii kwa mujibu wa takwimu na matarajio ya kidunia *Corona* itakwisha mwaka 2021. Kwa hiyo, ina maana *is something to live with now.* Hatuwezi kufunga nchi, lazima watu waishi na uchumi usonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa takwimu za kidunia, uchumi utaanza kufufuka tena mwaka 2021. Sasa nini kifanyike? Cha kwanza, Sekta hii ya Utalii na Ukarimu ni moja ya sekta ambayo imeathirika sana kwa sababu hakuna usafirishaji, hakuna biashara na hata watu waliokuwa wanakuja kufanya utalii hawawezi kuja. Leo hii *TANAPA* waliokuwa wanakusanya kwa siku zaidi ya shilingi milioni 500,

wanakusanya chini ya shilingi milioni 10 kwa siku. Uone kwamba sasa tumefika mahali pabaya sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote haya, sisi siyo kisiwa, lazima tuangalie tunachukua *measures* za aina gani? Kama nchi, sisi ni nchi masikini, tuko kwenye *group* la kuomba msaada. Sisi ni wanachama wa *IMF* n *World Bank* lakini tuna marafiki G20 na *Paris Club*. Tutumie fursa hii kuweza ku-*access* hizo fedha zisaidie kupunguza mdororo wa biashara na uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi tukakaa hivi hivi. Nategemea Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakuja na mpango mkakati *(a comprehensive recovery plan)* kwamba Tanzania pamoja na *Corona,* tumekumbwa na mafuriko na majanga mengine, yote yanahitaji kuwa *supported.* Uchumi wetu utakuwa umeyumba sana kwa kipindi hiki, lakini kama nchi hatuwezi kubabaika, tuondoe hofu Watanzania tuhakikishe tunapambana na vita ambayo tuna marafiki na maadui humo humo ndani ambao lazima tukabiliane nao vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, cha msingi, tuangalie suala la kuomba kusamehewa kulipa au ku-*suspend* kulipa malipo yetu ya kila mwezi kwenye taasisi mbalimbali za kidunia. Kwenye sura ya bajeti kuna kama shilingi trilioni 10 ambayo tumepanga kulipa kwa mwaka huu ujao wa fedha. Hizi ni fedha nyingi sana. Kwa hiyo, ina maana tukipata fedha kutoka nje itatusaidia kupunguza makali ambayo tunayo kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, pili, tuombe Benki Kuu ijaribu kukaa na mabenki na taasisi nyingine za kifedha hapa nchini ili wale wote ambao wameathirika katika sekta zao wasaidiwe namna gani ya kuweza kuendelea kunyanyuka. Tunahitaji tutengeneze uchumi tuweze kupata fedha na kuendesha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lazima tupunguze ukali na mdororo wa kiuchumi na hii tunaweza kuipata tu ikiwa tutajipanga

vizuri. Katika bajeti hii lazima tuangalie namna gani sasa sekta ambazo zimeathirika zinasaidiwa. Siamini kwamba kuendelea kukaa hivi hivi bila kufanya mkakati tunaweza tukatoka hapa tulipo.

Mheshimiwa Spika, tumeona wenzetu wa Uganda, Kenya, Rwanda wamepokea mwezi huu na wengine wamepata fedha, nasi tusizubae, tuchangamke. Kwa sababu naamini kwamba mtu anayekudai, mtadaiana mbele ya safari. Kwenye shida na dharura, pokea kwanza kilichopo ili baadaye kwenye kulipa mtasema jamani tulipane kwa kufuata utaratibu huu hapa. Hii itatusaidia Watanzania kuongeza fedha na kuweza kufufua uchumi wetu na kupigana na janga hili la *Corona*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ametuonyesha njia, amekuwa muwazi na amewaambia Watanzania kwamba hofu peke yake ni tatizo, tuondoe hofu. Leo hii hapa nimeambiwa kuna Mbunge mwenzetu anasaidia Wabunge wengine kuwapatia dawa ya kusaidia janga la *Corona*. Sasa hii ni *innovation.* Tumesikia Madagascar wana dawa na kadhalika. Tusidharau mambo ambayo tumekuwa nayo miaka nenda rudi. Tumeona kwamba tukiwa tunahangaika kuleta *ventilators* kwa ajili ya kusaidia wagonjwa, kumbe masikini pengine hatuhitaji gharama zote hizo. Kwa hiyo, tuna *alternative medicines* ambazo zitatusaidia kuweza kupunguza tatizo hilo. Naomba Watanzania turudi kwenye *basics.* Tufike mahali tusisahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amekuwa jemedari mkubwa sana kwa sababu hamkutetereka toka mwanzo. Aliyoyasema toka mwanzo na kuyasimamia ndiyo sasa nchi nyingine wameanza kurudi kule tulikotoka sisi. Hii unaangalia kabisa kama nchi unaona tumekuwa na kiongozi ambaye amekuwa na msimamo imara. Amesimama imara na Watanzania tumuunge mkono kwa nguvu zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashangaa wanaobeza na kwenye mitandao. Siri ya uzalendo ni pamoja na kuwa wamoja wakati wa shida. Wakati wa shida Watanzania

hatuwezi kuanza kudharau na kubezana, tunapunguziana nguvu na morali wa kupigana vita.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kupitia bajeti hii kwa kweli ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, tuangalie kuna vitu ambavyo ni vya muhimu. Leo hii *TANAPA* wana hifadhi nne ambazo zinafanya biashara na zina *break even.* Nyingine 16 ni za kusaidiwa, lakini kuna kodi wanatozwa. Leo tumeanzisha Jeshi USU linalofanya kazi nzuri sana, limelinda rasilimali zetu vizuri sana, lakini unakuta kwamba hata unapoagiza silaha za Jeshi USU, wanatozwa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo *TANAPA* wakitoa msaada kwenye (*Cooperate and Social Responsibility – CSR)* msaada kwa jamii wanatozwa kodi. Sasa haya yote tunawatendea siYo haki. Leo hii tumewapa jukumu kubwa sana *TANAPA,* wanahitaji tuwasaidie waweze kunyanyuka na wazidi kuhifadhi vizuri hifadhi zetu. Sitarajii Watanzania tukawa na hifadhi ambazo hazina wanyama kwa sababu lengo letu, tuna faida kubwa kwamba tunahifadhi wanyama kwa maana ya picha na uhifadhi wa uwindaji ambao unaleta faida sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na Naibu wako kwa kweli kwa kipindi hiki mmeitendea haki Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Mnyonge mnyongeni, lakini hawa watu lazima tuwape pongezi. Leo hii Maliasili na Utalii imekuwa ni *icon,* ni Wizara ambayo inachangia pato letu la Taifa asilimia 17.5 na kwa mapato ya fedha za kigeni ni zaidi ya asilimia 25 tunategemea kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, sasa huyu ni ngombe wa maziwa lazima tumlishe vizuri. Naomba sana tuwasaidie *TANAPA,* Ngorongoro, *TFS* na wale wote wanaohusika na uhifadhi wa mazingira yetu haya na maliasili zetu, lazima tuwape kila aina ya msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako, ile sheria ambayo inafanya *TANAPA* kuingiza silaha pamoja na

vifaa mbalimbali vinavyolinda maliasili yetu, viondolewe kodi ili tuweze kuwapa *TANAPA,* Ngorongoro na hata *TFS* nafuu ya kuweza kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Kengele ya kwanza!

**SPIKA:** Ya pili.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, basi nimalizie.

Mheshimiwa Spika, wewe binafsi kama muhifadhi, umefanya kazi nzuri sana na nakuomba tumia nafasi yako na kiti chako tuwasaidie hawa watu na hasa marekebisho ya kisheria ili kusudi waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, tunakushukuru sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Mjini, tafadhali.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, najua kuna habari ziko kwenye mtandao ingawa sio rasmi, lakini ni vizuri wananchi wakajua na hasa wanachama wa CHADEMA, kwamba sisi hatujampindua Kiongozi wetu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wala hatuna mamlaka ya kumpindua. Kwa hiyo sisi tumeingia kama Wabunge kwa ajili ya kuona namna ambavyo tunaweza tukasaidia Serikali katika kuwawakilisha wananchi katika wakati huu mgumu

ambapo Taifa liko katika misukosuko mingi na hasa janga hili la *corona*. Kwa hiyo tunataka wananchi watuelewe tu hivyo, lakini hatuna ugomvi na kiongozi wetu. *(Makofi)*

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa iko wapi?

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika, niko hapa.

**SPIKA:** *Okay,* ahsante.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Japhary Michael, kuna msemo wa Kiingereza unasema *if you want to kill a dog give it a bad name,* ukitaka kumuua mbwa mpe jina baya. Sisi tunachokisema ni kwamba hayo yanasemwa na watu lakini hatujampindua mtu yeyote, hatuna ugomvi na mtu yeyote na tunaomba wenzetu waje tufanye kazi. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael, taarifa hiyo.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa yuko sawasawa na nimeipokea taarifa yake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Sekta ya Utalii ni sekta ambayo itakuwa imeathiriwa sana na janga hili la *corona*. Nishukuru Waziri ameonesha vizuri kwamba athari ziko kwa kiwango gani. Sekta ambayo ilikuwa inaweza ikachangia pato la zaidi ya asilimia 25 kwenye mapato ya kigeni, leo itakuwa imedorora sana kutokana na athari zilizokabili dunia.

Mheshimiwa Spika, janga hili linalotukabili siyo uamuzi wa mtu yeyote, hakuna mtu ambaye alitarajia kwamba

kutakuwa na hili janga na limetokea. Sasa wajibu wetu kama viongozi na kama Wabunge ni kuona tunasaidiaje Serikali kuhakikisha kwamba tunakabiliana na matokeo ya janga hili. Ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla sekta iliyoathirika kwa sababu ni ya Utalii, kama ambavyo leo tunaona kwamba ndege hazisafiri zaidi ya mashirika 13 yameshafunga safari zake. lakini hata ndege zetu za *ATCL* hazisafiri nje na watu wamezuiwa kuingia katika nchi zingine. Kwa misingi hiyo mategemeo yetu ya kutegemea sana utalii kutokana na wageni wa nje maana yake ni kwamba kwa ujumla wake ndiyo maana hotuba ya Mheshimiwa Waziri inatuambia kwamba mapato yetu yaliyotarajiwa ya trilioni 2.6 yatashuka mpaka bilioni 500 na kitu. *TANAPA* imeathirika na taasisi nyingine zote zimeathirika.

Mheshimiwa Spika, sasa rai yangu ni kwamba, nadhani tunapaswa, kwanza kama alivyoshauri mzungumzaji aliyepita kusaidia hizo taasisi. Jambo la pili ni kuwasaidia wafanyabiashara ambao wako katika Sekta hiyo ya Utalii. Ni jambo la muhimu sana kwa sababu wafanyabiashara wamefunga biashara. Kanda ya Kaskazini ndiyo kanda ambayo ime-*invest heavily* katika eneo hili la utalii, ingawa kuna jitihada za kufanya kanda zingine katika nchi hii nazo zi-*invest* katika utalii, lakini Kanda ya Kaskazini, Kilimanjaro na Arusha wame-*invest heavily* katika eneo hili la utalii. Na…

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Ndiyo, taarifa kutoka Msekwa, nani?

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, mimi Emanuel Adamson Mwakasaka.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, huku Msekwa hatusikii hayo matangazo, ni mwangwi mtupu unatoka kwenye hizi *screens.*

**SPIKA:** Ahsante sana. Watu wa *IT.* Endelea Mheshimiwa Japhary.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nasema nchi nzima wafanyabiashara wanaohusiana na mambo ya utalii wameathirika, lakini Kanda ya Kaskazini imeathirika zaidi kwa sababu kwa muda mrefu wamewekeza sana; mahoteli ya kitalii Kilimanjrao hasa Moshi Mjini eneo ambalo mimi ni Mbunge; Arusha wameathirika, magari yamepaki, kila kitu kinachohusiana na utalii kimesimama, waliokuwa wameajiriwa kwenye sekta hii ambao ni *informal* na *formal* hawana ajira. Kwa hiyo kuna athari kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa la kwanza, ni vizuri Serikali kwenye bajeti yake kuu ione namna gani itayapokea maoni ya Wizara ya Maliasili na Utalii katika kuhakikisha kwamba wanawasaidia watu wanaofanya biashara ya mahoteli ya kitalii, watu wanaohusiana na biashara ya utalii, ili kwenye suala la kikodi waone namna ambavyo watakuwa wamesaidiwa au wawe na *grace period* fulani ya *tax holiday* ili waweze kujipanga vizuri baada ya janga hili kupungua katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nililiongea hili wakati nachangia kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara na naliongea hili kwa sababu najua kabisa kwamba utalii ulivyoathirika kwenye Mji wa Moshi umeathiri mpaka biashara zingine kwa sababu ndiyo kitu kikubwa ambacho kinategemewa kufanya vitu vingine katika Mji wa Moshi na Mikoa wa Kilimanjaro na Arusha na Kanda ile iende vizuri zaidi kwa sababu ni tegemeo kubwa sana la kibiashara katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni vizuri waangaliwe kwa jicho pana na kwa jicho ambalo litawasaidia wao kuona namna wanavyoendesha shughuli zao. Ni lazima sisi kama Wabunge na Serikali tujue kwamba wafanyabiashara wanatusaidia kupata kodi, tunapaswa kuwasaidia katika kuhakikisha kwamba wana-*sustain* biashara zao. Kwa hiyo naomba sana hilo lichukuliwe katika uzito wake.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni suala la utalii wa ndani. Janga hili litufundishe, ulazima sasa wa kuhamasisha sana utalii wa ndani, kwamba utalii kutegemea wageni wa nje peke yake maana yake ni kwamba kuna wakati jambo likitokea tutapata athari kubwa sana. Kwa hiyo ni vizuri pia Wizara ituambie, najua kuna jitihada wanazozifanya kuhusu kuimarisha utalii wa ndani, lakini watuoneshe mikakati thabiti waliyoipanga ya kufanya watu wajue kwamba wanapaswa baada ya janga hili la *corona* kutembelea mbuga zao na hifadhi zao ili wawe ni sehemu kubwa ya kuchangia mapato katika eneo hilo. Ni muhimu sana tuone namna tunavyohamasisha watu wetu ili washiriki katika suala hili la utalii wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ni suala la Uwanja wangu wa Ndege wa Moshi ambao kimsingi mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, nakushukuru sana kwa kuniweka kwenye Kamati hiyo kwa miaka mitano. Jambo hili nimelizungumza sana kule, lakini naomba Wizara ya Utalii inisaidie kulisukuma hili suala kule kwenye Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ili ule uwanja ujengwe, kwa sababu ule uwanja utasaidia sana Mlima wa Kilimanjaro kupata watalii.

Mheshimiwa Spika, kuna dhana inasemwa kwamba kuna Uwanja wa *KIA.* Uwanja wa *KIA* ni uwanja wa kimataifa, uwanja wa Moshi ni uwanja wa mkoa, ni *domestic airport*, mtalii akitoka Serengeti anaweza akasafiri moja kwa moja akaja Moshi kuliko kushukia *KIA* au kushukia Arusha ndiyo aje Moshi. Kwanza wanaiathiri Moshi yenyewe kimapato na kiuchumi, lakini wanasababisha mlolongo mrefu wa watu kufika Mlima Kilimanjaro kwamba mpaka washukie Nairobi ama washukie Arusha badala ya kushukia Moshi ambapo pana uwanja uliojengwa na malkia mwaka 1956.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo itafaidika sana na ule uwanja kuliko labda hata Wizara ya Ujenzi, wasukume uwanja ule wa Moshi uweze kujengwa ili uwanja ule ni mbovu, umeharibika sana. Ni jambo ambalo marehemu mzee Ndesamburo

amelizungumza sana na mimi naomba kuendelea kulizungumza nikiwa nimelizungumzia miaka mitano na naendelea kulizungumza muda huu ambao namalizia Ubunge wangu wa Moshi Mjini. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ya Maliasili na Utalii nilishaliomba kwa Waziri wa Maliasili aliyetangulia, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na sasa namwomba Waziri anisaidie kama anaweza kulisukuma hilo suala ili tukaweza kuhakikisha kwamba ule uwanja unajengwa kwa manufaa ya kuimarisha utalii katika Mji wa Moshi na hasa Mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kabisa, ni suala la *corona* linahitaji utulivu mkubwa sana. Tunatakiwa tupambane nalo kwa utulivu, mioyo yetu ikiwa imetulia kwa sababu hili ni janga kubwa, lisitufarakanishe, tunatakiwa turudi tuwe kitu kimoja. Bado nadhani wewe ni kiongozi wetu tunyekuamini, endelea kuona jinsi ambavyo unatuunganisha pamoja ili tuhakikishe kwamba tunamaliza hili tatizo kwa njia ya mshikamano na maelewano kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mungu akubariki sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Japhary Raphael Michael. Sasa hebu tu-*test* Msekwa, Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, kama utapatikana vizuri utafuatiwa na Mheshimiwa Cosato Chumi, Msekwa huko huko.

**MHE. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya bajeti ya Wizara yetu ya Wizara yetu ya Maliasili na Utalii. Nitangulie kutangaza msimamo kwamba na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Wizara hii na hivyo naunga mkono hotuba nzima na naunga mkono maoni tuliyotoa sisi kama Kamati na ushauri na mapendekezo ambayo tumeipatia Wizara.

Mheshimiwa Spika, sina haja ya kurudia yale ambayo tumeshaandika na kuwasilisha, lakini naomba nijikite kwenye hoja yangu katika hili janga la *corona* na jinsi ambavyo

linakwenda kudidimiza Wizara hii ya Maliasili na Utalii tusipoanza kutafakari sasa hivi kama Wabunge na kama Taifa mbinu na mikakati mbalimbali ya kusaidia kuinusuru katika maeneo mawili muhimu.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la kwanza ni kwenye eneo la kunusuru upatikanaji wa mapato. Kwa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii na hasa *TANAPA* ambayo wameongezewa hifadhi kutoka 16 mpaka 22 walikuwa na marejesho makubwa ambayo lazima watoe Serikalini na gawio wote na *NCAA* wanatoa na *TAWA.* Ningeishauri Serikali kwamba hebu sasa tuondoe hizo tozo ili kuilimbikizia Wizara ya Maliasili na Utalii fedha za kujikimu katika kipindi hiki kigumu cha mpito. Huo ni ushauri wangu katika Sekta ya Mapato.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa pili ni kwenye eneo la kunusuru rasilimali yetu ya maliasili isije ikaporomoka katika kipindi hiki kigumu cha janga la *corona*. Kwa mfano, katika tasnia ya uwindaji ambayo ndiyo tasnia inayofanya shughuli za utalii unaoingizia nchi hii fedha nyingi za kigeni kwa kufanya biashara katika maeneo ya jamii kama *Game Controlled Areas.* Kwa mfano ile iliyoko katika Wilaya yangu ya Longid ambayo asilimia karibu yote ni *Game Controlled Area* na baadhi ya mapori yaliyohifadhiwa watakaposhindwa kupata wageni kwa sababu ya nchi mbalimbali ku-*lockdown* na kwa sababu ya watu mbalimbali kuogopa kusafiri wakati huu, nachelea kusema kwamba siyo ajabu baadhi ya makampuni ya watalii, kama siyo yote yata-*withdraw,* yataondoka kwenye zile *blocks* ambapo ndipo unapofanyika uwindaji.

Mheshimiwa Spika, nashauri tuone, sisi kama Taifa tumejipangaje kuhakikisha kwamba endapo kuna wawekezaji watakaojitoa kwa sababu ya hili janga la *corona* na wanaona hawatafanya biashara mwaka huu na pengine mpaka mwaka kesho. Tumejipangaje kuhakikisha kwamba rasilimali ambayo kwa uwepo wa hawa wawekezaji iliendelea kuwa endelevu, licha tu ya kuwinda walikuwa pia wanatusaidia kulinda. Sisi kama Taifa tumejipangaje

kuhakikisha kwamba rasilimali hiyo kwa kipindi hiki cha mpito wa gonjwa hili ambacho nami naungana na Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli kuamini kwamba litapita, ni kama tu vita vingine vyovyote. Tulikuwa na vita na Idi Amin mwaka 1979, vita vya silaha za moto na ikapita na tukashinda na hii ya *corona* pia, vita vya adui anaitwa kirusi wa *corona*, *Covid 19* naamini pia itapita, lakini mpaka ije ipite na madhara yake itakayotuachia ya kiuchumi, haya mapori yetu, haya maeneo yetu, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba yataendelea kuwa endelevu?

Mheshimiwa Spika, kama tutapenda kuibebesha *TANAPA* mzigo ambayo tayari hata kwa ongezeko la hifadhi sita mpya, tayari ina mzigo wa kutosha na rasilimali hafifu ya kwenda kuli-*manage* wala *power* ambao nao wana upungufu mkubwa wa wafanyakazi na Sekta ya Wizara ya Maliasili wana upungufu mkubwa wa wafanyakazi ndiyo watabebeshwa huo msalaba.

Mheshimiwa Spika, napenda niishauri Serikali kwamba huu ndiyo wakati muafaka wa kuuhisha ile Sera ya Uhifadhi wa Jamii kupitia maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za *WMA.* Maana yake nikiangalia *trend* ni kama Serikali iliipokea hiyo dhana ikajua inafanya kazi, lakini ikalegeza kabisa usimamiaji wake kwa karibu na kwa sababu rasilimali iliyoko katika maeneo hayo ya jamii ambapo ndipo zilipo *blocks* nyingi za uwindaji, ni rasilimali ambayo jamii imekuwa ikifaidika kwayo kutokana na mgao wanaopata baada ya wale wanaofanya biashara ya utalii kufanya biashara zao.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu kuna hatari ya wao kutoka au kushindwa kuilipa Serikali na kuilipa jamii, basi Serikali izipatie sasa jumuiya zote nguvu na *TAWA* iwajengee uwezo wawe ndiyo walinzi halisi wa rasilimali ile. Kwa zile jamii ambazo wameshaomba kwa muda mrefu wapewe *WMA* zao kama ya Longido katika eneo la *Lake Natron,* sasa ndiyo wakati muafaka Mheshimiwa Waziri aitangaze ile jumuiya kwamba sasa ni jumuiya halisi. Jumuiya ya Hifadhi ya *Lake Natron,* tena bila kufikiria habari ya

kuondoa ziwa maana yake lile ziwa ndiyo kichocheo kikubwa cha kuiuza ile *WMA* na kuiletea mapato makubwa.

Mheshimiwa Spika, ziwa najua *ramsar site* na najua Wizara ina mikakati ya kutaka kuifanya *protected wetland,* eneo lililohifadhiwa la uoevu ndiyo, lakini taasisi hii ya Uhifadhi wa Jamii ambayo inatambulika kisheria pia ina hadhi ya kujengewa uwezo waweze ku-*manage wetland,* waweze ku-*manage ramsar site* na waendelee kufaidika na matunda yanayotokana na utalii kwa asilimia kubwa kuliko ilivyo sasa hivi tunavyongojea mgao kutoka kwa wawindaji.

Mheshimiwa Spika, suala hili katika eneo la *Lake Natron* ni rahisi kwa sababu kinachowasababisha watu kwenda katika eneo la *Lake Natron* ambayo Serikali labda inahofia wataharibu mandhari ya Ziwa, hasa wakati huu wakati wa mabadiliko ya tabianchi, ni vitu viwili tu; ni maji na magadi. Suala la maji ni suala rahisi kabisa kwa sababu Serikali yangu hii sikivu kama imeweza kututolea maji Mlima Kilimanjraro kwa bilioni 15 mpaka Longido Mjini, haiwezi kushindwa kuteka maji yanayotiririka kwenye ziwa kwenye vyanzo mbalimbali; kuna vinavyotoka upande wa Kenya sehemu ya Shompole, kuna yanayotoka kule kwenye Nyanda za Ngorongoro wapeleke maji mbali na ziwa wale wanaotegemea yale maji waweze kupata maji kwa ajili ya mifugo yao maana yale maji hasa ni kwa ajili ya mifugo maana yana magadi.

Mheshimiwa Spika, rasilimali ya pili ni magadi na yale magadi ni madini kwa mifugo. Yale magadi ukichota leo kesho ukija huwezi hata ukaona kwamba yamechotwa maana yake yanaumuka kama unga uliotiwa hamira na wananchi wanaweza wakawekewa utaratibu waendelee kuchota magadi kwa ajili ya madini ya mifugo yao bila kuharibu lile ziwa lakini walihifadhi wao kwa kuwezeshwa na Serikali na wahifadhi maeneo yote ya nchi hii ili kuisaidia Serikali kuyalinda katika kipindi hiki kigumu cha mpito.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nilibahatika kuona kanyaraka fulani hawa wenzetu wa tasnia ya uwindaji

waliandika na naomba Serikali iangalie jinsi ambavyo watakwenda kuisimamia. Wao wameomba pia ahueni, wamesema kwamba katika hali tuliyonayo sasa hivi ili na wao wasiporomoke kabisa pengine Serikali ipunguze tozo au ifute kwa kipindi hiki lakini wale ambao wameshafanya biashara naomba walipe jamii.

Mheshimiwa Spika, pili, wameomba *blocks* zao walizokuwa wameandaa kwa mwaka huu zipelekwe *forward* ili waanze kutumia mwaka kesho na wasihesabiwe chochote mwaka huu. Tatu, wameomba zile *quarter* ambazo zinatolewa kwa mwaka huu pia zihamishwe kwenda mwaka mwingine unaofuata. La zaidi pia walikuwa wanalalamikia ile tozo ya asilimia kumi na nane ya *VAT* kwamba bado inawaumiza na sasa ndiyo itakuwa mbaya zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa sababu muda wangu umesiha; kulikuwa na hoja kwenye Kamati yetu ya miaka miwili sasa ya Watanzania waliokuwa wanafanya biashara ya viumbe hai, wale viumbe hai ilifika mahali Serikali ikasema hiyo biashara ya viumbe hai ikome na utaratibu wa kuwafidia wale wale wanyama hai waachiwe au Serikali ifanye inavyotaka na mpaka sasa hivi jibu halijapatikana. Ningeomba Waziri atakapokuja kuhitimisha leo kuna Watanzania wanatulilia sisi kama Wajumbe wa Kamati kwamba tuulizieni Serikali imetufanya nini kuhusu wale viumbe hai.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia tena kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nawapongeza Mawaziri wangu na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa inayofanyika kwenye sekta hii na matunda ambayo sisi Wanalongido tumevuna; tunatoa miti, tunatoa michango katika *Corporate Social Responsibility,* ni mwezi Februari tu tulijenga Kituo cha Afya pale Ketumbene**,** *OPD,* kwa ushirikiano na *facilities* zote za uhifadhi na waliniomba nitoe salamu na shukrani zao za dhati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, sana sana. Nilikwishamtaja Mheshimiwa Cosato David Chumi na ajiandae Mheshimiwa James Kinyasi Millya.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru wewe mwenyewe na pia kuwashukuru wananchi wa Mafinga walionileta katika jengo hili. Napenda tu kusema kwa kweli, nimefurahia sana kipindi changu katika Bunge hili. Nimejifunza mambo mengi na ningesema kwa Kihehe cha Malkia, ningesema, *I am proud of you, I am proud of your team,* Naibu Spika, Katibu wa Bunge, Maafisa wako ambao wamekuwa wakitupa ushirikiano mkubwa. Mimi binafsi hapa Bungeni ambapo ni mara yangu ya kwanza nimejifunza mambo mengi sana. Nasema tu wote pamoja na wewe Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, Mungu awabariki sana wananchi wa Mafinga, leo tulikuwa na *Full Council* ya mwisho kule Mafinga. Nasema kwamba, kama ambavyo waliniamini mwaka 2015 waendelee kuniamini 2020 na sasa hivi ndiyo niko *fit* zaidi. Kama wanavyoona kipara kinaendelea kung'aa ni kwa sababu ya *support* yao lakini pia kwa sababu ya ushirikiano ninaoupata katika kazi. Kwa hiyo, bado nipo na nitaendelea kuwepo, natumaini ushirikiano wao kwa sababu kupitia ushirikiano tumefanikisha mambo mengi katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga, nikishirikiana na Madiwani wenzangu, Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Mufindi na mkoa kwa ujumla, Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa. Kwa kweli, ushirikiano umekuwa ndiyo msingi wa kuinyanyua Mafinga katika miaka hii mitano kama Halmashauri mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, napenda kusema jambo moja. Katika maisha omba sana Mungu akujalie akili za kujiongeza kwa sababu akili za kawaida kila mtu Mwenyezi Mungu amemjalia. Akikujalia akili za kujiongeza maana yake ni kwamba utaweza kukabiliana na mazingira

kulingana na unavyokutana nayo. Kwa hiyo, mimi napenda kuwapongeza sana Wabunge wenzetu ambao Mungu amewajalia akili ya kujiongeza na wakaamua kuungana na sisi tuendelee kuchapa kazi tofauti na wale wengine ambao wao wameamua kukaa nje. Kwa hiyo, nasema Mungu awabariki sana kwa kuwapa akili ya kujiongeza.

Mheshimiwa Spika, napenda na mimi pia niseme kuhusu hili janga la *Corona*. Mheshimiwa Rais amesema vizuri sana na kwa kweli, kulikuwa na hali kama ya kupotea *confidence* miongoni mwetu na miongoni mwa Watanzania lakini hotuba ile ambayo ina-*trend* duniani kote imetuongezea *confidence* sana katika namna ya kukabiliana na janga hili lakini pia kupunguza uwoga.

Mheshimiwa Spika, sisi kule kwetu kuna msemo unasema, *"muwe welikoko"* yaani uwoga ni kama lijinyama fulani la kutisha sana ambalo ni adui mkubwa katika mambo mbalimbali ya maisha. Kwa hiyo, hata katika *Corona* uwoga ulikuwa mkubwa. Kwa hiyo, niendelee kuwapa moyo Watanzania kwamba kadiri Mungu ambavyo mwenyewe ataendelea kutuongoza na kama nilivyosema katika mchango wangu siku ya TAMISEMI kwamba Bwana asipoulinda mji waulindao wakesha bure, tuendelee kumtumainia Mungu tukiendelea pia kuchukua tahadhari kama ambavyo tunaelekezwa na wataalam mbalimbali wa afya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake. Mimi Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla nimesoma naye, yeye akiwa Muhimbili mimi niko Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam; tulifanya shughuli pamoja wakati wa mambo ya *cost sharing.* Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla mimi namfahamu, wako watu wanaweza wakawa wamemfahamu hapa, huwa hashindwi kitu na kwa kweli katika hili amethibitisha mambo mengi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, pongezi zangu ni katika sekta ya mazao ya misitu. Napenda kuendelea kupongeza Serikali, Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa hivi

mazao ya misitu yanasafiri saa 24, hoja ambayo niliisema karibu miaka mitatu baadaye Serikali ikaipokea na kuifanyia kazi, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, napenda pia kupongeza ushirikiano ambao sisi watu wa Mafinga na Mufindi tunaupata kutoka Shamba la *Sao Hill* pale Mafinga. Uongozi, Meneja na watendaji wake wote, hivi napozungumza *grader* lilikuwa Mafinga, sisi tunajaza mafuta, tunatengeneza barabara kupunguza makali ya hali za barabara. Hivi napozungumza liko kwa Mheshimiwa Kigola linaendelea kufanya kazi tunaenda zamu kwa zamu, likipunguza kule makali linakuja tena Mafinga kumalizia sehemu iliyobaki, napongeza sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nipongeze uongozi wa *TFS.* Hapa napozungumza wanatujengea mabweni mawili kwenye Shule ya Sekondari Changarawe na Shule ya Sekondari Luganga. Yote hii ni kupunguza *distance* ya watoto kutembea kwenda na kutoka majumbani wanapokwenda shuleni matokeo yake sasa watoto watakaa shuleni katika mabweni na watakuwa na utulivu wa kitaaluma, lakini pia tutawaepusha na vishawishi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda sana kupongeza kama nilivyosema na naendelea kutoa shukrani kwa Wizara hii ambavyo imesimamia suala zima la upatikanaji wa vibali kwa wavunaji katika Msitu wa *Sao Hill.* Hiki ni kitu ambacho napoingia mimi hapa Bungeni ilikuwa ni uonevu mtupu, wasiostahili hawapati vibali, wanaostahili wanarukwa, matokeo yake kunatengenezwa *scarcity* ya vibali, watu wanauza vibali wanapata mamilioni wenye kustahili wanakosa vibali. Kwa hiyo, sekta kwa ujumla pamoja na upungufu wa hapa na pale imetulia, ni mambo ambayo binafsi ninaona Serikali inastahili kupongezwa kwa niaba ya wananchi wa Mafinga ambao wanategemea sana mazao ya misitu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo napenda kushauri mambo yafuatayo. La kwanza, pamoja na janga la *Corona*

lakini pia bei katika Msitu wa Mafinga wananchi wangu wanaojishughulisha na masuala ya mazao ya misitu wanasema ni kubwa. Ukizungumza na wataalam wanasema bei sio kubwa isipokuwa ukubwa unatokana na tozo mbalimbali ambazo zipo katika kufanya kazi katika Msitu wa *Sao Hill.* Tuna jumla ya tozo 12, niiombe Serikali iziangalie hizi tozo ili kusudi ziweze kutizamwa kwa macho mawili kupunguza makali kwa sababu bei inakuwa kubwa kutokana na hizi tozo ambazo ziko zaidi ya 10.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili niiombe Serikali na hili naendelea kulirudia, nimeomba sana Serikali waone uwezekano wa kuwa na Chuo cha Misitu Mafinga kama vile *Campus* ya Olmotonyi. Sababu ninazo, Mheshimiwa Spika wewe ni Mhifadhi, Wilaya ya Mufindi katika tarafa zake zote ni moja tu ndiyo ambayo haizungukwi na misitu. Pia Wilaya ya Mufindi ndiyo mwenyeji wa msitu mkubwa katika Afrika.

Mheshimiwa Spika, pia wananchi wa Mufindi walitoa maeneo yao tupande msitu ule. Vilevile wilaya ina eneo la kutosha, hali ya hewa nzuri na hivyo kuwa ni sehemu nzuri kwa mazoezi kwa vitendo. Kwa hiyo, naendelea kuisihi Serikali na kuishauri, ione uwezekano wa kuwa na Chuo cha Misitu katika Wilaya ya Mufindi kwa maana ya pale Mafinga na majengo yapo, itasaidia sana kuongeza weledi katika tasnia ya mazao ya misitu hivyo, kuongeza thamani lakini mwisho wa siku kuongeza mapato kwa Serikali na pato la mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa kumalizia, napenda kutoa wito pia kwa Serikali kwenye suala zima la maeneo ya kumbukumbu. Pale Bumilanyinga tuna kumbukumbu ya Nyawenzi. Kama ambavyo wanafanya kule Isimila na Mgagao ambako nilishauri, lile ni gereza lina wafungwa hawazidi 30 na Mheshimiwa Mwamoto anafahamu, hebu tufanye ile sehemu ya kumbukumbu ambayo walikuwa wanaishi wapigania uhuru kutoka South Africa. Kulifanya gereza tunaondoa ule mvuto wa kufanya watu pale wafanye sehemu ya kivutio cha utalii...

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Kwa sababu wao wangependa kuja kuona ni eneo la utalii lakini wanakuta kwamba wamewekwa watu ...

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, taarifa, Msekwa.

**SPIKA:** Taarifa, Mheshimiwa Mwamoto, nimeisikia.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa mzungumzaji kuhusu suala la Gereza la Mgagao. Mwaka jana tulipata wageni kutoka South Africa wakiongozwa na Balozi wao lakini waliposikia kwamba ni magereza walishindwa kuingia na Balozi aliugua akaamua kurudi. Kwa hiyo, nataka nimpe taarifa tuendelee kupigana kwa pamoja ili kuhakikisha kile kinakuwa kivutio ndani ya maliasili.

**SPIKA:** Taarifa hiyo Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa kutoka kwa kaka yangu kwa mikono miwili. Niiombe Serikali na Mheshimiwa Spika na wewe utusaidie kutia msisitizo kwa sababu sehemu walipokaa wapigania uhuru leo kufanya kuwa gereza kwa kweli inapoteza ule mzuka wa watu kuja kutembelea, unawakumbusha machungu walivyokuwa wao wanakaa jela kule South Africa. Kwa miaka mitano tumelisema hili, sasa ifike wakati jambo hili lishughulikiwe na hii *REGROW* inavyoendelea basi tunaongeza maeneo ya kuvutia watalii lakini mwisho wa siku pato kwa Taifa, pato kwa wana Iringa, pato kwa wana Mafinga. Kama mimi ambavyo huwa nasema, Iringa ikinoga na Mafinga pia imenoga.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, napenda kuunga mkono hoja, naomba kuwaambia wana Mafinga tuko pamoja, kama kipara kinavyong'aa

kitaendelea kung'aa 2020-2025. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cosato Chumi. Tunakushukuru sana kwa mchango wako.

Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Riziki Said Lulida na atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya.

**ME. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Nimpongeze Waziri wa Maliasili, Mheshimiwa Kigwangalla; Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Kanyasu; Katibu Mkuu, Prof. Mkenda na Wakurugenzi wote ambao wanaongoza hizi taasisi za *TANAPA,* Ngorongoro, *TFS* na TAWA.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu tumepata bahati kupata nafasi ya kuzunguka kutangaza utalii kupitia Sheria na Haki za Walemavu ambayo imepitishwa mwaka 2014, walemavu tumepata nafasi ya kuwa Mabalozi wa Utalii Tanzania. Tunashirikiana na walemavu wenzetu duniani kuwa Tanzania kuwa karibu na walemavu inawezekana.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mama Selous, Mama Tembo na Mama Mjusi. Nashukuru namalizia kipindi hiki tembo Tanzania wameongezeka vya kutosha na wanyama ambao walikuwa tayari majangili wanacheza nao wako katika mazingira salama. Hii yote ni kutokana na utendaji mzuri wa Mawaziri wetu hawa na watendaji wao kusimamia suala la wanyama hao kuendelea kuishi wakiwa tulivu katika nchi yao ambayo ni asili yao. Selous kama unavyoifahamu ulikuwa Liwale unaijua Selous ya tembo, leo nenda Selous tembo wako huru, ukienda Serengeti tembo wako huru na simba wako huru. Mimi nasema Mwenyezi Mungu aendelee kuwalinda wanyama wetu ili kutuletea utalii endelevu. Wenzetu Ivory Coast walikuwa na wanyama kama hao sasa hivi ni kama historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tufanye mabadiliko kidogo katika Wizara, wanapotangaza Kanda ya Ziwa

inajulikana, wanapotangaza Kusini; Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma inaachwa. Napenda badala yake Mikoa ya Lindi, Mtwara watumie *Mtwara Corridor* itatusaidia sisi kutujua kama msaada au vivutio hivyo vinavyopelekwa Kusini, urithi huu unaotaka kutangazwa Tanzania usijumuishwe kusema Mikoa ya Kusini, hapana, tuwekeni katika Ukanda wa Mtwara*,* tutajua kama na sisi tumo. Maeneo yote ya maendeleo yameainishwa lakini Lindi, Mtwara, hamna. Hivyo, Mtwara *Corridor* imeachwa katika masuala ya utalii na maendeleo ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunazungumzia janga kubwa la *Corona* na janga kubwa la mafuriko ambalo imezikumba Wizara ya Maliasili na Utalii na kuufanya uchumi wa Wizara hii kudorora vibaya mno. Napenda kutoa ushauri mmoja, tumeiona *IMF* wameamua kutaka kutoa mikopo, *World Bank* wameamua kutoa mikopo na nchi mbalimbali ambazo zimeamua kutoa *grants* mbalimbali kuhakikisha kipindi hiki uchumi ambapo umedorora wao wataweza kutoa misaada au mikopo ili tusiyumbe na tusitetereke.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe angalizo na wewe kama mdau wa maliasili, andaa mara moja, weka Kamati au Tume Maalum itakayokimbizana maana huu ni muda mfupi tu, wenzetu Wakenya wameifanyia haraka na tayari wameshapokea pesa kama mnavyosikia, Kenya na Rwanda wamepata sisi Tanzania mpaka leo hatujui, je, tuliomba au hatukuomba. Sasa tusikutane na kusema awali kuu hii ambayo inawasaidia wenzetu sisi itakuwa kama ni gumzo, wenzetu wameshapata misaada, wanaweza kujenga barabara kipidni hiki sisi tutakuwa tumekosa hiyo *grant* au huo mkopo ambao ungefanya leo mashirika yetu kama *TANAPA,* Ngorongoro, *TAWA, TFS,* wafaidike na hiyo mikopo, waweze kutoka na kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, *TANAPA* na Ngorongoro ni hifadhi, hivyo watu wanachanganya na mashirikika ambayo yako kibiashara. Hizi ni hifadhi lakini watalii wanakuja mle ndani ya hifadhi hivyo ndiyo yanapatikana mapato ya kusaidia kuboresha uchumi. Katika kuboresha ndiyo wanakuwa karibu

na majirani kama vile Serengeti kupeleka misaada ya ujirani mwema.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ina kigugumizi kikubwa na wewe ni shahidi, tozo wanazozitoza kwa *TANAPA* kwa ajili ya miradi yake**,** kwa kweli haistahili ni kama kuwaonea. Tozo wanazotoa kwa ajili ya kujenga barabara, kwa kweli wanawaonea. Sasa leo tunaona *TANAPA* imesimama, haina mishahara, pesa zote zimeshaondoka, je, itajiendeshaje? Kama haijiendeshi ina maana kama *Corona* hii itachukua mwaka mmoja, *TANAPA* na Ngorongoro tutafunga. Ni wakati muafaka, Spika tumia nafasi yako kuweka Tume Maalum itakayosaidia Serikali kuhakikisha mashirika haya yasije yakafa, yana wafanyakazi 5,500,000 utawaweka wapi? Ajira zao zitapatikana wapi?

Mheshimiwa Spika, mimi natoa angalizo kwa vile nimekaa humo ndani kwa muda mrefu na nina uzoefu na Spika wewe ulikuwa Mwenyekiti wangu mwaka 2005, umenifundisha mazuri na leo nimekuwa humu ndani kama balozi wa kutangaza utalii na wanyamapori. Bila juhudi zenu nyie mimi nisingefika hapa, hivyo na hili lichukue kwa umakini uhakikishe mashirika haya yasije yakapotea au yakaanza kufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia tena, leo Tanzania hii tuna misitu, leo tunaona China wamefaidika na misitu kwa ajili ya kutengeneza dawa za asili kupitia misitu yetu lakini ni eneo ambalo liliachwa nyuma kwa muda mrefu tulikuwa tunaiangalia *TANAPA,* Ngorongoro, ndiyo, lakini Idara ya Misitu inahitaji misitu kwa ajili ya tiba asili. Misitu hii itatusaidia kipindi hiki tupate mazao yanayotokana na misitu ambayo itasaidia kuleta tiba katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipata bahati ya kuhudhuria mikutano ya COP25 ambao ulifanyika Madrid, haya tunayoyazungumza, *floods, Covid,* yote walikuwa wameyashazungumza, walijua kwamba kutatokea *pandemic* baada ya muda fulani. Mimi nilichojifunza, tunawanyima viongozi wetu kuhudhuria katika mikutano

mikubwa wakapata taarifa nzito ambazo zinakuja kusaidia nchi hii. Tunakwenda mikutano ya *WTO* hakuna Waziri wa Maliasili anayekwenda akajua nini kinafanyika mle. Wenzetu Kenya wamekwenda, miradi yote na *grants* zote zimepelekwa Kenya kwa sababu ninyi hamuwaruhusu akina Mheshimiwa Kanyasu kwenda, hamuwaruhusu Mawaziri kwenda, wamekaa hapa ndugu yangu hawana wanalolielewa zaidi ya kuzunguka Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala la maendeleo, jifunze ndani na jifunze nje wenzenu wanafanya nini. Mimi nawaomba tutoe *fund* maalum kwa ajili ya hawa viongozi kwenda kushiriki katika mikutano mbalimbali. Kule watakutana na *grants* lakini sisi hatutumii, tunatumia hela ya ndani, hela ya ndani haitatutosheleza kwa miradi ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekwenda mimi katika mkutano wa COP25 Madrid, Wakenya zaidi ya 80 wamekuja wengine wamekaa nje kama ma-*observer* na wengine wataalam kuona kinachofanyika mle ndani, wanatoka pale wanakabidhi maandiko, sisi tunakwenda mtu kama Riziki. Nimekwenda pale kwa sababu nina *interest* ya kuona kinachoendelea nataka nitoe mafunzo haya, waliokwenda katika COP25 waje walitaarifu Bunge wamejifunza nini, hizi *grants* zinafanya nini? Ina maana watu wanakwenda na kurudi hawana ripoti wala nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake tunapitwa na wakati, wenzetu Wakenya, Waganda na Wanyarwanda wanatukimbia, sisi tuko wapi? Kigwagalla yuko wapi mbona hapelekwi katika mikutano kama hiyo? Kanyasu yuko wapi? Mkenda yuko wapi? Kijazi yuko wapi? Mmejikuta mmewafunga ndani ya chungwa hawatoki matokeo yake leo tumeshakuwa katika *disaster* kubwa. Ukiacha *floods,* barabara zote Ngorongoro zimeharibika, barabara zote Serengeti na madaraja yote Ruaha yamekufa. Tunahitaji *grants* maana ndani hatuna uwezo mkubwa kwa sababu taasisi zimesha-*collapse.*

Mheshimiwa Spika, naomba unda Tume mara moja iende kwa *action with solution* ambayo itatusaidia kuhakikisha tunaandika miradi mara moja tusije kupitwa na wakati, tuna miezi sita tu kuhakikisha tunapata hela hizi vinginevyo hela hizi zitakuwa zimeshatumika na wenzetu watakuwa wameshatuacha. Ikiisha *Corona* na sisi tutakuwa tumeendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, janga la *Corona* tunatambua ni ugonjwa ambao Mwenyezi Mungu mwenyewe atajua lini atalimaliza hivyo tusiwe na hofu, binadamu ulizaliwa na utakufa. Je, tukikaa ndani tutafanya nini ndani, hakuna kitu.

Mheshimiwa Spika, leo nikuulize watu waliokuwa kama Magomeni, nyumba moja ina watu 20 unawaambia nakufanyia *lockdown*, umemweka *lockup* huyu. Hii *lock up* hii utamtoa lini katika hii *lock up?* Ina maana atakuwa asifanye kazi, watoto wake wasipate chakula umemuweka jela huna cha kumpa na nchi haina uwezo wa kumpa yule mtu. Ninaungana na Mheshimiwa Rais hakuna *lock down* hapa watu waende wakafanye kazi. Tanzania ya wafanyakazi wafanye kazi tuweze kuleta uchumi, uchumi huu utatusaidia hata sisi angalau na watoto wetu waweze kuja kufanikiwa. Kipindi hiki kigumu sio kipindi cha kulaumiana ni kipindi cha kusimama kila mmoja afanye kazi na katika kufanya kazi hii itatusaidia nchi yetu kuitoa kutokana na umasikini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuko katika ushindani wa kibiashara.

**SPIKA:** Ahsante sana!

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Allah Wakbar! Naunga mkono kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki. Nakushukuru sana Mheshimiwa Riziki Lulida. Sasa nilishakutaja Mheshimiwa Magdalena Khamis Sakaya, utafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere kule Msekwa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa niweze kuchangia hoja ya Wizara hii ambayo iko mbele yetu. Na ninapongeza sana hotuba ya Kamati ya Maliasili na Utalii ambayo ni mjumbe na tumetoa ushauri mzuri sana ambao tunaomba Serikali ifuate ili iweze kupeleka Wizara hii mbele.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake, lakini pia kwa kuwa wazi kwa namna ambavyo sekta ya utalii imeathirika na tatizo la janga hili la corona. Nampongeza sana amekuwa wazi ili angalau apate michango ambayo itaweza kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhifadhi wa mbuga zetu hapa Tanzania nachukua ni zaidi ya pato la Taifa, nachukua ni zaidi ya uchumi kwa wananchi ambao wanazunguka hifadhi zile, nachukua zaidi kabisa ni kwamba, ni utajiri na vivutio ambavyo tumepewa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya vizazi vya leo na vizazi vya kesho. Suala la mapato ni suala ambalo tumenufaika nalo, lakini kikubwa zaidi tunahifadhi ili kwamba, viendelee kuwepo kwa ajili ya watoto wetu leo na wajukuu wa kesho waweze kuvikuta ni utajiri wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, janga hili la corona sio kwamba, linaathiri sekta hii kwa baadhi ya mapato tu kubwa zaidi ni kwamba, tusipoweka mkakati, tusipoweka mipango rasilimali iliyoko ndani ya hifadhi hizi yote itateketea. Serikali imefanya kazi kubwa sana kuweza kudhibiti ujangili, sana kabisa na tumepunguza ujangili kwa asilimia kubwa katika Tanzania nzima kwa muda wa miaka kama mitatu minne ambayo imepita, lakini kwa janga hili kama Serikali haijanyanyua mkono namna ya kuweza kusaidia hizi hifadhi ziendelee kuwepo ujangili unarudi asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, na mbuga zetu zitavamiwa vikubwa sana kwa sababu, majangili hawapo mbali wako wamezunguka. Kwa kuwa sasa hivi mashirika yetu ya uhifadhi hawana pesa na hata wale watumishi pia wanaelekea sasa hivi kwenda kushindwa kuwalipa, lakini pia doria hazifanyiki

kwa jinsi ambavyo zilikuwa zinafanyika, majangili wanajua kabisa kwamba, hifadhi ziko wazi, wataingia, watawinda, yatakuwa ni mashamba ya bibi, *by the time corona* inaisha hakuna rasilimali ndani ya zile hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali pamoja na kuwa ushauri umetolewa na Wabunge mbalimbali kwa hiyo, tuanze kutafuta mikopo labda, tuombe hata kupunguziwa riba, lakini lazima tutafute nguvu ya ndani ya haraka tusisubiri huko nje, nje tutachukua muda mrefu, tutafute nguvu ya ndani ya haraka. Leo kama *TANAPA* inashindwa kulipa watumishi askari wanaoenda kulinda, nataka nikuhakikishie kwamba, askari wale watajilipa wenyewe kwa kutumia raslimali iliyoko mle ndani watajilipa kwa hiyo, tukisubiri mpaka tupate nje tunazidi kuchelewa, naiomba Serikali ichukue hatua za haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia leo bado *TANAPA* niliwahi kushauri na kila mwaka huwa nashauri hapa kwenye Bunge. Ninasema kwamba, lazima Serikali ione namna gani mashirika ya uhifadhi yaweze kuwa na amana ya akiba ikitokea *crisis* yoyote iwe ni ndani ya nchi au nje ya nchi waweze kuendeleza rasilimali hizi. Yale ninayosema miaka yote hata kwenye *Hansard* mkienda mtakuta, leo yametokea, tayari ndani ya miezi miwili tu ya corona *TANAPA* mwezi mzima hawana mtalii hata mmoja na hawana akiba na hawana mradi wowote wamekaa wanaangaliana na Serikali ilikuwa inatujibu hapa Bungeni kwamba, ikitokea *crisis* Serikali ipo; sasa leo Serikali ipo, wapi!

Mheshimiwa Spika, naiomba lazima tujifunze kutokana na makosa. Lazima mashirika haya ya uhifadhi ili yaendelee kuwa *sustainable* tuwe na mfuko wa amana tusiendelee kuchuma tu tunakamua ng'ombe mpaka tunamaliza maziwa yote, hiyo *crisis* ndio yanayotokea sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo *TANAPA* inatoa 20% ya pato lake kwenda Serikalini, lakini leo sasa *crisis* ndani ya miezi miwili hata ile 20% iliyokuwa inapelekwa Serikalini hakuna

hata *percent* moja irudi kwenda kuwasaidia, barabara zimeharibika, leo kila kitu ni hovyo. Lazima mpango mkakati wa haraka sio kusubiri. Ikifika miezi mitano minne na hii corona inavyoendelea inaweza ikachukua mwaka, hatuna hifadhi, hatuna wanyama. Itakuja kuchukua gharama kubwa sana kuweza ku-*restrain* ile hali, lakini pia hata watalii wakija tena vile vivutio na ule utamu wa hifadhi zetu utakuwa tena haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana tusisubiri tu-*scale down.* Muda huu ni muda wa janga, Serikali i-*scale down* baadhi ya miradi ambayo ni mikubwa inayotumia fedha nyingi ipunguze kiasi cha fedha angalau tuisubirie kidogo kwa sababu, miradi ipo itaendelea kuwepo, lakini hawa wanyama wakindoka kuwarudisha itakuwa ngumu, ku-*restrain* ile hali itakuwa ngumu. Tu-*scale down activities* kubwa zinazotumia fedha nyingi, ili fedha ile iweze kwenda kwenye kusaidia Shirika la *TANAPA* kuhakikisha kwamba, watumishi wanalipwa, barabara zile zipitike, doria ifanyike, rasilimali zetu ziendelee kuwepo, lakini pia kwa ajili ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi tumeanzisha Wakala wa Misitu. Na ninashukuru kwamba, wakala wa misitu amefanya kazi kubwa sana tena nzuri, *TFS,* wamefanya kazi kubwa kwelikweli, lakini tumekuwa tunaomba kama kamati wapewe mamlaka waweze kusimamia vizuri rasilimali zetu wajitegemee kama ilivyokuwa *TANAPA* leo au Ngorongoro leo, lakini leo ni mwaka wa tatu kwa nini kinatuchelewesha?

Mheshimiwa Spika, tunaomba *TFS* wapewe mamlaka, wapewe *authority* inayojitegemea waweze kufanya kazi kubwa zaidi. Leo katika nchi yetu ukiangalia 53% ya misitu yetu inamilikiwa na Serikali za Mitaa, 47% inamilikiwa na Serikali Kuu kwa hiyo, ukiangalia kwamba, asilimia kubwa ya misitu yetu inamilikiwa na Serikali za Mitaa, lakini ukiangalia kwamba, Serikali za Mitaa wako chini ya TAMISEMI kwa hiyo, kuna mgongano wa usumamizi wa misitu. Napenda kujua ni lini tutahakikisha kwamba, mgongano huu unaondoka kwa maana ya kisitu iweze kusimamiwa vizuri?

Mheshimiwa Spika, leo Serikali za Mitaa zina uwezo au Mwenyekiti wa Kijiji ana uwezo wa kwenda kutoa vibali tu kuvuna misitu ya Serikali, misitu ya kijiji au msitu wa Serikali za Mitaa, lakini wakati huohuo Serikali imezuwia kwenye eneo lile hakuna kuvuna misitu. Kwa hiyo, kuna migongano mikubwa na ndio maana unaona asilimia kubwa ya misitu ya asili ya Serikali za Mitaa imeangamia, imeondoka, yani ni matatizo. Kwa hiyo, tunaiomba kuondoa migogoro hii lazima kuwepo na *syncronization* kwamba, namna gani misitu yote nchi nzima iweze kusimamiwa kiutaratibu ili kuhakikisha kwamba, uhifadhi wetu wa misitu unakuwa ni mzuri na unakuwa unamgusa kila mtu na Serikali Kuu isimamie.

Mheshimiwa Spika, namna ambavyo napendekeza kabisa, namna ambavyo Mheshimiwa Rais aliruhusu kwamba, ardhi waweze kumiliki kuanzia mpaka chini wale watumishi wasimamiwe na Serikali Kuu. Naomba pia, wakati huohuo watu wa misitu wasimamiwe na Serikali Kuu, ili Waziri awe na *mandate* na mamlaka ya ku-*order* kule chini nini wafanye kuhusiana na misitu ya Serikali za Mitaa ambayo iko kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho suala la *WMA.* Nashukuru kwamba, uanzishwaji wa *WMA* ulikuwa ni tija kubwa sana. Na ni mfumo ambao kiukweli lengo lake kubwa ni kushirikisha Wananchi kushiriki kikamilifu kwenye uhifadhi wa maliasili zao. Na wamefanye kazi nzuri, wameupokea mfumo huu mfumo huu vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wananchi wengi ambao wananufaika sana na mfumo huu, maeneo ambayo tayari zile *WMA* zilipata *full mandate,* maana yake AA – *Authorised Association* na wanaingiza vipato vikubwa kwa ajili ya jamii zinazowazunguka. Maeneo ambapo bado na ambayo mengine yalianzishwa na wafadhili wakaondoka yameachwa sana, hakuna ile nguvu tuliyokuwa tunaiona kuhakikisha kwamba, maeneo yote ya *WMA* yanapata nguvu, doria zinakuwepo, Serikali Kuu itoe nguvu iwezeshe.

Naiomba Serikali kwa kuwa, bado hatuwezi kuwaacha wananchi nyuma kwenye uhifadhi tuhakikishe kwamba, maeneo yote ambayo yalianzishwa na hayajafikia kwenye *level* ya *AA* kwa maana ya mamlaka ya kutumia rasilimali zilizoko mle ndani, Serikali iwekeze mle.

Mheshimiwa Spika, najua corona itaisha bado tutarudi kwenye *business as usual.* Serikali iwezeshe mle ili rasilimali iliyo kule ndani mle ndani ya zile hifadhi iweze kutunzwa na wananchi walioko kule waweze kuona faida yake na kila mmoja awe ni *part and parcel* kushiriki kikamilifu kwenda kwenye uhifadhi wa maliasili ambazo zinazunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiacha hivi maeneo haya kwanza tunawakatisha tamaa Wananchi wale ambapo wamekuwa wanajitolea, wanalinda kwa kutumia rungu, mapanga, wanakesha porini, leo rasilimali ambayo imekuwa kule kwa muda mrefu itaangamia na hata nguvu iliyowekezwa pale itakuwa imepotea, lakini pia sisi kama Taifa pia tutapoteza nguvu kubwa, tutapoteza mapato mengi kutokana na kwamba, maeneo haya licha ya kwamba, yananufaisha jamii ile, lakini pia yanaingiza kipato kikubwa kwa ajili ya Taifa letu na kwa ajili ya mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, yangu ni hayo machache kwa leo. Nikushukuru sana kwa nafasi, niendelee kuwapa Watanzania pole kwa corona na tuendelee kuzingatia masharti. Hakuna sehemu ambapo hakuna corona, ukikaa ndani corona ipo, ukitoka nje corona ipo, kikubwa ni kufuata maelekezo, kikubwa ni kuweza kujikinga, kikubwa ni kuhakikisha kwamba, wote tunachukua hatua stahiki tupambane na gonjwa hili; hata ukijificha ardhini bado waliopoteza maisha hawakuwa wanazurura walikuwa nyumbani kwao, lakini bado pia waliondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikushukuru pia, wewe, umechukua nguvu kubwa kuwalinda Wabunge wako kwa kila namna na gonjwa hili, endelea. Umetulinda na kweli

asiyetaka kuelewa asielewe, lakini umechukua jitihada hizo zote, *initiative* kubwa kuhakikisha kwamba, Wabunge wanakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mungu akubariki sana. Ahsante kwa kunisikiliza, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kamishna Magdalena Sakaya, tunakushukuru sana. Nilikwishakutaja Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere kule Msekwa na baada yake tutakwenda visiwani, tutaanza na Mafia halafu Zanzibar, Mheshimiwa Mbaraka Dau na Mheshimiwa Ally Salleh. Mheshimiwa Getere, tafadhali!

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuendelee kupiga kura.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nafasi uliyonipa ya kuchangia Wizara ya Maliasili na Utalii. Nikushukuru kwanza kwa kazi ambayo unaifanya kubwa, kazi kubwa sana ambayo unatufanyia hapa Wabunge, umetulinda miaka mitano kwa hali na mali; Mwenyezi Mungu ndio ataona ulichokifanya, wanasema tenda wema nenda zako.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Waziri wake Kigwangala. Na mara nyingine kunakuwepo na maneno mara hela zimetumika, mara nini, lakini kusema kweli Mheshimiwa Kigwangala ametufanyia kazi nzuri kwenye Wizara hii, yako mambo mengi hata *channel* yenyewe tunayoizungumza ni nzuri sana tulikuwa hatuyajui mambo mengi sana; tulikuwa hatujui hata utamaduni wetu umekaaje, tulikuwa hatujui kwamba, kuna mbuga zina nini kuna kitu gani kinafanyika maeneo ya huko nje, lakini sasa tunaona mambo yanaenda. Hongera sana Mheshimiwa Kigwangala Mungu akulinde uende ufike kwenye maeneo yako, utakapofika hapo ukishinda basi na

wewe unapokuwa huko utukumbuke na sisi wajumbe wako wa kamati kwamba, tumekaa na wewe muda wote huu tulikuwa tunakulinda na unaendelea kuishi vizuri.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru kamati, Mheshimiwa Kemilembe tunamshukuru sana. Ni Makamu wetu, lakini Mwenyekiti ameshika vizuri na Mungu amsaidie na Kamati nzima ya Maliasili na Utalii. Naibu Waziri, Watendaji wote na katibu katika Wizara hii wamefanya kazi nzuri. Makamishna wa *TANAPA,* Kamishna *TAWA,* Kamishna *TFC,* wamefanya kazi nzuri sana na hali ya hewa imebadilika, lakini Mungu atawasaidia mtarudi kwenye hali yenu ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa uvumilivu wake. Na kwa kweli, tumempongeza kwa hali ilivyokuwa yote mambo alikuwa anafanya; mwanzoni dunia ilimuona kama vile anafanya vitu vya kituko, lakini sasa imekuwa kama wale wanamuziki waliosema wamebana sana, lakini wameachia, tatu bila. Kwa hiyo, wote nchi zote duniani, nilikuwa naangalia hapo wale wakubwa wote, Marekani, Russia na nchi kama Uingereza, Brazil, Italy, German, zote zile *ten* bora za u-corona ziko kwenye nchi zenye hela.

Mheshimiwa Spika, Marekani kwa mfano imetoa *2.5 billion* kuweka watu *lock down,* imeshindikana wametoa nje. China wametoa *6.5 billion* imeshindikana wametoka nje, kwanza China sasahivi ni ya 11 huko. Kwa hiyo, tunapokuwa tunazungumza Wizara hii ya Utalii tusitegemee kwamba, kuna corona itaisha leo. Nilikuwa naangalia sasa hivi kesi zilizoko ni kama milioni tatu na watu waliokufa ni kama laki mbili. Ukiangalia hizo kesi zilizopo asilimia yake ni kama asilimia 9.1 ya watu wanaoishi Newyork milioni 40. Sasa kama dunia ina watu wote hawa waje wapimwe, corona ionekane kwamba, haipo ni 2025 wengine tutakuwa tumeshakufa. Kwa hiyo, habari ya corona ni kujiandaa kuishi na corona, corona hatutegemei itaisha leo kwa hiyo, ni kujiandaa kuishi na corona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na nimshukuru Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Shekilindi, maana watu wanaoteshwa, lakini

inaonekana kwamba, hali yake ni nzuri sana sasa hivi. Ile dawa yake ambayo ameileta tusiifanyie mzaha, tuombe watu wa *NEMC* waende wakaifanyie uchunguzi na madaktari wakaifanyie uchunguzi. Wengine ambao tumeifanyia utafiti wa kawaida ni dawa nzuri sana, tusiogope kuitaja kwa hiyo, kwa wote ambao wanaweza kukubalika kwamba, kikombe kiko hapahapa hakuna namna ya kusubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia hapa najiuliza jana ulikuwa umezungumza mambo mazito ya juu ya kulinda Bunge letu. Nchi yetu wanasema *three pillars of the Government,* maeneo yale ambayo Serikali inakuja tunakuwanayo tuna *Executive* – Serikali, tuna *Parliament* – Bunge, tuna *Judiciary* – Mahakama, tuna sehemu tatu ambazo ndio zinalinda Serikali. Sasa leo tumepata janga, nchi 215 zimepata janga, wengine Mahakama wanafanya kazi, Jaji Mkuu anahangaika na watu wake. Serikali inafanya kazi kina Jemadari wetu Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Polisi, madola wote wanafanya kazi, leo sisi Wabunge tunakuja humu kazi yetu hii ambayo tumepangwa zile nafasi tatu, tumepangiwa, watu wanaenda kujifungia.

Mheshimiwa Spika, wanajifungia humo ndani eti badae watoke nje waende kupigiwa kura. Umeshindwa kutatua matatizo ya wananchi Bungeni unajifungia baadaye uende kumuomba kura, sheria ipitishwe ipitiwe upya, watu hao katika janga hili la corona wameasi nchi. Tuangalie kama kuna uwezekano wa kuwafungia kutogombea, ili wapate adabu katika mambo haya ambayo tunaendanayo, hatuwezi kuwa na watu ambao sasa tumefika vita yetu ndio tunaenda mstari wa mbele, halafu wao wanaenda kujifungia wakitoka hapo waende kuomba kura, hilo nalo sasa muangalie namna ya kutafuta sheria ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, nizungumze habari ya Bunda; niishukuru Wizara ya…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa, naomba nimpe Taarifa Mchangiaji.

**SPIKA:** Taarifa!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Wabunge wengi wametaharuki kuhusu hiyo dawa ya Mbunge mwenzetu; je, haitakuwa sahihi sasa iletwe hapa Bungeni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Getere unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, wazo zuri sana kama watu wanasafirisha dawa na ndege kutoka nchi, sisi kuna haja gani ya dawa hizo kuletwa huku zikafanye utafiti?

Mheshimiwa Spika, dawa iko hapahapa. Mheshimiwa Shekilindi badaye utawaona wahudumu wanaohusika na mambo haya, Katibu wa Bunge na utamuona Spika watafanya utaratibu. Kwa hiyo, dawa tuweze kui-*confirm* kwa watu wetu na watafiti wetu waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nazungumza habari ya Bunda, Jimbo la Bunda limekuwepo toka mwaka 1980 na uharibifu wa mazao ya wakulima umekuwepo muda mrefu sana na watu wamekuwa wakidai hela kwa muda mrefu sana, lakini sasa toka nimekuwa Mbunge naishukuru Wizara ya Maliasili na Utalii wamelipa milioni 233. Si hela kidogo ni hela nyingi kwa hiyo, kwenye Vijiji vya Unyali, Kihumbu, Maliwanda, Mgeta, Kwandege, Kingilima na Nyangee na Kiloleni, wamelipwa fedha na sasa kuna watu 1,548 wanadai. Nimeona hapa wananiambia, nilikuwa naongea na mtaalam mmoja anasema tulikuwa tunakwenda kufanya tathmini sasa corona imetokea.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie Wataalam wa Wizara corona haitaisha kwa hiyo, tuendelee kuwahudumia watu kadiri wanavyokuwa na mahitaji kwenye meneo yao. Kwa hiyo, baada ya Bunge hili kuendelea wakati tukimaliza

hii bajeti watu waende Bunda watu walipwe hela zao, watu 1,548 wanadai na tunaomba mkawalipe, nawashukuru mmefanya kazi nzuri ya kuwalipa wale waliokuwepo.

Mheshimiwa Spika, kuna miradi ya kijamii, niishukuru Wizara ya Maliasili, *TANAPA, TAWA* na *TFS. TANAPA* wametoa milioni 125 Kituo cha Afya Unyali na wametoa milioni 55 na wametoa milioni 105 zinakwenda kujenga nyumba ya mganga Zahanati ya Kihumbu ambayo na wao wananchi wamejiandaa kwamba, ile zahanati wanataka iwe kituo cha afya. Tunawashukuru sana, lakini pia maombi ya Maliwanda ya milioni 75 ya kujenga wodi tuendelee kuwapelekea tukawafanyie hiyo kazi, ili waweze kupata wodi yo ya watoto. Nawashukuru Wizara kwa ujumla mmefanya kazi nzuri Mungu awasaidie na sisi mtuombee; Wabunge wako mwingine alikuwa aaniambia hapa kwamba, tunakwenda kugombea, mwingine akasema tunaenda kugombea au tunaenda kuendelea?

Mheshimiwa Spika, sasa wanaoenda kuendelea wapo na wanaoenda kugombea wapo. Kwa hiyo, kila mtu atakwenda na maombi yake anayoweza kuyaona kwamba, yanakuwepo, lakini nadhani kwa kazi nzuri ambayo tumefanya hatuna budi kwamba, kwa Wabunge wote walio kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano watakwenda kugombea na Mungu atawasaidia watafaulu kwenye majimbo yao.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna lugha iko huko nje, hata watoto wangu wananipigia simu wanasema Bungeni huko tunasikia corona ndio imekomaa. Corona iko mahali nchi 215, eneo la Bunge liko salama watu ndio wanaugua corona sio Bunge linaugua corona kwa hiyo, Bunge liko salama, Bunge liko vizuri, lakini watu tunaoishi kwenye maeneo haya kwa shughuli mbalimbali tunazozifanya unaweza ukapata corona, sio Bunge lina corona. Kwa hiyo, ni Kiswahili ambacho kwa kweli, kinatakiwa kutafsiriwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, Mungu akusaidie. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere. Nilikwishakutaja Mheshimiwa Mbunge wa Mafia Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi hii, nianze kwa kukushukuru na kukupongeza sana kwa namna ambavyo unakitendea haki hicho Kiti ulichokikalia hapo na hata wale wachache wanaojaribu kuku-*beep-beep* umeweza kuwaonesha kwamba, uko imara kabisa. Nakushukuru na ninakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna alivyo mstari wa mbele katika kupambana na hili janga la gonjwa la *Corona*. Mheshimiwa Rais, Watanzania wamekusikia na wanakuunga mkono na kwa pamoja tutalishinda hili janga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtoa hoja, Waziri wetu Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Constantine Kanyasu, wanafanya kazi nzuri sana. Binafsi tu kwa mfano mdogo, nilitoa hoja kwao kwamba mimi natokea Mafia ambacho ni kisiwa cha kitalii. Nikaenda kumwona ndugu yangu Mheshimiwa Kanyasu nikamwambia, mbona ile *Television* ya Utalii ya *Safari Channel* hakuna chochote kinachohusiana na Mafia ambacho kinaoneshwa mle? Akaniambia subiri tunalifanyia kazi. Ndani ya wiki mbili, wataalam wakaenda wakafanya *shooting* na sasa Mafia imo katika kituo kile cha *Safari Channel,* tunawapongeza sana. Hii inaonesha ni namna gani wanafanya kazi nzuri na iliyotukuka.

Mheshimiwa Spika, leo nitatofautiana kidogo na wachangiaji wengine kwa namna ambavyo nitawasilisha hoja yangu. Wengi wanazungumzia, (na ndiyo bajeti yetu ilivyo) kwa kiasi kikubwa sana bajeti hii kila mmoja anavuta, anataka kwake kwa maana ya kutumia, kutumia, kutumia. Eneo la kuishauri Serikali iweze kupata pesa kwa ajili ya hayo matumizi, kunakuwa na maelezo machache sana.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu wa leo kwa sababu hii ni Wizara ambayo inaleta mapato kwa kiasi kikubwa sana, nitatumia muda wangu kuishauri Serikali namna bora ambavyo inaweza ikaongeza mapato kupitia Sekta hii nyeti kabisa ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema awali, mimi natokea Kisiwa cha Mafia ambacho ni kisiwa cha kitalii. Kama ambavyo ilivyo Zanzibar na Mafia zinafanana fanana. Zanzibar walikuwa wanategemea sana karafuu pamoja na uvuvi na Mafia tunategemea nazi pamoja na uvuvi. Baadaye karafuu kwa upande wa Zanzibar ikaanguka na uvuvi nao ukayumbayumba, uchumi wao ukanyanyuliwa na utalii. Nasi Mafia hivyo hivyo tunapata matatizo kama hayo; nazi zimeanguka, uvuvi nao haufanyi vizuri sana na sasa tunaelekea kwenye utalii.

Mheshimiwa Spika, Kisiwa cha Zanzibar na ndugu yangu Mheshimiwa Alberto najua ndiye atakayefuata baada yangu anaweza kunisaidia zaidi. Kisiwa cha Zanzibar kinapata watalii wastani wa 400,000 mpaka laki 600,000 kulingana na misimu, lakini Mafia ambayo kwa kiasi kikubwa ina-*offer* zaidi ya vivutio vya Zanzibar inapata watalii; nilipoingia pale mwaka 2015 tulikuwa tunapata watalii 4,000, sasa hivi ndiyo tumesogea tupo kwenye watalii 8,000. Utaona tofauti ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sasa ipo haja ya wadau wa utalii ndugu yangu Mheshimiwa Kigwangalla tukae chini kujua, kwa nini Mafia haipati watalii wengi? Moja ya shida na ambayo niliizungumza hapa takribani siku nne au tano zilizopita ni suala la *accessibility.* Kuingia Mafia ni shida; lazima uende na ndege, usafiri wa maboti unasumbua.

Mheshimiwa Spika, sasa nilizungumza sana wiki iliyopita kwamba tuna shida ya usafiri na tuna meli ipo pale. Sasa inawezekana zaidi ni suala la watu wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, lakini Serikali ni moja. Mheshimiwa Kigwangalla wewe ni *very aggressive,* mwende huko mkakae kwenye Serikali mshauriane, hivi inakuwaje? Inaingia akilini

kiasi gani? Meli ipo, ina uwezo wa kupakia abiria 260, lakini mpaka leo tunahangaikia kibali kwa mwezi mmoja, halafu kuna Maafisa wanatukwamisha kutoa kibali tu, wanatoa visingizio vingine vya ajabu ajabu.

Mheshimiwa Spika, kuna Afisa katumwa kutoka Dar es Salaam kwenda kufanya ukaguzi pale Nyamisati, kutwa nzima hajafika. Tunakwenda kulielezea hili suala, meli imeondoka imekwenda Mafia. Sasa taasisi inalazimika kuchukua wataalam wengine. Ni gharama nyingine hizo kuwapeleka waende wakafanye kazi ile ile ambayo alitakiwa aifanye mtu mwingine kule Nyamisati. Matokeo yake wananchi wanateseka na watu wanapoteza mali zao.

Mheshimiwa Spika, leo hii watalii wote wanaokuja Mafia wanatumia usafiri wa ndege. Hawawezi kuja na maboti. Ndugu yangu Mheshimiwa Chumi hapa kuna wakati alinijia anasema, kuna watalii wako Iringa kule wanataka kuja Mafia, lakini wamesema hawataki ndege, wanataka kuja na boti. Nikawaambia, bora wasije kwa sababu huku kwenye boti hakupitiki.

Mheshimiwa Spika, sasa leo tumepata meli, ipo bandarini, mwezi mzima tunahangaikia vibali tu. Kama haifai kama mwenyewe unavyosema, basi semeni iondoke tuendelee kusubiri hiyo ya Serikali ambayo wametuahidi wakubwa itapatikana hivi karibuni, badala ya kuendelea kuiweka pale bandarini, mtu ana njaa unampitishia sahani ya biryani inakuwa kama vile unamtia ushawishi halafu baadaye humpatii kile chakula.

Mheshimiwa Spika, sasa nalizungumza hapa kwa maana ya kwamba wenzetu wa Wizara ya Ujenzi kwa kushirikiana na ninyi watu wa utalii, mfike mahali sasa, tunataka tutoke kwenye watalii 8,000 twende angalau 20,000. Tunayo *capacity* ya kwenda mpaka 100,000 lakini kama ni kupitia kiwanja cha ndege peke yake, haitawezekana. Kama meli ipo, basi ipewe kibali, ianze kazi. Imekaa pale toka tumezungumza, kesho yake naambiwa wataalam wakaenda pale, lakini mpaka leo hakuna majibu,

Mheshimiwa Spika, hatulazimishi kwamba lazima watoe kibali, wakiiona haifai, waseme haifai iondoke, basi tutaendelea kupanda yale magogo ambayo wao ndio wanasema yanafaa. Chombo ambacho kina injini mbili za kisasa na vifaa vyote vya usafiri kinaonekana hakifai, linafaa gogo lenye injini moja ambalo kila siku linazimika watu wanahatarisha maisha yao katikati ya bahari.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa tu nawashauri wenzangu wa Wizara ya Utalii pamoja na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano wakae pamoja kuangalia ni namna gani watatutoa hapa. Inakuwa inatusumbua sisi katika kuwaelezea wananchi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nasikia kengele imegonga. Nilikwenda kwake Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Mafia kuna viboko pale. Kuna viboko, wanyama wamekuja, sijui wamefikafika vipi, lakini wapo pale Mafia. Wamekuwa wengi sana kiasi kwamba wameanza kuhatarisha maisha ya watu na tayari mtu mmoja ameshapoteza maisha na mazao pamoja na mimea imekuwa ikiliwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho tulipoongea, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla akaniambia kwamba wamekubaliana watakuja kuwafanyia mnada. Wakishawafanyia mnada watavunwa kwa sababu *space* ya Mafia ni ndogo na wale wanazidi kuzaliana na inaleta hatari ya mwingiliano baina ya viboko na wananchi.

Mheshimiwa Spika, ule mpango wa kuja kufanya mnada, naona mpaka leo hauja-*materialize.* Sasa atakapokuja kufanya *winding-up* namwomba sana atuambie. Kwa sasa hivi hatujasikia matukio, lakini tusisubiri mpaka mtu mwingine apoteze maisha au watu wengine wapoteze maisha halafu ndiyo tuanze kuchukua hatua. Ni vizuri sana Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla aje haraka sana

Mafia wafanye utaratibu ama wa kuwa-*reallocate* wale viboko waende maeneo ya Rufiji huko ambapo ndiyo kwenye *origin* yao, kwa akina Mheshimiwa Mchengerwa.

Mheshimiwa Spika, lingine, ni *entrance fees;* nililizungumza hili. Japokuwa kuna *entrance fees,* kuna eneo la hifadhi ya bahari kule Mafia ambalo ili mtalii aingie lazima alipe dola 24, lakini sasa imekuwa ni kikwazo kwa biashara ya utalii. Natambua kwamba ile *entrance fees* siyo sehemu na hairatibiwi na Wizara yako ya Utalii, inaratibiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Ipo haja mkakaa sasa Wizara mbili kwa sababu wadau wa mahoteli wanalalamika kwamba gharama za utalii wa Mafia ni kubwa sana. Mtu kabla hajafanya chochote anatakiwa alipe dola 24 kila siku atakayoitumia ndani ya maeneo ya hifadhi. Kwa hiyo, imeonekana ni gharama kubwa na imekuwa kama ni kikwazo fulani hivi cha kufanya utalii mkubwa sana pale Mafia.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na mwenzake Mheshimiwa Waziri Mpina kule Wizara ya Mifugo na Uvuvi lifanyiwe kazi hilo ili liweze kuondoka na watalii wapate kuongezeka.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunivumilia na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau na poleni sana wananchi wa Mafia kwa kufiwa na Mbunge wenu wa awamu iliyopita Mheshimiwa Abdul Karim Shah, maarufu kwa jina Burji.

Nilishakutaja Mheshimiwa Ally Saleh na baada ya hapo tutaenda Kigoma kwa Mheshimiwa Peter Serukamba. Mheshimiwa Ally Saleh kutokea Ukumbi wa Msekwa.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii tukijua kwamba utalii ndiyo roho ya Zanzibar. Kusema kweli katika hotuba zote zilizokuja, hii ndiyo ya kwanza kabisa imetendea haki *Corona* na uchumi au na maendeleo. *I was not expecting less* kutoka kwa mzee wa nje ya *box.* Nilikuwa natarajia tu kwamba kitu kama hiki tungekiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa duniani uchumi wa utalii utasinyaa kwa *minus three*. Tunaambiwa na mashirika makubwa ya Kimataifa kwamba kazi milioni 75 zitapotea duniani na tunaambiwa kwamba ili kuja kufufua uchumi huo na kama wengine walivyosema pengine siyo mwaka huu, zitahitajika zaidi ya dola trilioni 2.1 na katika hizo sisi tumo, kwa sababu tutakuwa ni wale ambao tumeathiriwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi duniani tunaambiwa *small and medium enterprises* ambazo makampuni yote ya Tanzania ukiyarudisha duniani ni *small and medium enterprises* zipo kwa *80%* ambazo zinafanya shughuli za utalii. Hizo karibu zote au karibu nyingi sana zitakaribia kufilisika kama hakutakuwa na programu maalum ya kuwainua.

Mheshimiwa Spika, pia tujue kwamba utalii ni jambo ambalo ni *very sensitive; sensitive* kwa siasa, risasi na kwa maradhi. Wasiwasi wangu ni kwamba tunaweza tukajikuta tupo pabaya ikiwa hatukufuata vigezo vinavyokubalika na *WHO* katika suala zima la kukabiliana na maradhi ya *Corona*. Inawezekana nitakachokisema kisiwe *popular* na nisipendeze lakini ukweli siridhiki na namna ambavyo mengine tunayafanya.

Mheshimiwa Spika, tumesema hatuwezi *lockdown* na *curfew* lakini je, tunasimamia vipi suala la *social distance* na namna ambavyo watu wetu wanaweza kujilinda ikiwa hatufuati vigezo vinavyokubalika? Tutachelewa katika kuondoa maradhi kwa sababu hatutafuata masharti yanayofanana ambayo ni *international,* lakini pia tukichelewa wakati wengine wanafunguliwa milango, sisi tutakuwa hatujafunguliwa milango.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri kama hatuwezi *lockdown* na *curfew* basi angalau Serikali iwe na msimamo *nationwide* wa *social distance* na watu kuvaa barakoa. Ziko nchi mojawapo ni *Czech Republic* na Taiwan maradhi yameondoka kwa *social distance* na barakoa. Sasa kama tunataka utalii wetu tuje tuuokoe, basi hayo mengine hatuyawezi, basi tufanye hiyo iwe ni sharia na lazima kila mtu katika kujitenga lakini siyo tunavyoona hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa Zanzibar ni utalii. Utalii unategemewa Zanzibar kwa asilimia 27 ya *DGP* na asilimia 30 ya *foreign currency earning.* Uchumi wetu wa utalii umeunganika na uchumi wa Bara kwa sababu utalii mara nyingi unakuwa *sold* kama *one destination Tanzania* ingawa pengine Zanzibar inaweza ikafanya juhudi zake yenyewe za ziada na Bara za ziada lakini watu wanakuja hapa kwa ajili ya kupata *beach* na mbuga.

Mheshimiwa Spika, pia utalii wa Zanzibar unasaidia sana wakulima wa bidhaa na viwanda wa Bara kwa sababu bidhaa na mazao yanakuja Zanzibar kwa asilimia kubwa sana. Utalii wa Zanzibar unatengeneza ajira 66,000 *direct* na ajira zisizokuwa *direct* 150,000. Hizo ni karibu ajira 200,000 na kitu. Ukweli ni kwamba wanaofaidika na ajira hizo sasa ni wakulima na huleta mazao Zanzibar kutoka Bara. Wafanyakazi kutoka Bara ni wengi sana katika Sekta ya Utalii, kwa hiyo, wanafaidika.

Mheshimiwa Spika, mimi nimetoka katika mji wa utalii, *Stone Town; it is a ghost town.* Mji wote umelala na umekufa kwa sababu maduka ya kitalii karibu 90 kwa 100 ni maduka ya watu ambao wanatokea Tanzania Bara. Nasema hivi makusudi. Tanzania Bara, nimerudia makusudi mwone kwamba hatuwezi kuepuka mfungamanisho wa utalii baina ya Bara na Zanzibar na kama hatuwezi kuepuka, ina maana lazima tufanye kazi kwa pamoja. Lazima kuwe na programu ya pamoja katika kufanya *salvation* ya kukomboa utalii wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar inapata watalii kama alivyosema Mheshimiwa Dau, karibu 550,000 kwa mwaka kutokana na hoteli zake karibu 540 ambazo 26 ni za *five star,* lakini hizo hoteli zote sasa hivi zimefungwa kama ambavyo huku zimefungwa. Ni suala la dunia nzima. Sasa hivi tunaelekea katika kilele cha msimu, kwenye mwezi wa Juni, Julai mpaka Septemba, lakini nina hakika Septemba au mwaka huu 2020 pengine mwisho wa mwaka ndiyo tutaanza kuona angalau *trickling* kidogo ya utalii.

Mheshimiwa Spika, sasa nafikiri kuna haja ya Serikali ya Tanzania programu yetu tutakayofanya kuishirikisha Serikali ya Zanzibar kikamilifu kwa sababu Zanzibar peke yake katika hili haitaweza kufanya kitu. Kama nilivyosema, mapato ya Serikali yanategemea sana utalii na nina hakika kutakuwa na dhiki kubwa miezi miwili au mitatu ijayo kwa Serikali ya Zanzibar kulipa hata mishahara kwa sababu bila ya utalii Zanzibar haiwezi kusimama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, programu yoyote inayofanywa ilenge katika kuhakikisha kwamba pande hizi mbili zinakuwa pamoja katika kufanya mambo hayo kwa sababu hali ilivyo hivi sasa, Zanzibar haiwezi kutoka yenyewe kwenda kujiombea misaada. Kwa hiyo, napenda kufanyike utafiti wa kutosha kabisa ambao wataalam wanaita *Tourism Satellite Account (TSA)* ili kuhakikisha kwamba kila *area* ya utalii inatazamwa kutokana na waendesha magari, wenye mahoteli, wenye kufanya *tours* ili kuhakikisha kwamba Zanzibar inanusulika kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa naambiwa kutokana na *source* mbalimbali Zanzibar, Zanzibar inaweza kuhitaji siyo chini ya *three billion shillings* kuweza kurudi katika hali yake na kushindana na angalau na Mombasa au Seychelles, kuzuia baadhi ya watalii badala ya kwenda kule wakaja huku.

Mheshimiwa Spika, kuna hatari nyingine kwamba hivi sasa nchi imeingia katika hali mbaya sana na hili ni kosa ambalo Watanzania tumefanya. Kwa muda wote hatukutengeneza *sovereign fund* ambayo ingeweza kusaidia

kujiokoa wakati kama huu. Sasa hivi itabidi tutegemee mikopo, misaada na mashirika makubwa, lakini naona kwamba lazima tufanye vizuri ili tuisaidie Serikali ya Zanzibar kwa sababu ni dhooful-hali.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kwenye *Corona* tu Zanzibar imeshalemewa. Nami naamini tajuri lake halina kitu hivi sasa. Kwa hiyo, nashauri Waziri Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla chochote mnachofanya kama ni *BOT,* Serikali Kuu au kuomba misaada ama vitu gani mshirikiane pamoja na Serikali ya Zanzibar ili kuhakikisha uchumi wa Zanzibar unaokolewa, la sivyo utakuwa mzigo sana wa kuilemea Serikali ya Muungano na itakuwa na *impact* kubwa ya kijamii na pia ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Saleh. Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nianze kwa kweli kwa kumpongeza sana Waziri Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla. Nadiriki kusema toka tumeanza bajeti ndiyo Waziri pekee ameeleza matatizo ya yanayotokana na *corona.* Wabunge watakubaliana nami tatizo la *corona* siyo la utabibu zaidi ni tatizo la kiuchumi, leo Mheshimiwa Dkt. Kigwangala amelieleza sawasawa. Mheshimiwa Dkt. Kigwangala hongera sana, lakini nisingeshangaa hivi ndiyo viwango vya Mheshimiwa Dkt. Kigwangala.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mheshimiwa Dkt. Kigwangala amesema vizuri sana, mapato yanayotegemewa kupotea kutokana na tatizo hili la ugonjwa wa *corona* ni 75%, lakini mimi naamini zaidi ya 75%, kwa sababu anaongelea *direct* ambacho kingeenda kwenye *coffer* za Wizara na taasisi zake. Unaposema matatizo yanayotokana na *corona* kwa *industry* ya *tourism* maana yake hujaongelea wenye mahoteli, wenye *bar*, wenye *restaurant*, mama ntilie

na wanaouza vitu sokoni, kwa hiyo *multiply effect* ya matatizo ni kubwa sana kulingana na ugonjwa huu wa *corona* kwa kutokuwa na mapesa haya ya utalii.

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba Serikali nadhani umefika wakati lazima tulieleze kwa kinagaubaga matatizo ambayo tunaenda kupambana nayo kwa miezi 18 ijayo ambayo kwa kweli yanasababishwa na ugonjwa wa *corona.* Ugonjwa huu haujaletwa na yeyote, ugonjwa huu ni wa kidunia, *so* lazima na sisi tupambane nao kama wanavyofanya wengine.

Mheshimiwa Spika, lazima kwa mfano *TANAPA* amesema mtu mmoja hapa, *TANAPA* walikuwa wanapata fedha nyingi ndiyo wanatunza mbuga zetu zote nchini hata mbuga zisizokuwa na mapato makubwa. Sasa hawana fedha tunafanyaje kama nchi? Lazima tuje na *stimulus package* ya kuiokoa *TANAPA* na Ngorongoro *otherwise* tutapoteza kama alivyosema dada yangu Magdalena Sakaya. Tuna tatizo la haraka hapa wasipokuwa na fedha za kutunza mbuga hizi tutapata matatizo makubwa zaidi. Kwa hiyo, ningeomba sana Serikali ije na mkakati wa kuhakikisha tuna fedha za kui-*bell out TANAPA* hawa watu wa Ngorongoro lakini na wenye mahoteli na wenye *restaurant*, wenye bar na wafanyabiashara wadogo wadogo lakini wengine tutawa-*bell out* siyo kwa fedha ni kwa maamuzi ya *physical decision*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano lazima *Central Bank by now* ingekuwa imeshatoa *direction* kuyaomba mabenki yasimamishe *loan repayment* kwa hawa *small holders* wote. Kwa sababu hawa leo wanatakiwa walipe benki, watu wote wanaoshughulika na utalii na wewe unajua wengi wanachukua hela *in advance* kwamba watalii wangekuja mwezi wa Juni, wangekuja mwezi wa Julai. Baada jambo hili la *corona*, wanalipa fedha za watu *back* na fedha zenyewe wengi wameshazitumia tunawafanyaje hawa? Tuna *lay out* wafanyakazi tunawafanyaje hawa. Kwa hiyo niombe sana lazima tuje na mkakati haraka, mkakati huo ni wa nini?

Mheshimiwa Spika, moja ni huo wa *Central Bank* na Wizara ya Fedha ije na *physical decision* kwa ajili ya kusaidia hawa wafanyabiashara ndogo ndogo wenye mahoteli ili angalau wasimamishe *loan repayment.* Pia kama nchi sasa tuwaombe *international lenders* wote Tanzania inalipa kati ya bilioni 600 mpaka 900 kwa mwezi kulipa deni la Taifa, watu waliotukopesha, nadhani umefika wakati twende *aggressive* tuwaombe angalau kwa miezi 18 hii waturuhusu tusilipe ili fedha ile tuiingize kuokoa biashara na uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, hili naamini linawezekana kwa sababu tukijenga hoja na lazima tuonekane hoja hii tunaijenga kwa nguvu na tuoneshe kweli hili jambo limetu-*cost* kwenye uchumi. Nimemsikiliza vizuri sana Mheshimiwa Dkt. Kigwangala hapa, nimekuwa nakuja kwenye Wizara zote hakuna aliyeonesha kwamba kuna kwamba kuna matokeo ya ugonjwa huu wa *corona,* kwasababu tusipopata *tourists* zaidi ya 17%, 18% ya GDP imekwenda. Leo Shirika letu na Ndege *ATC* lazima tui-*bell out*. *ATC* kwa wiki ilikuwa inaruka mara 91 leo kwa sababu ya *corona* inaruka mara 19. Dodoma kwenyewe inakuja mara tatu, ilikuwa inakuja mara saba. Hii inapoteza mapato ya *ATC,* mapato ya shirika letu, sasa tunafanyaje, tunakaa tu tunasubiri mpaka tutakapoambiwa *corona* imeisha?

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ni *post,* jambo hili la *corona,* lazima tuhangaike nalo, najua Serikali inafanya juhudi kubwa sana na kwa kweli Rais ametuongoza vizuri, ameondoa *panic,* tumebakia kuwa wamoja, lakini cha muhimu sasa lazima tuhangaike tunafanyaje baada ya hapa kwa sababu lazima tuendane na *standards* za *WHO* kwa sababu baadaye *WHO* itatoa *certificate* nchi ambazo zimefanya vizuri kwamba hawa wako *okay* sasa wako *free from corona virus.* Tusipopata hiyo *certificate* uchumi wetu utapata shida kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana watu wa Serikali tukubaliane wote, tuone namna tunavyoweza kufanya. Ukiangalia leo hata biashara zingine za mabasi, *petrol station,*

wote ukiangalia *revenue* zao zime-*drop* by 60%. Ukienda leo Arusha na Moshi, *petrol station* zote za Arusha na Moshi *revenue* zimeshuka by 80%. Watu hawa wana mikopo kwenye mabenki, lakini tumenyamaza siyo sawa, nawaombeni tufanye kazi, tukubali ndiyo hali halisi, amesema mtu pale lazima tu-*scale out* baadhi ya miradi, tu-*scale out* baadhi ya program ili tuhangaike na *effect* hii ili tuendelee kubaki na mafanikio haya ambayo tumekuwa nayo kama nchi kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, niwaombe watu wa *TANAPA* hali itakapokuwa nzuri tuna barabara yetu ya kwenda Gombe ni muhimu Gombe iweze kufikika kwa barabara na tumeshaianza waendelee kushirikiana na *TANROAD* ili tuweze kufika na iwe rahisi tutakapoanza biashara yetu hii utalii, lakini niseme ukweli tatizo ambalo naliona tunaenda kupambana nalo ni la uchumi zaidi kuliko la afya.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niombe sana, tuwaombe Watanzania umefika wakati tufanye mazoezi vya kutosha. Kitakachotuokoa pamoja na dawa hizi za mitishamba pamoja na vitu vyote, naamini tufanye mazoezi, watu wengi watakaofanya mazoezi tunaweza tukapambana na ugonjwa huu. Watu wamepata magonjwa haya wamefanya mazoezi wameweza ku-*come out* kwa hiyo tuwaambie watu wetu tufanye mazoezi tuendelee kuheshimu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunakushukuru kwa *emphasis* yako ya kwamba *corona* ni tatizo pana, linaathiri sekta nyingi na sekta ya utalii inaathirika kipekee kabisa. Nilikuwa nafuatilia mahali fulani wanasema kwa sababu ndege nyingi

duniani, hizi za abiria maana ndege nyinginezo zimekuwa *grounded* na *certification* ya ma-*pilot* huwa ni kwamba *pilot* asipoendesha ndege kwa siku 90 huwa lazima a-*reapply permit* yake ya kuendesha, haruhusiwi. Kwa hiyo ma-*pilot* karibu asilimia tisini na kitu, ma-*pilot* duniani, maana yake ni kwamba wawe *retrained,* warudi tena kwenye *simulators* na kadhalika *how expensive is that exercise going to be* na *effect* yaani kila mahali. Sasa wako watu wanafikiri wanaitangazia nchi kwamba *corona* imeletwa na Ndugai, imeletwa na Magufuli imeletwa na Fulani, yaani hawa watu wa ajabu kweli hawa.

Sasa Waheshimiwa wanaofuata naomba twende kwa dakika tano tano kwa sababu maombi ni mengi mno *at least* nijaribu tu kupata nafasi ambayo Mheshimiwa Waziri atasikia mlichotaka kumwambia tu moja kwa moja. Tuanze na dakika tano tano sasa ukisikia kengele moja tu basi imekwisha. Tuanze na Marwa Ryoba Chacha, atafuatiwa na Mheshimiwa Anthony Calist Komu.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana. Pia naomba nichukue nafasi hii nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuondoa hofu iliyokuwa imetanda kwenye mioyo ya Watanzania wengi na kwa kweli ilikuwa hali ni mbaya kila mtu alikuwa na hofu kila kona, kwa hiyo naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais. Kama Watanzania tunaweza kuona hotuba ya Rais imekuwa na *impact* kubwa duniani kote kila sehemu wanamjadili Rais wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri ambayo anaifanya yeye pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu na wote wanaohusika na Wizara hii. Jambo la kwanza ambalo nataka nichangie ni kanuni za *WMA* imeundwa na vijiji, kuna kanuni ambayo kidogo ina ukakasi, ina *segregation* ya kielimu kule vijijini, vijiji vimetoa maeneo yao vikaunda chombo kinaitwa *WMA* na tunafahamu wale wajumbe wa *WMA* wanachaguliwa miongoni mwa wanakijiji kwenda kuwakilisha kule kwenye *WMA*.

Mheshimiwa Spika, leo imetengenezwa kanuni inayosema *form four* wawe watatu, darasa la saba wawe wawili hii haikubaliki inaenda kinyume na katiba ya nchi. Katiba sisi wenyewe Wabunge inasema ujue kusoma na kuandika sasa leo mtu wa kijijini unataka kwamba awe *form four, it is not possible*. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri, tulienda na Naibu Waziri kule Serengeti na wataalam wake walijionea hali halisi. Inafikia sehemu sasa wale wajumbe, wale wanavijiji hawaoni *ownership* ya *WMA,* naomba kanuni hii irekebishwe.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano wajumbe wanatoka kwenye kijiji watano, watatu wawe *form four* wawili wawe darasa la saba hii si nzuri haikai vizuri ilivyokuwa tangu mwanzo kwamba awe na elimu kuanzia darasa la saba na kuendelea, *form four* walikuwepo, wa Chuo Kikuu walikuwepo, hakuna shida tunaomba irudi kama ilivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni kuhusu migogoro ya vijiji na hifadhi. Kuna vijiji ambavyo vilikuwa vimeenda mahakamani, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutoa *ruling* nzuri, kwamba vile vijiji visihamishwe wala wananchi wasisumbuliwe, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Kuna jambo la kiufundi ambalo lilifanyika kule kwangu Serengeti Mheshimiwa Waziri, kuna vijiji vilivyokuwa vimeenda mahakamani 2013, 2014 vikagawanywa sasa vile vijiji mama havipakani na hifadhi tena sasa ukiangalia kwenye ile orodha unaona kwamba vile vijiji mama ndivyo vimeondolewa lakini kwa mfano Kijiji kama Nyamburi kilichokuwa kimoja pamoja na Tamkeri kimeondolewa, naomba kwa sababu Tume haikwenda pale Serengeti haikwenda kuona *physically,* kwa hiyo kuna shida ya kiufundi wataalam wa Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri waliliona lile kwa uhalisia, kwa hiyo naomba marekebisho yafanyike pale.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, ilikuja timu ya Serikali ya Kijiji cha Paki Nyigoti kumwona, namshukuru kwamba alituma wataalam

wakafika pale. Tunaomba yale ambayo wataalam walipendekeza yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni tembo, kipindi changu cha Ubunge nimepiga kelele sana kuhusu tembo, tumetumia kila aina ya mbinu kuhakikisha kwamba tunapambana na tembo. Sasa naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Kampuni ya Grumeti pamoja na Wizara, pamoja na Mheshimiwa Waziri kwa msaada mkubwa walioutoa kwa kuweka *electric fence* kwenye maeneo yanayozunguka Vijiji vya Serengeti. Kwa sasa wananchi wa Vijiji vya Mbirikiri, Rwamchanga, Miseke wanalima hawana shida tembo anaenda pale anagusa, anapigwa shoti, anarudi hifadhini. Naomba nichukue nafasi hii nimshukuru sana Waziri kwa sababu kama asingetoa ruhusa jambo hili lisingefanyika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anthony Calist Komu atafuatiwa na Mheshimiwa Willy Qambalo.

**MHE. ANTHONY C. KOMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti ya Wizara hii ambayo kwetu sisi kule kwenye Jimbo la Moshi Vijijini ni bajeti muhimu sana kwa sababu ya *nature* ya shughuli ambazo tunazifanya. Kwa sababu ni mara ya kwanza naongea katika Bunge hili kwa maana ya Mkutano huu na hasa toka nitangaze kwamba ikifika mwisho wa Bunge hili la Kumi na Moja nitajiunga na chama cha *NCCR* Mageuzi na nichukue fursa hii kuwashukuru sana viongozi wa *NCCR* Mageuzi ambao wamekubali ombi langu kwamba wakati ukifika basi watanipokea na wamenipa kazi ya kulitetea tena Jimbo la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii vilevile kuwapa pole sana wananchi wa Moshi Vijijini ambao wamekumbwa na majanga ya mafuriko kule Arusha chini na Mabogini na Old Moshi Magharibi kuna sehemu zingine ambazo nimeweza kwenda na zingine ambazo sikuweza kwenda kwahiyo nawapa pole sana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba Sekta ya Utalii ni muhimu sana kwa nchi yetu kwa sababu inatuletea mapato kama Waziri alivyosema, sina haja ya kurudia hizo *data* na ni kweli kwamba tutaathirika sana kutokana na tatizo hili la *COVID-19,* sina haja ya kurudia *data*. Jambo la msingi sana ni hatua zipi ambazo tunazichukua ili tuwe salama na tuweze kukabiliana na athari ambazo zitatokea. Kwanza kwetu sisi pale Moshi katika Mkoa mzima wa Kilimanjaro, Arusha na maeneo mengine ni kwamba sasa hivi watu wameacha biashara kabisa kwa sababu ya hizi athari ambazo zinatokea; watalii hawaji lakini lazima waendelee ku-maintan magari, lazima waendelee ku-*maintain* wafanyakazi, lazima waendelee ku-*maintain* mahoteli. Ingekuwa busara sana kama Serikali ingeamua kufanya kwa makusudi tathmini ya matatizo ambayo yanawakabili wadau wa utalii ili waweze kuchukua hatua stahiki ili hali itakapotengamaa watu waweze kuendelea na biashara kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, nimeona kule Moshi Vijijini, kule Moshi Mjini bado watu wanalipishwa tozo mbalimbali wakati hawafanyi kitu chochote. Hii ni sawa sawa na wafugaji ng'ombe akiugua wa maziwa uache kumlisha na kumtunza kwa sababu tu hazalishi. Sasa niwaombe sana Serikali kwamba wana wajibu wa kujenga mazingira ambayo ni rafiki na wezeshi ili wakati hali itakapokuwa ya kawaida tuweze kuendelea kukamua kutokana na hii Sekta ya Utalii kwa kuhakikisha kwamba wafanyabiashara na wadau wote walioko kwenye sekta hii wanakuwa *sustainable,* wanaweza kuendelea kurudi katika biashara.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Serukamba amezungumza vizuri sana kwamba wako watu

ambao wamekopa kwenye mabenki kwenye taasisi za fedha, wanapaswa kuendelea ku-*service* mikopo yao wakati walitarajia watumie mapato yanayotokana na biashara wanayoifanya sasa hivi ambayo haipo waweze ku-*service* hiyo mikopo. Kwa hiyo ni lazima Serikali i-*intervene*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nafikiri ni la msingi sana ni kujiweka katika hali ambayo itatufanya baada ya tatizo hili la *corona* kupata suluhisho tuaminike duniani. Kama hatutachukua hatua ambazo *World Health Organization* watakubaliana nazo, matokeo yake ni kwamba tunaweza tukachukuliwa kama mahali ambapo si salama. Matokeo yake tukapata matatizo sana baada ya janga hili kwisha na hasa tukizingatia kwamba wateja wetu walio wengi ni watu wanaotoka katika mataifa mengine ambayo sasa hivi kuna kampeni nyingi sana ambazo ukisoma kwa makini kwenye mitandao mbalimbali na matamko mbalimbali, kwamba inaonekana kana kwamba sisi hatuchukui hatua ambazo ni za makusudi sana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Willy Qambalo atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya.

**MHE. WILLY Q. QAMBALO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii jioni hii ili nami niweze kuchangia sekta hii muhimu sana. Sisi kwetu Karatu utalii ni nguzo muhimu sana. Wako wananchi wetu wengi ambao wanajishughulisha na utalii kwa namna moja au nyingine lakini pia Mji wa Karatu ni mji wa kitalii, ni lango kuu la utalii katika kanda yetu ya kaskazini, lakini pia Karatu imezungukwa na hifadhi za kutosha, kwa hiyo nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasemea wananchi wangu hawa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, niishukuru Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Wizara hii yenye hoja, nimeona kwenye ukurasa wa 57 wameamua kuhamisha makao yao kuja katika Mji wa Karatu. Tunawakaribisha sana,

Karatu ni Ngorongoro lakini Ngorongoro ni Karatu. Tunashukuru kwa uamuzi huo na tuna uhakika tutawapeni ushirikano wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, pia naishukuru mamlaka kwa kutupa fedha za kuanza ujenzi wa hospitali yetu ya wilaya shilingi milioni 600. Baada ya kupata fedha hizo majengo ya kutosha yamejengwa lakini tunaomba Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla huyu ngo'ombe umeshamla hadi kwenye nundu umebakiza shingo na kichwa maalizia. Unakuja Karatu basi ile iwe ni hospitali yetu, sisi ni sehemu ya Ngorongoro. Tunawashukuru sana kwa mchango wetu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye eneo la wanyama waharibifu wa mazao ya mashamba lakini pia wanyama wanaotishia usalama wa wananchi wetu. Jambo hili limekuwa la kujirudiarudia lakini jambo hili ni kama halikomi. Niwaombe sana ndugu zangu wa *TANAPA* na *NCAA*, hili jambo linawezekana wekeni doria ya kutosha lakini wawezesheni wale wanaofanya doria wawe na silaha za kutosha na usafiri ili waweze ku-*respond* kwenye maeneo yale ambayo wanyama wanatoka ili waweze kuwarudishia kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Spika, wanyama hawa hawatoki mmoja mmoja, kundi nyati wanaweza kuwa hata 100, fikiria wanaingia kwenye shamba la mwananchi hawabakizi kitu. Tunaomba wanyama hao wadhibitiwe wabaki kule kwenye maeneo yao hasa vijiji vya Holidani, Kambi ya Simba, Atoma, Upper Kitete, Lositete, Kilimatembo, Ryotia na maeneo yote ya Kilima Moja, wanyama wamekuwa wakiharibu sana maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wanyama hawa wamekuwa wakitishia usalama wa wananchi. Mbaya zaidi kama ambavyo Kamati imesema na nishukuru Kamati kwa kuweka jambo hili wazi, zile fidia za kisheria zinachelewa sana. Ni jambo ambalo linaumiza, mtu anaumizwa, utaratibu ule wa kuomba fidia unafanywa lakini fidia haipatikani miaka mitano, miaka sita. Wapo wananchi

wengi wanadai fidia hizo hadi wengine baadaye wanaenda mbele ya haki. Hebu Wizara itafute namna nzuri ya kutoa fidia hizo pale ambapo jambo hili limetokea. Inakosa maana fidia inatolewa miaka mitano baada ya shamba kuharibiwa ambayo pia ni dogo sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni hili suala la migogoro ya mipaka, bado tuna migogoro michache. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ulikuja Karatu tuliongea sana na uliahidi utakuja utembelee maeneo hayo ili hiyo migogoro midogo midogo iliyokuwepo iweze kwisha. Imepita miaka miwili, ulikuja kwenye *Ngorongoro Marathon*, ukaja safari nyingine, hukuja tena. Naomba utembelee maeneo yale ili mkubaliane na wale wananchi, maeneo tunayogombania ni mita chache wala siyo kilomita, nafikiri ukienda migogoro ile inaweza kwisha kwenye Kata ya Buge lakini pia kwenye Kata ya Kambi ya Simba, Kata ya Mbululu na Kata Endamaka.

Mheshimiwa Spika, suala la *Covid-19* limeongelewa sana. Waziri amekiri athari kubwa ambayo Serikali na Wizara hii inaenda kupata kutokana janga hili, upotevu wa zaidi ya 75%. Nikubaliane na Mheshimiwa Serukamba kwamba inaweza kuwa zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeathirika lakini wananchi mmoja mmoja na wenyewe wameathirika kwa kiasi kikubwa sana. Wapo wananchi wamewekeza kwenye kujenga hoteli na vitu mbalimbali vya kitalii lakini leo anguko hili pia na wenyewe limewakumba. Hoteli zote zimefungwa, wafanyakazi wote wamerudi nyumbani hata haijulikani maisha yao yataendelea vipi. Watu hawa wamechukua mikopo kwenye benki na benki bado zinadai riba na fedha zao, tusiposaidia sekta hii itafika mahali sekta hii itakapoanza hawa watu hawezi hata kuinuka tena.

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali ifanye utaratibu wa haraka, wa muda mfupi na wa muda mrefu ili kuona namna gani ya kuwasaidia watu hawa. Wapo watu ambao wana mawazo mazuri sana, ni watu ambao unashirikiana

nao watumie kuona ni namna gani mnaweza kusaidia sekta hii ili anguko hili lisiwe kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Qambalo. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa John Danielson Pallangyo. Kama Leah hayupo, Dkt. Pallangyo, pia simpati, Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka. Mheshimiwa Dkt. Pallangyo nimekuona sasa endelea.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo kwenye hoja ambayo ipo mezani.

Mheshimiwa Spika, nitangulie kwanza kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kunipa afya njema na kunipa kibali kusimama hapa mbele yako ikiwa ni takribani mwaka mmoja tangu uliponiapisha 22 Mei, 2019.

Mheshimiwa Spika, ukubali nikupongeze pia, nakupongeza kwa dhati kabisa wewe na Naibu wako Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa uongozi thabiti ambao mmetuonyesha hapa Bungeni. Hakika karibia kila Mbunge atakiri na kutoa ushuhuda kwamba Bunge lipo imara, thabiti na tunaendelea vizuri kusema kweli. Kwa kazi nzuri unayoifanya, nikuombee kwa Mungu aendelee kukuinua na naamini kabisa kwamba kule Kongwa watakupitisha bila kupingwa na pia kule Mbeya, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson atapita kwa mshangao mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme pia kidogo kuhusu jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais wetu amendelea kusimamia nchi hii. Mussa alivyokuwa anapewa kazi ya kuwaondoa wana Israel utumwani kuwapeleka nchi ya ahadi alikuwa anasita sana mpaka akamuomba Mungu akamwambia tafadhali sana kama uso wako hautaambana nami tafadhali usinipe kazi hii. Mungu akamwambia uso wangu utaambatana nawe na nitakupa raha.

Mheshimiwa Spika, Rais wetu naye alisita, niliona *clip* moja kabla hatujafanya uchaguzi, alikuwa anazungumzia habari ya makinikia wenzake wakamwambia nenda kachukue fomu, akasema nani afanye hivyo. Kwa kuwa Mungu alipenda alichukua fomu na sasa tunaye kama Rais. Tumeshuhudia akifanya kazi nzuri akiongozwa na roho wa Mungu. Amefanya kazi njema kwa wananchi wa Tanzania, ameisha ahadi zake na nchi nzima imeonja neema hii.

Mheshimiwa Spika, hata kule Arusha ambapo ni kitovu cha utalii tumeona hii neema. Kuna barabara aliizindua mwaka 2015 ya njia nne ambayo sasa hivi imeshakuwa tayari na inachangia kwa kiwango kikubwa sana kwenye huduma za kitalii. Kama vile haitoshi ilijengwa barabara ya mchepuo kutoka Ngaramtoni kwenda Usa River nayo imemalizika. Huduma za barabara zipo vizuri Arusha na watalii wanapata huduma nzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini Mlima Meru pia nao ni kituo cha utalii. Nishauri barabara itakayo Manula Kibaoni - King'ori – Marurango –Leguruki – Ngarenanyuki – Ngabobo - Uwilo - Oldonyo Sambu nayo ijengwe kwa kiwango cha lami iwe kama *eastern bypass.* Kwa maana hiyo Mlima Meru na vivutio vya utalii vilivyopo pale vitakuwa *accessible* na tunaamini kwamba navyo vitachangia katika kuongeza pato la taifa.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye hoja. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla kwa kazi nzuri ambayo anafanya. Siyo peke yake ni pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, ndugu yangu na rafiki yangu Mheshimiwa Constantine Kanyasu pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na hata watendaji wote wa Wizara na viongozi wa taasisi zote ambazo zipo chini ya Wizara wanafanya kazi nzuri. Taasisi hizi hususan *TANAPA, NCAA, TFS* zinaingiza pato kubwa sana kwa taifa hili lakini kama unavyojua biashara ya utalii ni *fragile,* huwa inaumia haraka zinapotekea *shock* za magonjwa ya mlipuko na vita...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, naomba unipe nafasi kidogo nimalizie.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili hiyo mashirika haya yameumia. Nilikuwa nyumbani wiki mbili zilizopita kulikuwa hakuna mtalii hata mmoja kule mjini Arusha pamoja na kwamba ndiyo *center* ya utalii nchi kwetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kamati tulishauri kwamba mashirika haya yaweke utaratibu wa kuweka mafungu ambayo yatawasaidia wakati wa *shock* kama hii lakini kwa sababu ya mfumo wa makusanyo ya maduhuli hali hiyo ilikuwa bado haijatekelezeka, sasa iwe ni fundisho. Sasa katika hali hiyo ambapo wameshashindwa, tunashauri Serikali iweke mpango wa ku- *bailout* haya mashirika ambayo kwa kweli yamefanya kazi nzuri, yameingiza fedha nyingi sana kwenye pato la taifa.

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, nikupe pole wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu watatu mfululizo lakini bado ukawa mvumilivu na mwenye busara ukatuongoza hadi kufikia leo. Mwenyenzi Mungu awapokee wenzetu waliotangulia mbele ya haki na awasamehe makosa yao, *Inshallah*.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia hotuba hii kwa kuiomba Wizara, ilitaifisha usafirishaji wa viumbe hai kutoka

mwaka 2006 hali ya kuwa wasafirishaji waliokuwa wakifanya biashara hiyo wameshanunua wanyama na wana vibali na leseni zote na wengine wana mikopo benki. Hadi leo miaka mitano sasa na Serikali ilisema itawafidia watu wale haijawafidia hali zao ni mbaya sana. Miaka mitano watu wale hawajafidiwa wanaishije na wengine walichukua mikopo benki. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali itakapochukua hatua kama hizi ambazo zinagusa maisha ya watu basi iwe imejipanga ili kuona watu wale wanawapa mbadala wa maisha kulikoni hali hii hususani Serikali hii ya wanyonge ambayo inasimamiwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Spika, hawa wengine walikuwa wamepewa vibali na leseni lakini tuchukulie wale wafugaji wa vipepo kule Amani Tanga wale akina mama walikuwa wameanzisha vitalu vyao kwa ajili ya shughuli hii lakini mpaka leo wamekaa tu miaka mitano mitaji yao imeenda wapi? Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iliangilie suala hili na ilipe umuhimu mkubwa kuona wanyonge hawa wanafaidika.

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala hili la *TANAPA* lazima wote tulizungumzie kwa sababu limetupa wasiwasi mkubwa. Wewe ni mdau na tulikuwa tunatoa angalizo hili muda mrefu kwamba *TANAPA* hawa itakapotokea tatizo kutatokea balaa kubwa. Hapo zamani walikuwa wana-*fixed deposit, Treasury bill* na *Treasury bond* sasa hivi mabadiliko yalipokuja pesa yote ikawa inaenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali wao hawana akiba yoyote. Leo imetokea miezi miwili tu hii sasa hivi *TANAPA* na Ngorongoro wanaanza kupata shida na wataendelea kupata shida kwa sababu hawana akiba yoyote ya kuwasaidia. Sasa inabidi Serikali iliangalie suala hili na ichukue hatua za haraka kwa sababu si tu kwamba tutapoteza mapato lakini suala zima la uhifadhi litaondoka na likiondoka ndiyo tutapata shida kubwa.

Mheshimiwa Spika, *Corona* iondoke leo yaani duniani kote imalizike bado tutakuwa na miezi sita ya ku-*suffer* hakuna mtalii atakuja hapa, nazungumza kwa uzoefu nilionao katika sekta ya utalii. Kwa sababu gani, kwanza tuchukue nchi zote

hizo ambazo zinaleta watalii; Uingereza, Marekani, Ufaransa, Italy, Ujerumani na Hispania ndiyo zimeathirika kwa kiasi kikubwa na Corona. Kwa hiyo, wana kama miezi sita au zaidi kuweza kujipanga kuja tena huku. Kwa hiyo, bado *TANAPA,* Ngorongoro wataendelea kupata shida sana kuendelea. Kwa hiyo, Serikali suala hili iliangalie kwa haraka ione namna gani italipatia ufumbuzi kwa sababu tulishauri na hii imetokea sasa hakuna wa kumlaumu hapa kwa sababu sisi tulishauri na Serikali hii ni sikivu tunaamini itatusikia.

Mheshimiwa Spika, lakini tuangalie tena mbali zaidi kwa mfano Ngorongoro, kama Ngorongoro hali ni hiyo kwa miezi miwili, sasa ikichukua tena miezi sita hawana mapato wale wafugaji wanaoishi ndani ya Ngorongoro hali itakuwaje? Wale wananchi wanategemea chakula na huduma zote muhimu zitoke kwenye pato linalotokana na Ngorongoro, hali itakuwaje? Kwa hiyo, hata *Corona* iishe sasa hivi bodo hali ya Ngorongoro na *TANAPA* itaendelea kuwa ngumu sana, kwa hiyo, Serikali lazima ichukue hatua za dharura kukabiliana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nizungumzie suala la mwisho. Suala langu la mwisho, Wizara hii ndiyo itakayonyooshewa kidole hiyo hatari inayokuja mbele yetu. Niliisema wakati nachangia wakati  Wizara ya Muungano na Mazingira suala la kupotea kwa hekta 470,000 kila mwaka za misitu na tunazopanda ni hekta 13,000 ni hatari moja kubwa sana ambayo Tanzania inakuja na haitachukua hata miaka kumi athari yake itaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara inapanda hekta 9,000, jamii inapanda kama hekta 5,000 ni hatari hatujafikia hata 10%. Kwa hiyo, lazima tuwe na mkakati ambao utafanya angalu kila mkoa wapande hekta 2,000 angalau tupate 10% ya misitu ili tuweze kujirudisha katika hali ile ya kawaida.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Salim Hussein.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunakushukuru sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Sannda.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa nafasi hii. Kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai anayoendelea kutupa na afya njema. Tuwaombee ndugu zetu ambao wametangulia mbele za haki.

Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli. Huyu ni mmoja wa Marais wa viwango vya juu kabisa hapa duniani. Pia Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ni mzalendo katika nchi hii na ni kiongozi mwenye hofu ya Mungu. Anayekubaliana na maneno haya anaweza akapiga makofi pia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe pamoja na Naibu wako mmeliongoza Bunge hili kwa weledi mkubwa sana na hekima ya hali ya juu sana. Tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwenye hoja, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Naibu Waziri ndugu yangu Mheshimiwa Constastine Kanyasu, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara hii nawapongeza sana. Kasi yenu kwa kweli ilikuwa ni kubwa sana, tumeiona, tumeshuhudia lakini kwa janga hili ambalo limetupata tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu kwa sababu mapato kwa kweli yatashuka kama ambavyo umeeleza kwenye hotuba yako. Tumeona zile ndege ambazo zilikuwa zinabeba watalii wako sasa tubabea mizingo lakini tumuombe sana Mwenyezi Mungu atunusuru na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nirudi sasa kwenye Jimbo langu la Manyoni Mashariki. Niendelee tu kukumbusha, hii ni mara

ya pili nasema kuhusu migogoro ya ardhi baina ya hifadhi za misitu pamoja na vijiji.

Mheshimiwa Spika, Manyoni pale nina vijiji 12 vimegusana na hifadhi, kwenye Hifadhi ya Muhesi. Mwaka jana nilizungumza jambo hili kwenye kipindi kama hiki cha hotuba ya bajeti. Mheshimiwa Rais ameruhusu vile vijiji 920 tayari vimeshasajiliwa lakini bado vile 343.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha anipe *comfort* vile vijiji 12 Manyoni kwenye ile Hifadhi ya Muhesi vipo kwenye utaratibu wa kusajiliwa? TAMISEMI pamoja na hii Tume ya Ardhi sasa inafanya matayarisho ya kuvisajili vijiji hivi, je, hivi vijiji vyangu vya Manyoni vipo? Maeneo yake yalichukuliwa na hifadhi hizi nakumbuka mwaka 1992 na vijiji hivyo 12 vikaguswa kwa maana ya vitongoji 9 ambavyo ni Chisola, Msisi, Itowelo, Machocholoni, Mkindilya, Chigugu, Ngongolelo, Chibwee na Iluma. Maeneo haya yalikuwa yanatusaidia sana, tulikuwa tunalima, tunachimba madini na kurina asali. Hebu Mheshimiwa Waziri wakati unahitimisha utueleze jambo hili kama na sisi vijiji hivi vipo? Nimetumwa na wapiga kula wangu huko wakitaka niwaulizie suala hili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, niliseme kwa ufupi sana ufugaji wa nyuki. Mwaka jana kwenye hotuba yako ya bajeti ulisema mnafanya mpango kwamba sasa kuruhusu miradi rafiki ambayo itakuwa inafanyika kwenye hifadhi kwa vibali maalum kama ufugaji wa nyuki wale majirani ambao wanakugusana na hifadhi hizi. Tumefikia wapi, naona hapa tu mmeelezea utungaji wa sheria lakini sasa sijasikia…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtuka, ahsante sana.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Spika, tumefikia wapi utaratibu huu ili tuweze kufuga na sisi, kwa mfano Manyoni sisi ni wafutaji wa nyuki na asali bora kwa nchi hii inatoka Manyoni. Hebu tuelezeni sasa utaratibu mturuhusu tuanze kufuga nyuki na kurina asali ili tuwalishe Watanzania na tuwape afya bora.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii, muda hautoshi lakini nashukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Mtuka, Mbunge wa Manyoni na niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge wasiofahamu Mheshimiwa Mtuka amehamasisha kilimo cha korosho katika wilaya yake katika kiwango cha kutisha na wanazidi kupata mafanikio makubwa sana. Mtwara, Lindi jiandaeni huko, Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Salehe Mollel.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, niseme tu itifaki ya kiungwana ya shukrani pamoja na ya pongezi kote imezingatiwa, kwa ajili ya muda nitaenda moja kwa moja kwenye mchango wangu. Pamoja na pongezi kwa Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri na ya kihistoria ya kimapinduzi ambayo mnaifanya liko tatizo moja kubwa sana la uadilifu na weledi kwenye baadhi ya askari wetu wa wanyama pori lakini pia na kwenye baadhi ya watumishi pale wizarani.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano wa Kondoa pori la akiba la Swagaswaga lakini nazungumzia pia nchi nzima kwenye mapori ya namna hiyo. Askari wanakwenda wanabambikiza kesi, wanakwenda vijijini wanapiga silaha za moto hewani mifugo inakimbilia porini wanakwenda wanawakamata wanaanza kunyanyasa wananchi. Wanawapiga, wanawatesa kabisa kwa adhabu kinyume kabisa na haki za binadamu wanadai rushwa na wanauza ile mifugo, awanachinja wengine wanakwenda kula wanafanya ni mboga. Nashangaa nyamapori zipo za kutosha wanataka kula mbuzi na kondoo na ng'ombe vilevile.

Mheshimiwa Spika, nina kesi mahsusi kabisa mwaka jana kijana mmoja alichukuliwa mifugo yake 145, baada ya kesi kuendeshwa imekuja kubainika kwamba kijana hana hatia na hakuwa na kosa wameweza kurudisha mifugo 33 tu, mingine yote imefanyiwa uhaini inauzwa mpaka Singida huko. Yuko bibi, tena bibi wa miaka 60 anachukuliwa mifugo

22 anarudishiwa mifugo mitatu halafu wanamuomba bibi yule rushwa ya shilingi 1,500,000. Niombe Mheshimiwa Waziri na timu yako, najua nimemfikishia hata Mkurugenzi wa *TAWA* na wamepeleka kamati kule kwa ajili ya uchunguzi. Hebu tutengeneze mkakati wa kubaini hao watu waovu namna hiyo wanaichafua Wizara.

Mheshimiwa Spika, watengeneze mkakati kama wa *random* au *sport checking* watu waende wakawashtukize, ziara za kushtukiza mkiwapanga wale watajiandaa halafu watficha maovu yao. Lakini pia inawezekana tuwe na utaratibu wa *surveillance* na jinsi ya kufanya *monitoring* za haraka haraka lakini kama haitoshi hiyo Mheshimiwa Waziri adhabu kwa watakaobainika ziwe kali. Mwaka juzi vijana wako pia waliua kijana wa Kongoa mmoja *case* imeenda lakini baadaye yule askari aliyeua anazagaa mtaani na anaonekana. Kumbe kuna kule hali ya kulindana lindana mwisho wa siku baada ya kubainika kwa makosa matokeo yake wanaona tabia hizi zitalindwa na zitaendelea. Nikusihi hebu tuchukue hatua katika utaratibu huo tatizo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hilo la kwanza, la pili utaratibu wa malipo ya vifuta jasho pamoja na vifuta machozi umekuwa unachukua muda mrefu sana na wakati mwingine anakuja analipwa mtu wa miaka ya mbele anaachwa yule wa miaka ya nyuma na yanasahauliwa. Maana yake nini, tafsiri yake ni kwamba baadhi ya watumishi pia siyo waadilifu ikipita muda mrefu wanatumia mwanya ule kupotea na yale malipo. Na hili hebu naomba ulifanyie kazi sana, utakuja kubaini kwamba lipo tatizo na baadhi ya watu wako wanatakiwa wachukuliwe hatua kali sana kuhakikisha suala hili halitokei.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kabla ya mambo ya malipo hebu tuangalie utaratibu wa kuwekeza mle ndani ya zile hifadhi au haya mapori. Hawa wanyama wanaotoka wengi wanatoka kwa ajili ya kwenda kutafuta maji, tuwe na visima, tuwe na mabwawa mle ndani hii itasaidia sana kuliko kuwekeza kuanza kulipa vifuta jasho. Lakini ukiwekeza

huku unapunguza gharama za kuwalipa wananchi kwasababu wanyama watakuwa wengi hawatoroki. Nimeona kwenye hotuba yako kuna mkakati mzuri tu wa kufanya mapitio kwenye taratibu hizo na viwango lakini tuhakikishe tunawekeza kwenye kuwa na vyanzo vya maji kule ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, la tatu nadhani moja ya mkakati mzuri sana, najua kuna dosari ambazo zimeendelea kutokea, moja ya mkakati mzuri kwenye ile *buffer* ya baina ya hifadhi ni kuweka hizi *WMA*. Zirekebishwe dosari lakini *WMA* zitatusaidia sana kupunguza migogoro baina ya wananchi na maeneo ya hifadhi yote kwasababu wananchi sasa pale wana-*own* ile *process* ya uhifadhi na wenyewe wote watakuwa wahifadhi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda ahsante sana, nilikwisha kutaja Mheshimiwa Amina Salehe Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwasababu ya muda dakika ni chache nitakwenda moja kwa moja kwa kuchangia maeneo matatu. Kutokana na mvua nyingi ambazo zilianza kunyesha tangu mwaka jana mwezi wa kumi Hifadhi ya Serengeti, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na hifadhi nyingine nyingi maeneo mengi barabara zimeharibika sana. Ningeomba tuone umuhimu wa kuunda tume ambayo itapita kuangalia athari ya mvua na miundombinu jinsi ilivyoharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo sasa tuone kwamba ni kwa jinsi gani Serikali inazisaidia hifadhi hizi kuboresha miundombinu ili janga hili la Corona litakapoondoka basi na watalii watakapoanza kuja barabara miundombinu itakuwa salama. Kwasababu mojawapo ya barabara ambayo imekuwa kero sana unapokwenda maeneo ya Ngorongoro endapo gari likiharibika na lika-*cross* ile barabara hakuna tena mahali

pengine pa kupita. Na hasa wakati wa mvua tatizo linakuwa ni kubwa, kwa hiyo, niombe tuone ni kwa jinsi gani tunazisaidia *TANAPA,* Ngorongoro na maeneo mengine yote ambayo kwa kweli kwa namna moja au nyingine ni maeneo ya utalii.

Mheshimiwa Spika, pili, Arusha ni miongoni mwa mikoa ambayo itaathirika sana na janga hili hasa kutokana na kwamba ni kitovu cha utalii na matokeo yake katika Mji wa Karatu ambao umekuwa ukikua kwa kasi sana tayari tumekwisha anza kuona athari zake. Tuone ni kwa jinsi gani kama wengine ambavyo wameshauri na mimi pia nashauri kuona kwamba ni kwa jinsi gani sasa Serikali inajipanga kuweza kukabiliana na athari hizi ili basi janga hili lisiendelee kuathiri na hasa *TANAPA* pamoja na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, pili nashauri kwamba *channel* ya *TBC* Safari ambayo imekuwa ikionesha vivutio mbalimbali, Serikali ninaiomba kuona ni kwa umuhimu gani itawekeza katika *channel* hii wakati huu wa janga hili la Corona basi maeneo tofauti na hasa *channel* hii tukiipeleka kimataifa zaidi itasaidia sana kutangaza utalii wetu na janga hili litakapoondoka basi watalii wengi watakuwa pia wamejionea. Kwa hiyo, tuone ni kwa jinsi gani tutawekeza kwa *channel* hii ya *TBC* na kuwawezesha wafanyakazi kwenda maeneo mbalimbali kuandaa *documentary* ambazo zitaweza kutangaza utalii wetu na utaweza pia kuhimiza utalii wa ndani ili Watanzania waweze kwenda katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, la tatu katika magofu ya kale ya Kaole katika Mji wa Bagamoyo inawezekana kwamba kuna wengine ambao bado hawajaona. Mojawapo ya yale majengo lipo sanduku ambalo lina uzito wa tani tatu na sanduku lile tangu limefungwa na Wajerumani katika vita vile vya Wajerumani mpaka leo hii halijawahi kufunguliwa. Na wanakuambia kwamba sanduku lile hofu yao kwamba je, wakilifungua hawajua kwamba kuna nyaraka gani kule ambazo zinaweza kuwa zina athari zikaleta athari kubwa

lakini pia hawajui kwamba kwa namna moja au nyingine kutofunga labda kuna nyaraka pia muhimu ambazo zingeweza kusaidia. Ninaomba atakapokuja kuwasilisha Mheshimiwa Waziri atuambie basi wana mpango gani na hilo sanduku lenye uzito wa tani tatu kuona kwamba ni kipi ambacho kipo mle ndani.

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme tu kwamba sekta ya utalii ni muhimu sana tusipokuwa na jitihada za haraka basi ni dhahiri kabisa kwamba tutatetereka kwa namna moja au nyingine. Kwa hiyo, Serikali naiomba sana kushirikiana na Wizara hizi kuona ni kwa jinsi gani wanaweza kusaidia na hasa kwa mfano kama hivi sasa tulizoea katika barabara Arusha kwenda Serengeti, kwenda Ngorongoro kila baada ya dakika mbili, dakika tatu unakutana na magari. Lakini hivi sasa hakuna gari hata moja wale waliokuwa wakifanya kazi katika zile hoteli wote hao wafanyakazi wamerudishwa nyumbani. Kwa hiyo, kwa kweli tuone ni kwa jinsi gani ambavyo tutaweza kusaidia katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kabisa, mwaka jana tulipata bahati ya kutembelea maeneo tofauti ya utalii, naipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kulijumuisha kundi la watu wenye ulemavu kuweza kutembelea maeneo mbalimbali ya utalii. Kipekee kabisa nampongeza Mkurugenzi Allan Kijazi lakini pia nimpongeze sana Dkt. Manongi wote hawa walitoa ushirikiano mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana na ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mwalimu Benardetha Kasabagu Mushashu.

**MHE: BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda ni mfupi niende moja kwa moja kwenye hoja. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri sana ambayo wamefanya katika Wizara yenu wakisaidiana na Makatibu Wakuu.Tumemsikiliza Mheshimiwa Waziri akiwa anawasilisha

na akaonesha athari zitakazopatikana katika hii tasnia ya utalii kwasababu ya gonjwa la Corona.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nilimsikia siku moja hapa Mheshimiwa Waziri wa Fedha anasema imeundwa tume ambayo inaangalia sasa kuna athari gani zitatokea katika nchi kwasababu ya gonjwa la Corona. Naomba mtakapofika kwenye sekta kama sekta ya utalii, sekta ambayo inachangi pato la Taifa kwa zaidi ya asilimia 17 ambayo inachangia zaidi ya asilimia 25 kwenye fedha za nje lazima tuiangalie kwa jicho la ziada.

Mheshimiwa Spika, lazima pamoja na kuainisha matatizo yatakayotokea lakini tuje na *stimulus package* ya kuhakikisha kwamba sekta kama hizi hazianguki kwasababu zikianguka ina maana kwamba uchumi mzima wa Tanzania utaanguka. Kwa hiyo, tunachotaka kuona kwa kutumia fedha yetu na nguvu yetu ya ndani tunazisaidiaje hizi sekta ambazo ndiyo kichocheo cha kuweza kukuza uchumi wetu kuweza kuinuka. Kwa hiyo, namtegemea Waziri wa Fedha atakayowasilisha atakuwa ameliangalia na kutuambia tufanye nini.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera tuna mapori ya akiba matano ambayo sasa hivi zimepandishwa hadhi yamekuwa hifadhi za Taifa, Birigi - Chato, Rumanyika - Karagwe na Ibara - Kerwa. Na faida zake zitakuwa ni kubwa kwasababu sasa itachochea utalii katika Kanda ya Ziwa lakini vilevile wawekezaji wataweza kujenga hoteli pamoja na nyumba za wageni. Wajasiriamali wadogo na wakubwa wataweza kupata masoko ya bidhaa zao na hata zile halmashauri zilizozizunguka zitaweza kupata gawio kutoka kwenye mapato ya hizo hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa hifadhi ndiyo mara yao ya kwanza zimeingia Mkoa wa Kagera nilikuwa nashauri Serikali kwamba kuna haja ya kuja sasa, kuja kujaribu kutoa elimu na uhamasishaji kwenye vijiji vinavyozunguka hifadhi vilivyo Muleba, Biharamulo, Ngara, Kyerwa na Karagwe kusudi watu waweze kujua sasa faida hasa ya hifadhi hizi ni

nini? Waweze kujua wajilindaje kutoka kwenye hawa wanyama wakali wanapoingia, mnajua siku hizi wanahama wanatoka kwenye hifadhi wanaingia kwa watu, wanajilindaji? Lakini wajifunze na uhifadhi na mkishafanya hivyo ina maana kwamba hawa watu watakuwa wameelewa wataendelea kulinda na watakuwa sehemu ya kuhifadhi hizi hifadhi za wanyama.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa hotuba yake ya juzi, watu wa Tanzania walishakuwa na hofu lakini hotuba yake ya juzi imewapunguzia hafu na kuwatuliza Watanzania zaidi ya asilimia 90. Lakini kinachopendeza sasa hivi ukisikiliza kwenye mataifa ya nje kila mtu ooh, unajua na sisi tunataka kuchukua *steps* kama za Tanzania kumbe hakuna haja ya *lock down* tutaendelea kuchukua tahadhari. Wameshagundua kwamba kuna matatizo kwenye *lock down* kwa hiyo tunampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kuweza kuchukua hayo maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Rais alipotoka mwenyewe akaamua akawa na ujasiri akawaeleza watu dunia nzima na Watanzania kwamba jamani hivi vipimo nafikiri vina shida. Mbona tumepeleka *sample* ya mapapai, tumepeleka *sample* kutoka kwenye mbuzi wakaonekana wana Corona inakuwaje, kuna tatizo gani kwenye vipimo? Mmeona, mmesikia kwenye taarifa za habari za nje wameanza na wao kutoka ooh mnajua *testing kits* ziko *fake,* mbona siku zote walikuwa hawajasema? Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa ujasiri huo tunachowaomba Watanzania wameshaona kwamba Mheshimiwa Rais amefanya mambo makubwa na mazuri. Inapofika Oktoba mwaka huu hakuna mwingine ni kumchagua Mheshimiwa Magufuli andelee kutuletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mazingira kama hayo unashangaa unamuona mtu mmoja ambaye ni Mwenyekiti wa Kambi ya Upinzania anatangaza kwamba watu watoroke wasipitishe bajeti waache Watanzania wanakimbia Corona. Kwa maana kwamba na polisi

wakimbie, manesi wakimbie, madaktari wakimbie watu wafe kwa njaa, wafe kwa magonjwa haiwezekani. Nawapongeza kweli wale Wabunge wa Upinzani ambao wamekubali kuendelea kukaa kwenye bunge tukaendelea kupitisha bajeti kusudi Serikali ipate fedha ya kununua madawa, ya kulipa mishahara na kuendelea kukuza uchumi. Kwa hiyo, wampuuze na majibu yake aje ayapate vizuri sana kwenye sanduku la kura itakapofika Oktoba mwaka huu wa 2020 kwasababu Watanzania walituchagua ili kusudi tuje kuendelee kuwatumikia.

**SPIKA:** Ahsante sana Mwalimu.

**MHE: BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Benardetha Mushashu, ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Balozi na Mheshimiwa Mlinga atakuwa wa mwisho.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii, naomba nianze kwa kutoa pole kwa wana Nkenge na hasa wananchi wa Kata ya Kyaka na Kata ya Kasambya kwa mafuriko makubwa ambayo yametukabili na mafuriko hayo yakapelekea kuanzisha kambi tatu ili kuwahifadhi wananchi ambao wameshindwa kuendelea kukaa kwenye nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Mkuu wa Wilaya kwa hatua ambazo amezichukua kwa kuanzisha kambi hizo lakini niombe Serikali ichukue hatua pia za kusaidia waathirika kwasababu mafuriko hayo bado yanaendelea na watu wengi zaidi wataendelea kuingia kwenye kambi na jambo hili tusipoliangalia linaweza likapelekea hata milipuko ya magonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nashukuru *Red Cross* kwa kazi nzuri ambayo wamefanya na nashukuru pia *World Vision* kwa jinsi ambavyo wametuunga mkono wanaendelea kutuunga

mkono, niombe basi na Kamati ya Kitaifa itusaidie katika eneo hili Kamati ya Maafa.

Mheshimiwa Spika, pia nachukua nafasi hii kuwapa pole wana Minziro kwa upepo mkali pamoja na mvua ya mawe iliyosababisha madhara makubwa ya kukausha migomba, kuangusha migomba na mibuni na mambo mengine. Eneo hilo la Minziro ndiyo eneo hilo hilo ambapo tetemeko la ardhi lilianzia. Kwa hiyo, wananchi wako katika masikitiko makubwa naomba pia kamati husika za kitaifa zitusaidie kwasababu majanga haya ni makubwa, tunajitahidi kufanya tuloweza lakini itakuwa vizuri kupata pia msaada wa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuomba Wizara husika itusaidie kumaliza migogoro ya mipaka ya hifadhi zilizo kule hasa msitu Minziro kule kuna changamoto kati ya vijiji na msitu Minziro. Kuna hifadhi ya Rwasina, Kikuru, Lubale, Munene, Luchwezi pamoja na Kikongoro kwasababu hifadhi hizi zimekuwa zikiongeza mipaka na kuingilia vijiji jambo ambalo siyo la lazima.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwa haraka tu kwamba dunia inatuonaje kwa jinsi tunavyopambana na *Covid 19*? Nadhani Mheshimiwa Waziri anafahamu hili, ukifungua tovuti ya Shirika la Utalii Duniani, linaonyesha kila nchi imechukua hatua zipi. Sasa ukiitembelea ile utaona wameweka vigezo sita ambavyo wanatarajia kila nchi ichukue hatua mbalimbali. Sasa ukitembelea ile tovuti ambayo iko wazi kwa nchi yoyote duniani utagundua kwamba nchi nyingi zilizotuzunguka zimechukua hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nasi tunatambua ziko hatua tulizochukua, lakini tatizo ni kwamba zile hatua ambazo tumezichukua hatujataarifu shirika hilo ili iweze na sisi kutuweka katika tovuti hiyo. Matokeo yake ni kwamba watalii mbalimbali watakapoanza sasa kutaka kuanza kwenda nchi mbalimbali, wakiangalia Tanzania watakuta hatujachukua

hatua. Kwa hiyo, hatua tumechukua lakini hatujawasilisha taarifa kwenye Taasisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa leo nisingependa kuzungumza sana lakini niseme hivyo vigezo sita. Kigezo cha kwanza ni *comprehensive;* wanahitaji uoneshe kwenye *monetary policy* umefanya nini? Ukiangalia majirani zetu, wameshachukua hatua tayari, kwenye *physical policy* unatakiwa uonyeshe umefanya nini? Waliotuzunguza wameshachukua hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pia kuna kitu kinaitwa *economic intelligence unit,* inatakiwa uonyeshe umefanya nini? Waliotuzunguka wameshachukua hatua. Hatua pekee ambayo Tanzania tumeonyesha tumechukua ni ile ya kufunga mipaka. Natambua kwamba ziko hatua nyingi na nyingine Mheshimiwa Waziri wa Fedha alizizungumza humu. Tatizo ni kwamba taarifa hizi tunazo na tumekaa nazo hatujaziwasilisha kwa hizi Taasisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunakuwa tunajifungia bila sababu na hivyo inaweza ikapelekea tukakosa hata misaada ambayo wenzetu wengine wameanza kuipata. Kwa mfano, tayari Kenya wameshapokea *Kenya Shilings* milioni 500 za kusaidia changamoto hiyo. Wenzetu wengine wamepokea, Uganda kuna nyingine wamepokea leo hii. Sasa Tanzania sijui kama tumeshapokea au hatujapokea, Mheshimiwa Waziri wa Fedha atatuambia.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii niseme mambo mawili ambayo lazima tuyafanye tukitaka kunufaika na fedha hizi. Jambo la kwanza ni lazima tuwe na *comprehensive plan;* na jambo la pili, ni lazima tu-*engage IMF* na *Word Bank*. Sasa tunaweza tukachagua kuziacha hizi, lakini sidhani kama kuna sababu ya kuziacha kwa sababu nadhani hizo fedha tunazihitaji.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme, Shirika la Utalii Duniani linasema…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Balozi nakushukuru. Sasa ni Mheshimiwa Goodluck Mlinga na baada ya hapo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza napenda kwa namna ya pekee kukupongeza kwa kazi kubwa ambayo unaifanya, ukiacha tu kwa kitendo cha kuliongoza Bunge vizuri, lakini umekuwa mlezi wa Wabunge wote. Kwa hilo napenda kukupongeza hasa kwa sisi Wabunge vijana ambao bado tunakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nakupongeza kwa kuchukua tahadhari ya kuwalinda Wabunge katika janga hili la *Corona.* Unajua tafsiri ya wenzetu, wanachukulia, Wabunge kazi tunayoifanya humu ndani kama tunakanyagana kanyagana. Napenda kuwaambia wananchi kwamba huku hatupakatani, huku tunakaa kwa nafasi. Kila Mbunge hana nafasi ya kuambukiza mwenzake ugonjwa kama anao, kwa sababu hatusalimiani, hakuna vyombo ambavyo tuna-*share*.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua anazozichukua kwenye janga hili la *Corona.* Wako watu ambao walitokea kudhihaki, wanasema Rais yuko Chato. Katika kusoma kwangu kote sijawahi kuona kuwa Rais kuna maeneo ya nchi ambayo akiwepo ile nafasi ya Rais inaondoka.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hasa kwenye Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Wewe uliwahi kufanya kazi Ulanga, *Selous Game Reserve.* Unafahamu Jimbo la Ulanga nusu yake limepakana na Mbuga ya Selous. Kuna kero kubwa sana ya tembo. Sasa hivi tunaenda kwenye uchaguzi. Kwa kweli siwezi kukubali kukosa kura kwa sababu ya tembo.

Mheshimiwa Spika, nichangie sasa kwenye suala la utalii. Tunafahamu watalii wote tunaoona wanakuja katika nchi yetu, ile inakuwa ndoto yao, yaani ni *plan* ya muda mrefu; *plan* ya miezi sita hadi miaka miwili. Kwa hiyo, unapomwona mtalii amekuja Tanzania siyo kwamba ni jambo la bahati mbaya. Sasa limetokea balaa la *Corona,* fedha zote ambazo watu walipanga kujanazo kufanya utalii Tanzania, wamezitumia kutokana na hii hali ya *lockdown.* Sasa Wizara ina kazi kubwa ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Wizara, tuna nchi ambazo zina watu wengi kwa mfano China, Brazil, Urusi, Indonesia, *USA*, Peru, Canada na Malaysia; tuboreshe tuwe na mkakati katika Balozi zetu ambazo ziko katika hizo nchi, tuwawekee malengo, kila Balozi ambaye yupo katika nchi hizo anafanya jitihada gani katika kutangaza utalii? Tuwe na *data base* ya Watanzania wanaoishi katika nchi hizo. Kwa mfano, wanafunzi; tuhakikishe kila wanafunzi ambao wanakuwepo huko, tunawapa kazi ya kuutangaza utalii na wawe wanaturudishia *feedback.* Wagonjwa wanaoenda nje, kama wenzetu Wazungu wanavyofanya, ujue kila Mzungu anayekuja Tanzania ana kitu ambacho anatangaza kuhusiana na nchi yake.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, wafanyabishara wanaoenda China, Watumishi wa Serikali ambao wanaenda katika nchi hizo, siyo wanaenda tu kwa ajili kufanya mambo ambayo wamekubaliana kwenda kufanya, lakini awe na jukumu kwa ajili ya kuutangaza utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa utalii wa ndani sasa; kwa mfano, kwa kipindi hiki hapa, kama Wizara ingeweka mikakati kwa ajili ya kuutangaza utalii wa ndani kwa kipindi hiki ndiyo ingeweza ku-*save* hilo janga la kukosa mapato katika utalii. Kwa mfano, nakumbuka katika enzi zetu wakati tunasoma tukiwa wanafunzi, tulikuwa tunatamanishwa na tulikuwa tunatamani kwenda katika mbuga za wafanyama, lakini sasa hivi hiyo mikakati haipo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke hilo katika sera, yaani wanafunzi wanaposoma kuwe na utaratibu wa kwenda kutembelea mbuga za wafanyama kuanzia Shule za Msingi mpaka za Sekondari. Wafanyakazi kuwe na utaratibu huo wa kwenda katika mbuga za wafanyama.

Mheshimiwa Spika, kwa viongozi, nikupe taarifa tu, kuna Waziri mmoja simtaji jina lake, mpaka amekuwa Waziri hajawahi kumwona tembo. Wakati tunasafiri, tunaenda Ulanga, akasema naomba tupite Mbuga ya Mikumi mchana ili tuweze kuona tembo. Sasa hiyo inaonekana ni kwa namna gani katika nchi yetu hakuna sera nzuri ya watu kutembelea mbuga za wafanyama...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga, kwa Wazanzibar wakisikia Mheshimiwa Waziri hajawahi kuona tembo, eeeh, endelea kuchangia Mheshimiwa Mlinga. *(Kicheko)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, mwisho tu niseme, Tanzania tuna vitu vingi ambavyo viko *unique,* siyo tu kwenye masuala ya mbuga za wafanyama, wenzetu wanauza hata tabia zao ambazo zipo, wanaweza kuuza nje. Kwa mfano...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kiswahili kipana sana na nchi yetu ni kubwa.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John

Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassimu Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri na Viongozi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza Mhimili wa Bunge hasa katika kipindi hiki tunapopambana na janga la *Covid-19*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, imetekeleza kwa ufanisi kuboresha mazingira ya utalii kiasi cha kuvutia watalii katika maeneo mbalimbali ikiwemo Mataifa ya Mashariki ya mbali na hata China. Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, utalii umechangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa. Kutokana na maafa ya *Covid-19*, Sekta ya Utalii imeathirika sana ambapo kutapelekea upungufu mkubwa wa pato la Taifa na hasa fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya maeneo yetu ya utalii na kipindi hiki taasisi za utalii zisaidiwe bajeti za kuendelea na shughuli zake. Pia Serikali iangalie jinsi ya kupunguza mzigo wa kodi na michango ya *TANAPA* ili ijielekeze kuwekeza kwenye vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na Watendaji. Ushauri wangu, kutokana na ugonjwa wa *corona* hali ambayo imeshusha mapato ya utalii ni vyema sasa tukaimarisha utalii wa ndani Serikali ishirikiane na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

kuendeleza mradi wao wa utalii wa ndani. Sambamba na hilo kila mkoa sasa kuna haja ya kuanzisha vyanzo vya utalii kwa wananchi wake.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Spika, Bajeti inayozingatia uhalisia wa *Covid-19 (Covid19 Sensitive Budget)*

Mheeshimiwa Spika, kwa kuzingatia mchango wa Sekta ya Maliasili na Utalii katika ukuaji wa pato la Taifa na mapato ya Serikali, katika mchango wangu nimedhamiria kuishauri Serikali namna ya kuibadilisha taswira ya bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuzingatia uhalisia wa *Covid-19 (Covid-19 sensitive budget)*.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimeangalia mwenendo wa ukusanyaji wa mapato katika tovuti ya *TRA* kwa robo mwaka ya tatu ya mwaka wa fedha 2019/2020. Mwenendo bila kuangalia vyanzo vya mapato vinavyotokana na Sekta ya Maliasili na Utalii kwa ujumla mapato ya ndani, mapato ya ushuru wa forodha na mapato ya walipakodi wakubwa yanaonekana kupungua katika robo ya tatu ya mwaka 2019/ 2020 ukilinganisha na robo ya pili ya mwaka huo.

Mheshimiwa Spika, sababu za kupungua zinaweza kuwa nyingi; ndio sababu mchango wangu nitauelekeza kwenye ushauri wa nini Serikali ifanye ili kuweza kukabiliana na athari ya *Covid-19* katika mapato ya nchi yatokanayo na utalii.

Mheshimiwa Spika, robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2019/2020 mwezi Machi mapato ghafi *(gross revenue)* ya mapato ya ndani, mapato ya ushuru wa forodha na mapato ya walipakodi wakubwa yalikuwa shilingi trilioni 4.42, wakati robo ya pili ya mwaka huo mapato yalikuwa shilingi trilioni 4.88. Katika Mapambano ya *Covid-19* usafiri wa anga umesitishwa hivyo sekta nzima ya utalii hasa kupokea wageni kumesitishwa. Jambo hili litaathiri ukuaji wa mapato ya Serikali na pia ukuaji wa pato la Taifa; jambo hili pia linatarajiwa kuathiri utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, wakati ambapo hatukuwa na janga la *Covid-19* mapato ya utalii yalionekana kupungua; ukiangalia robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2019/2020 mwezi Machi mapato ghafi *(gross revenue)* kwenye Idara ya Mapato ya Ndani *(Domestic Revenue Department)* mapato ya *VAT* kutoka kwa *Tour Operators* yalipungua mpaka shilingi bilioni 8.62 kutoka shilingi bilioni 13.35 robo ya pili, na shilingi bilioni 18.23 robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, wakati ambapo hatukuwa na janga la *Covid-19* Mapato ya Idara ya Walipakodi Wakubwa kwenye tozo za *VAT* kwa *Tour Operators* mapato yalipungua kutoka shilingi bilioni 5.72 robo mwaka ya pili mpaka shilingi bilioni 5.02 robo mwaka ya tatu. Katika Idara ya Mapato ya Ndani mapato ya *VAT* kwenye Huduma za Hoteli *(Hotel Service)* y alishuka kutoka shilingi bilioni 16.58 robo ya kwanza, shilingi bilioni 11.56 robo ya pili na kushuka mpaka shilingi bilioni 10.19 robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2019/ 2020.

Mheshimiwa Spika, hakuna shaka kuwa mwaka wa fedha wa 2019/2020 utakapokuwa unaisha mwezi Juni 2020 na mwaka Mpya wa Fedha wa 2020/2021 utakapokuwa unaanza mapato kwenye Sekta ya Utalii yatapungua kwa kiwango kikubwa sana kwa sababu ya janga la *Covid-19*. Ushauri wangu kwa Serikali kwa sababu Sekta ya Utalii imeathiriwa na janga la *Covid-19* kwa nchi nyingi kufunga mipaka yake na sisi pia kufunga mipaka yetu na kuzuia ujio wa wageni wa sekta hii, jukumu la kwanza la Serikali kujenga ni *confidence* kwa wageni kuwa Tanzania ni nchi salama kwa Watalii kuendelea kuja hata kama janga hili litaendelea kuikabili dunia.

Mheshimiwa Spika, *confidence* ya watalii kuja nchini itategemea na hatua ambazo Serikali inazichukua sasa hivi katika mapambano dhidi ya *Covid-19*. Naishauri Serikali kuongeza uwazi katika takwimu za ugonjwa huu ili kuongeza *confidence* ya wageni pale ambapo Serikali itatangaza kufungua mipaka yetu kwa ajili ya utalii.

Mheshimiwa Spika, uwazi katika Takwimu ni pamoja na kuonesha ni kwa kiwango gani mikoa inayoongoza kwa shughuli za utalii imedhibiti kusambaa kwa maambukizi ya *Covid-19*. Pia ni pamoja na kuamua kuanza kwa mkakati maalum wa kuwapima *Covid-19* kwa hiyari wadau wote wanaohusika na tasnia ya utalii katika mikoa inayoongoza kwa utalii ili kuweza kujenga *confidence* ya wageni endapo mipaka itafunguliwa kwa ajili ya utalii.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuanzisha Mkakati wa Kufungua Sekta ya Utalii dhidi ya Ugonjwa wa *Covid-19*. Mkakati huu uende sambamba na hatua za makusudi za upimaji wa hiyari kwa watu kwenye maeneo ya utalii ili kuiwezesha Serikali kuwa na takwimu za kiwango cha maambukizi na kuchukua hatua za ziada katika kudhibiti maambukizi mapya.

Mheshimiwa Spika, mwaka mpya wa Fedha 2020/ 2021, Serikali imetenga fedha za bajeti ya maendeleo Fungu 69 kwa ajili ya Wizara ya Maliasili na Utalii jumla ya shilingi bilioni 45.02 huku fungu dogo 5203 la fedha za Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali kwa ajili ya Ukuaji wa Utalii *(Resources Management for Tourism and Growth Project (REGROW)* likitengewa fedha za ndani milioni 200 na fedha za nje bilioni 30.29. Bajeti hii haina fungu maalum la kuiwezesha Wizara kujiandaa kuifungua Sekta ya Utalii dhidi ya ugonjwa wa *Covid-19*.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwa kuzingatia unyeti wa sekta hii Serikali ifikirie kuwa na fungu maalum litakalogharamia gharama mahususi za kuifungua upya sekta ya utalii hasa kuhusu ushauri wangu juu ya Mkakati wa Kufungua Sekta ya Utalii dhidi ya Ugonjwa wa *Covid-19*.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umakini na weledi wa hali ya juu sana. Mungu aendelee kukupa hekima zaidi za kuendeleza kazi yako hii. Aidha, nakushukuru

sana kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake wote kwa kuweza kutayarisha na hatimaye kuiwakilisha hotuba hii kwa ufanisi wa hali ya juu sana. Katika kuchangia hotuba hii napenda kuzungumzia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, utambulisho wa utalii wetu katika Ofisi zetu za Kibalozi. Kama inavyojulikana kuwa utalii ni miongoni mwa vyanzo muhimu sana vya mapato katika nchi yetu. Tanzania imebarikiwa kuwa na aina nyingi sana za utalii kama vile wanyama ambao wamezagaa katika kila pembe ya nchi yetu. Hata hivyo, hali hii ya kuwepo wanyama katika mapori yetu ni nchi chache sana wanaoifahamu. Bado kuna nchi nyingi sana hazielewi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika kutatua suali hili kwa Serikali kupitia Wizara zetu mbili ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Mambo ya Nje ni kuweka Maafisa wetu katika kila ofisi yetu nje ya nchi ambaye atakuwa anashughulikia na kuyatangaza maeneo yetu akiwa huko nje ya nchi . Hii itarahisisha kuyatangaza vyema maeneo yetu ya kitalii. Aidha, njia hii haitakuwa na gharama kubwa kwa vile Afisa anayeshughulikia atakuwa yuko nchi husika badala ya kutoa mtu maalum hapa nchini kwenda kutangaza nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Maliasili kwa Hotuba yake nzuri ya Bajeti aliyoisoma leo Bungeni tarehe 7 Mei 2020. Waziri amefanya tathmini nzuri ya madhara yatokanayo na athari za janga la corona katika sekta ya utalii. Uchumi wetu kama ulivyo uchumi wa nchi nyingine utaathirika kwa kiasi fulani lakini lazima tusonge mbele tujipange tuje na mikakati mizuri na endelevu.

Mheshimiwa Spika, jimboni kwangu yapo majanga ya wananchi kuuawa na mamba waliomo kwenye mito mikubwa ya maji hususan Mto Mvuha na Mto Ruvu. Leo hii nimepata taarifa ya mama aliyeuawa kwa kuchukuliwa na mamba katika Kijiji cha Bwila, Kata ya Selembala mama huyu ameacha mtoto wa miaka miwili. Maafa haya yanajirudia mara kwa mara na nimeshazungumzia hapa Bungeni mtoto wa Shule ya Msingi Selembala aliyeuawa na mamba mwezi uliopita. Hatuwezi kuacha watu wanauawa na mamba Maafisa wa Maliasili hawachukui hatua zozote za kuepusha maafa haya haiwezekani kudharau maisha ya binadamu kwa ajili ya mamba. Inawezekana mamba wamezidi idadi kwenye Mto Mvuha na Ruvu kwenye maeneo ya Mvuha, Selembala na maeneo mengine ya Jimbo la Morogoro Kusini mito hiyo inamopita, hivyo tunaomba uvunaji wa mamba hao haraka sana ili wananchi waishi kwa amani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa mchango wangu wa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, natambua *TANAPA* walitupa kiasi cha shilingi bilioni 1.7 kutengeneza madaraja mawili. Daraja la Mto Lagosa na Daraja la Mto Rukoma. Kwa bahati mbaya ujenzi ulikuwa haukuzingatia wingi wa maji, hivyo mvua za msimu huu zimeharibu sana madaraja hayo hivyo kupelekea wananchi na watalii kupata tabu katika kuvuka kwenye madaraja hayo. Tuiombe *TANAPA* kusaidia kurekebisha madaraja na kipande cha barabara cha kilometa 30 kutoka Rukoma hadi Hifadhi ya Mahale.

Mheshimiwa Spika, mchango wa pili ni kuhusu kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Rais kutembelea vijiji vyote vyenye migogoro na Hifadhi na migogoro na misitu. Tangu Tume hii

iundwe iliyokuwa ikiongozwa na Mheshimiwa Waziri Lukuvi na kukabidhi taarifa kwa Mheshimiwa Rais haijatoa majibu kwa wananchi. Ni vema wawakilishi wa wananchi tupatiwe majibu ili basi iwe rahisi kutoa majibu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa tatu najielekeza kwenye umuhimu wa Wizara/*TANAPA* kutupa gari la maliasili ikiwezekana kutoa gari lenye uwezo wa kupanda milima kwenye mazingira ya barabara za vijiji vya Wilaya ya Uvinza hususan upande wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, nichangie pia suala la *TANAPA* kutoa asilimia mbili za kuchangia miradi ya kijamii. Natambua sheria inawataka wasizidishe asilimia mbili na mara nyingi huwa wanatoa misaada ya ujenzi wa miradi ya kijamii hadi asilimia tano na kujikuta *TRA* inawatoza kodi ili hali *TRA* inatambua fika asilimia hiyo tatu inayozidi imetumika kwenye miradi ya kijamii kama zahanati na mashule, hivyo tuiombe Wizara ya Fedha kupitia marekebisho ya *Finance Bill* kufanya marekebisho ya sheria hiyo ili kutoa hiyo kodi ya asilimia tatu inayozidi.

Mheshimiwa Spika, nichangie pia suala la Wizara ya Maliasili kutozwa kodi wanapoagiza vifaa vya jeshi husu la kulinda hifadhi mbalimbali, cha ajabu vifaa hivi yaani silaha na sare za jeshi husu vinaagizwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, vifaa vya jeshi havitozwi ushuru, vifaa vya jeshi husu vinatozwa ushuru. Hii haingii akilini, hivyo tuiombe Serikali kuliangalia hili na kutoa msamaha wa kodi kama wanavyotoa msamaha kwenye majeshi mengine.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Utalii kuwa, kwa kuwa tatizo la *Covid 19* limepelekea nchi nyingi duniani kusitisha safari za ndege hivyo kupelekea watalii kutokuwepo na kuyumbisha uchumi wa nchi na mapato yaliyokuwa chini ya Taasisi za Wizara kama *KINAPA, TANAPA* na kadhalika, hivyo ni vema Serikali ikakubaliana na pendekezo la Kamati la kupunguza *visa* pindi vizuizi vitakapofunguliwa.

Mheshimiwa Spika, suala la wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini kuliwa au kujeruhiwa na mamba na viboko na wanaojeruhiwa na baadhi wanaopoteza maisha hawalipwi fidia, tuiombe Wizara kuliangalia hili kwani wapo waliokufa na kuacha wake na watoto.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze kwa uendeshaji mzuri wa Bunge lako Tukufu katika kipindi chote cha miaka mitano ya uhai wake. Aidha, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuonyesha wazi uchungu alionao juu ya maliasili zetu kwa niaba ya Watanzania wote, hakika Magufuli ni jembe la Watanzania. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba nisemee mambo mawili tu kwa umuhimu wa kipekee. Jambo la kwanza ni kuhusu lango kuu la watalii kuingia katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ambalo ni Ndabaka lililoko Wilaya ya Bunda Mkoa wa Mara. Niishauri Serikali kuweka wazi msimamo wake juu ya lango hili kwani bado ipo dhana potofu kwamba lango kuu la kuingilia hifadhini liko katika Hifadhi ya Ngorongoro. Aidha, tunaishukuru Serikali kufungua Ofisi za Kanda za *TANAPA* katika Wilaya yetu ya Bunda kwani Wilaya yetu na maeneo ya jirani yatanufaika sana na masuala ya utalii.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, niishauri Serikali kulipa fidia ya uharibifu wa mazao ya wananchi unaofanywa na wanyama watokao kwenye hifadhi zetu, mapori tengefu, mito pamoja na maziwa. Aidha, kwa muda mrefu sasa Serikali haijawalipa familia za wananchi ambao wameuawa na wanyama wakali kutoka hifadhini. Mathalani, kuna wananchi wa Jimbo la Mwibara ambao wamejeruhiwa au kuuawa na wanyama wakali akiwemo kijana wa mzee Sumuni wa Kijiji cha Namalama aliyeliwa na mamba.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa na nimwombe Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangala, Waziri wa Maliasili na Utalii atatue changamoto ya wananchi wa Semeni katika Kijiji cha Lingusenguse, Wilaya ya Namtumbo watambulike kama wananchi wanaoishi katika maeneo yao halali na sio ndani ya eneo la *WMA* ya Kisungule. Ombi hilo tulimkabidhi wakati wa kupitia maeneo ya hifadhi ambayo yana changamoto ya makazi lakini hajatupa mrejesho. Tafadhali Mheshimiwa Waziri atusaidie kutatua changamoto hiyo kabla ya mwaka huu haujafikia tamati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha mahali hapa salama, nami nishiriki kikao hiki cha kujadili hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya mwaka wa fedha 2020/2021. Hotuba hii inakwenda sambamba kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2015 - 2020, ambayo kwa pamoja imeeleza mambo mengi mazuri na ya msingi hususani katika Sekta ya Utalii na Maliasili. Nitumie fursa hii pia kumpongeza Waziri pamoja na wasaidizi wake kwa kuandaa hotuba nzuri ambayo itakwenda kuleta mapinduzi makubwa katika Sekta ya Utalii na Maliasili.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii ni miongoni mwa nguzo muhimu katika uchumi wa Tanzania kutokana na mchango wake mkubwa katika ukuaji wa pato la Taifa kila mwaka. Watalii wa ndani na kutoka maeneo mbalimbali duniani wamekuwa wakitembelea vivutio vya utalii nchini na kulala katika hoteli za watalii ambazo pia ni miongoni mwa vyanzo vya mapato na ajira kwa Watanzania. Kwa kutambua jitihada mbalimbali ambazo Serikali imekuwa ikizichukua katika kuhakikisha Sekta ya Utalii inaendelea kufanya vizuri kwa umuhimu wake wa kuchangia pato

Serikalini, sekta hii imekuwa tegemeo hasa kwa kuchangia pato kubwa Serikalini kutokana na vivutio mbalimbali tulivyobarikiwa kuwa navyo ambavyo tumekuwa tukipokea wageni kutoka mataifa mbalimbali kuja kutembelea vivutio hivyo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kutokana na hali halisi inavyoendelea hapa nchini na duniani kwa ujumla, janga la *Corona Virus (Covid-19)* limeathiri kwa kiasi kikubwa Sekta hii ya Utalii na nchi kwa ujumla, Makampuni ya Utalii yamesimama kazi, wafanyakazi wamesimama kazi, mahoteli yamefungwa pamoja na wafanyakazi wao kurudi majumbani, hakuna mzunguko wowote wa fedha unaopatikana kwa sasa kwa sababu hakuna wageni wanakuja kutembelea vivutio vyetu. Hali hii imetikisa uchumi wa dunia nasi pia imetupata, ni kipindi sasa cha kutafakari na kuangalia ni kwa namna gani tutaweza kuwashawishi watalii kuanza kuja kwa wingi tena hata baada ya janga hili kupungua ama kuisha kabisa. Nazungumza haya sababu janga hili limeua watu wengi hasa nchi za Ulaya, Amerika na Asia ambazo ndio tumekuwa tukipokea watalii wengi kutoka kwenye mataifa hayo.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto ya kuwepo kwa uharibifu wa mazingira na uvamizi wa mifugo na makazi ya watu katika maeneo ya vivutio vya utalii vya asili, ni baadhi ya sababu zinazochochea kushuka kwa ubora wa vivutio vingi vya utalii vya asili. Vitendo hivi vimepelekea kushuka kwa ubora na sifa kwa baadhi ya vivutio vyetu. Chanzo kikuu ni uharibifu wa mazingira na uvamizi wa maeneo ya hifadhi, hata hivyo bado kama nchi tunashika nafasi ya kwanza barani Afrika kutokana na kuwepo kwa sera na mikakati madhubuti ya kulinda na kuendeleza rasilimali za asili ambazo zimekuwa zikihitajika zaidi katika kuvutia watalii.

Mheshimiwa Spika, natambua jitihada mbalimbali zinazofanywa na Wizara katika kuhakikisha tunatangaza vivutio vyetu ili kuongeza watalii nchini, ni mkakati mzuri na wa kupongezwa. Aidha, nisiishie hapo, bali naishauri Serikali

kuongeza nguvu na kuangalia mbinu mpya za kuvitangaza vivutio vyetu. Hii itasaidia sana kuongeza idadi ya watalii na hasa katika kutangaza vivutio hivyo Wizara iangalie namna ya kuongeza vivutio vingine vya asili ili navyo vilete tija kwa Taifa letu. Nchi yetu ni miongoni mwa nchi 12 za kibaolojia kwa Afrika na duniani kote kwa idadi kubwa ya wanyama, ya pili kwa ukubwa wa mimea, ya tatu kwa idadi kubwa ya ndege na ya nne kwa idadi kubwa ya *amphibians* na *reptile*, vyote hivyo vinatunzwa na misitu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuna zaidi ya hekari 46 milioni za misitu Tanzania, sawa na inavyokadiriwa asilimia 50 ya eneo lote la ardhi ya nchi. Zaidi ya asilimia 30 ya misitu inalindwa. Japokuwa uharibifu wa misitu nchini kwetu ni changamoto isiyozuilika au kuepukika, zaidi ya makadirio ya hekari 500,000 za misitu hupotea kila mwaka kutokana na kutokuwa na matumizi endelevu ya ardhi, uvunaji wa mazao yatokanayo na misitu na shughuli za kibinadamu. Kwa mwitikio wa mafanikio ya mpango wa majaribio mbalimbali pamoja na mabadiliko ya sera mwanzoni mwa miaka ya 1990, Taifa letu lilianzisha mpango wa kitaifa wa usimamizi wa misitu kwa kushirikisha watu katika kuhifadhi na kutunza misitu.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa misitu wa jamii ni mojawapo ya aina za mpango wa kitaifa wa usimamizi wa misitu kwa kushirikisha watu *PFM* kwa kushirikisha watu katika utunzaji wa misitu. Usimamizi wa misitu wa jamii ni moja wapo ya aina za *PFM* ambazo zinatumika kwa misitu ambayo inamilikiwa au kusimamiwa na Halmashauri za vijiji na zitapelekea kuanzishwa kwa hifadhi za misitu na ardhi. Taifa letu ni miongoni mwa nchi zinazoongoza Barani Afrika kwa kutekeleza hizi sera, kukiwa na zaidi ya hifadhi za ardhi na misitu, 500 zilizoanzishwa kuanzia mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya misitu ya Angai ni makubwa miongoni mwa maeneo ya hifadhi ya ardhi na misitu yaliyotangazwa na mengine 11 yapo katika hatua tofauti za *CBFM*. Japokuwa kuanzishwa kwa Angai *VLFR* ilikuwa taratibu kutokana na uhaba wa uwezo wa kuanzishwa umilikishwaji na usimamizi wa mazao ya misitu,

ni vema sasa Serikali ikaangalia faida na maliasili tulizojaaliwa kuzitumia ipasavyo kama vivutio hasa kutuingizia kipato.

Mheshimiwa Spika, ukataji miti, uharibifu wa misitu na mabadiliko ya matumizi ya ardhi ni sababu kuu mbili zinazosababisha uzalishaji/ kusambaa kwa hewa ya ukaa ambayo inachangia asilimia 17 ya uzalishwaji wote duniani. Kiwango cha ukataji wa misitu Tanzania kwa mwaka inakadiriwa kuwa zaidi ya hekari 500,000 kwa mwaka na inakadiriwa kuwa ni asilimia moja ya misitu ya Taifa. Ukataji miti huu unapelekea uharibifu wa mazingira na kupotea kwa makazi ya asili ya wanyamapori. Kisababishi kikubwa cha ukataji wa miti ni usafishaji wa maeneo na matumizi yasiyo endelevu ya ardhi kwa ajili ya kilimo, ufugaji wa mifugo inayozidi malisho, uchomaji moto, ukusanyaji na ukataji wa kuni kwa ajili ya kupikia na shughuli zinazoendana na hizo, ukataji wa magogo kinyume cha sheria kwa ajili ya kujengea na kupata mbao kwa ajili ya kuuza, kuchoma mikaa na uchimbwaji wa madini katika hifadhi za misitu.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mkaa ambao ndio chanzo kikuu cha mapato kwenye baadhi ya misitu. Kuzalisha mkaa, watu wanatumia njia za asili kwa kuchimba matanuru kama njia rahisi, haihitaji ujuzi wowote na inatumia mtaji kidogo kuwekeza. Njia hii ya asili ya kubadili kuni/mbao kuwa mkaa hupoteza zaidi ya kama asilimia 70 ya thamani halisi ya miti kwa sababu kufukia matanuru/mashimo ni vigumu na ni hatari kwa opereta kukarabati. Matokeo yake kuvuja kwa hewa hakuwezi kudhibitiwa na mkaa unakuwa majivu na baadhi ya sehemu ya rundo la mkaa kabla haujakamilika vizuri. Njia hii isiyo na ufanisi katika uzalishaji wa mkaa inaongeza shinikizo katika baadhi ya misitu nchini, kwani katika hali nyingi wazalishaji wa mkaa hawapandi miti kama mbadala/kuchukua nafasi ya miti iliyokatwa hivyo kupelekea uharibifu wa misitu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuendelea kuchukua hatua mabalimbali za kisheria na kimkakati pale inapowabaini wale wote wanaokiuka taratibu na sheria

zilizowekwa kwa kukata miti hovyo na kuchoma mkaa, ama kukata miti hovyo pasipo kuwa na vibali na kufaidika na rasilimali hiyo pasipo uhalali wowote.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kuchukua hatua mbalimbali za kimkakati katika fursa zilizopo kwenye sekta hii ya maliasili; wananchi waambiwe ni kwa namna gani wanaweza kushiriki kikamilifu wakatunza mazingira kama kupanda miti na mambo mengine mazuri yatokanayo na misitu ili tuepukane na janga linaloweza kutokea hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, pia wananchi waambiwe ni kwa namna gani misitu inaweza kuwanufaisha hasa wakiwekeza katika mizinga ya uvunaji wa asali na kufaidika, ni fursa kubwa ambayo kama Wizara wakishirikiana kwa karibu na wananchi na kuwapa elimu basi itasaidia sana kukabiliana na vita hii ya ukataji miti hovyo na wananchi kufaidika na aina ya uwekezaji watakaoufanya katika misitu hiyo kama kuvuna asali.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali iangalie namna ya kuwaelimisha wananchi kutumia njia mbadala ya nishati mkaa, ili kupunguza ukataji miti na uchomaji wa mkaa ambao umekuwa ukiharibu mazingira kwa muda mrefu. Hali kadhalika Wizara ichukue hatua kwenye maeneo yote ambayo kumeripotiwa kuwa na wanyama korofi wenye kuleta madhara kwa wananchi, wanyama hao wapunguzwe na kama wanafaa kwa matumizi ya binadamu kama kitoweo basi wakivunwa wauzwe kwa wananchi kwa bei nafuu ili kukabiliana na changamoto ya wananchi kushambuliwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mungu kwa kunipa uwezo wa kuchangia kwa maandishi ndani ya Wizara hii. Pia natoa pongezi za dhati kwa Waziri, Naibu na watumishi wote kwa ujumla wao wakiongozwa na Katibu Mkuu wao. Kwa kazi nzuri

waliyofanya kwa uzalendo na kutufikishia gawio la pato la Taifa kufikia 17%, ni hatua kubwa, yenye mwelekeo wa kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara ya Fedha kubadilika katika kutoa fedha kwa ukamilifu wake kwa kuzingatia bajeti zinazopitishwa na Bunge, ziwasilishwe kwa wakati kwa maendeleo ya Wizara hii ambayo inatuingizia gawio kubwa ndani na nje. Penye mafanikio penyeza rupia ili uweze kupata zaidi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na funzo tulilopata sasa, kwenye hili janga la *corona* na kupelekea uchumi wetu kushuka na hifadhi kuzorota na ulinzi kutoweka, tutaendelea kurudi nyuma zaidi. Tunaomba Serikali kukubaliana na Kamati kuwa na Mpango wa kudumu siyo wa dharura wa Mfuko wa Hifadhi kwa uhifadhi wa akiba ya fedha zitakazokuja kusaidia Mashirika, Taasisi za Uhifadhi na Utalii kiujumla. Tungekuwa nao hizi changamoto za *TANAPA* zisingekuwepo kwa watumishi, walinzi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kutoa shukrani za dhati kwako Mheshimiwa Spika kwa kazi ya malezi yaliyotukuka kwetum Mola akujalie, akupe afya na maisha marefu na mafanikio ya ushindi ndani ya Jimbo lako. Bila kumsahau Naibu Spika aliyeonyesha umahiri mkubwa sana, naye Mungu amjalie ushindi mkubwa kwenye Jimbo la Mbeya Mjini. *Inshallah*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, niungane na viongozi wote wa Taifa letu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka, ulinzi, amani na mafanikio kwa kipindi cha miaka yote mitano ya uhai wa Bunge letu kwani kila jambo ni kwa mpango wake. Aidha kupitia imani zetu maombi, sala, dua kwa pamoja tuendelee kumwomba sana Mwenyezi Mungu atuondoshee janga hili

la *corona* ndani ya nchi yetu na uso wa dunia nzima. Ewe Muumba wetu uturehemu. Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naungana na viongozi wote wa Taifa letu kuwapa pole nyingi ndugu zetu waliofariki dunia kwa namna mbalimbali, awapokee katika ufalme wake usio na mwisho na kuzilinda familia zao.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini, nachukua nafasi hii kuwapongeza sana viongozi wakuu wa nchi yetu kuanzia kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika, Mawaziri wote na waandamizi wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa jinsi walivyoliongoza Taifa letu na kutekeleza Ilani ya CCM kwa kiwango cha juu sana. Hakika Tanzania imepiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu kwa Serikali kupitia Wizara hii:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali yetu ifanye utafiti, mapitio, ili kupunguza vikwazo, masharti, katika biashara ya utalii kwa ajili ya kuvutia watalii na wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali ifanye mapitio ya Sheria mbalimbali za Maliasili na Utalii kwa ajili ya madhara makubwa ya maisha ya wananchi na mali zao ili kuleta mahusiano mazuri kati ya Maafisa wa Serikali na wananchi katika meneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, tatu, Wizara iwe na mpango/ ratiba ya kufanya vikao vya ujirani mwema ili kuendeleza mahusiano mazuri kati ya jamii na Maafisa Mamlaka za Hifadhi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali ielekeze uanzishwaji wa miradi mbalimbali ya ujirani mwema kati jamii na Mamlaka za Hifadhi zinazozunguka vijiji ziwe wazi kwenye

mipango yao toka mwanzo ili kuondoa malalamiko wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, tano, Halmashauri ya Mbulu Mji haina Maafisa Wanyamapori toka mwaka 2016, rejea ni barua yangu kwa Katibu Mkuu 2018.

Mheshimiwa Spika, sita, kwa kuwa shughuli za kilimo katika vijiji vinavyozunguka Hifadhi za Taifa na Misitu ya Asili zinaathirika na wanyama, Wizara ione umuhimu wa shughuli mbadala kama ufugaji wa nyuki, ng'ombe, mbuzi wa maziwa ili kupunguza shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, saba, kwa kuwa wanyama wengi huja kwenye makazi ya watu kwa ajili ya kutafuta maji, Serikali ifanye utafiti wa kuchimba mabwawa ya maji kwenye viwanja vya wazi ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, nane, kwa kuwa utamaduni wetu, masalia ya mambo ya kale ni sehemu ya utalii wetu mzuri sana hivyo basi televisheni ya Tanzania Safari iweze kupanua wigo wa vipindi vya utamaduni na vivutio vya mambo ya kale. Hali hii itahusisha utalii wa ndani na wageni kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mungu kwa kunipa afya njema ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Maoni; naishauri Serikali fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitolewe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali miundombinu katika mbuga zetu iboreshwe maana kipindi cha mvua ni changamoto, barabara hazipitiki inakuwa sio rahisi kwa watalii kufika maeneo ambayo wataona wanyama.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kifuta jasho kizingatiwe kwa wale wananchi waliojeruhiwa na wanyama na kuuawa na wanyama walipwe kifuta machozi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naishauri Serikali itenge misitu ili miti yake itumiwe na watafiti kutengeneza dawa kwa ajili ya tiba.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mungu kwa uhai na kuweza kuchangia kwa njia hii ya maandishi katika hotuba hii muhimu ya Maliasili na Utalii. Naomba niongelee kwa ufupi juu ya maeneo matatu. Kwanza, shukrani zangu kwa Wizara. Pili, masuala ya mipango ya mipaka kati ya Hifadhi na Vijiji vinavyozunguka Hifadhi husika na tatu ni janga la Covid 19 na Utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe na uongozi wako wa Bunge kwa uendeshaji mzuri wa Taasisi hii muhimu ya Bunge katika kipindi hiki cha miaka mitano. Nakupa pia pole kwa vifo mbalimbali vya Wabunge wenzetu kwa muda huu wote tunapoenda kuhitimisha shughuli za Bunge kwa miaka hii mitano. Naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na kumshukuru sana kwa kujitoa kwa moyo wote katika kusimamia maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nimeridhishwa sana binafsi kwa namna nchi yetu inavyopiga hatua chini ya uongozi wake mahiri. Kila kukicha naona faraja kwamba imani yangu na nafsi yangu iliyonituma nifuate njozi za mtu anayeipenda Tanzania kwa moyo wote toka chama cha kupinga kila kitu cha CHADEMA, sijakosea na kwamba moyo wangu una amani sana kwa maamuzi niliyofanya mwaka 2018 ya kuondoka miongoni mwa watu wasio na njozi na upendo wa kweli na nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maamuzi aliyochukua juu ya tatizo hili la kirusi cha

*Corona*. Hakika anaifahamu nchi yake na kipato cha watu wake. Ukiwafungia ndani watu wengi hata wale ambao wana afya nzuri ya kupambana na ugonjwa wa *Covid 19* watakufa na njaa. Nchi hii bado si tajiri ya kuweza kuwahudumia Watanzania majumbani kama wanavyoweza kufanya nchi zenye uchumi wa juu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie hotuba. Naishukuru Wizara hii ya Maliasili kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kwa miaka hii mitano na kwa hakika tangu timu ya Dkt. Kigwangala iingie kwenye Wizara hii, mambo yamekuwa mazuri sana. Changamoto haziishi, lakini kazi imefanyika ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi wafugaji wangu walivyopata changamoto ya kushikiliwa kwa mifugo zaidi ya 300 kule kwenye pori tengefu la Mkungunero nilipata ushirikiano wa kutosha wa Wizara hii na kwa kweli Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Kanyasu alifika mpaka Kimotorok na kuongea na wananchi na hakika kwenye mkutano huo wa hadhara ambao mimi na yeye tulipata bahati ya kuhutubia wananchi walituelewa sana. Nawashukuru wafanyakazi wote wa Hifadhi ya Tarangire na Mkungunero, sisi ni majirani wa kudumu ni vema tutafute namna ya sisi kwa sisi kuishi kwa amani. Nashauri tungeunda timu za ushirikiano ili mara kwa mara matatizo yakiwepo timu hizi ndizo zifanye kazi ya kusuluhisha matatizo badala ya kuyaleta huku Wizarani.

Mheshimiwa Spika, pili, suala la vijiji vinavyozunguka hifadhi zote nchini. Kwa Wilaya ya Simanjiro kijiji kilichokaribu mno na hifadhi ya Tarangire na Pori Tengefu la Mkungunero ni Kijijji cha Kimotorok. Kwa kuwa mimi kama Mbunge wa Jimbo la Simanjiro bado nakumbuka ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitolea maelekezo na mpango mkakati kwa ajili ya vijiji vyote nchini vinavyozunguka Hifadhi, aliunda timu ya Mawaziri nane ikiongozwa na Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kazi hii ilikuwa ya nchi nzima. Pamoja na maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. John

Pombe Magufuli, bado maeneo ambayo yamekuwa na mgogoro kati ya vijiji na hifadhi hizi hazijatengwa na ramani kushirikisha wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni vema kwa ushauri wangu, zoezi hili liwe la uwazi sana kuliko wahifadhi ambao mara zote wamekuwa na nia ya kutaka ardhi hii iporwe toka kwa wanakijiji wakaachiwa kazi hii kusimamia wenyewe na watu wa Serikali toka taasisi mbalimbali. Ni vizuri wanakijiji na jamii ishirikiane na Serikali ili mwisho wa siku, kila upande utambue na kuridhika kwa kiwango kikubwa na maamuzi ya mipaka mipya itakayowekwa. Amani ya kudumu juu ya suala hili na kutimiza njozi za Mkuu wetu wa Nchi ni kuridhiana wote.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni kuhusu ugonjwa wa *Covid 19* na jinsi ulivyoathiri utalii duniani na kuwa *very precise* hapa nchini kwetu. Kwanza nitoe pole kwa Wizara kwani hata zile taasisi ambazo zilikuwa mwanzoni zinachangia kwenye pato la Taifa kwa kiasi kikubwa nao sasa wataanza kutegemea Hazina kuu moja kwa moja katika kuendesha mambo yao. Hali ya kipato kwao ni ngumu sana. Shirika kama *NCAA, TANAPA* kwa kweli mimi nawaonea huruma na kuwatakia kheri katika changamoto hii ya kidunia. Tuombe hali itengemae mapema iwezekanavyo. Tutegemee dawa ya wenzetu wa Afrika, nchi ya Madagaska itaponya na tutaanza kurudi kwenye hali ya mwanzo mapema iwezekanavyo. Kutokana na hilo naomba nishauri yafutatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara na Taasisi zote zitumie janga hili kama fursa ya kurejesha mbuga, hifadhi na mapori yetu na maeneo ya utalii kama pembezoni mwa bahari katika hali yake ya asili. Usafi ufanyike, maeneo ya unyevunyevu yaangaliwe zaidi ili dunia itakaporejea katika hali yake ya utalii kama hapo mwanzo tuweze kuwa washindani wazuri na kuwavutia watalii wengi zaidi. Tusinyong'onyee hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, Wizara na Taasisi za kitalii ziendeshe uongezaji wa uwezo wa wafanyakazi wake ili

kujiandaa na upokeaji wa wageni wengi mara baada ya janga hili kuisha.

Wizara hii ishirikiane na Wizara ya biashara katika kuokoa hali mbaya wanayopitia wadau wa utalii kama kampuni binafsi za utalii na mahoteli inayokabiliwa na mikopo na riba ambazo kwa namna moja au nyingine kwa hali ilivyo hawawezi kuzilipa kabisa. Ni vema mkono wa Wizara hii uonekane katika kujali na kwenda mbali zaidi kwa kuwaorodhesha wadau hao ili wawasaidie kwenye taasisi za kifedha ili wasifilisiwe na mali zao kutaifishwa. *Referee* wa kweli ni Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Watu wengi niliokutana nao Arusha ambao maisha na ulipaji wao wa kodi ulikuwa mzuri kwa sasa wanapata tabu sana. Wanaomba msaada wa Mheshimiwa Waziri na Viongozi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache, nawatakia kila la kheri katika bajeti inayotegemewa kupitishwa na Wabunge na utekelezaji mwema. Ahsante sana.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali karibu sana, nikupe dakika 10 na Mheshimiwa Waziri dakika 15 ili tuweze kumaliza, kwa sababu Wabunge wengi kwa kweli wamechangia kuwaunga mkono na kukubaliana nanyi na kuwasilisha mambo tu fulani fulani kama maoni ya kufanyia kazi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza naomba kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa neema yake ya uhai ambayo ameendelea kutujalia, lakini kipekee naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kuweza kumsaidia katika Wizara hii. Kipekee tunamshukuru sana kwa juhudi zake kubwa ambazo amezionyesha katika

kutuunga mkono kuhakikisha kwamba Wizara hii ya Maliasili na Utalii inaendela kuwa Wizara yenye manufaaa na inayoingiza mapato sana kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka tu Watanzania kwamba kabla yake tulikuwa tunalalamikiwa nchi nzima kwamba hatuwezi kufika sehemu yoyote kwa sababu hatuna Shirika la Ndege na tumegundua sasa umuhimu wa usafiri wa anga katika kuimarisha utalii baada ya *Corona*. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana viongozi wangu wengine; Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri wote na kipekee Mheshimiwa Waziri wangu Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwa ushirikiano mkubwa ambao uliuonesha na ameuonesha kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Kamati yetu. Hii ni Kamati ya mfano, tumefanya nayo kazi vizuri sana na Wajumbe wote wametusaidia sana, wametushauri vizuri. Kwa kweli tunaamini kwamba mafanikio haya yanatokana na ushauri mzuri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Katibu Mkuu na safu yake nzima Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wake wote, tulifanya kazi nzuri kwa pamoja na sifa nyingi ambazo tunazipata ni kwa sababu kwa kweli tuna watendaji wazuri sana, wanaangalia mbele, wako *very proactive* na mambo mengi tunashirikiana nao vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, bila kusahau, nawashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Geita Mjini. Nafahamu kwamba siku chache zijazo tutakwenda tena kuomba ridhaa yao ya kuweza kurudi hapa. Naamini katika kipindi hiki kifupi cha miaka mitano sijawaangusha, ninaomba tena waweze kuniunga mkono.

Mheshimiwa Spika, naishukuru pia familia yangu kwa sababu katika kipindi hiki cha kutumikia kazi ya Unaibu Waziri

ni tofauti na miaka mingine, sikupata muda wa kutosha kukaa nyumbani, lakini wamekuwa wavumilivu.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naomba sasa kwanza niseme naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Vile vile nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia kwenye Wizara yetu, kama ulivyosema, wengi wameunga mkono hoja na wachache ambao wametoa ushauri, naomba nikuhakikishie tumeuchukua na tutaufanyia kazi. Niwahakikishie kwamba kama ambavyo wameona katika maeneo mengi ambayo walitushirikisha, tulikwenda na tulitoa majibu. Ndivyo tutakavyofanya katika kipindi hiki ambacho mengi yalisemwa.

Mheshimiwa Spika, nianze kujibu hoja na Mheshimiwa Riziki Lulida alizungumza hapa. Kwanza namshukuru sana yeye ni mhifadhi mzuri kwa kweli, ushauri wake siku zote katika hotuba amekuwa akizungumzia masuala ya uhifadhi na utalii; ni mama anayepambana kweli na ujangili kususu tembo, amekuwa akizungumzia kuhusu utalii Kusini na hajifichi na amehudhuria katika mikutano mingi na kila anaporudi amekuwa akileta mrejesho.

Mheshiiwa Spika, kwa hiyo, namshukuru sana kwa mchango mzuri na ushauri wake ambao amekuwa akitupatia. Amezungumzia kwanza kuhusu utalii Kusini kwamba tutofautishe utalii Kusini na utalii wa Mtwara na Lindi. Wizara inafahamu kwamba kuna utalii Kusini kwa maana ya Nyanda za Juu Kusini. Kwa maana ya utalii wa Lindi na Mtwara tumeweka katika Ukanda wa Mashariki Mikoa yote ya Pwani kuanzia Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara. Huu ni Ukanda mmoja ambapo Wizara ilikuwa inakamilisha andiko la kufanya na lenyewe kuleta maonyesho ambayo yataunganisha maeneo yote haya. Kwa hiyo, hatujasahau maeneo hayo. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Riziki Lulida, naamini Mungu ataendelea kutulinda atashuhudia Wizara ikifanya kazi yake vizuri katika Serikali ambayo itakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lulida pia amezungumzia habari ya *TFS* kuhusu utafiti wa dawa za asili. Ni kweli kwamba sisi ndio tunaolea misitu. Kwa hiyo, kama unazungumzia dawa zote za asili, lazima kwanza maeneo haya yalindwe. *TFS* wanafanya kazi yao vizuri kwa kushirikiana na maeneo mengine ya Halmashauri. Pia Taasisi yetu *TAFORI* ambayo pia inafanya utafiti wa kufahamu matumizi ya aina mbalimbali ya miti imekuwa ikishirikiana vizuri sana na Kitengo cha Tiba Asili kilichoko Muhimbili. Kwa hiyo, namhakikishia kwamba suala hili tunalifahamu na tunalichukua, tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na wenzetu wa Muhimbili ambao wamepewa dhamana ya kuangalia matumizi mbalimbali ya misitu na dawa za asili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Cosato Chumi alizungumzia kuhusu bei za mazao. Ni kweli maeneo mengi tumezungumza na wadau na Mheshimiwa Waziri alifanya Mkutano na wadau kule Iringa, walizungumzia habari ya gharama kubwa za mazao ya misitu kutokana na gharama kubwa ambazo zina tozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tozo hizi sisi katika Wizara yetu, nyingi tumezifanyia kazi lakini zipo nyingine zipo TAMISEMI na nyingine ziko Wizara ya Fedha. Naamini Wizara husika pia zitafanyia kazi. Tumeendelea kushauri kama Serikali ili kuona ni kwa namna gani tunafanya kuona mazao ya misitu yanakuwa nafuu yasiendelee kuwa ghali. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili tulilizungumza na tulilifanyia kazi na maeneo mengi ambayo yalikuwa yanatuhusu tumeyafanyia kazi na gharama zimepungua.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni eneo la kupandisha hadhi *TFS*. Tayari Wizara ilishakamilisha andiko kwa ajili ya kupata andiko ambalo limekusanywa na kupata maoni. Tumepokea maoni mbalimbali kutoka kwa wadau na Wizara inakamilisha kazi ya andiko hili ili kupeleka kwenye Kamati ya *Cabinet, Secretariat* kwa ajili ya kuendelea na taratibu nyingine.

Mheshimiwa Spika, Kamati inafamu vizuri kabisa kwamba Mheshimiwa Magdalena Sakaya ni Mjumbe wa Kamati, tuliwaahidi kwamba kabla suala hili halijafikia kwenye hatua ya mwisho, tutawapeleka kuweza kupata maoni. Kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba suala hili lipo kwenye mchakato na tunaendelea nalo vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu biashara ya viumbe hai na hasa kuhusu wananchi ambao wanafanya biashara ya viumbe hai ambao pesa zao bado ziko Serikalini, ni kweli na sehemu zote ambazo tumefanya ziara tumekutana nao. Suala hili Wizara yetu ilishalishughulikia na madai yao na orodha tulishayapeleka Hazina na yanafanyiwa kazi. Kwa hiyo, nawamba tu Waheshimiwa Wabunge suala hili liwe na subira. Ni kweli muda mrefu umepita lakini lazima tufahamu kwamba suala hili pia lilikuwa linagusa watu wengi, halikuwa la mtu mmoja. Kwa hiyo, lilihitaji uhakiki ambao Serikali imeshafanya na tumelipeleka Hazina linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya kifuta jasho, ni kweli kwamba malipo ya kifuta jasho, maeneo mengine yalikuwa yanachelewa lakini mwaka huu peke yake tumelipa takribani shilingi bilioni moja katika maeneo mbalimbali na tunayo madeni ya shilingi bilioni 2.2 ambayo tunaendelea kuyashughulikia. Kwa kweli ucheleweshaji ulikuwepo kutokana na uchelewaji wa taarifa kutoka kwenye Wilaya. Tunapopokea taarifa kutoka kwenye Wilaya, huwa tunazifanyia mchakato na baadaye kupeleka fedha. Zilikuwa zinachelewa sana kufika, lakini tumefanya marekebisho, tumeteua Afisa Maalum ambaye anasimamia eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaamini kwamba kama fedha zipo, ucheweshaji huo hauwezi kuwepo tena. Tunakubaliana na hoja kwamba kinga ni bora kuliko kusubiria kulipa na ninampongeza sana. Natumia nafasi hii kuwapongeza Gurumeti, nilikwenda Gurumeti na nikakuta wameweka uzio wa takribani kilometa 38 wa *electict shock,* wameweka pale kwa kutumia *solar power.* Hiyo imesaidia sana tembo na wafanyama wengine na majangili kwenda

kwenye vijiji na kuvuka kwenda kwenye hifadhi. Juhudi hizo tunaamini kwamba tunaendelea na maeneo mengine kwa kuweka walinzi wetu tumeongeza *Park Rangers* na idadi ya vikosi vya ku-*respond* na matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunafahamu yamekuwepo madhara haya, lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa kwamba Seriakli inathamini sana maisha ya wananchi kuliko maisha ya wanyama na tutaendelea kulishughulikia suala hili.

Mheshimiwa Spika, ilikuwepo hoja ya Mheshimiwa Daniel Mtuka, kuhusu juhudi za Wizara katika eneo la ufugaji wa nyuki. Mheshimiwa tunalifanyia kazi vizuri, tulisema hapa katika bajeti yetu ya mwaka 2019 tulitenga Mikoa 10, Singida ikiwemo *pilot* wa ufugaji wa nyuki. Kitabu chetu kwenye hotuba aya ya 77 ukurasa wa 34 na aya 81 ukurasa wa 36 tumeeleza vizuri hatua ambazo zimechukuliwa. Singida tumefungua kiwanda cha asali na tumepeleka pale mitambo na tayari tumefanya semina mbalimbali na kupeleka mizinga...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Constantine Kanyasu, tunakushukuru sana kwa ufafanuzi huo. Sasa nikukaribishe Mheshimiwa uweze kuhitimisha hoja yako, dakika 15. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na ufafanuzi mzuri uliotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, nitagusia hoja mbili ama tatu tatu, lakini kabla ya kufanya hivyo, naomba nitumie fursa hii kwa

namna ya kipekee kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na kwa kutuwezesha kwa mara nyingine tena kukutana hapa Bungeni siku ya leo kutimiza wajibu wetu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na shukurani hizo, kwa namna ya kipekee pia naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuniamini na kunipa heshima ya kuwa Waziri kwenye Serikali yake. Wabunge tuko wengi, sijui kwa nini Mheshimiwa Rais aliona kwamba nami ninafaa kupewa Wizara nzito kama hii ambayo nimepewa, lakini ninaamini sijamwangusha na ninaamini sijaiyangusha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimwa Waziri Mkuu kwa mwongozo na maelekezo mbalimbali ambayo wamekuwa wakitupa ili kuweza kutimiza wajibu wetu kama Mawaziri ndani ya Serikali. Bila wao pengine maisha yangekuwa magumu sana kwa mazingira ambayo sisi sote tunayajua. Kwa hivyo Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Makamu wa Rais wamekuwa *shock absorbers* wazuri na nawapenda kwa dhati. Nitoe shukrani zangu kwao na niwaombee kila la kheri katika siku zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru sana familia yangu kwa kuendelea kunipa moyo na kunitia nguvu ya kuendelea kupambana. Pia wananchi wa Jimbo letu la Nzega Vijijini kwa kuendelea kuniunga mkono na kunivumilia pale ambapo nimekuwa *busy* nikipambana na majukumu mbalimbali ya kitaifa kama Mbunge na kama Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe mwenyewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Uongozi wote wa Bunge letu Tukufu kwa kutupa miongozo mbalimbali, lakini pia kutupa ushirikiano mbalimbali ambao umetuwezesha kwa kweli kutimiza wajibu wetu ndani ya Serikali, wengine sisi ilikuwa mara yetu ya kwanza kuwa kwenye Serikali. Changamoto ni nyingi namna ya ku–*balance*

Bunge na Serikali na Jimbo na vitu kama hivyo, lakini kwa busara na hekima zako pamoja na Viongozi wengine wa Bunge, hatukuweza kupungukiwa hekima ya ku–*fit* kwenye viti ambavyo tulikuwa tumepewa.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru pia Mawaziri wenzangu wote kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa. Katika utekelezaji wa majukumu yangu sana sana kwa kweli *Chief Whip* wetu dada yangu, mtani wangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa namna ambavyo amekuwa akitu–*accommodate* na vurugu zetu. Sisi wengine kidogo tuliingia kwenye Uwaziri tukiwa bado vijana vijana kwa hivyo tunakuwa na *energy* ya kupitiliza, bila kuwa na akina mama kama hao wanatutuliza tuliza pengine kazi yetu ingekuwa ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba pia nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge Mheshimiwa Kemilembe Lwota na Kamati yetu yote kwa ujumla kwa ushauri, mwongozo na maelekezo mbalimbali ambayo wamekuwa wakitupa katika hatua mbalimbali za kutimiza wajibu wetu. Pia na Mwenyekiti aliyetangulia Mheshimiwa Nape tulifanya naye kazi vizuri kama Mwenyekiti wa Kamati hiyo na kwa mimi nawashukuru sana kwa kuniwezesha kutimiza wajibu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wajibu huu wa Waziri wa Maliasili na Utalii sio wajibu rahisi sana. Mara zote imekuwa ni vita, kupitisha bajeti ya Wizara hii kwa sababu nyingi mbalimbali, lakini nashukuru Mungu katika kipindi changu angalau nimeweza kushirikiana vizuri na Kamati na Wabunge wenzangu wote. Tumeweza kutimiza wajibu wetu ipasavyo na leo tunamaliza muda wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nimeteuliwa watu walisema pengine sintodumu zaidi ya mwaka mmoja, kwa sababu kwa historia ya Wizara hii Mawaziri walikuwa hawamalizi miaka miwili. Mwaka mmoja, mwaka mmoja

na nusu unatoka, namshukuru Mungu mimi nakaribia kutimiza wa tatu, kwa hiyo kama ni mwiko nimeuvunja, namaliza kipindi hiki. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majibu ya kina yatatolewa kwa maandishi na yatawasilishwa kwa watoa hoja na Wabunge wote ambao watapenda kuyapata. Naomba tu nijikite kwenye kufafanua kwa kirefu kidogo suala la namna ambavyo tunaitikia kutokana na janga la *corona* ambalo limeikumba dunia.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, baada ya janga hili kutangazwa na Shirika la Afya Duniani kwamba ni janga linalohitaji *emergency response,* nchi mbalimbali zilianza kuchukua hatua kali, zingine hatua za wastani, nyingine hatua za nafuu kidogo. Katika hatua ambazo zilichukuliwa na nchi nyingi mbalimbali mojawapo ni hatua ya kufunga mipaka, kuzuia safari za ndege, wengine kufunga mahoteli, kufunga *restaurants, bar*s na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, nyingine kuwafanya watu wao wakae ndani wasitoke nje, kwa maana hiyo hata kusafiri kwenda nje ya nchi ilikuwa ni jambo lisilofikirika. Kwa sababu hiyo sasa Sekta ya Utalii ambayo inaendana na uchukuzi kwa maana ya watu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ikaathirika sana duniani kote. Sisi hatukupata madhara ya haraka baada ya nchi hizo kuanza kuchukua hatua na badala yake madhara makubwa tumeanza kuyaona mwezi wa Tatu, wiki ya tatu kuanzia tarehe 20 kuja mbele.

Mheshimiwa Spika, madhara hayo yalianza kuonekana kwa baadhi ya Wageni ambao walikuwa wame–*book* safari za mwezi wa Nne, mwezi wa Tano, mwezi wa Sita na mwezi wa Saba kuzisogeza mbele. Wengi wakiamini pengine janga lingeweza kuisha mapema wangeendelea na ratiba ya shughuli zao kama ilivyokuwa.

Mheshimiwa Spika, sisi hatukukaa kimya kama Wizara lakini pia kama Serikali, tukiwa kama Wajumbe wa ile Kamati ambayo iko chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuliamua kufanya utafiti wa kina wa mezani na kuchambua taarifa mbalimbali ambazo zilikuwa zinapatikana. Katika utafiti ule ambao tulitumia njia ya kutazama *scenarios* tofauti tofauti tunaita *scenarios analysis* ambapo kwamba kama janga la *corona* litaisha mwezi Juni, 2020, nini kitakuwa kimetokea, tutakuwa tumepata madhara gani, picha halisi itakuwa nini. Kama janga litaisha mwezi Oktoba, 2020 nini kitatokea. Kama janga litaisha mwezi Desemba nini kitatokea, kama litaisha baada ya mwaka mmoja nini kitatokea. Kwa hivyo tulitazama *scenarios* tofauti tofauti tukafanya *simulation* na tukaweza walau kupata *picture* fulani ya kitu ambacho tutarajie kama sekta ambayo inatoa mchango wa zaidi ya asilimia 17.6 kwenye pato la Taifa. pia ni Sekta ya pili kwa kutoa ajira nyingi zaidi ukiondoa Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo kwa kweli majibu ya utafiti wetu hayakuwa mazuri sana kama nilivyoeleza kwenye ripoti yangu na kwa uchache tu ni kwamba, kama tutafungua biashara kuanzia mwezi wa Sita, wa Saba tutakuwa tumepoteza takribani ajira laki nne sabini na saba elfu na tutakuwa tumepoteza mapato kwa kiasi kikubwa sana kwa zaidi ya asilimia 75 ambayo tungeweza kuyapata katika kipindi hiki kama *corona* ingekuwa haijaathiri uchumi wa kitalii duniani.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho napenda kukisema ni kwamba, katika taarifa yetu ile tumepeleka mapendekezo ndani ya Serikali bado yanaendelea kufanyiwa kazi. Baada ya kupokea maoni na ushauri wa Wadau mbalimbali kwenye Sekta ya Utaliii na sisi tukayafanyia uchambuzi, tukapata *picture* Fulani, tukaona kuna mambo fulani ambayo kama yatapata *approve* ya Serikali basi yanaweza yakasaidia walau kupunguza madhara ambayo yameweza kujitokeza kutokana na ugonjwa wa *COVID 19*.

Mheshimiwa Spika, kuna mapendekezo ambayo tumeyaweka kwenye maeneo ya kikodi ambayo

watayazungumza wenzetu wa Wizara ya Fedha wakati muafaka utakapofika. Kwa mfano, tumesema *quarter* ile ya kwanza mwezi wa kwanza mpaka wa tatu tulikuwa hatujapigwa na *corona*, maana yake na ndio *quarter* ambayo watu wanafanya makadirio ya kodi wale wafanyabiashara wetu. Wanafanya makadirio ya kodi zile *provisional taxes*, wanapofanya zile wanakadiria *quarter* zote nne mpaka mwisho wa mwaka, sasa wanatakiwa walipe mpaka kufikia tarehe 31 mwezi Machi.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo wakati wanakadiria alikuwa ana uhakika wa wageni kulikuwa hakuna *cancelations* kulikuwa hakuna *restrictions* za kusafiri huko duniani, kwa hivyo alikuwa ana uhakika atapata yale mapato, lakini leo baada ya hii *corona* kutokea sasa yale makadirio aliyoyafanya hawezi kupata hizo pesa. Kwa hivyo tukiendelea kumdai ataamua ku–*declare bankrupt* atafunga biashara, ata–*lay off* wafanyakazi na madhara ya kiuchumi na kijamii yatakuwa makubwa zaidi kuliko ambavyo itakuwa. Kwa hivyo tumeona ni jambo la muhimu lazima tulipendekeze kwa wenzetu walitazame na pengine tupate ridhaa ya Serikali tuweze kutoa hiyo ahueni kwa wafanyabiashara kwenye Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, pia tumeona ili ku–*respond* pale tutakapoamua kuanza kufungua biashara ni lazima tuweke ahueni kwenye *landing fees*, kwenye *parking fees* za ndege ili kwa sababu kutakuwa kuna ushindani kila nchi itaanza kufungua kwa hivyo yale mashirika makubwa ya ndege yatachagua yaende wapi kwa hivyo sisi tukiwa tumefungua mapema, tumetoa ahueni vizuri, tumezitangaza vizuri ahueni zetu, maana yake mashirika yanaweza yakaanza kufungua safari zake kuja Tanzania kuliko kwenda kwenye sehemu zingine.

Mheshimiwa Spika, pia kuna mapendekezo tumeyaweka kwenye *banking sector* kuhusu zile riba, kipindi hiki ambacho wafanyabiashara hawafanyi biashara. Pengine tungeweza ku–*consider* kama Serikali kupitia wenzetu wa Hazina kutoa ahueni fulani kwa kuziahirisha baadhi ya riba

ama baadhi ya *payment* za kisheria kama zile *Pay As You Earn, SDL,* kuahirisha sio kuzifunga kabisa. Kuziahirisha ili tu mtu asidaiwe katika kipindi hiki ambacho yeye hatengenezi pesa, kwa hivyo kuna mambo kama hayo ambayo tumeyatafakari.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tathmini yetu inaonesha kwamba katika Sekta ambazo zitawahi ku–*bounce* mapema zaidi tutakapoanza kufungua milango ya biashara ni Sekta ya Utalii. Kwa hivyo pamoja na habari mbaya tulizonazo pia kuna habari njema kwamba pengine hii ni sekta ambayo itakuwa ya kwanza kuanza ku–*recover* kuliko sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo tumeamua kujipanga vizuri sasa hivi mwezi huu Mei na tayari tumeshaanza kuomba ridhaa kwa Viongozi Wakuu waturuhusu kufanya baadhi ya ahueni kwa mfano ile *mandatory quaranteen* ya siku kumi na nne iondolewe kuanzia mwezi Juni. Kwamba mtu akija na ndege akatua Uwanja wa Ndege wa KIA ama Dar es Salaam anatakiwa akae yeye mwenyewe kwenye *self quaranteen* kwa gharama zake. Mtu hawezi kuja kutalii, *it's obvious* kwa nini sasa aje akae kwanza *quaranteen for fourteen days at his own cost and then* ndio aende kutalii, haitowezekana.

Mheshimiwa Spika, kama Wizara tukaona hilo ni sharti ambalo kwa sasa hali–*make sense* kwa sababu tuliliweka wakati ule mwanzoni wakati ambapo tulikuwa tunazuia *imported cases* za *corona* kutoka nchi nyingine kuja hapa nchini, lakini sasa *corona is no longer imported,* corona *is local*, *corona* ipo na sisi, tupo nayo Bungeni, tupo nayo kila sehemu. Kwa hivyo kwa kuwa *corona* ipo tujifunze kuishi nayo, hatuwezi kuikwepa. Tujifunze kuishi na *corona* turudi kwenye shughuli zetu, tufanye kazi, tuzalishe, tukuze uchumi kwa sababu mpaka sasa hivi vifo vya *corona* havijafika hata 100, lakini watu wetu wakikosa chakula kwa miezi mitatu tu tutapata maafa ya watu wengi zaidi kufa kwa njaa kuliko hata kufa kwa *corona*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukaona ni vyema tukatafakari sana jambo hili na sisi kwenye Sekta ya Utalii, tunaona kwamba kwa kuwa sekta yetu inaweza ikawa ya kwanza ku–*recover* kwa sababu nchi zitakapoanza kufunguka tu watu watataka kwenda kupumua, watataka kwenda ku–*breath,* kwa hivyo watataka kusafiri kwa sababu ni kitu ambacho wameki–*miss* wa muda mrefu, kwa hivyo watakapoanza kutaka kutoka Tanzania iwe tayari kuwapokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tayari tunaanza ndani ya Serikali kuzungumza kuondoa zile siku 14 za *quaranteen* ili iwe rahisi kwa ndege kuanza kufikiria kuja Tanzania, lakini pia kufungulia ndege zinazotaka kuja Tanzania zianze kuja. Tayari nilikuwa napitia taarifa mbalimbali, Mashirika makubwa ya ndege yameanza kufunguka. Kuanzia mwezi wa Nne tarehe 3 *Emirates* wameanza kufunguka kwa ajili ya kufanya safari zile wanaziita *essential travels,* wanasafiri kwenye *destinations* fulani kadhaa kwa malengo fulani fulani, ama malengo ya kuleta *essential goods and services*, ama kwa malengo ya kuwarudisha watu makwao, kimsingi wameanza kufungua.

Mheshimiwa Spika, tarehe 3 Mei, 2020 juzi hapa Shirika la ndege la *KLM* na lenyewe limeanza kufungua safari zake. Tarehe 8 Mei Shirika la ndege la SWISS na lenyewe linaanza kufungua safari zake. Maana yake ni kwamba wameshagundua kwamba *corona* ipo, tuanze kuishi nayo. Kwa hivyo tunaanzaje kuishi nayo, sisi tumeamua kuitisha kikao cha Sekta ya Utalii, Wadau wote wa Sekta pamoja na Wadau wa ndani ya Serikali, tutakutana Arusha siku ya Jumatatu wiki ijayo kuangalia ni namna gani tufungue biashara yetu kufikia Juni.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kama Mashirika makubwa ya ndege yanaanza kufungua, Mashirika ya Mahoteli yanaanza kufungua biashara zake. Sisi ni lazima tukae tayari kwa ajili ya kufungua biashara zetu pengine kuanzia mwezi Juni, 2020. Kwa hiyo tutatengeneza *safety protocol, cleanness protocol, social distancing protocol* na kuweka masharti ya lazima kuhusu kuvaa barakoa,

*sanitization* na vitu vingine na kuweka *protocol* nzuri ya namna chumba kinavyosafishwa, kinavyotunzwa, chakula kinavyopikwa, kinavyoandaliwa, kinavyokuwa *saved* na mtu awe na amani kwamba akija Tanzania atakuja atatalii na atatalii kwa usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo kuanzia Jumatatu tunajifungia tunatengengeza hivi *guidelines* zote, tunakuwa tayari kwa ajili ya kupokea wageni. Na pengine kama tutaruhusiwa ndani ya Serikali baada ya kupeleka mapendekezo yetu Mwezi Juni, tuanze kupokea wageni. Kwa hivyo yale masharti ambayo yalikuwa yanazuia ndege kutua, mahoteli yamefungwa, yaondoke, turudi kwenye biashara, mwendo wa barakoa, mwendo wa *social distancing,* tunakuwa *strict* kwenye usafi, biashara zinarudi kama kawaida, Serikali haisimami, mapato hayakwami, nchi inasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muda wangu umeisha nini.

**MBUNGE FULANI:** We endelea tu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, sijui kama bado nina dakika huko lakini ...

**SPIKA:** Muda umeshaisha.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache niliyoweza kuyasema nashukuru na katika hatua hii naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili Dkt. Hamis Kigwangalla kwa hitimisho zuri na lenye kutia moyo, linaloonyesha kwamba sasa karibu kunapambazuka katika sekta hii, taratibu tuanze kurudi kwenye *normality*.

Sasa Mheshimiwa Waziri ameshahitimisha hoja yake na kura zimekwishapigwa kwa maana ya kwamba naomba sasa mkubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kura zinaonesha kwamba walio wengi wameafiki kwamba hoja hii ipite. *(Makofi)*

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2020/ 2021 yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii…..Sh.69,573,850,000/=

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii…..sh.45,020,102,000/=

**SPIKA:** Nichukue nafasi hii kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Kigwangalla; Mheshimiwa Naibu Waziri, Constantine Kanyasu; Katibu Mkuu, Profesa Mkenda; Makamishna, Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa sana ambayo mmekuwa mkiifanya. Kipekee sana jambo la ujangili mmelidhibiti kisawasawa. *(Makofi)*

Ni historia kabisa katika nchi yetu kunaweza kukawa na kipindi ambacho pamekuwa na unafuu mkubwa sana katika masuala ya ujangili kama kipindi hiki, hongereni sana na kupitia kwenu mtupelekee salamu na kwa wahifadhi wenzangu wote kokote kule waliko. Tunajua ni watu wanaofanya kazi katika mazingira magumu sana. Poleni sana maeneo mengine yana mbung'o, maeneo mengine yana wanyama wakali, maeneo mengine ni mbali na huduma zozote zile lakini wana-*persevere* hawa watu na ni watu ambao wana moyo mkubwa katika kufanya kazi yaani wanajitahidi sana na baadhi yetu ndio tulipata ungangari kutoka huko huko, ndiyo. Kwa hiyo tunawashukuruni sana muendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

Yako mambo hata Wabunge wamechangia na tuliwahi kusema miaka yote ambayo tumekaa hapa kwa Wizara ya Fedha nao wanajua, najua wanaendelea na mjadala na Kamati ya Bajeti, natumai ipo siku mtaangalia baadhi ya ushauri ambao huwa tunawapa, kuyatazama kama haya Mashirika, haya mashirika *vision* na *mission* yake si Mashirika ya kibiashara ni uhifadhi, ndio *objective number one*, uhifadhi. Uhifadhi huo lengo lake ufanyike kwa rasilimali ile kuzalisha uwezo wa kujihifadhi na ziada iende kwenye Serikali na matumizi ya wananchi. Sio tuchukue hela za wananchi tuende tutumie katika kumlinda tembo ndio madhumuni yake. Kwa hiyo inapotokea *crisis* kama hii basi Serikali inaangalia nini cha kufanya.

Huko nyuma kuliwahi kuwa na fikra na walianza kuwa na *endowment fund* na ikawa na hela nyingi tu kwa sababu lazima kwenye mambo ya utalii haya lazima ujue unapokuwa na *boom* ipo siku utalii ni kitu *very sensitive*, kitu kidogo tu kikitingishika, utalii unakata. Kwa hiyo walikuwa wanajipanga kwa maana hiyo ya siku ya jua, lakini katikati pale ikaamuliwa kwamba fedha zote ziende Hazina. Kwa hiyo hawana kitu cha namna hiyo. hali inayotokea hapa inatupa funzo kwamba tukivuka, huko mbele ni vizuri kufikiria nyakati kama hizi au zinazofanana na hizi kwamba wanaweza labda wakawekeza hata kwenye sekta ambazo sio lazima ni *related* sana na utalii ili katika wakati wa mtikisiko basi badala ya kurudi kwa mama kule Hazina *(Treasury)* wanaweza wakawa na kipato kutoka maeneo mengine ya uchumi wa nchi au uchumi wa dunia ili waweze ku–*sustain* na kwa maana hiyo usije uhifadhi ukafutika duniani.

TAWA hawa wana matatizo makubwa mengi, muangalie kipekee sana huko tunapokwenda Mwenyezi Mungu akijalia. *TFS* wanajitahidi wanakwenda vizuri, wanahitaji kulelewa ili waweze kuimarika zaidi na wengine hawa ndiyo hivyo mtihani ni mkubwa wa kuweza kuvuka, kwa hiyo tunawashukuruni sana.

Sasa nikirudi kwenye matangazo ya mwisho mwisho, niseme kwanza kwamba Wabunge wengi kama tulivyosema

siku zote ni Wabunge wa mara ya kwanza na hasa wa Upinzani, ni Wabunge wa mara ya kwanza na kwa hiyo baadhi ya viongozi wao wamekuwa wakiwateka nyara kwa umara ya kwanza wao, kwa nini nasema hivyo? Wamewajaza imani za kufikiri kwamba Chama chao peke yake ndicho chenye *alfa na omega* katika kazi zao za Ubunge kitu ambacho si kweli kwa kiasi hicho. Mbunge kwa lolote analolifanya Bungeni anapochangia, anapofanya shughuli zozote zile za Kibunge ana mambo kama matano ya ku-*balance,* kwanza lazima aangalie taratibu za Kibunge kwa maana ya Katiba ya Nchi Sheria mbalimbali, Kanuni za Bunge na kadhalika.

Pili, Mbunge huyo lazima atazame je, jambo linaloendelea ambalo anatakiwa yeye afanyie kazi lina maslahi gani kitaifa au halina maslahi? Hiyo ni *balance* ya pili. *Balance* ya tatu kwa Mbunge lazima angalie Jimbo lake, wananchi waliomtuma kuja je, hili linalozungumza, hili linalojadililwa, hii shughuli inayofanyika kwa wananchi wangu walionituma lina maslahi yoyote au halina maslahi yoyote na pale anapochangia anaweza akasema wazi kabisa mimi hili kwa sababu ya wananchi wangu sikubaliani na mnamwelewa Mbunge wa namna hii.

*Aspect*, ya nne ni Chama kilichomtuma, je, katika jambo lile kina mtazamo gani. *Aspect* ya tano ni Mbunge mwenyewe, wewe mwenyewe hiyo barua ya Mbowe hiyo, wewe mwenyewe unaona ina mantiki, wananchi wa Jimbo lako wanakubali kwamba wewe ukakae ndani, usifanye Shughuli za Bunge? Je, hilo jambo lina maslahi kitaifa? Je, hilo jambo limetokana na vikao vya chama chako au ni amri ya mtu, maana mtu siyo chama. *(Makofi)*

Sasa Wabunge ni watu wazima, sasa kwa sababu ni mara ya kwanza wanajazwa vichwani kwao kwamba bwana Mbowe akitaka, Mbowe asipotaka, wewe unakuwa Mbunge au hauwi Mbunge kwa ajili ya mtu mmoja, hilo jambo halipo. Kwa hiyo katika hayo usipo-*balance* vizuri wewe ukabeba hili moja tu, itakula kwako. Sasa wamekuwa waki-*rob* nchi, wanatumia neno *lockdown,* sasa

wananchi wengi kule Kongwa na mahali pengine hawaelewi *lockdown* ndiyo nini? Labda ni jambo jema hilo kwa nini wanakataa hawa, *lockdown* kwa nini Serikali inakataa? Yaani *lockdown* wananchi wote muwekwe rumande ya hiari, kila mtu awe pale kwake utakayekutwa Morogoro, ubananishwe hapo hapo, utakayekutwa Tabora hapo hapo, nyumbani kwako haya *lock down* hakuna kutoka kuzunguka kufanya biashara, kwenda mashambani haiwezekani inabidi mkae ndani.

Sasa nani anataka kukaa rumande na pia hata hiyo rumande katika nchi hizo zilizo nyingi Mabunge ya nchi hizo ndiyo yameshauri Serikali, Bunge kama Taasisi kwamba Serikali hebu wekeni *lockdown,* sisi hatujaishauri Serikali jambo hilo na hatudhani kama wapigakura wetu kweli wanataka jambo hilo. Maana kama kweli wanataka hebu waseme siku moja Bunge bado lipo, tuishauri Serikali ijaribishe tu *lockdown* hata ya siku saba, Watanzania hawa waelewe hiyo *lockdown* ni kitu gani? Hiyo rumande ni hatari kubwa, kwa hiyo, mwongozo ambao Mheshimiwa Rais wetu anatuongoza na Serikali yake tunadhani ni jambo la maana sana. *(Makofi)*

Wale wanaoeneza maneno ni hawa hawa kwamba pale Bungeni pako hivi na hivi, wakumbuke katika muda wa masaa 24, Mbunge anakuwa hapa kwa lazima tuseme, masaa manne haya ya Kikao kama hiki katika masaa 24, *four hours only* katika masaa 24 kwa hiyo hizo saa nne ndiyo zinafanyaje na hizo saa 20 nzima ambazo mtu anakuwa huko.

Sasa nilielezea jana kuhusu kuchukua fedha maana wamelipwa tangu tarehe mosi mpaka tarehe 17 mwezi huu wa Mei, halafu wakaamua kuwa watoro na kutokufanya kazi. Naendelea kusisitiza ambao hawatarudisha fedha hizo tutawachukulia hatua kwa sababu tutahesabu ni wizi tu, ni wizi wa kuaminiwa, ulipewa fedha umeaminiwa kwamba zitakusaidia kufanya kazi, wewe unaamua kutoroka, nilisema jana ni utoro na warudishe. Ukirudisha hatuna maneno hii habari ya kusema tutakata baadaye haipo hiyo, fedha

inapochukuliwa *illegally* kama hizi ni za kurudisha wakati huo huo na hasa kwa Kiongozi. Kwa hiyo wanaobanisha huko wakiamini hawatarudisha haiwezekani lazima zirudi hizi fedha.

Waheshimiwa Wabunge, bado natafakari kwa mtu ambaye amekuwa mtoro kwa wiki mbili kazini kwake, kule Serikalini kabisa *proper* siku tano unafukuzwa kazi, bado sifikirii kwenda huko lakini kwa kawaida ya mtu ambaye hajaenda kazini wiki mbili, hivi huwa analipwa mshahara? Kwa hiyo huko waliko wajue mshahara wa mwezi Mei, wakiendelea kufuata hilo nimesema una-*balance* mambo matano, wewe ukilibeba moja katika mzani ukaacha manne, sasa huu mshahara wa mwezi wa Tano huu labda wanieleze ni kwa nini walipwe mshahara wa mwezi wa Tano. Nikieleza mambo haya Wabunge hawa wananielewa, mwezi huu una mazingira haya, hayaruhusu mchezo mchezo wa mtu kuwaingiza katika mtihani mkubwa kama huu. *(Makofi)*

*Opportunity lost* ni kubwa sana, ni kubwa sana, lakini kazi kwenu. Pia natoa tangazo kwamba tumeshapokea kutoka taasisi mbalimbali za kifedha nchini taarifa za bakaa ya mikopo ya Waheshimiwa Wabunge wote. Mikopo mbalimbali ambayo itatumika katika kukokotoa na kulipa mafao ya hitimisho ya kazi ya Ubunge tumeshapokea tayari. Kwa hiyo kesho nawaelekeza watu wangu wa uhasibu watoe barua kwa Wabunge waliopo kwa kumkabidhi kwa *dispatch*, siyo kwa *email* wala kupeleka kwenye *tablet* kwa sababu hii hatutaki iwe tangazo, atapewa Mbunge moja moja kwa *dispatch* waliopo. Hawa wasiokuwepo, waendelee kukaa huko wakose hizi *information* na mwisho wa mwezi huu kuna shughuli inaendelea ambao wao wanaifahamu vizuri kuliko mwananchi mwingine, basi watashangaa kwa yatakayoendelea.

Nasema tena nawaasa Wabunge hawa kurudi, wapo kwenye mtihani mkubwa kweli kweli wa kuendelea kumtii huyo jamaa yao au kurudi ili sasa tuweze kuendelea katika utaratibu unaotakiwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya shughuli zangu kukamilika katika meza hii, naomba sasa niahirishe Shughuli za Bunge hadi kesho saa nane kamili mchana.

*(Saa 12.09 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 8 Mei, 2020, Saa Nane Mchana)*